

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kumi na Nane - Tarehe 28 Juni, 2010

(Mkutano ulanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WAZIRI WA MIUONDOMBINU:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 121

Matatizo Katika Hospitali ya Wilaya - Geita

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Wilaya ya Geita inahudumia Kata 33 na madaktari Bingwa ni wawili (2) tu, na kwa kuwa upanuzi unasuasua na utawala ni mbovu:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha matatizo hayo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Hospitali ya Wilaya ya Geita ilijengwa mwaka 1957 kwa lengo la kuwahudumia wakazi wapatao 100,000 kwa kipindi hicho. Hadi kufikia Mei, 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina jumla ya Vijiji 191, Kata 33, Tarafa 7, Majimbo matatu ya Uchaguzi na wakazi wapatao 899,614. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina jumla ya vituo vya huduma ya Afya 61 ambavyo ni: -

Hospitali 1 ya Wilaya, vituo vya Afya 9, Zahanati 39 za Serikali, Zahanati 8 za Mashirika yasiyo ya Kiserikali, na vinne (4) za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Geita ina watumishi wenyewe taaluma mbali mbali 218 kati ya watumishi 504 wanaohitajika sawa na asilimai 56.7 ya mahitaji. Kati ya watumishi hao madaktari wa magonjwa ya kawaida ni wawili (2) na Daktari mmoja wa kinywa na afya (*DO*).

Suala la upungufu wa madaktari bingwa sio la hospitali ya wilaya ya Geita peke yake bali ni tatizo la Nchi nzima. Hata hivyo Serikali kuititia Mpango wa MMAM inachukua juhudhi za makusudi kuimarisha vituovya kutolea huduma za afya vilivyopo kwa kuviboresha na kuongeza idadi ya watumishi wa kada mbalimbali. Katika mwaka 2010/2011 hospitali ya wilaya ya Geita inatarajia kupata madaktari wawili (2) na madaktari wasaidizi watatu (3).

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za afya ziendane na ongezeko la idadi ya watu na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya wilaya, halmashauri ya wilaya ya Geita imejenga kituo cha Afya cha Nyankumbu kilichopo mjini Geita na kimeanza kutoa huduma za afya.

Vituo viwili vya Kharumwa na Nzera vinaendelea kufanyiwa ukarabati ili kuvipanua viweze kuhudumia wagonjwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala mbovu katika Hospitali ya Wilaya ya Geita, Serikali itafuatilia ili kuhakikisha kwamba watumishi wanafanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali sana kuona umuhimu wa wilaya ya Geita kuiweka katika mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, Waziri yeche amekiri kabisa kwamba wananchi wa Wilaya ya Geita ambao sasa wako kwenye mkoa wa Geita walikuwa watu wengi sana na huduma wanayoipata si ndogo sasa imekuwa Mkoa wa Geita. Je, Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba sasa hospitali ya Mkoa wa Geita inaleta wataalam wengi ambao wanawenza kuhudumia hasa akinamama wenge magonjwa yanayokidhi haja yao na watoto?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ni kwamba sasa Geita imekuwa Mkoa, kwa hiyo tunasubiri ili iweze kutolewa katika *Government Notice* ili shughuli ziendelee.

Naamini kabisa kwamba kwa sababu ni Mkoa basi Geita itapata hadhi yake, Bajeti itatengwa ili iweze kupata huduma zote kama mkoa. Lakini wakati huo huo zile wilaya nyingine tutakuwa tunaziendeza kuzishauri ziweze kujenga ili hata hivyo ikiwa mkoa isiwe inaleta tena msongamano kwa kutegemea hospitali ya mkoa. (*Makofî*)

Na. 122

Ukosefu wa Maabara Shulenii

MHE. HAFIDHI ALI TAHIR aliuliza:-

Kwa kuwa, moja kati ya sababu zinazosababisha wanafunzi wengi kufeli katika mitihani yao ni ukosefu wa maabara mashulenii.

(a)Je, ni asilimia ngapi ya shule za Serikali (za Sekondari na msingi) zenye maabara na ngapi hazina maabara?

(b)Je, ni asilimia ngapi ya shule za Seminari zina maabara na ngapi zisizo na maabara ambazo Serikali imezisaidia?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, maabara ni muhimili wa masomo ya sayansi shulenii hasa shule za sekondari. Kukosekana kwa maabara kunasababisha kufeli masomo ya Sayansi. Serikali kwa kuliona hilo, inasisitiza sana kuitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kuwa shule zote za Sekondari sharti ziwe na maabara za Sayansi, kwa madhumuni ya kuwa na wanasayansi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana kujenga maabara mpya katika shule mpya zinazoanzishwa pamoja na kuimarisha zilizopo na hivyo kuwa na idadi ifuatayo.

Shule za skondari za Serikali zilizopo hadi Desemba 2009 ni 3,283, kati ya shule hizo zenye maabara ni 728 na zisizo na maabara ni 2,555 ambazo ni zile zilizojengwa na Serikali pamoja na kwa nguvu za wananchi.

Kiasilimia shule zenye maabara ni asilimia 22 na zisizo na maabara ni aslimia 78. Shule za msingi za Serikali katika kujifunza somo la Sayansi kwa vitendo zina vivunge vya Sayansi ambavyo zina vifaa muhimu vya kufanyiwa majaribio ya sayansi kwa vitendo. (*Makofii*)

Mkazo kwa hivi sasa ni kuimarisha shule za Sekondari zilizojengwa kwa mchango mkubwa wa wananchi ili ziwe na miundombinu kamilifu ikiwemo maabara za sayansi. Katika mpango wa maendeleo ya elimu ya Sekondari awamu ya pili (MMES) miundombinu muhimu kama maabara na nyumba za walimu imetiliwa mkazo.

(b) Mheshimiwa Spika, shule Seminari zilizopo ni 104 na kati ya shule hizo 103 zina maabara ambayo ni asilimia 99% ya shule za semiari. Shule moja ya seminari ya Kipata iliyoko katika Manispaa ya Ilala haina maabara na hadi sasa ina kidato cha tatu. Aidha, Serikali haina mpango wowote wa kuisaidia Seminari hiyo.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu lakini kama Serikali inafahamu kuwa kuwepo kwa maabara katika shule zetu za sekondari kunasaidia sana watoto kutokufeli na kutokuwepo watoto wengi wanafeli.

Sasa Serikali ina mpango gani basi mbadala ambao utawafanya wanafunzi katika shule zetu hizi waweze kufaulu katika somo hili la Sayansi ambalo ni muhimu sana ukizingatia zaidi kwamba sasa hivi kuna shule 2,555 ambazo hazina maabara hivyo wanafunzi watapelekwa wapi katika suala hili? Serikali ina mpango gani mbadala?

Mheshimiwa Spika, anaweza kuliambia Bunge hili ni sababu gani kubwa iliyopelekea shule za Seminari kufikia katika kiwango cha asilimia 99? Kwa kutokuwa na

maabara katika shule hizo lakini anaweza kuniambia ni kada gani inayosoma katika shule hizo za Seminari?

SPIKA: Ni nini, kada sikuelewa.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Ni kada gani ya kipato inayosoma katika shule hizo za Seminari?

NAIBU WAZIRI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mpango mkakati ambao katika hotuba ya bajeti mwaka 2009/2010 Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya elimu alieulezea kwamba baada ya kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga madara kwa kushiriana na wananchi katika awamu inayofuata ya mpango wa elimu ya sekondari kipaumbele cha kwanza ni maabara hivi sasa tunavyozungumza andiko limekamilika limegawanywa katika awamu tatu na kwamba maabara zitaanza kujengwa mara baada ya hotuba ya bajeti ya 2010/2011 kwa kushirikiana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, suala la mbadala walimu wamepewa mbinu za kutumia badala ya maabara kamilifu. Hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Spika Serikali imeanzisha mpango maalum wa kufufua maabara na kuimarisha mbinu za ufundishaji kwa walimu wa sayansi kambi kubwa iko mkoani Iringa inaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la kada gani wanaosoma kwenye shule za sekondari za wamisionari nadhani anafahamu kwamba hizo ni shule binafsi mwenye uwezo anakwenda.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa pamoja na uhaba wa maabara sababu nyingine inayofelisha vijana kwa wingi ni uhaba wa mwalimu na kwa kuwa Serikali sasa hivi inafanya jitihada kubwa za kutengeneza walimu zaidi.

Je, wakati tunasubiri matunda hayo mazuri isingekuwa jambo zuri kwa Serikali kuwaruhusu vijana wa *form four* wanaofeli mitihani yao kwa sababu ya uhaba wa walimu labda mmoja wa sekondari wafanye mitihani ya marudio kama *school candidates*, kwa sababu sio kosa lao wala si kosa la wazazi wao?

NAIBU WAZIRI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba idadi kubwa ya wanafunzi hawafanyi vizuri katika mitihani yao kutohana na kukosa walimu na masuala mengi muhimu. Suala la kurudia kama wanafunzi shulenii ni la kisheria, sheria tulizonazo hivi sasa za Baraza la mitihani haliruhusu. Tutaomba kama kuna umuhimu

huo basi Mheshimiwa Mbunge alilete tutalijadili kuitia advisory board tuone namna gani tunaweza kulifanyia.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kutoa tu taarifa rasmi kwamba wanafunzi wanayo fursa ya kurudia mitihani kama wanafunzi wa kujitegemea, hiyo ni haki yao ya msingi.

Na. 123

Mnara wa Mawasiliano wa Tigo Ulioko Lituhi

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA) aliuliza:-

Kampuni ya simu ya *TIGO* ilijenga mnara wa mawasiliano kwenye mji mdogo wa Lituhi tangu mwaka 2007 lakini hadi sasa haujaanza kutumika:-

(a)Je, mnara huo utaanza kutumika lini, na mawasiliano yanaweza kuwafikia wananchi wa maeneo ya Kata ya Ngumbo umbali wa kilometra 35?

(b)Je, ni nani atalipa gharama ikiwa uharibifu wowote utatokea hasa ikizingatiwa kuwa hakuna mlinzi kwenye eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Ni kweli kampuni ya simu ya mkononi ya *TIGO* ina mnara wa mawasiliano katika eneo la Lituhi tangu mwaka 2007. Mnara huo haujaanza kutumika kutohana na kutounganishwa katika masafa na minara mingine ili kuweza kusambaza mawasiliano ya simu.

Hata hivyo, kampuni ya *TIGO* inaendelea na jitihada za kuunganisha mnara huu, na utaanza kufanya kazi kwenye mwaka wa fedha 2010/2011. Mnara huu ukianza kutumika utawezesha mawasiliano kuwafikia wananchi wa maeneo ya kata ya Ngumbo umbali wa kilometra 35.

(b)Mheshimiwa Spika, mnara huu ni mali ya kampuni ya simu ya *TIGO*. Hivyo uharibifu wowote utakaotokea utagharamiwa na kampuni hiyo.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba hali ya mawasiliano katika ukanda wa ziwa Nyasa ambayo kwa shukrani kabisa sasa hivi ni wilaya kwa kweli ni duni sana.

Mara ya mwisho nilivyokuwa kule wiki iliyopita ni kwamba kuna watu wamefariki ziwani kwa sababu ya kukosa mawasiliano ya kuomba msaada. Matatizo hayo yapo katika kijiji hicho cha Ngumbo, kijiji cha Kihagala kwenye Bandari ya Nchambe, kijiji cha Matuta na hali kadhalika katika Jimbo la Peramiho, Muhukulu.

Mheshimiwa Naibu Waziri utatusaidia vipi kwa kutumia mtandao wowote ule ili mradi watu hawa waweze kuishi katika hali ya mawasiliano?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye katika maeneo fulani ya maeneo ya ziwa hakuna mawasiliano mazuri ni kutokana na Jiografia ya milima ambayo inaziba sana kupeleka mawimbi minara inapowekwa.

Napenda tu niyachukue maombi haya ya Mheshimiwa Stella kwa sababu hajawahi kunipa toka nipo Bunge hili maombi hayo ili niweze kuyafanya kazi.

Lakini niseme pia ipo minara Mbamba Bay na Lihuli ambayo *TTCL Mobile* imefanya na inafanya kazi vizuri tutaendelea tu kuwashamasisha wenzetu waone umuhimu wa kutafuta teknolojia muafaka kwa maeneo haya ili wenzetu nao wasikose mawasiliano muhimu hasa kwa huduma zao za muhimu zinapojitokeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona kwanza kabisa naomba nimpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia sekta hii na imeonyesha mafanikio makubwa.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifanya ziara katika wilaya yangu ya Namtumbo na kuzindua mnara wa *VODACOM* na katika ziara ile maafisa wa *VODACOM* waliahidi mbele ya mkutano wa hadhara kwamba watejenga mnara katika kata iliyompakani kabisa na Msumbiji ya Magazine na kata Namabengo mwezi Desemba mwaka jana na hawajafanya hivyo mpaka sasa lakini pia ni kampuni ya *TIGO* nayo iliahidi kujenga katika kata ya Kitanda nao bado hawajafanya hadi sasa. Je, Serikali kwa kutumia busara yake inaweza kuwakumbusha kampuni hizo ili waweze kufanya utekelezaji wa ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa mbunge kwamba nimefanya ziara katika maeneo yake na makampuni haya yalituahidi kutekeleza wajibu wao.

Lakini si kwake yeye tu lakini kwa Mheshimiwa Mbunge wa Peramiho kwa Mheshimiwa Kumchaya, kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, sehemu zote hizo mimi ambazo nimepata nafasi ya kuzitembelea ni meziandikia na

nimesisitiza na nimewaita ofisini kwangu kuwaomba kwamba ahadi walizozitoa wanawajibu wakuzitekeleza.

Napenda nikiri mbele yako kwamba inawezekana labda wana matatizo ya kifedha au vipi lakini mimi nitaendelea as *long as I m here* nitaendelea kusitisitza kwamba umuhimu wa mawasiliano katika maeneo husika hasa maeneo niliyoyatembelea Loliondo Longido, kwa Mheshimiwa Kumchaya, kwa Mheshimiwa Mbunge wa Namtumbo na kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Peramiho. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa kwa kuwa wote mmetajwa ndiyo mmejibiwa hivyo.

Na. 124

Bei ya Zao la Kahawa Karagwe

MHE. DIANA. M. CHILOLO (K.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES) aliuliza:-

Bei ya kahawa inayolipwa kwa wakulima wa Karagwe iko chini ikilinganishwa na ile inayolipwa nchini jirani ya Uganda.

Je, ni kwanini bei ya kahawa inayolipwa kwa wakulima wa Uganda isilipwe kwa wakulima wa Karagwe?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO- (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna tofauti ya bei anayolipwa mkulima wa kahawa nchini Tanzania ikilinganishwa na mkulima wa kahawa ya Robusta nchini Uganda. Kwa mfano, kati ya mwezi Juni na Desemba, 2009 kilo moja ya kahawa ya Tanzania iliuzwa kati ya shilingi 750 na 1,200 na Uganda kilo moja iliuzwa kati ya shilingi za Tanzania 874 na 1,888.

Mheshimiwa Spika, ili wakulima wa Karagwe waweze kulipwa bei nzuri kama wenzao wa Uganda Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Kuanzia msimu huu, Bodi ya Kahawa itaanza kutoa bei elekezi itakayokuwa inaonyesha bei anayostahili kulipwa mkulima kulingana na soko la dunia na ile ya mnada wa Moshi.

(ii) Bodi ya Kahawa itaendelea kuhawa ya Tanzania kupitia maonesho ya kimataifa, kama vile *specialty coffee Association of Japan (SCAJ); Eastern Africa Fine Coffee Associations (EAFCA)* na *Specialty Coffee Association of America (SCAA)* ili kupanua masoko mapya.

(iii) Bodi ya Kahawa itaendelea kutoa leseni ya kuza kahawa moja kwa moja nje kwa wazalishaji inayomwezesha mkulima kuza kahawa kwenye masoko ya nje yanayotoa bei ya juu. Mfumo huu wa soko ndio unatumika Uganda. Hivyo, natoa wito kwa wakulima wa kahawa Tanzania wakiwemo wakulima wa Karagwe kutumia fursa hii kujipatia bei nzuri kupitia ushirika na vikundi vya wakulima.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, asante kwa kuwa Mheshimiwa ameonyesha mikakati ambayo Serikali inajivekea ili ifike mahali wakulima wakahawa wa huko Karagwe waweze kuza kahawa kwa bei ya juu, na kwa kuwa utekelezaji huu hautaanza mara moja lazima utaenda na utaratibu maalum. Je, kwa kipindi hiki Serikali itakuwa tayari kutoa asilimia fulani ya nyongeza ili wakulima hao waweze kupata bei yenye tija ili wasikate tama katika kulima zao la kahawa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba kuanzia mwaka ujao msimu ujao wa mauzo kwa hiyo Mheshimiwa Chilolo akubaliane na mimi kwamba hatuhitaji kufanya utaratibu mwingine wa kuwalipa asilimia yoyote ya fedha kwa ajili ya kuongezea fedha ambazo anazipata wakati huu kwa msimu unapoanza tu mwaka huu unaokuja moja kwa moja hizi hatua ambazo nimezisema hapa zitaanza kufanya kazi na wakulima waatanza kupata manufaa.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza kwa kuwa katika nchi yetu katika maeneo ya vijiji vya Kalinzi Kigoma Kaskazini imeonekana wanalima kahawa vizuri na ni ya kwanza katika Afrika Mashariki na Kati na bei yake imefika shilingi 4500 kwa kilo na wana *export* kwa bei hiyo, inaonekana Serikali imewatekeleza, je Serikali inaweza ikafuatilia na hatimaye ikafanya utaratibu wakulima wote wa kahawa wakaona ni utaratibu gani wafanye ili wapate kahawa safi na bora?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Spika, siamini kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza ikawatekeleza wakulima wa zao la kahawa au wa zao lingine lolote. Kama wakulima hao wanazalisha na wanaiza mpaka wanapata 4000 kwa kilo hii ni dhahiri kabisa kwamba kuna mifumo ya Serikali

ambayo ipo imewekwa mahali ya kuwafanya wao waweze kuuza waweze kupata fedha hizo walizosema.

Lakini kama Mheshimiwa Mbunge anaushahidi kamili kwamba labda kuna wakulima wa kipindi fulani ambacho kinahitaji kusaidiwa Mheshimiwa Mbunge anawenza akanipa taarifa hizo na nitafikishia Mheshimiwa Waziri kwa utekelezaji. (*Makofi*)

Na. 125

Kilimo cha Tumbaku ya Kukausha Tabora

MHE. TATU M. NTIMIZI aliuliza:-

Mkoa wa Tabora ni moja ya Mikoa inayolima Tumbaku ya kukausha kwa wingi na ndio zao la kiuchumi kwa wananchi wa Tabora:-

(a)Je, Serikali itawasaidia vipi wakulima wa zao hilo ikiwa wao hutumia kuni kukaushia tumbaku na Serikali hukataza ukataji wa miti ovyo?

(b)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wakulima hao makaa ya mawe kama njia mbadala ya kukaushia tumaku yao ili kuzuia ukataji ovyo na hivyo kuepusha Tabora kuwa jangwa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BISHARA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA USHIRIKA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Masoko, napenda kujibu swalii la Mhesimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Duniani, vyanzo vyta nishati kwa ajili ya kupata joto la kukaushia tumbaku ni pamoja na mafuta, umeme mkaa ya mawe na kuni ambazo ndio chanzo pekee cha nishati ya kukaushia tumbaku hapa kwetu.

Katika kuhakikisha kuwa tunatunza mazingira na ili kujenga uendelevu wa kilimo cha zao la tumbaku, Serikali kwa kutumia sheria ya Tumbaku Na. 24 ya mwaka 2001 inamtaka kila mkulima kuonesha eneo alilopanda na analotarajia kupanda miti kwa madhumuni ya utunzaji mazingira kabla ya kupatiwa usajili wa kulima tumbaku na bodi ya Tumbaku Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza sheria hiyo, Wadau wa Sekta ya tumbaku husussan vyama vyta Msingi, Makampuni yanayokununua tumbaku na Halmashauri za

Wilaya, huotesha miche ya miti, na kuigawa kwa wakulima kwa ajili kupanda kila msimu.

Aidha, kampuni ya Philip Morris kwa ushirikiano na Japan Tabacco *International* (*JTI*) kupitia kampuni ya *Total Land Care*, wanashiriki katika miradi ya upandaji miti, na hifadhi ya miti ya asili, katika wilaya za Sikonge, Uyui, Tabora, Nzega na Urambo mkoani Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, juhudhi nyingine zinazoteklezwa ni pamoja na kuhamasisha ujenzi wa mabani bora ya kisasa yenye majiko sanifu kwa lengo la kupungza matumizi ya kuni kwa zaidi ya asilimia arobaini (40%).

(b) Mheshimiwa Spika, matumizi ya makaa yam awe yangesaidia kupunguza matumizi ya kuni kama nishati kwa wakulima na tumbaku. Ugumu wa matumizi ya makaa yam awe kwa wakulima wa tumbaku ni kutokana na nishati hiyo kutoendelezwa vya kutosha kuwezesha matumizi yake kwa sekta mbalimbali ambazo zinahitaji makaa hayo na kutokuwepo kwa miundombinu madhubuti ya kufanikisha matumizi hayo. (*Makofii*)

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini Wizara hii imefanya utafiti kuona kwamba haya aliyoeleza kuna upandaji wa miti ya asili na miti mingine katika jimbo langu la Igalula linafanyika kwa sababu sijaona wataalam wowote wale kupita na kueleza hayo ambayo ametoa jibu.

Lakini la pili, kwamba katika utafiti wa makaa ya mawe kama kuna ugumu huo. Je Tabora itaacha kuwa janga kwa sababu zao hili mkoa mzima unatumia kuni na sasa hivi mapori yameanza kuisha sio jimbo la Igalula tu karibu mkoa mzima. Je, hamuoni kama kuna hatari hii kama hatukuharakisha mbadala wa kuni katika mkoa wetu wa Tabora?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Spika, ameuliza kama utafiti umefanyika jimboni kwake napenda tu kumhakikishia tu kwamba utafiti umefanya kitu ambacho cha kufanya kazi kikubwa ni utekelezaji wa hayo ambayo nimeyasema.

Kama tumesema kwamba mbinu hizi zinazofanyika zifanyike, kama kuna mtu labda hajafanya vizuri Wizara pamoja na Serikali yako kwa ujumla itafanya jitihada tu kuhakikisha kwamba utekelezaji unafanyika kwa wakati.

Swali la pili la utafiti wa makaa yam awe kuchelewa nakubaliana naye kwamba tungekuwa tumemaliza utafiti wananchi wengi ambaa wanatumia nishati kuni wangeweza kutumia makaa ya mawe.

Lakini nimtie tu matumaini kwamba mchakato wa Mchuchuma utakapokamilika nafikiri wananchi wa eneo hilo na maeneo mengine ambayo wanahitaji nishati hiyo watapa. Kwa hiyo, ni suala tu la kuwa na subira lakini jitihada ambazo tumezisema hapa kama majiko ya kisasa ambayo yanatumia kuni kidogo nayo ni hatua ambayo itasaidia katika kupunguza matumizi ya kuni na kupunguza hiyo kasi ya mkoa wa Tabora kugeuka kuwa janga.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema nishati zinazoweza kutumika ni makaa ya mawe, kuni na umeme lakini hakuelezea ni namna gani Serikali imejipanga kuwapatia wananchi wa mkoa wa Tabora umeme ambao asilimia 75 ya tumbaku yote nchini inatoka mkoa wa Tabora na hasa Urambo, je, kuna mkakati wowote wa kuhakikisha inatumia nishati ya umeme badala ya kuni na makaa ya mawe ambayo bado?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba umeme ni nishati muhimu sana ambayo ingesaidia kama makaa ya mawe vilevile yangesaidia katika kupunguza matumizi ya kuni na kwa kweli umeme ni rahisi kutumia kuliko kuni adha ya kupata kuni ni kubwa.

Lakini tumesikia katika Bunge hili sio la moja mikakati ambayo Serikali inafanya kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali ya Tanzania nimhakikishie tu Mheshimiwa Selelii kwamba nitachukua ili maoni yake haya aliyoyatoa na kuongezea juu ya yale maoni mengi ambayo yametolewa kuhusu umuhimu wa kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali na tuone kwamba kilimo cha tumbaku ni sababu nyingine muhimu ya Wizara yetu ya Nishati na Madini kuhakikisha kwamba mkoa wa Tabora unapewa kipaumbele katika mkakati ujao wa kupatiwa umeme.

Na. 126

Kutelekezwa Kiwanda cha Ngozi cha Ilemela

MHE. MARIA I. HEWA aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa mkutano wa Bajeti mwaka 2008/2009 kulitolewa hoja kuhusu kutekelezwa kwa kiwanda cha ngozi cha Ilemela na Waziri Mhusika aliombwa kutembelea kiwanda hicho.

Je, Waziri alitimiza ombi hilo na anasema nini kuhusu kukifufua kiwanda hicho?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo, Mheshimiwa ni kwamba wakati wa mkutano wa Bajeti ya mwaka

2008/2009 ilitolewa hoja kuhusu kutelekezwa kwa kiwanda cha ngozi cha Ilemela na kwamba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Msoko aliomba kutembelea kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Masoko anakifahamu vyema kiwanda na kiwanda hiki kilitembelewa na watendaji na maafisa wa Wizara yangu wakati wa kufanya uperembaji wa viwanda vyote vilivyobinafsishwa nchini. (*Makofi*)

Kiwanda cha Ilemela, ni mojawapo ya viwanda vilivyobinafsishwa na kilibinafsishwa mwezi Mei, mwaka 1993 kwa kampuni ya Afrika *Trading Development Limited* ukarabati mdogo ulifanyika na kiwanda kikaanza uzalishaji.

Hata hivyo uzalishaji huo haukudumu kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa malighafi na uchafuzi wa mazingira uliosababishwa na uwekezaji usiolizisha katika mfumo wa maji taka kufikia mwaka 1998 uzalishaji ulisimama tangu wakati huo kiwanda hicho hakijafufuliwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katikam mukutano wa bajeti wa mwaka 2008/2009 uperembaji wa makampuni na viwanda vilivyobinafsishwa chini ya sekta ya viwanda, biashara na masoko ulikuwa umekamilika kwa kanda ya mashariki inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, zoezi hilo lilikuwa liendelezwe katika kanda zilizobakia za Kaskazini yaani mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, nyanda za kati na juu Kusini yaani mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya, na Kaskazini Magharibi yaani mikoa ya Tabora, Mwanza na Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuliharifu Bunge lako Tukufu kuwa zoezi la uperembaji limekamilika na tayari tumeandaa waraka wa Baraza la Mawaziri ya kuwasilisha mapendekezo ya hatua za kuchukua kulingana na mambo yaliyobainishwa.

Taarifa kamili ya hatua za kuchukua dhidi ya wale ambao hawajatekeleza mikataba ya mauzo na hasa wale ambao hawajafufua viwanda na mashirika walionunua itawasilishwa katika Bunge hili mara mapendekezo husika yatakaporidhiwa na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi maamuzi yatakapotolewa na Baraza la Mawaziri na kuwasilishwa katika Bunge hili. (*Makofi*)

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli kupongeza Wizara hii kwa utekelezaji wa ombi langu kwamba Waziri alipaswa aende atembelee pale na ninaamini nadhani amekiona kiwanda hicho kilivyo kizuri na kila kitu safi.

Katika hali halisi ya kiwanda chenyewe na kwamba jibu linasema suala zima wameandaa waraka wa kupeleka kwenye Baraza la Mawaziri, labda niseme niliweke swalii hili katika ombi niombe sasa Wizara ifanye haraka kuweza kutupatia majibu ndani

ya Bunge hili kuhusu uperembaji huu na kwamba viwanda hivi kwa kweli vinatakiwa kufufuliwa na hasa hasa kiwanda hiki cha ngozi kilichopo Mwanza kwa manufaa ya ajira za watoto wetu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Biashara na Masoko kupokea pongozi zake kwa Wizara kutembelea kiwanda hiki kama tulivyofanya kwa viwanda vingine na napenda kumhakikishia kwamba Wizara yetu itaendelea kusikiliza maoni na maombi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake ambalo ni sawa na ombi kwamba tufanye haraka nataka nimhakikishie tu kwamba kwa upande wa Wizara tumemaliza na tunangojea maelekezo ya kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri na nimhakikishie tu kwamba, pale ambapo nafasi itapatikana ya kupeleka baraza la Mawaziri tutafanya hivyo mara moja na vilevile baada ya baraza la Mawaziri tutafanya mara moja kuleta hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufahamu nini kimeamuliwa kuhusu viwanda hivyo. (*Makofi*)

Na. 127

**Serikali Kujenga Mahakama na Kupeleka Mahakimu
Wilaya ya Longido**

MHE. WILSON M. MASILINGI (K.n.y. MICHAEL L. LAIZER) aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Longido haina Hakimu wa Wilaya, jambo linalowafanya wananchi wake kufuata huduma za kimahakama kwenye Mahakama ya Wilaya ya Monduli umbali wa zaidi ya kilomita 160:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya?

(b) Je, Serikali ipo tayari kumleta Hakimu wa Wilaya ili kupunguza usumbufu wa kwenda Mahakama ya Monduli?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI aliibui:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kipindi hiki Serikali imeamua kumaliza kwanza miradi ya ujenzi wa Mahakama za Wilaya

inazojenga sasa, na baadaye ndio ianze ujenzi mpya wa Mahakama nyingine. Hii inatokana na Bajeti finyu inayotengwa kwa dhumihi hilo. Kwa mantiki hii ujenzi wa Mahakama ya Longido utapangwa katika awamu zijazo. Aidha, wazo la kumpeleka Hakimu wa Wilaya huko Longido, sasa linafanyiwa kazi na Mahakama itatoa uamuzi chanya katika suala hili, na kwa vile hii ni Serikali sikivi ninaamini Mahakama itatoa uamuzi chanya katika suala hili.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza baada ya jibu fupi la Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Swali la kwanza, kwa kuwa, muuliza Swali Mheshimiwa Michael L. Laizer, ameeleza mazingira maalamu ya Wilaya yake ya Longido kwamba, wananchi inabidi watembee zaidi ya kilomita 160 kwenda kupata haki na ninaamini Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakubaliana na mimi kuwa, huu ni umbali mrefu.

Je, Serikali haiwezi kuwapa kipaumbele wananchi wa Longido ili katika hizi awamu zinazokuja na ninaamini ni mwaka huu wa fedha, na wenyewe wafikiriwe kwa kupewa kipaumbele ili kupunguza adha wanayoipata?

Swali la pili, kwa kuwa nakubaliana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba, Serikali hii ni sikivu na mimi nina imani na Mahakama kama Serikali ilivyo na imani na Mahakama yetu, na kwa kuwa Hakimu wa Wilaya anaweza akaendesha kesi mahala popote ili mradi umuandalie chumba na yule Karani wake na huduma zingine zozote ambazo Mahakimu wenyewe wanajua.

Je, Serikali haiwezi ikachukua hatua madhubuti ikizingatia hali ilivyo ngumu, si Longido tu, bali ni karibu nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Muleba, watu wanasafigi umbali mrefu, nauli, wengine wanashindwa kupeleka mashahidi, ili Mahakimu wa Wilaya wapewe magari na waweze kusafiri na kuongoza Mahakama za Wilaya kwenye Kata, ikishindikana huko basi kwenye Tarafa ili kupunguza adha ya wananchi wetu katika kutafuta haki ambayo inapelekea watu wengi kupata hasara kesi zinapoahirishwa? (*Makof*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli kwamba Longido ina mazingira yake maalum, lakini si Longido tu bali sehemu nyingi za Tanzania zina mazingira hayohayo. Suluhisho la ujenzi wa Mahakama hizi, kwa maoni yangu kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ni kuziomba Halmashauri za Miji na Wilaya zihamasishenye wananchi kujenga Mahakama kama wanavyofanya katika shughuli za kujitolea na kila inapowezekana Mahakama itatoa mabati kutegemeana na Bajeti ambayo

inatolewa. Wazo lake la kwanza, nitalifikisha kwa Mheshimiwa Waziri tuone namna ya kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu Mahakama kutembelea Kata, Tarafa na Vijiji ni, wazo zuri sana, nilitembelea nchi ya Malaysia na nikaona kwamba, kule wana utaratibu wa justice on the wheels, kwamba Majaji, Mahakimu wanatoka ofisini wanakwenda kwenye maeneo maalum ambako wanasikiliza kesi. Hilo linawezekana lakini katika kufanya hivyo pia, ni muhimu kuangalia usalama wa Mahakimu na Majaji katika maeneo mengine kama kule Muleba, lakini niseme tu kwamba hilo pia litawezekana. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Nilidhani ungesema Tarime, lakini Muleba! (*Kicheko*)

MHE. JOHN S. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua juzi juzi ya kuongeza Majaji wa Mahakama Kuu, tunaipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kuuliza swali la nyongeza. Tunaomba kwamba tuwaombe wananchi wajenge Mahakama ambayo wanaweza kujenga, lakini ziko Mahakama sasa hivi ambazo hazina Mahakimu, na ndiyo sababu tunafikia hatua ya kusema Hakimu *on the wheel*. Kwa kuwa tunao watu ambao wamemaliza masomo ya Sheria. Je, hawa hawawezi wakachukuliwa kwa dharura wakafundishwa halafu wakapelekwa vijijini kama Mahakimu? (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali ya Mzee wangu, Babu yetu, Mheshimiwa John S. Malecela kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninafarijika sana kuulizwa swali na Mheshimiwa Malecela, kwa sababu mimi nilipoanza darasa la kwanza bado nilikuwa namsikia yuko katika mambo ya siasa, na leo niko hapa na nimefurahi sana kuulizwa swali na huyu Mzee. (*Makofi/Kicheko*)

Pili, kwa niaba ya Serikali ninapokea pongeza za Mheshimiwa Malecela na ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais atashauriwa kuteua Majaji kila itakapoonekana inafaa kufanya hivyo. Nakushukuru sana Mheshimiwa Malecela kwa kufanya hivyo, lakini nitumie nafasi hii kukupongeza kwamba, katika hao Majaji walioteuliwa mmoja ni Judith Malecela, ambaye pia nimefanya naye kazi na ninajua umahiri wake katika kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazo la *ku-train* Wanasheria kwa dharura kwa ajili ya kuendesha hizo mahakama ni wazo zuri, lakini ni vizuri kuchukua tahadhari kwamba, siyo kila mtu anaweza kufanyakazi ya uhakimu kwa sababu ni kazi inayohitaji maadili mema.

Lakini tunavyofahamu hivi sasa ni kwamba, tunataka kuondoa Mahakimu ambao hawana *degree* ya Sheria katika Mahakama zetu za Mwanzo ili kusudi waingie wale

ambao ni *graduates*. Hilo nalo ni lazima tulifanye kwa tahadhari kubwa sana, kwa sababu katika maeneo mengine Mahakimu wa Mwanzo wana uelewa mpana sana wa Sheria za Asili kuliko wengine ambao tunamaliza *University*.

Kwa hiyo, wazo lako Mheshimiwa Malecela nitalichukua na kama ulivyosikia Mheshimiwa Waziri alivyosema, hayo yote tutayaafanya. Lakini, ni kweli kwamba suala la kuwaomba wananchi wachangie kujenga Mahakama tunalifanya kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti mwaka hadi mwaka. Lakini hali itakapokuwa nzuri Mahakama zetu tungependza ziwe nzuri na zinazokidhi kwa kila hali.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kirua kwenye jimbo la Vunjo, Mahakama ya Mwanzo ilikarabatiwa vizuri sana na Waziri alifika eneo hilo na kuifungua. Wakati huo aliahidi kwamba, atapeleka Hakimu kwenye Mahakama hiyo, takribani mwaka mmoja sasa Hakimu hajafika.

Je, tuelewe kwamba Waziri alidanganya wananchi wangu wa Vunjo au ana mpango gani?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali ya Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hawezi kudanganya na tatizo ni hilohilo la uhaba wa Mahakimu hao. Lakini Mheshimiwa Waziri popote pale ulipo huko Nachingwea kama unanisikia ulichukulie suala hili la Vunjo kama ni la kipaumbele. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kimaro nakuhakikishia kwamba, nitamfikishia Mheshimiwa Waziri ombi lako. (*Makofi*)

SPIKA: Huyu Mheshimiwa amelitumia Bunge kutuma salamu kwa Waziri. (*Kicheko*)

Na. 128

Matengenezo ya Barabara ya Sumbugu – Mbarika

MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. JACOB D. SHIBILITI) aliuliza:

Kwa kuwa, *TANROADS* imekuwa ikifanya matengenezo mazuri barabara ya Misasi-Kasololo – Sumbugu – Mbarika, lakini bado kuna maeneo ya Manawa, Ginnery na sehemu za Sumbugu hadi Mbarika.

Je, Serikali inasemaje juu ya kufanya matengenezo hayo kwa mwaka huu?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Misasi – Kasololo –Sumbugu – Mbarika ni barabara ya Wilaya ambayo kiutaratibu inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia Bajeti inayopitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Hata hivyo, Wizara yangu imekuwa ikiihudumia barabara hiyo kupitia Mfuko wa Maendeleo (*Consolidated Funds*) ambapo kwa mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya shilingi milioni 70 zilitumika kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe.

Jumla ya kilomita sita (6) ziliwekwa changarawe maeneo ya kutoka Nduha hadi Kasololo kwa kutumia fedha hizo. Wizara yangu kwa kushirikiana ba TAMISEMI itaendelea kuitengea fedha kadri Bajeti itakavyoruhusu ili kuendelea kufanya matengenezo sehemu zilizobakia za *Manawa Ginnery*, Sumbugu na Mbarika.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hiyo ni ya Halmashauri ya Misungwi na ni kweli TAMISEMI na Serikali kuu wamekuwa wakiifanya matengenezo. Kwa kuwa barabara hiyo ina kilomita 89.5 na kwa kuwa, kila mwaka wanatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kilomita sita (6).

Je, ni lini maeneo sumbufo kama yale ya *Manawa Ginnery* na Sumbuku yatafikiwa ili barabara ile ikarabatiwe kwa uhakika kwa kiwango cha changarawe?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swal la msingi ya kwamba Wizara yangu pamoja na TAMISEMI itaendelea kuitengea fedha barabara hii kadri itakavyokuwa inaruhusu, napenda tu kuahidi tu kwamba tutaendelea na utaratibu huu na kwa sababu Wizara yetu inawasilisha makadirio kesho naomba basi Mheshimiwa Mbunge asubiri. Lakini kwa kudokeza tu ni kwamba, barabara hiyo mwaka huu imetengewa fedha tena kwa ajili ya kuendelea kuifanya matengenezo.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la barabara ya Misungwi ni sawasawa na tatizo la barabara ya Uhuru. Barabara hii tunaipigia makelele na sasa ni mwezi mzima sasa ubovu wa barabara hii unaonekana kwenye magazeti, na umuhimu wa barabara hii kila mtu anaufahamu.

Mheshimiwa Spika, juzi Serikali imesema kutengeneza barabara kilomita moja inafika takribani shilingi bilioni 1. Barabara hizi za mjini hazihitaji shilingi bilioni 1, *ku-re surface* barabara gharama yake iko chini sana.

Je, Serikali sasa baada ya ushauri huu wataichukulia maanani barabara hii ya kihistoria?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Zungu kwa kuifuatilia sana barabara hii ya Uhuru ambayo ni ya kihistoria na sisi tunakiri kabisa kwamba, haya anayoyaeleza yanastahili yatiliwe maanani.

Sasa niseme tu kama nilivyokuwa nimesema awali kwamba, tunawasilisha Bajeti yetu kesho lakini huu ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge, wa kuangalia gharama zenye unafuu kidogo ili kuweza kuifanyia ukarabati barabara hii ili iweze kulingana na hadhi tutauzingatia.

Na. 129

Leseni za Maeneo ya Utafutaji Madini

MHE. HERBERT J. MTANGI aliuliza:-

Maeneo yanayotolewa leseni za utafutaji wa madini ni makubwa kiasi cha kuingia hata ndani ya maeneo ya wananchi, ndani ya vijiji vilivyopimwa na mashamba yenye Hati.

Je, kwanini taarifa za utoaji wa leseni za utafutaji wa madini kwenye maeneo ya kijiji kilichoandikishwa zisiwekwe bayana kwa kijiji kinachohusika?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mbunge wa Muheza, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini Namba 123 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2006, leseni za utafutaji Madini ni za aina mbili ambazo ni leseni ya utafutaji wa awali wa Madini yaani *Prosperity License with Reconnaissance period (PLR)* na leseni inayoruhusu utafutaji wa kina wa Madini yaani *Prospecting License*

(PL). Leseni ya utafutaji wa awali wa Madini inaweza kutolewa kwenye eneo lisilozidi kilomita za mraba 5,000 wakati ile inayoruhusu utafutaji wa kina wa Madini huweza kutolewa kwenye eneo lisilozidi kilomita za mraba 200. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria Mpya ya Madini iliyopitishwa na Bunge hili katika kikao cha Bunge kilichopita leseni ya utafutaji Madini wa awali (PLR) imefutwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo hutolewa leseni za utafutaji Madini hujumuisha vijiji na mashamba yanayomilikiwa na wananchi ama Taasisi mbali mbali. Hata hivyo, utoaji wa leseni za utafutaji Madini katika maeneo yenye vijiji ama mashamba yanayomilikiwa kisheria haumwondolei mmiliki wa ardhi haki ya kumiliki ardhi hiyo. Vilevile leseni hizo hazizui shughuli zingine za kijamii kama vile kilimo kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini Na. 123 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2006, kinamtaka mwenye leseni ya utafutaji au ushimbaji Madini kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa mmiliki wa ardhi ambayo anakusudia kufanya utafutaji ama uchimbaji Madini ndani ya leseni aliyopewa.

Kwa maana hiyo, mwenye leseni ya utafutaji ama uchimbaji Madini atakuwa amevunja Sheria ya Madini iwapo ataingia katika maeneo aliyopewa leseni bila kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwenye vijiji husika ama mmiliki ye yote wa ardhi ambayo itahusika katika mipango ya utafutaji ama uchimbaji Madini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa utoaji wa leseni za utafutaji Madini, hauna athari yoyote katika umiliki wa vijiji na mashamba yanayomilikiwa kisheria. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa, wamiliki wa leseni za utafutaji Madini katika maeneo mbalimbali nchini wanazingatia ipasavyo Kifungu Na. 95 cha Sheria ya Madini kilichotajwa hapo juu kwa kujitambulisha kwenye vijiji ambavyo leseni hizo zimetolewa kabla ya kuanza shughuli zao za utafutaji Madini.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara hii kwa kuitisha hii Sheria mpya ya Madini. Lakini, hata hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza wapo wawekezaji ambao *coordinates* za Madini zinaonesha kwamba, wamepewa maeneo na leseni zaidi ya hizo kilomita za mraba 200. Kama hivyo ndivyo na inawezekana maeneo hayo yametolewa kwa kuzingatia Sheria ya zamani.

Je, kuna utaratibu gani wa kuyarekebisha maeneo hayo ili yawe na uwiano na Sheria mpya?

(b) Mheshimiwa Spika, bado wapo wawekezaji wengi amba wana leseni za uchimbaji wa madini. Lakini hata mara moja hawajawahi kukutana na vijiji licha ya kwamba sheria inawataka wafanye hivyo kwa kifungu Namba 95.

Je, Wizara ina utaratibu gani sasa wa kutoa elimu ili kwanza wana vijiji wenyewe waelewe sheria inavyosema na majukumu ambayo wawekezaji wanapaswa kufanya kwa vijiji hivyo?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tutaongeza dakika chache kwa sababu mwanzoni tulikuwa na Hati kadhaa za kuwasilisha mezani ambazo zimechukua muda wa maswali na majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niabaya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, labda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo la utoaji wa leseni kwa muda mrefu limekuwa linatutatiza.

Kadri siku zinavyozidi kwenda tumejaribu kuboresha utoaji wa leseni na hasa kwa kutumia vyombo vya kisasa kule Wizarani tunaita *Mining Cadastral* ambazo sasa hizi *Computers* zinakuwa zinamiliki takwimu na kadhalika ili zile leseni zenyewe ziwe zinakuwa. Sasa si jambo la kusubiri mtu akuandikie kwa mkono ujue kwamba leseni yako imekwisha au leseni hii imeingia kwenye leseni nyingine. Kwa hiyo, hayo yote yanafanywa kwa ajili ya kuboresha utoaji wa leseni.

Lakini hata tulipoingia kwenye sheria mpya tulisema hizi sheria za aina nyingine ambazo kwa sasa hivi ziko leseni ya *prospecting license, retention license, partial mining license, mining license, primary mining license, processing and refining license* hayo yote yanatolewa kwa ajili ya kuboresha ile hali ya utoaji leseni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria mpya imezingatia hayo na sasa sisi wajibu wetu Wizarani ni kuhakikisha kwamba usimamizi wa sheria mpya unaondoa kero katika usimamizi wa utoaji wa leseni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kifungu Namba 95 ni kweli mimi mwenyewe nimekwenda kwenye maeneo mbalimbali na nimelikuta lakini sheria iko pale pale, kwamba ukienda una leseni yako wewe unakusudia kufanya uchimbaji au *prospecting* au uchorongaji wa namna yoyote ile bado unatakiwa ukifika pale ujisalimishe kwenye ofisi ya kijiji na useme kwamba *coordinates* zangu ni moja, mbili, tatu. Wao watakuambia kwamba hili linaingia kwenye eneo la Mheshimiwa Mwera. Sasa kama linaingia kwenye eneo la Mheshimiwa Mwera wewe inabidi uende ukazungumze naye ili mpate uwiano wa *mining rights vis a vis surface rights* ili shughuli za kilimo na shughuli zingine ziweze

kuendelea. Wakati huo huo uchimbaji uweze nao kuendelea. Wasipofanya hivyo wanavunja sheria. Ilikuwepo kwenye sheria iliyopita na sasa tumeisisitiza tena na ninaomba niseme tu kwamba katika hili tutaendelea kulifanyia kazi sana kwa sababu ni kero kwa wananchi ambao wanaathirika na watu wanaotoka Mjini kuja kuwafanyia fujo katika maeneo yao.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ilitusaidia watu wa Lushoto kupambanua maeneo ambayo yana madini na kwamba kuna madini ya aina 16 lakini haikuonyesha yako katika sehemu gani. Katika hifadhi za misitu au vyanzo vya maji na kwamba ramani imerudishwa Mkoani ili sasa waainishe ni maeneo gani ambayo hayatakiwi kuchimba. Je, itakuwa tayari lini hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hii kazi ya uchoraji wa ramani imefanywa kwa hatua ya awali. Tumejaribu kuifanya kwa nchi nzima na inasimamiwa na ndugu zetu wa *GST* wakala wa geolojia wa Tanzania chini ya kazi nzuri sana inayofanywa na Profesa Mruma na kusema kweli *GST* yenyewe iko hapo nyuma karibu na Bunge hata tukitoka hapa tunafika ndani ya dakika tano. Sasa naomba nimwombe Mzee Shellukindo kwamba kwa sababu sijajua hatua ya utekelezaji wa kutambua yale maeneo maalum ya Wilaya ya Lushoto ambayo yana madini haya yako wapi na haya yako wapi, ninaomba tuungane baadaye twende *GST* ili tukapate maelezo ya kazi hii na kama haijakamilika itakamilika lini.

Lakini pia pana kazi ya ziada zaidi ambayo inahusu watalaam kwenda pale kwa macho *physically* kubaini kwa ramani. Kwa hiyo na hilo nalo nitawasisitiza ili tupate sura nzuri zaidi ya vyanzo vya madini pale na namna vinavyoingiliana na kazi zingine na vitu vingine pale ndani ya ardhi ya Lushoto.

Na. 130

Wilaya ya Nanyumbu kupatiwa Umeme

MHE. DUSTAN D. MKAPA aliuliza:-

Umeme wa gesi wa *Mnazi Bay* Mkoani Mtwara sasa umeishafika Masasi:-

(a) Je, ni lini umeme huo utafika Wilayani Nanyumbu?

(b) Je, kuna mipango mingine mbadala ya kuipatia umeme Wilaya ya Nanyumbu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2010 kampuni ya Umoja *Light* ya *Artumas* ilifikisha umeme unaotokana na gesi asili ya *Mnazi Bay* katika mji wa Masasi. Kampuni ya *Umoja Light* inaendelea na ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mtwara, Tandahimba hadi Masasi na kuwezesha umeme kupatikana Newala, Masasi na Nachingwea na unategemewa kukamilika mwaka huu wa fedha 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato wa awali wa kupeleka umeme Wilaya ya Nanyumbu umekamilika. Tathmini imebaini kuwa gharama za kupeleka umeme wa 33 kV umbali wa kilomita 54 toka Masasi na kusambazwa Mangaka pale Makao Makuu ya Wilaya ni takribani shilingi bilioni 2.1 Serikali inakusudia kufikisha umeme katika Wilaya ya Nanyumbu ndani ya kipindi cha mwaka 2010/2011.

Kama ilivyo katika Wilaya zingine za Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Nanyumbu nayo itapata umeme unaozalishwa kutokana na gesi asili ya *Mnazi Bay*. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, mpango mbadala uliopo ni kuipatia Wilaya ya Nanyumbu umeme unaozalishwa kwa kutumia mitambo ya dizeli, ingawa kwa sasa kipaumbele ni kufikisha umeme unaotokana na gesi asili ya *Mnazi Bay* kama nilivyotoa kwenye maelezo yangu ya awali. (*Makofi*)

MHE. DUSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kubwa sana kwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanatia moyo. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

- (a) Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi afike yeye mwenyewe Mangaka Wilaya Nanyumbu ili maneno haya mazuri na maelezo haya mazuri ayatoe yeye mwenyewe kwa wananchi wa Nanyumbu? (*Makofi*)
- (b) Kwa kuwa umeme huu utatoka Masasi kwenda Nanyumbu. Je, vijiji ambavyo umeme huu utapita kama Namatumbusi, Mikangaula, Nangaramo, Nang'omba watasambaziwa umeme huu ili wananchi hawa nao waweze kufaidi matunda ya umeme? (*Makofi*)

SPIKA: Ikiwa umepata majina hayo sijui.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hili la kupeleka umeme kutoka Masasi kwenda Mangaka kama nilivyosema pana kilomita 54 pale na hivi vijiji kama Mikangaula, Nangaramo, Nang'omba na vile vingine bahati nzuri ninavifahamu ninaamini kwamba ule utaratibu wa kawaida ambao tunafanya nyanya za kV 33 za *high tension* zinapopita juu tutafanya maamuzi ya kushusha waya chini na kujenga *transformer* na *sub-station* itazingatiwa kwa sababu kuna tathimini inayotakiwa kufanywa, wingi wa watu, mahitaji na kadhalika. Naamini mimi vijiji vile navifahamu

naamini kwamba vinastahili kupata umeme njia hiyo itakapokwenda Mangaka. Kwa hiyo, naomba aniridhie kwamba niwasilishe katika maombi nitakayowasilisha *TANESCO* kwa niaba yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hili lingine la kufika Mangaka ili nikatoe maelezo mimi mwenyewe naomba niseme tu ye ye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, amekuwa analifuatilia hili na kama wananchi wa Mangaka wanataka wasikie basi ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia kwa karibu sana ili mradi huu kufika Masasi ufile mpaka Mangaka. Lakini naomba nimwambie kwamba kwa sababu itakuwa kama nakwenda nyumbani basi naridhia kwamba mwaliko huu wa kwamba twende wote tukatoe maelezo Mangaka muda ukipatikana tutafanya hivyo. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Naomba Waheshimiwa Wabunge, mtambue kurejea kwa mwenzetu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ambaye ametoka kwenye msiba mzito sana baada ya kufiwa na mume wake. Itapendeza kama ilivyo kawaida yetu mwenzetu akiwa amefiwa na amerejea basi mnakwenda kumfariji nyumbani.

Najua wengi mlituma salaam za rambirambi lakini kwa kuwa, amerejea basi wale wanaopata nafasi ni vizuri kuendelea kumfariji kwa sababu msiba kama huo ni mzito sana wa kupotelewa na mwenzi wake.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia kwamba bado umri si mkubwa sana sasa kuanza kuitwa mjane mapema hivi. Lakini tunamwombea Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Mumewe Leonard mahali pema peponi, na ye ye mwenyewe apate faraja ya Mungu ambayo ndiyo pekee njia ya kuweza kutuliza pigo hilo. Ahsante sana. (*Makofî*)

Matangazo tunaanza na wageni. Tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, kama ifuatavyo:-

Nadhani hawa watakuwa pale *Speaker's Galley*, kwanza ni Ndugu Blandina Nyoni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamiui, karibu sana. Halafu wafuatao ni maafisa waandamizi Dr. Deo Mtasiwa, Mganga Mkuu wa Serikali, Ndugu Danford Makala, Kamishna wa Ustawi wa Jamii - yule pale karibu sana. Ndugu Domick Hazen, Mwakilishi wa Benki ya Dunia - yule kule *please welcome*. Sijui kama anajua Kiswahili, lakini karibu *means welcome*.

Ndugu Christopher Armstrong, mwakilishi wa Balozi wa Canada hapa nchini, *thank you*, karibu sana. Ndugu Rosemary Slaa, Mkurugenzi wa *Programme* za *Clinton HIV Aids Initiatives*. Dr. Ellen Senkoro Mkurugenzi Mtendaji wa Benjamin Mkapa

Foundation yule pale karibu sana Doctor. Ndugu Rufaro Chatora - Mwakilishi wa Shirika la Afya Dunia (*WHO*) nchini Tanzania, Ndugu Mary Mwanjelwa - mwakilishi wa Shirika la Kutoa Afya ya Jamii (*PSI*) Tanzania, ye ye amejitenga kidogo huku karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Dr. Godfrey Mtei, Mganga Mkoo wa Mkoa wa Dodoma - ahsante sana. Balozi Ben Moses, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri Mamlaka ya Chakula na Dawa - yule pale karibu sana Mheshimiwa Balozi. Ndugu Vicky Makani - Mjumbe wa Bodi ya Hospitali ya Muhimbili, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Balozi Eva Nzaro - Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Bohari ya Dawa - yule pale karibu sana. Profesa Samuel Masele - Mwenyekiti Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu - karibu sana Profesa, hatujakuona siku nyingi sana hapa Dodoma, karibu sana. (*Makofi*)

Wapo Wakurugenzi wanane (8) na Wakuu wa Idara wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, nawaomba wasimame tu kwa pamoja - wale pale ahsanteni sana - Karibuni sana. Tunao pia Wakurugenzi 13 nadhani ndiyo wote waliosimama kwa pamoja na kuna wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Uuguzi Mirembe, karibuni sana. (*Makofi*)

Ndugu zangu wauguzi, kazi yenu ni ya kipekee kabisa maana yake Mirembe tunasikia kuna matatizo maalum huko.

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni binafsi wa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, amba ni Mama Amina Jahazi, Mama yake Mdogo, Ndugu Neema Malambo ni mwanaye Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Farida Wandi Mdogo wake Mheshimiwa Waziri na mdogo wake mwingine anaitwa Ndugu Ali Kirumba, wale pale - Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni kutoka Mfuko wa Bima ya Afya Taifa (*National Health Insurance Fund*), yupo Ndugu Emmanuel Humba - Mkurugenzi Mkoo, Ndugu Hamisi Mdee Mkurugenzi wa Wanachama na Uendeshaji Bima ya Afya na Ndugu Athuman Rehani - Meneja Mfuko ya Afya ya Jamii Makao Makuu - karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati ni Ndugu Mbaruk Abdul Rahman Kanyama - yule pale upande huu karibu sana. Ingawa naona mwenyeji wako hayupo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Herbert Mntangi ni kutoka shule ya Msingi Ubembe Wilaya ya Muheza na hawa ni Wabunge Watoto kutoka Bunge la Shule ya Msingi.

Hawa Wabunge watoto wanaongozwa na Spika wao ambaye ni Frank Martin, mnawona Spika huyo, mambo mazuri hayo. Halafu kuna Mawaziri 5 wasimame, wale pale Waheshimiwa Mawaziri wa Shule ya Msingi, wale pale na Wabunge 7 wanaongozwa na Mwalimu Mkuu Ndugu Frank Ngwilizi. Ninyi mnapendeza sana, mnafurahisha sana. (*Makofi*)

Naomba shule nyingine za msingi katika nchi yetu ziwe na utaratibu mzuri kama huu wa Shule ya Msingi Ubembe kule Muheza hongera sana mmefanya jambo zuri. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo wawakilishi wa Shirikisho la SHIVYAWATA ambao wamekuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naona pale kuna mkalimani anafanya lugha ya alama naomba SHIVYAWATA viongozi muweze kusimama tafadhali wale wanaoweza kusimama, karibuni sana. Bunge hili liko nanyi hatua zote kabisa na tunapenda kuwahakikishia kwamba tutawasaidia kwa kila hali. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wapo wanafunzi 5 kutoka Chuo cha Biashara Tawi la Mwanza (*CBE – Mwanza*), wako wanafunzi kutoka Chuo cha St. John's - Dodoma, ambao idadi haikutajwa. Wanafunzi watano (5) kutoka Seminari Dodoma, wale wa Seminary. (*Makofi*)

Wapo wageni Ndugu Akisa Kasesela na Brown Mwangomale ambao wamekuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - wale pale, ahsante sana. Kuna Ndugu Tina Limbu kutoka Azimio Sekondari - naye amekuja kusikiliza majadiliano ya Bunge - Ahsante sana. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi zetu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba leo saa 7.00 mchana, Wajumbe wote wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama mkutane katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu mkutane leo katika Ukumbi Namba 227, Jengo la Utawala, saa 7.00 mchana.

Waheshimiwa Wabunge, ninatangaza kwamba, ratiba ya mpangilio wa jinsi Wizara zitakavyowasilisha hotuba zao imebadilishwa; kwa hiyo, mzingatie ratiba mpya ambayo tumeipanga katika Kamati ya Uongozi juzi, itakuwa imegawiwa hivi sasa.

Tulipokea ombi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, akiomba tuchangie fedha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake inayoitwa *Twiga Stars*. Taratibu zimekwishafanywa na siku yoyote wiki hii, tutakabidhi rasmi mchango wetu wa Wabunge wote kuweza kuipa moyo Timu hii ambayo bado inaendelea kuiletea heshima Taifa letu.

Kuna tangazo moja limeletwa sasa hivi; kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wa CCM saa 2.00 usiku leo mara tu Bunge litakapoahirishwa. Taarifa hii imeletwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa niaba ya Katibu wa Wabunge wote wa CCM. Kwa

hiyo, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, saa 2.00 usiku kikao Ukumbi wa Pius Msekwa. Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Ninamwomba sasa Katibu atusogezo katika shughuli inayofuata.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Unatumia kanuni ya 68 siyo?

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Ndiyo Kanuni ya 68 Mheshimiwa Spika.

Tunapoanza shughuli zetu Bungeni asubuhi tunapopata *Order Paper* wakati mwingine kunakuwa na Hati za Kuwasilisha Mezani, wakati mwingine kunakuwa hakuna Hati za Kuwasilisha Mezani. Panapokuwa na Hati za Kuwasilisha Mezani ambazo ziko kwa mujibu wa Kanuni, pamoja na maswali yenye, Hati za Kuwasilisha Mezani zinakula muda wa Maswali na hatimaye inafika mahali Maswali hayajamalizika, lakini muda umekwisha na Mheshimiwa Spika, unatumia neno la kusema kulikuwa na Hati za Kuwasilisha Mezani lakini zimekula muda tumalize Maswali yaliyobaki. Ninaamini kwamba, Hati za Kuwasilisha Mezani ziko kwenye Kanuni.

Sasa naomba mwongozo wako Spika tunalifanyeje hili ili Maswali yapate saa yake kamili na Hati za Kuwasilisha Mezani pia ziwe zinakamilika kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, ahsante sana.

SPIKA: Ninadhani liko wazi tu, hata leo nimefanya hivyo, tulitumia kiasi cha kama dakika 10 hivi kupokea Hati Zinazowasilishwa Mezani na nikaongeza muda wa dakika 10 kufidia ili tupate saa moja au dakika 60 za kuweza kujibiwa maswali. Kwa hiyo, hatuna njia nyingine kwa sababu Bunge linaanza saa 3.00, kipindi cha maswali ni 3.00 hadi saa 4.00 lakini zinapokuwepo hati basi yule anayekuwepo katika Meza hii huangalia ule muda ili uweze kufidiwa baada ya saa 4.00 na ndivyo tutaendelea hivyo mpaka ambapo tutajipangia utaratibu mwingine.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2009/10 na Malengo ya Wizara katika Bajeti ya Mwaka 2010/11. Aidha, naliomba Bunge lako

Tukufu likubali kupidisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii ya pekee, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza na kutupatia maelekezo katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Aidha, nampongeza kwa kuchukua hatua ya kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria, vifo vya wanawake wajawazito na watoto. Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari na uzinduzi wa “Zinduka, Malaria haikubaliki, tushirikiane kutokomeza Malaria”. Vilevile, tunamshukuru kwa kuweza kutuunganisha na Taasisi za Kimataifa ambazo zimetuwezesha kutumia teknolojia ya kisasa katika kuboresha huduma za tiba na kinga.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri ya Hali ya Uchumi Nchini, Mipango ya Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/11. Ninampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake inayotoa dira ya jinsi Serikali ya Awamu ya Nne itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2010/11. Ninampongeza Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), ambaye tunashirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii. Ninapenda vilevile, kuwapongeza Mawaziri wote wa Wizara zilizokwisha wasilisha bajeti zao, ambazo kwa namna moja au nyingine, zinachangia katika utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba zilizotangulia, michango yao imesaidia sana kuboresha hotuba yangu. Ninawaahidi kwamba, Wizara itazingatia ushauri wao katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuungana na Mawaziri wenzangu waliotangulia kusoma hotuba zao, kutoa masikitiko na salamu za pole kwa familia, ndugu na jamaa, kwa vifo vya Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu katika Awamu ya Kwanza na Mheshimiwa Sigifrid Selemanni Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa. Aidha, ninatoa salamu za pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu zao kutohana na mauaji katika Wilaya ya Musoma, mafuriko katika Wilaya za Bukombe, Chato, Kilosa, Kongwa na Muleba, maporomoko ya ardhi katika Wilaya ya Same na ajali za vyombo vya usafiri nchi nzima. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishukuru kwa dhati, Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge lako Tukufu, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa ushauri iliyoutoa ambao umeboresha matayarisho ya Bajeti ya Wizara ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu mawili kama ifuatavyo: Kwanza ni Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 na Majukumu kama

yalivyoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka 2009/10; na pili ni Mipango, Majukumu na Maombi ya Fedha ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara imepata mafanikio katika maeneo ya uratibu wa sera na mipango ya afya, huduma za kinga, tiba, mafunzo, ubora wa huduma za afya na viwango, uchunguzi wa kemikali na makosa ya jinai, udhibiti wa vyakula na dawa, huduma za lishe, utafiti, utawala na utumishi, udhibiti wa rasilimali, huduma za ustawi wa jamii na masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya kugatua madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa, katika mwaka 2007, Wizara ilifanya mapitio ya Sera ya Afya ya mwaka 1990, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III (2009-2015), miongozo ya uandaaji Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri na uanzishaji wa Bodi za Afya za Halmashauri na Kamati za Vituo vya kutolea huduma za afya ili kutekeleza dhana ya kugatua madaraka kwa wananchi kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Decentralization by Devolution – D by D*). Lengo la Serikali la kufikisha huduma za afya kwa Watanzania wote na hasa wale wanaoishi vijijini linatekelezwa kwa kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata na hospitali kila wilaya, kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), 2007- 2017.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto 2005-2010 na Mpango Mkakati wa kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya watoto na vile vinavyotokana na uzazi 2008-2015, ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia Namba 4 na 5. Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimeendelea kupungua kutoka 112 kati ya watoto waliozaliwa hai 1,000 mwaka 2004/05 hadi vifo 91 kati ya watoto waliozaliwa hai 1,000 mwaka 2007/08. Vifo vya watoto wachanga wenye umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 68 kati ya watoto waliozaliwa hai 1,000 mwaka 2004/05 hadi 58 kati ya watoto waliozaliwa hai 1,000 mwaka 2007/08. Aidha, kulingana na takwimu za mwaka 1999, vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka 5 vimepungua kwa asilimia 38 na vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kwa asilimia 41.

Mheshimiwa Spika, huduma za chanjo ziliendelea kupanuka kwa kuongezeka vituo vya kutolea huduma hiyo, kutoka 2,954 mwaka 2005 hadi 4,535 mwaka 2009. Chanjo zilizotolewa zinakinga watoto dhidi ya magonjwa ya kifua kikuu, polio, kifaduro, pepopunda, donda koo, homa ya ini na surua. Idadi ya watoto waliopata chanjo iliongezeka kutoka 1,249,388 mwaka 2005 hadi 1,356,421 mwaka 2009, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 8. Aidha, watoto waliopata chanjo ya Surua waliongezeka kutoka 1,267,716 hadi 1,455,100, sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilianza kutoa chanjo mpya ijlukanayo kama *Haemophilus Influenza Type B (Hib)*. Chanjo hiyo inakinga watoto wote chini ya mwaka mmoja dhidi ya kichomi na homa ya uti wa mgongo. Chanjo hiyo mpya ya *Hib* imeunganishwa na chanjo nyingine nne ambazo zilikuwa zinatolewa awali. Mchanganyiko huo wenye chanjo tano za *DPT-HB-Hib* unaitwa *pentavalent*. Chanjo

hiyo inakinga watoto dhidi ya kifaduro, pepopunda, donda koo, homa ya ini na kichomi pamoja na homa ya uti wa mgongo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania haijapata mgonjwa wa polio tangu mwaka 1996. Kati ya wagonjwa 299 waliopata ulemavu wa ghafla mwaka 2005 na 494 mwaka 2009, walichukuliwa sampuli za kinyesi na hakuna mgonjwa hata mmoja aliyepatikana na ugonjwa wa polio. Wizara iliendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria 2008 – 2013, kwa kutoa vyandarua vyenye viuutilifu kwa Hati Punguzo na dawa ya kukinga Malaria kwa akina mama wajawazito nchi nzima. Aidha, ilisambaza vyandarua 9,000,000 kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano. Vilevile, ilipuliza dawa ya ukoko yenye viuutilifu ya kuua mbu ndani ya nyumba katika Mkoa wa Kagera. Utekelezaji huo umewezesha Mkoa wa Kagera kudhibiti milipuko ya ugonjwa wa Malaria na kupunguza kiwango cha Malaria kutoka asilimia 40 hadi 10.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI ilipitishwa mwaka 2008. Aidha, Wizara iliandaa Mpango Mkakati wa Pili wa Afya na UKIMWI 2008 - 2012 pamoja na Mwongozo wa utoaji huduma muhimu za kudhibiti UKIMWI katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kupima Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Hadi Machi 2010, jumla ya watu milioni 11.3 walikuwa wamepima Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Kati ya hao, watu wapatao 648,055 wako kwenye matunzo na tiba ya UKIMWI na 335,292 wanapata dawa za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watoto 746,823 waishio katika mazingira hatarishi wametambuliwa katika Halmashauri 86 na kupatiwa huduma za msingi. Wazee 6,512 wasiojiweza wamepata huduma ya matunzo katika makazi 17 yanayoendeshwa na Wizara. Aidha, vifaa mbalimbali vya kujimudu vilitolewa kwa watu wenye ulemavu 232 na mitaji ya biashara kwa watu 173. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu 2,500, pia, ilikamilisha kutunga sheria ya watu wenye ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 244,895,993,044.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 104,831,750,600.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Kiasi cha shilingi 140,064,242,444.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 21 Juni, 2010, kiasi cha shilingi 219,112,981,968.00 kilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Mishahara, fedha hizo zilitumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilipata kibali cha ajira ya watumishi 513 wa Wizara na 6,257 kwa ajili ya Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na Wizara mbalimbali. Watumishi 472 sawa na asilimia 92, walijiriwa na Wizara. Aidha, wataalam 4,020 wa kada za afya sawa na asilimia 64 walipangwa kwenye Halmashauri, Sekretarieti za Mikoa na Wizara mbalimbali. Vilevile, watumishi 731 wa Wizara walipandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilipokea jumla ya malalamiko 66. Kati ya hayo malalamiko 29 yalihusu masuala ya Rasilimali watu na malalamiko 37 yalihusu utoaji wa huduma. Malalamiko 52 yameshughulikiwa hadi kukamilika na malalamiko 14 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, Wizara ilifanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kubaini upungufu uliopo na kuupatia ufumbuzi, ikiwemo kujumuisha katika mkataba huo kazi zifanywazo na Idara ya Ustawi wa Jamii. Vilevile, Wizara iliendelea kushirikiana na Wakandarasi binafsi kuhakikisha kuwa huduma hizo zinatolewa kwa viwango vilivyokubalika.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango ni kiungo muhimu katika kusimamia na kuratibu Sera za Wizara, uandaaji wa mipango, mikakati, bajeti na uratibu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii, pamoja na vyuo vya mafunzo. Aidha, inasimamia mabadiliko katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Huduma za Afya (MTUHA) na tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara imepitia Sera ya Uchangiaji wa Huduma za Afya ya Mwaka 1997, Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango Shirikishi ya Afya ya Halmashauri ya Mwaka 2007, Mwongozo wa Uundaji wa Bodi za Afya za Halmashauri ya Mwaka 2001 na Mkakati wa Uzazi wa Mpango Mwaka 2010. Aidha, Sera, Miongozo na Mikakati hii imewezesha Wizara kutekeleza Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA na Malengo ya Milenia na kuleta mafanikio katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatumia mfumo wa Mpango wa Upendo wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework - MTEF*). Katika Mpango huu, fedha zote zinajumuishwa zikiwemo fedha za Serikali, Wadau wa Mfuko wa Pamoja (*Basket Fund*) na walio nje ya Mfuko kwa kutumia Miradi Misonge na Taasisi zisizo za Serikali na *Global Fund*). Ili kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa kwenye vipaumbele vya sekta, Wizara imekuwa ikifanya tafiti za PER na NHA ili kubaini maeneo ya kipaumbele. Aidha, tafiti hizo zimesaidia kuandaa bajeti inayoendana na Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA na Milenia Namba 4, 5 na 6.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wadau mbalimbali wa Maendeleo wakiwemo wa Mfuko wa Pamoja na wengine wanaosaidia maeneo maalumu ya huduma za afya na ustawi wa jamii. Wizara inawashirikisha wadau wote katika hatua zote za kupanga, kutekeleza, kufanya tathmini na kupima mafanikio kwa uwazi. Hii imeongeza imani kwa wadau hao na kuwa chachu ya kuongeza fedha wanazotoa kwa sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Aidha, Wizara inatumia Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) katika kukusanya takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango Mkakati

wa Sekta ya Afya, MMAM na mipango mbalimbali. Vilevile, Wizara ilifanya majaribio ya programu ya kompyuta itakayotumika kutunza na kuchambua takwimu za MTUHA katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi ilikamilisha utaratibu wa kufanya malipo ya kiwango kikubwa kwa kupitia mfumo wa malipo kwa mtandao wa kibenki badala ya kuandika hundi. Hatua hii imepunguza muda wa kusubiri kupitisha hundi kwa malipo kutoka siku saba hadi siku moja. Aidha, Wizara iliweka mfumo wa kufuatilia mwenendo wa fedha kwa akaunti zote za Wizara kwa nia ya kufunga zile ambazo hazitumiki baada ya muda wa mradi husika kwisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilikamilisha Daftari la Mali ya Serikali ili kuonesha idadi na thamani ya mali zilizopo na ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa maafisa ugavi 15 kati ya 30 ili kuboresha utendaji kazi wa maafisa hao. Aidha, Kitengo cha Ugavi kiliimashwa kwa kuongeza idadi ya maafisa ugavi wenye ujuzi na kuajiri Mshauri Mwelekezi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kusimamia na kudhibiti matumizi ya mifumo ya fedha, ununuzi na usalama wa mali za Serikali kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali iliyopo. Aidha, Wizara ilikagua usambazaji wa dawa kwenye vituo 230 vya kutolea huduma za afya katika Mkoa wa Mbeya na makazi ya wazee, watu wenye ulemavu, wasiojiweza na mahabusu za watoto zilizoko nchi nzima. Katika zoezi hilo, jumla ya vituo 34 vilikaguliwa. Kutokana na yaliyoyitokeza katika ukaguzi huo, Wizara imetekeleza yafuatayo: Makazi ya Bukumbi, Yombo na Singida yamepatiwa gari na jumla ya watumishi 24 wamepangiwa kazi katika makazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya ukaguzi wa fedha za ruzuku ya mishahara zinazotolewa na Serikali kwa Watumishi wa Kada ya Afya waliko kwenye Vyuo vya Afya, Vituo vya Ustawi wa Jamii, Hospitali Teule na za Mashirika ya Dini. Lengo lilikuwa ni kuhakiki watumishi na matumizi ya fedha za mishahara, jumla ya vituo 137 vilikaguliwa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukaguzi huo, Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuwaondoa katika *Pay Roll* watumishi ambao wameacha kazi au hawapo katika vituo vyao vya kazi. Aidha, Wizara imetoa maelekezo kwa Hospitali za Mashirika ya Dini na Makazi kutoa taarifa kila robo mwaka ya watumishi wanaoacha kazi, kufukuzwa au kufariki. Vilevile, Wizara imeimarisha Mfumo wa Usimamizi wa *Pay Roll* ya Hospitali za Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano na vyombo vya habari katika kutoa taarifa kwa wananchi. Aidha, imefanya mikutano na wanahabari katika kutoa ufanuzi wa masuala kuhusu huduma za afya na ustawi wa jamii. Vilevile, imetoa taarifa kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali yanayohusu afya na ustawi wa jamii kupitia magazeti, redio na televisheni na Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa ya Saba Saba na Nane Nane.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliandaa na kuwasilisha Serikalini, Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutunga Sheria ya Kusimamia Huduma za Afya Nchini (*The National Health Services Act*). Waraka huo, upo katika ngazi ya Kamati ya Kitaalam ya Makatibu Wakuu (*Inter-Ministerial Technical Committee*). Aidha, Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutunga Sheria mpya ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku, umepita katika ngazi ya Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu. Wizara imefanya mawasiliano na wadau mbalimbali ili Waraka huo uweze kuwasilishwa katika ngazi ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliandaa Kanuni moja chini ya Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2008. Aidha, Kanuni nne chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Mwaka 2003, Kanuni mbili chini ya Sheria ya Usajili wa Maafisa Afya Mazingira ya Mwaka 2007, Kanuni nne chini ya Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala ya Mwaka 2002 na Kanuni moja chini ya Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Maabara za Afya ziliandaliwa. Vilevile, Kanuni nyingine zimewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi na nyingine zinasubiri vikao na wadau. Pia, mchakato wa kutunga Kanuni mbalimbali chini ya Sheria za Afya ya Jamii ya Mwaka 2008 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya upembuzi yakinifu kuhusu uundwaji wa Baraza moja la kitaaluma litakalounganisha Mabaraza yote kabla ya kuandaa Sheria. Aidha, Wataalamu walitembelea Nchi za Afrika Kusini, Uingereza, Thailand na Zimbabwe ili kujifunza muundo na taratibu za uendeshaji wa Baraza kama hilo.

Matokeo ya ziara hizo yilibaini kuwa ni vigumu kuunda Baraza moja. Nchi hizo zina Mabaraza manne ya Madaktari, Wauguzi na Wakunga, Wafamasia na Wataalamu wa taaluma nyingine. Suala hilo linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali inaratibu, inasimamia na kuimarisha huduma za Uboreshaji wa Afya, Kinga na Tiba ya magonjwa na Utengamao. Aidha, Ofisi inasimamia mafunzo, upatikanaji na uendelezaji wa wataalamu wa Afya katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Vilevile, Ofisi kupitia Wakala na Taasisi zake, inasimamia ubora na usalama wa dawa, vifaa, vifaa tiba, kemikali, viini lishe, utafiti, maadili na ubora wa viwango vya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi, kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyoandaliwa na Wizara. Pia, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali inasimamia na kuimarisha huduma za uuguzi na ukunga, ukaguzi na ubora wa huduma za afya za dharura.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Vyama vya Kitaaluma vilivyo chini ya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii, inasimamia maadili ya wataalamu wa afya kwa kutumia Mabaraza yao. Mabaraza hayo ni pamoja na Baraza la Madaktari na Madaktari wa meno, Wauguzi na Wakunga, Wafamasia, Wataalamu wa Radiolojia, Maabara, Optometria, Mazingira, Tiba Asili na Tiba Mbadala na Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilichapisha nakala 20,000 za Mwongozo wa Uuguzi na Ukunga na Utoaji wa Huduma za Msingi kwa wagonjwa (*Basic Nursing Procedure Manual*) na nakala 1,200 za Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa Huduma za Uuguzi (*Minimum Standards for Nursing Practice*) na ilisambazwa katika Hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya ukaguzi wa vituo 195 vya kutolea huduma za afya vya Serikali na binafsi vikiwemo vya mashirika ya dini katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Mbeya kwa lengo la kupima ubora wa huduma za afya na ustawi wa jamii zinazotolewa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kutoa huduma za dharura za afya pamoja na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza (kama mafua makali ya nguruwe na kipindupindu), mafuriko, ajali za vyombo vya usafiri, ukame uliosababisha njaa na kadhalika. Aidha, Wizara ilipeleka timu ya wataalamu, dawa na vifaa tiba katika Wilaya za Same, Handeni, Kilosa, Chato, Muleba na Bukombe kutoa huduma za kiafya kwa waathirika wa mafuriko na maporomoko ya udongo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mabaraza ya Kitaaluma yaliyo chini ya Wizara yaliendelea na maandalizi ya mfumo wa taarifa (*Database*) na Tovuti ili kuboresha huduma na mawasiliiano kwa wanataaluma pamoja na wadau. Aidha, Mabaraza hayo yameandaa kanuni na miongozo ya kusimamia miiko, mwenendo na utendaji wa wanataaluma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilidurusu na kukamilisha rasimu ya mwongozo wa kuelimisha na kuboresha afya. Aidha, ilikamilisha rasimu ya Mpango Mkakati wa Kuboresha na Kudumisha Afya (2010 – 2015); pamoja na Mpango Mkakati wa Kudhibiti Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku 2010 - 2015. Wizara ilielimisha Wananchi kwa kutumia redio, televisheni na machapisho kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau, iliendelea kuimarishe huduma ya Afya mashulen kwa kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza kwa waratibu 23 wa huduma za afya shulen waliotoka katika Wilaya zote za Mikoa ya Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilidurusu mwongozo wa kudhibiti taka nchini, kutoa mafunzo ya udhibiti taka zitokanazo na huduma za afya kwa watumishi katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Morogoro, Mtwara, Pwani na Tanga na katika Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Kasulu na Korogwe. Aidha, ilianda mfumo wa kukusanya takwimu kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya athari za kiafya zitokanazo na uchafuzi wa mazingira. Vilevile, ilianda andiko la mradi juu ya athari za kiafya zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilianda mwongozo wa ujenzi wa vyoo bora ili kuinua hali ya usafi wa mazingira katika jamii. Aidha, Wizara ilichapisha na kusambaza nakala 500 za Sheria ya Afya ya Jamii katika Mikoa na Halmashauri zote nchini na kuweka katika Wavuti ya Serikali. Vilevile, Wizara iliunda Baraza la Usajili wa Wataalamu wa Afya ya Mazingira ili kusimamia maadili, mwenendo na utendaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi 57 waliopo katika vituo vya afya bandari, viwanja vya ndege na mipakani kuhusu Kanuni za Afya za Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya tathmini kubaini uwezo wa vituo vya afya vya bandari, viwanja vya ndege na mipakani katika kutekeleza kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kutekeleza mikakati na shughuli muhimu za kuwakinga wananchi dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Magonjwa ya kuambukiza ni pamoja na magonjwa makuu matatu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Mengine ni Usubi, Vikope, Matende, Kichocho na Minyoo. Magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni pamoja na Kisukari, magonjwa ya Moyo na Kiharusi, Saratani, ajali na majeraha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kushirikiana na wadau kudhibiti magonjwa ya milipuko kama kipindupindu, mafua makali ya *Influenza*. Aidha, Wizara iliimarisha ufuutiliaji wa magonjwa na kutoa taarifa, kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kuandaa na kusambaza miongozo na vielelezo mbalimbali, kutoa mafunzo na huduma za kinga. Aidha, Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wa mfumo maalum wa ufuutiliaji na udhibiti wa magonjwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitekeleza afua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa Malaria ikiwa ni pamoja na usambazaji wa vyandarua 9,000,000 vyenye viuatilifu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vilitolewa bila malipo. Aidha, vyandarua vya Hati Punguze 4,200,000 kwa ajili ya mama wajawazito na vyandarua 1,257,020 kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, viliuzwa kwa bei ya shilingi 500.00. Vilevile, upulizaji wa viuatilifu Ukoko majumbani ulifanyika katika Mkoa wa Kagera kufuatia mlipuko wa Malaria katika Wilaya za Muleba na Karagwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilinunua na kusambaza dozi milioni 13 za dawa mseto ya Alu ya kutibu Malaria katika vituo vya tiba vya umma na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Aidha, Wizara ilianzisha matumizi ya Kipimo cha

Haraka cha uchunguzi wa Malaria katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Iringa, Pwani na Kagera, jumla ya vipimo 750,000 vilisambazwa katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilinunua na kusambaza dawa za Kifua Kikuu nchini zikiwemo za Kifua Kikuu Sugu. Aidha, Wizara iliongeza wigo wa huduma za wagonjwa wa Kifua Kikuu kwa kuhusisha vituo vya binafsi. Kati ya wagonjwa 64,366 waliouguwa Kifua Kikuu mwaka 2009, wagonjwa 6,400 sawa na asilimia 10 walitibiwa katika vituo 650 vya tiba vya binafsi. Vituo hivyo vilipewa dawa na vifaa vya ugunduzi wa Kifua Kikuu zikiwemo hadubini mpya 21 ili kuviwezesha kutoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa bila malipo. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita jumla ya wagonjwa 316,122 waligunduliwa kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na kutibiwa. Wagonjwa walitibiwa na kupona ni asilimia 87.5, hivyo kuifanya Tanzania kuvuka lengo la Shirika la Afya Dunia la asilimia 85. Katika kipindi hicho, idadi ya wagonjwa imeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutoka wagonjwa 167 kwa kila watu 100,000 mwaka 2005 hadi 154 mwaka 2009

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliimarisha huduma za maabara kwa kuweka mashine za teknolojia mpya zenye uwezo wa kuharakisha kutambua Kifua Kikuu Sugu katika Maabara Kuu ya Kifua Kikuu Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya na Kibong'oto. Lengo ni kuongeza uwezo wa kubaini wagonjwa wenyе Kifua Kikuu na Kifua Kikuu sugu kwa haraka zaidi na kuimarisha uwezo wa kufuutilia kwa karibu zaidi mwenendo wa Kifua Kikuu sugu nchini. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha huduma za matibabu ya Kifua Kikuu sugu katika Hospitali ya Taifa ya Kifua Kikuu ya Kibong'oto, hadi mwezi Mei 2010, jumla ya wagonjwa 23 wenyе Kifua Kikuu sugu walikuwa wanaendelea na matibabu. Wizara pia ilikamilisha ujenzi wa jengo jipya lenye uwezo wa kuchukua wagonjwa wapya 20 wenyе Kifua Kikuu sugu kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia na kuifanya hospitali hii kuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa 40 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliandaa Mwongozo mpya wa kudhibiti maambukizi ya Kifua Kikuu katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Wizara iliboresha huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kuweka mkazo katika kuchunguza Kifua Kikuu kwa wagonjwa wa UKIMWI na kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa walibainika kuwa na magonjwa yote mawili. Kwa sasa hospitali zote za wilaya na vituo vyote vya afya vikiwemo vya binafsi, vimewezeshwa na vinatoa huduma shirikishi. Kwa mwaka 2009 wagonjwa wa Kifua Kikuu 56,162 sawa na asilimia 87 ya wagonjwa wote walichunguzwa na kati yao asilimia 37 walibainika kuwa na maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wagonjwa wa Ukoma nchini imeendelea kupungua kutoka wagonjwa 4,237 mwaka 2005 hadi 2,663 mwaka 2009, ambayo ni sawa mgonjwa 0.7/10,000 na hivyo kuvuka lengo la kimataifa la kutokomeza ukoma la mgonjwa 1/10,000. Wizara ilitoa dawa za kutibu wagonjwa 2,663 wenyе ukoma na kutoa viatu maalum jozi 6,950 kwa walioathirika na ugonjwa huo bila malipo. Aidha, Wizara ilitoa huduma za utengemao kwa watu 542 wenyе ulemavu utokanao na Ukoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wengine, iliendelea

kutekeleza afua mbalimbali za kudhibiti maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI. Afua hizo ni pamoja na huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI, ushauri nasaha na upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa hiari. Vituo vya ushauri nasaha viliongezeka kutoka 1,743 mwaka 2008/09 na kufikia vituo 2,134.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10 jumla ya watu 1,225,869 walipima VVU. Idadi hiyo inafanya watu waliopima VVU kuanzia mwaka 1988 hadi sasa kufikia watu 11,741,480. Aidha, watu 654,982 wenye VVU waliandikishwa na kati yao 337,854 wameanzishiwa dawa za UKIMWI. Mwongozo mpya wa kumwanzishia mgonjwa dawa za UKIMWI kwa kufuata kiwango kipyga cha chembechembe za CD4 kutoka 200 hadi 350 utaongeza idadi ya wagonjwa watakaohitaji kuanzishiwa dawa za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilizindua Mpango Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele (*Neglected Tropical Diseases – NTDs*). Aidha, magonjwa yanayohusika katika mpango huu ni pamoja na Usubi, Matende na Mabusha, Trakoma, Kichocho na Minyoo. Utaratibu wa kutibu magonjwa haya umewekwa nchi nzima hadi ngazi ya jamii. Jumla ya watu 5,200,000 wamepewa dawa kwa ajili ya kinga na tiba ya magonjwa haya. Vilevile, utaratibu huu ukiimarishwa kwa kutumia dawa kwa miaka 3-5 mfululizo, magonjwa haya hayatakuwa tatizo la afya ya jamii tena. Hivyo, ninawaagiza Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuhakikisha kuwa dawa za magonjwa haya zinakuwepo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo yao kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikabitihhi magari mapya 4 na kufikia magari 17 na baiskeli 800 mikoa ya majaribio ya Morogoro, Tanga, Iringa, Ruvuma na Mbeya ili kusaidia utekelezaji wa shughuli za kukabiliana na maradhi hayo. Vilevile, Wizara iliendelea kutumia na kuboresha uwezo wa wagawa dawa wa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa unaozingatia Dira 2020 ya Dunia ya kutokomeza ulemavu wa kutoona unaozuilika ifikapo mwaka 2020. Wizara kwa kushirikiana na wadau, iliendelea kusimamia na kutoa huduma za macho kwenye hospitali zote za ngazi ya mikoa na taasisi za Serikali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilianzisha huduma ya mkoba kama jaribio la kukabiliana na uhaba wa wataalamu katika Mikoa ya Lindi, Tabora na Kigoma. Pia, katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Manyara na Pwani ambapo watu 3,400 walifanyiwa matibabu ya upasuaji mdogo wa kusawazisha kope na kwa Jiji la Dar es Salaam, watu 5,764 walitibiwa, kati ya hao watu 1,870 walipatiwa miwani na watu 368 walipatiwa huduma za upasuaji bila malipo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kusimamia na kutoa huduma za macho za ubingwa za kuzuia ulemavu wa kutoona utotonii na kurekebisha makengeza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa KCMC na Hospitali ya CCBRT. Aidha, huduma za macho za ubingwa zinapelekwa katika hospitali maalum za kanda kwa awamu na kwa kuanzia

Mikoa ya Mwanza na Mbeya. Vilevile, Wizara inaagiza kuwa Hospitali zote za Wilaya na Mikoa ziwe na dawa za macho za kutosha kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ilizindua utekelezaji wa mradi wa kudhibiti ugonjwa wa kichaa cha mbwa katika wilaya 24 za Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalamu wa mikoa yote kuhusu jinsi ya kupambana na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hususan milipuko na magonjwa mapya yanayojitekeza hivi sasa, ikiwa ni pamoja na magonjwa ya Ebola, Marbug, Homa ya Bonde la Ufa na Homa ya Mafua Makali ya *Influenza*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilisaidia mikoa na wilaya kudhibiti milipuko ya (kipindupindu na Mafua Makali ya Influeza) katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Mara, Manyara, Shinyanga, Mwanza na Dar es Salaam. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha ufuutiliaji wa ugonjwa wa mafua makali ya influenza katika mikoa yote na vituo maalum vitano. Vilevile, iliimarisha Maabara Kuu ya Wizara kwa kuiongezea uwezo wa kupima ugonjwa wa Mafua Makali ya Influenza, Homa ya Bonde la Ufa na Homa ya *Dengue*. Jumla ya wagonjwa 774 walithibitishwa kuwa na ugonjwa wa mafua makali ya influenza ambapo mgonjwa mmoja alifariki. Wagonjwa 31 kati ya 100 walithibitishwa kuwa na Virusi vya *Dengue*. Wagonjwa hao waligundulika katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilisimamia na kufuatilia utekelezaji wa huduma za uzazi wa mpango, uzazi salama, mkakati wa kudhibiti magonjwa ya watoto kwa uwiano unaolenga watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ufuutiliaji wa maendeleo ya ukuaji wa mtoto, afya shulenii, chanjo, afya ya jamii, afya ya uzazi kwa vijana na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kutambua saratani ya shingo ya kizazi na matiti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilianda mwongozo wa utoaji huduma kwa mama na mtoto baada ya kujifungua hadi siku 40. Aidha, Wizara ilihamasisha maafisa waandamizi 340 kutoka ngazi za Wilaya na Mikoa, wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Waheshimiwa Wabunge ili kusimamia na kufuatilia utoaji wa huduma za afya za uzazi na mtoto. Vilevile, ilitoa mafunzo kwa watumishi 408 juu ya stadi za kuokoa maisha na huduma ya dharura kwa wenye matatizo yatokanayo na uzazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilianda Programu ya Utekelezaji wa Uzazi wa Mpango 2010 – 2015 inayolenga kuiongeza watumiaji wa njia za kisasa za uzazi wa mpango kutoka asilimia 20 hadi 60. Aidha, Wizara ilihamasisha viongozi katika ngazi ya familia, kata na tarafa juu ya umuhimu wa uzazi wa mpango na faida zake. Jumla ya Maafisa Watendaji wa Kata 4,500 na Watendaji ngazi ya Tarafa 3,750 pamoja na viongozi wa madhehebu ya dini 2,500 walishirikishwa katika uhamasishaji huo. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo kwa Waandishi wa habari 100 ili kuwawezesha kuandika taarifa sahihi za kusaidia kuondoa imani potofu dhidi ya matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitekeleza Mpango Maalum wa Chanjo kwa kuweka mkakati wa kumfikia kila mtoto. Watumishi 510 kutoka wilaya 51 zenyne idadi kubwa ya watoto ambao hawakupewa chanjo ya DPT3 mwaka 2008 walipewa mafunzo ya jinsi ya kumfikia kila mtoto kwa chanjo. Mkakati huo umepunguza idadi ya Wilaya zenyne watoto wengi wasiopata DPT3 kutoka 51 hadi 24. Aidha, Wizara ilipanua huduma za chanjo kwa kutumia njia ya huduma za mkoba na kliniki tembezi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliimarisha huduma za chanjo kwa kutoa chanjo kwenye kliniki za Afya ya Uzazi na Mtoto na kutumia njia ya huduma za mkoba na kliniki tembezi (*mobile clinics*). Katika kipindi cha Julai – Desemba 2009 kiasi cha kliniki tembezi 33,719 kati ya 38,658 zilifanyika katika mikoa yote. Kiasi hiki ni asilimia 87 ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitekeleza mkakati wa udhibiti wa magonjwa ya watoto kwa uwiano. Wizara ilitoa mafunzo ya jinsi ya kumhudumia mtoto mgonjwa sana na kufanya tathmini ya ubora wa huduma za afya kwa watoto kwa watoa huduma 228 kutoka hospitali 71 katika mikoa 13. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wavezeshaji 60 kutoka Mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Morogoro na Pwani juu ya kuwahudumia watoto wachanga na wenyewe uzito pungufu. Pia, Wizara ilitoa mafunzo kwa wavezeshaji na watoa huduma 647 kutoka Kanda zote za Mafunzo, juu ya kumsaidia mtoto kupumua baada ya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Kudhibiti Maambukizi ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto. Aidha, ilifanya usimamizi na ufuutiliaji katika vituo vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto katika hospitali za mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati zinazotoa huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto katika Mikoa 10 ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Iringa, Kigoma, Rukwa, Morogoro, Tanga, Dodoma, Pwani na Singida. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo elekezi kwa watoa huduma 2,255 juu ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Pia, ilitoa mafunzo kwa watoa huduma 2,000 kuhusu utambuzi wa mapema wa maambukizi ya VVU kwa watoto waliozaliwa na akina mama wenyewe maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya uraghibishi kwa viongozi wa mikoa na wilaya kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya huduma rafiki za afya ya uzazi na vijana kwa wavezeshaji 242 kutoka sekta ya afya na elimu, katika wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, huduma za tiba zinajumuisha mfumo mzima wa utoaji matibabu, uchunguzi na rufaa kuanzia ngazi ya kaya, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya hadi hospitali za rufaa za mikoa na hospitali maalum (*super speciality hospitals*) katika Sekta za Umma na Binafsi. Katika ngazi ya Kaya, huduma zinatolewa na Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kwa utaratibu wa mkoba (*outreach services/home based care*). Huduma za afya ya msingi zinatolewa na zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya. Huduma za rufaa zinatolewa na hospitali za mikoa, kanda na taifa. Aidha, Serikali inagharamia miundombinu, vifaa, vifaa tiba, dawa, vitendanishi na

watumishi katika hospitali za Serikali na inachangia dawa, vifaa tiba, vitendanishi na mishahara ya baadhi ya watumishi katika hospitali zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, katika kupanga upya ngazi za utoaji huduma za afya nchini, Serikali imezipa jukumu la kutoa huduma za ubingwa wa juu (*super speciality*), Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Mirembe na Isanga na Hospitali ya Kibong'oto. Hospitali hizi zinaendelezwa kwa majengo, vifaa na wataalam na zimeanza kutoa huduma hizo za ubingwa maalum kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Hospitali nyingine za ubingwa maalumu zinazohudumia kanda ni kama ifuatavyo:-

Hospitali za Rufaa za Kanda na Mikoa inayohudumiwa:

Hospitali	Kanda	Mikoa
Bugando	Ziwa na Magharibi	Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tabora

KCMC	Kaskazini na Kati	Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Dodoma na Singida
------	-------------------	--

Mbeya	Nyanda za Juu Kusini	Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma
-------	----------------------	-----------------------------------

Hospitali ya Taifa Muhimbili	Mashariki na Kusini	Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara.
------------------------------------	---------------------	--

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya huduma za ubingwa na ili kukidhi mfumo wa rufaa, Wizara imezipandisha hadhi Hospitali zifuatazo kuwa za ubingwa maalum: Hospitali ya Jeshi Lugalo na Hospitali ya CCBRT zitakazohudumia Kanda ya Mashariki yenye Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro na pia Kanda ya Kusini yenye Mikoa ya Lindi na Mtwara ambayo ujenzi wa hospitali yake umeanza katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani. Hii itatoa nafasi kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Taasisi ya Saratani Ocean Road kutoa huduma za ubingwa ngazi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarishe mfumo wa rufaa katika mikoa yote nchini na kwa kutambua mahitaji maalum ya mkoa/jiji la Dar es Salaam, Wizara imezipandisha hadhi Hospitali za Manispaa za Kinondoni (Mwananyamala), Ilala (Amana) na Temeke kuwa hospitali za rufaa ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ongezeko la mahitaji ya huduma za ubingwa na kwa kutambua huduma za ubingwa zinazotolewa na Hospitali za Taasisi zisizo za Kiserikali, Wizara imezipandisha hadhi Hospitali zifuatazo kuwa hospitali za rufaa ngazi ya mkoa: Peramiko (Ruvuma), Ndanda (Mtwara), St. Gaspar-Itigi (Singida), St. Francis-Ifakara (Morogoro), Hydom (Manyara) na *Arusha Lutheran Medical Centre* (Arusha).

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutambua uwezo wa hospitali zifuatazo za Kabanga (Kigoma), Illembula (Iringa), Nkinga (Tabora), Bumbuli (Tanga), Mchukwi (Pwani), Ndolage (Kagera), Kolandoto (Shinyanga), Igogwe na Itete (Mbeya), Chuo Kikuu Dodoma (Dodoma), Nyangao (Lindi) na Atman (Rukwa) kulingana na vigezo ili ziweze kupewa hadhi zinazolingana na huduma zinazotoa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaimarisha huduma binafsi katika hospitali za umma hasa Hospitali za Kanda kama zinavyotolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Wizara itahakikisha kwamba, madaktari na wafanyakazi wengine katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma hawataruhusiwa kufanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya za binafsi bila utaratibu. Pale ambapo mtaalamu atahitajika kwenda kutoa huduma ili kuokoa maisha ya mgonjwa kutoka pande zote mbili za umma na binafsi, itafanyika hivyo kwa makubaliano maalumu kati ya taasisi husika. Hata hivyo, wataalamu hawa watapewa fursa ya kuamua kubakia Serikalini au kwenda kufanya kazi katika vituo binafsi vya kutolea huduma za afya. Utaratibu huu pia utawahusu wafanyakazi katika vituo vya afya na vyuo vya ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2009/10, Wizara imepitia mwongozo wa uchangiaji wa huduma za afya na kuelekeza kuwa wazee wote wenye umri zaidi ya miaka 60 wapatiwe huduma za afya bila malipo. Aidha, imewaaagiza Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa kutenga sehemu katika vituo vyao vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kuwahudumia wazee. Lengo ni kuhakikisha wazee wanapewa kipaumbele katika kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2009/10, Wizara imetayarisha Mpango Mkakati wa Huduma za Afya ya Kinywa na Meno (2010-2014). Aidha, Wizara kupitia MSD ilinunua na kusambaza vifaa vya matibabu ya meno katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma katika mikoa na wilaya zote. Vilevile, ilisambaza mashine za kutibu magonjwa ya meno katika vituo 33 vya afya na hospitali 75 nchini pamoja na kununua vifaa vya kisasa vya kutibu meno kwa ajili ya Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Ruvuma na Dodoma. Pia, ilinunua mashine za *X-ray* kwa ajili ya matibabu ya meno kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea na uhamasishaji wa wamiliki wa vituo vya kutolea huduma za afya vya binafsi, mashirika ya kujitolea na makampuni kuingia makubaliano na halmashauri, ili vituo vyao vitoe huduma za afya kwa niaba ya halmashauri. Aidha, Hospitali ya Peramiko iliingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Hospitali ya Illembula iliingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Vilevile, Hospitali ya Kilindi Lutheran iliingia

mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi na Hospitali ya Babtist Kigoma iliingia mkataba na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10 Wizara kwa kushirikiana na wadau, ilifanya ukarabati wa Maabara katika Hospitali za Amana (Ilala), Temeke, Tumbi (Kibaha), Dodoma, Morogoro, Singida, Sokoine (Lindi), Ligula (Mtwara), Maweni (Kigoma), Sumbawanga, Shinyanga, Bukoba na Bombo (Tanga). Aidha, Wizara ilipeleka mashine za *X-ray* na *Ultrasound* katika Hospitali za Wilaya za Bukombe, Chato na Tandahimba na Hospitali za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha ujenzi wa vituo 34 vya afya vitatu katika Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke. Vituo hivyo vitatoa huduma sawa na hospitali ya Wilaya. Pia, Wizara ilikamilisha ukarabati wa karakana za Tabora na Tanga na kununua vitendea kazi vya karakana hizo.

Mheshimiwa Spika, fedha za Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinatumika kununua dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Aidha, fedha zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo zimetumika kununua dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo chini ya miradi msonge ya Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na Afya ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitumia shilingi 40,923,123,297.00 kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na dawa za UKIMWI. Kati ya fedha hizo, Serikali ilitoa shilingi 26,124,341,297.00, Mfuko wa pamoa wa Wadau wa Maendeleo (*Basket Fund*) shilingi 14,899,782,000.00.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Bohari ya Dawa ilisambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Zahanati 4,158, Vituo vya Afya 480, Hospitali 135 za Wilaya na Teule, Hospitali 20 za Mikoa, Hospitali 3 za Manispaa, Hospitali 7 za Rufaa Maalum (*Super Speciality Hospitals*), Hospitali 1 ya Taifa, Hospitali 4 za Jeshi la Wananchi na 1 Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitoa mafunzo ya mfumo wa uagizaji dawa, vifaa na vifaa tiba kulingana na mahitaji (*Integrated Logistics System – ILS*) na mgao wa fedha kwa watumishi katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za Serikali, hospitali za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na mashirika ya dini. Mafunzo hayo yalitolewa kwa watumishi 338 katika Mkoa wa Arusha, 807 Mkoa wa Kilimanjaro, 278 Mkoa wa Manyara, 286 Mkoa wa Mara, 426 Mkoa Mtwara na 643 Mkoa wa Shinyanga. Zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma zinatumia mfumo huo kuagiza dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya Dawa na Kanda zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilikamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuthibiti Madhara ya Matumizi ya Bidhaa za Tumbaku kwa Binadamu. Aidha, Wizara ilikamilisha kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Akili Na. 21 ya Mwaka 2008. Vilevile iliandaa miongozo ya kuhudumia wagonjwa wa akili na waathirika wa dawa za kulevyaa walio magerezani. Pia, Wizara itakamilisha mpango wa

utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa huduma za magonjwa yasiyo ya kuambukiza, afya ya akili na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilipeleka wagonjwa 535 kutibiwa nje ya nchi. Kati yao watoto walikuwa 300, sawa na asilimia 56 na wakubwa ni 235, sawa na asilimia 44. Kati ya wagonjwa hao asilimia 69 walikuwa na matatizo ya moyo, asilimia 11 matatizo ya figo, asilimia 9 magonjwa ya saratani na asilimia 11 magonjwa mengine. Aidha, madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Apollo, India walikuja nchini kutoa huduma kwa wagonjwa. Vilevile, walifanya tathmini ya mahitaji ya vifaa na vifaa tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Taasisi ya Mifupa Muhimbili na kuhudumia jumla ya wagonjwa 361. Wagonjwa 250 walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na 111 katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Madaktari hao walitoa miadhara kwa madaktari na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi za Jamii, Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilisimamia na kuratibu tiba asili na tiba mbadala, ili kuboresha afya ya jamii nchini. Aidha, Wizara imekamilisha Mwongozo na mfumo wa usajili wa waganga na wakunga wa tiba asili. Mamlaka ya Chakula na Dawa imeanza kudhibiti dawa za tiba asili na tiba mbadala nchini. Udhibiti huo utazuia utoaji holela wa dawa za asili na tiba mbadala na watu wasiosajiliwa au katika sehemu zisizohusika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 296,376. Kati yao 51,428 walilazwa na 244,948 walitibiwa na kuondoka. Aidha, Wizara inaijengea uwezo hospitali ili itoa huduma za ubingwa maalum (*super speciality*) kwa kujenga Kituo cha Tiba ya Magonjwa ya Moyo na Mafunzo ambacho kilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 31 Machi, 2010. Ujenzi huo unagharimiwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Vilevile, vyumba vyaa upasuaji na wataalam waliongezwa. Jumla ya wagonjwa 186 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo. Maandalizi ya kuanzisha huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo yalikamilika kwa kununua mashine ya kusafisha maji. Pia, ukarabati wa majengo yote ya Hospitali ya Taifa Muhimbili umekamilika na huduma zote zinatolewa.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ilianzisha huduma za dharura (*Emergency Medicine*) Februari, 2010, baada ya ukarabati mkubwa kukamilika na vifaa tiba vyaa kisasa kuwekwa. Aidha, Hospitali ilianzisha huduma ya mkoba kwa wagonjwa wa macho katika Kituo cha Afya cha Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Jumla ya wagonjwa 15,451 walihudumiwa. Huduma hiyo itapanuliwa baada ya kupatikana gari maalum. Wizara iliagiza vifaa vyaa upasuaji kupitia tundu dogo (*Laparoscopic surgery*) kwa ajili ya hospitali hiyo. Aina hii ya upasuaji inapunguza sana muda wa wagonjwa kukaa hospitali na hivyo kuwezesha wagonjwa wengi kuhudumiwa. Vilevile, Hospitali imeimarisha uhusiano na Hospitali za Appolo ambapo madaktari kutoka India watakuwa wanashirikiana nao katika kutoa huduma za ubingwa. Hospitali imeanzisha mfumo wa kupima afya za wananchi kila Jumamosi ili wananchi waweze kutambua afya ya miili yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ilihudumia wagonjwa wa kutibiwa na kurudi nyumbani 41,922. Kati yao wagonjwa 9,811 walikuwa ni majeruhi. Wagonjwa 12,094 walilipia gharama za matibabu. Aidha, jumla ya wagonjwa 5,316 walilazwa ambapo 126 walikuwa wagonjwa mahututi. Wagonjwa 572 waliolazwa, walilipia gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, wagonjwa 3,144 walipasuliwa. Kati ya hao 1,950 walifanyiwa upasuaji wa kawaida na 1,194 upasuaji wa dharura. Aidha, wagonjwa 62 walifanyiwa upasuaji wa saratani ya ubongo (*brain tumour*) na 32 upasuaji wa mifupa ya uti wa mgongo (*spine stabilization*). Vilevile, wagonjwa 75 walifanyiwa upasuaji wa kubadilisha mifupa ya nyonga (*total hip replacement*) na 37 upasuaji wa kubadilisha mifupa ya goti (*total knee replacement*). Hadi sasa wagonjwa wapatao 272 wamewekewa viungo bandia vya nyonga tangu huduma hiyo ianze mwaka 2004 na wagonjwa 90 wamewekewa viungo bandia vya magoti tangu huduma hiyo ianze mwaka 2007. Pia, Taasisi ilianzisha huduma ya mkoba kwa wagonjwa majeruhi katika Hospitali ya Bombo, Tanga. Jumla ya wagonjwa 30 walifanyiwa upasuaji wa viungo. Taasisi ilianza kutoa mafunzo kwa wataalam wa fani ya upasuaji wa viungo bandia vya nyonga na goti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa wapya 3,842 wa Saratani. Kati yao 2,968 walilazwa na 874 walitibiwa kama wagonjwa wa nje. Aidha, Taasisi ilihudumia wagonjwa 10,455 wa marudio katika kliniki. Vilevile, jumla ya wanawake 11,897 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya shingo ya kizazi na matiti. Kati yao 833 waligundulika kuwa na dalili za awali za saratani ya shingo ya kizazi na 72 saratani ya matiti. Pia, Taasisi ilitoa mafunzo kwa wataalam 146 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Pwani na Ruvuma. Taasisi kwa kushirikiana na wadau ilitoa mafunzo ya tiba shufaa kwa watumishi katika Hospitali za Rufaa Maalum za Bugando, KCMC na Mbeya na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ilianda mukutano wa kisayansi wa AORTIC, ulioshirikisha wataalamu wa saratani na huduma za afya zaidi ya 700 kutoka nchi zaidi ya 60 duniani. Washiriki 120 walitoka Tanzania. Mukutano huo umewezesha taasisi za kimataifa kuja nchini kuanzisha huduma za upimaji wa dalili za awali za saratani hususan ya shingo ya kizazi, tafiti za saratani za VVU/UKIMWI na chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ilianza kujenga jengo la hospitali litakalokuwa na wodi zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 170. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, imenunua mashine mbili mpya za tiba ya saratani ya shingo ya kizazi kwa mionzi inayotolewa ndani ya mwili, yaani *Intracavitary therapy*. Vilevile, Taasisi iliingia makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuwawezesha wagonjwa wa saratani ambao ni wanachama wa Mfuko huo walipiwe gharama za matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali ya Mirembe iliendelea kutoa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa wa akili na walioathirika na dawa za kulevyta. Aidha, jumla ya wagonjwa 30,937 walihudumiwa katika hospitali hiyo ambapo 27,769 walitibiwa na kuondoka na wagonjwa 3,168 walilazwa. Ujenzi wa Kituo cha utengamao kwa waathirika wa dawa za kulevyta cha Itega unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Isanga katika mwaka 2009/10, iliendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wa akili waliofanya makosa ya jinai. Wagonjwa wapya waliopokelewa ni 211 kutoka katika sehemu mbalimbali nchini, waliopewa ruhusa ni 229 na waliobaki katika taasisi ni wagonjwa 221.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali ilitoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu waliopata rufaa kutoka mikoa mbalimbali nchini. Wagonjwa wapya waliogundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa 511. Aidha, wagonjwa 23 wa Kifua Kikuu Sugu walianzishiwa tiba. Hospitali ilihudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu 1,565, kati yao 683 walitibiwa na kurudi nyumbani na 882 walilazwa. Vilevile, Hospitali iliwhahudumia wagonjwa wa kawaida 13,199, kati yao 12,606 walitibiwa na kurudi nyumbani na 593 walilazwa. Jumla ya wagonjwa 2,387 walianzishiwa dawa za UKIMWI kati ya waathirika 4,272.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali ilitoa elimu ya afya kwa umma kupitia radio na televisheni juu ya tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu. Aidha, Hospitali iliadhimisha Siku ya Kifua Kikuu Duniani kwa kutoa huduma kwa wananchi ambapo 18 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, watumishi 35 wa ngazi mbalimbali walihudhuria mafunzo ya Kifua Kikuu Sugu hapa nchini na nchi za Uganda, Ethiopia na Lesotho. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuwaongezea stadi katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu. Aidha, Hospitali ilikamilisha ukarabati wa jengo la utawala na uzio.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Bugando ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa inamilikiwa na Baraza la Maaskofu Katoliki na kuendeshwa kwa ushirikiano kati ya Baraza la Maaskofu na Serikali kwa kusimamiwa na Bodi ya Utawala. Hospitali inahudumia Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tabora yenye wakazi wapatao milioni 13.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali ilihudumia wagonjwa 989,666, kati yao 325,085 walilazwa na 664,581 walitibiwa na kuondoka. Aidha, Hospitali ilipokea majeruhi 90,244 na kati yao 31,626 walilazwa na 58,618 walitibiwa na kuondoka. Hospitali ilikarabati wodi za akina mama na watoto na maabara. Hospitali ilipokea madaktari 44 na wafamasia 5 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, ili kutimiza lengo la kutoa huduma za ubingwa wa juu kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Magharibi, Hospitali kwa kushirikiana na taasisi kutoka nje ya nchi, ilifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 72, ambapo 6 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo. Aidha, Hospitali ilikamilisha maandalizi ya ujenzi wa jengo la matibabu ya saratani. Michoro ya jengo hilo iliidhinishwa na Shirika la Taifa la Mionzi ya Atomiki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Hospitali kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha ujenzi wa jengo la kliniki ya kutolea huduma za matunzo na tiba ya watu wanaoishi na VVU lenye uwezo wa kuhudumia wagonjwa 150. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na wadau, ilianza ujenzi wa kituo kitakachotoa huduma ya utafiti kwa watoto wenye VVU.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya *Kilimanjaro Christian Medical Centre* (KCMC) inamiliikiwa na Shirika la Msamaria Mwema la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hospitali hiyo inaendeshwa kwa ushirikiano na Serikali kwa kusimamiwa na Bodi. Hospitali hiyo inahudumia Mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, ilihudumia wagonjwa 144,741. Kati yao 21,822 walilazwa na 122,919 walitibiwa na kuondoka. Aidha, Hospitali ilitibu majeruhi 555. Hospitali ilipokea madaktari 28, wafamasia 4 na wauguzi 4 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Ujenzi wa jengo kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wenye magonjwa ya ngozi umefikia asilimia 40 na wodi ya upasuaji wa mifupa na viungo pamoja na kitengo cha tiba rekebishi umefikia asilimia 30. Hospitali ya Rufaa Mbeya katika mwaka 2009/10, ilihudumia jumla ya wagonjwa 201,419. Kati yao 31,183 walilazwa na 170,236 walitibiwa na kuondoka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Huduma ya Damu Salama, ilikusanya chupa za damu 165,000 nchi nzima. Kati ya hizo, asilimia 90.5 zilikuwa na damu salama, asilimia 2.8 ziligundulika kuwa na Virusi vya UKIMWI. Aidha, asilimia 6 ziligundulika kuwa na *Hepatitis B*, asilimia 0.5 kuwa na *Hepatitis C* na asilimia 0.2 kuwa na Kaswende. Waliochangia damu wote walipewa ushauri nasaha kabla na baada ya kupima na kupewa majibu. Waliogundulika kuwa wana matatizo, walielekezwa kwenda kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Bohari ya Dawa iliongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka asilima 80 hadi asilimia 85. Aidha, ilianza kutumia mikataba maalum na wazabuni inayowezesha kupatikana kwa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa muda mfupi. Vilevile, Bohari ilianza mchakato wa kubadilisha Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kukidhi ongezeko la huduma zinazotolewa na kuwezesha wateja kupata taarifa za upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Pia, Bohari imeajiri Maafisa Huduma kwa Wateja katika Bohari zote za Kanda kuwezesha ufuatiliaji wa mahitaji ya wateja na kushughulikia malalamiko yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Bohari ya Dawa ilifunga mitambo ya kufungasha dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Bohari zake za Kanda ili kuimarisha utekelezaji wa mfumo wa uagizaji dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji na kutoa mafunzo juu ya mfumo huo kwa kushirikiana na wadau. Aidha, ilifanya majaribio ya kusambaza dawa na vifaa tiba hadi kwenye zahanati na vituo vya afya vya umma katika Mkoa wa Tanga, kwa lengo la kueneza mfumo huo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Bohari ya Dawa ilikasimu madaraka ya kiutendaji, kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi kwa Bohari zote za Kanda. Aidha, Bohari kwa kushirikiana na wadau imejenga upya Bohari ya Dawa, Kanda ya Mwanza na maghala katika Bohari za Kanda za Mtwara na Tabora yenyе mita za mraba 2,580 ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 - 2017 kwa kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya kutoka 1,013 mwaka 2005 hadi kufikia 4,147 mwaka 2009. Ongezeko hili ni asilimia 64 ya lengo la kudahili wastani wa wanafunzi watarajali 6,450 kila mwaka.

Jumla ya vyuo 36 vipo katika ngazi mbalimbali za ukarabati na ujenzi wa miundombinu ili kukidhi ongezeko la wanafunzi katika vyuo hivyo. Aidha, Wizara imeongeza idadi ya wanafunzi wa uzamili kutoka 56 mwaka 2005 hadi 265 mwaka 2009 ili kuimarisha huduma za afya za rufaa katika Hospitali za Mikoa, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa. Ongezeko la wahitimu kutohana na Mpango huo, limepunguza pengo la uhaba wa wataalam katika sekta ya afya kutoka asilimia 68 hadi 62.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilianza mchakato wa kupitia mitaala ya mafunzo ya kada za Maafisa Afya Mazingira, Takwimu za Afya, Wazoeza Viungo, Tabibu Meno na stashahada za juu za afya ili kuendana na vigezo vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii. Vyuo vya Afya 55 kati ya 117 vipo katika hatua mbalimbali za kupata ithibati kutoka Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilianzisha Mfumo wa kukusanya takwimu za rasilimali watu katika Sekta ya Afya na kuunganishwa na Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA). Mfumo huo utawezesha kupata takwimu sahihi za rasilimali watu kwa ajili ya kuandaa mipango ya maendeleo ya rasilimali watu katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilianzisha Chuo cha Madaktari Wasaidizi, Arusha Lutheran Medical Centre na inakamilisha ukarabati wa Chuo cha Madaktari Wasaidizi Peramiho. Aidha, ujenzi wa vyuo vya Madaktari Wasaidizi unaendelea katika Hospitali za Mikoa ya Tabora na Mtwara. Kuanzishwa kwa vyuo hivyo vitatu, kutaongeza idadi ya vyuo vya aina hiyo nchini hadi kufikia nane na kuwa na uwezo wa kutoa wastani wa Madaktari Wasaidizi 400 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakufunzi 24 kutoka kanda zote nane za mafunzo, juu ya uongozi na uendeshaji. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha kusimamia na kuimarisha vyuo vya mafunzo vya afya katika mikoa na wilaya wanazozisimamia. Aidha, Kanda nne za Mafunzo za Kusini, Mashariki, Kaskazini na Kati zilitoa mafunzo kwa viongozi wa afya 81 kutoka halmashauri za wilaya 47. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuwajengea viongozi hao uwezo wa kuandaa na kutekeleza Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji kazi wa watoa huduma, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inabadilisha mfumo wa kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo kuitia kwenye vituo wanavyotolea huduma za afya viliyyopo karibu na jamii (*on site clinical mentorship*) kuliko kufanyika katika hospitali za rufaa na maalum tu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Tume ya Vyuo Vikuu na Serikali ya Cuba iliandaa hatua za awali za kuanzisha mafunzo ya aina hiyo kwa madaktari katika Manispaa ya Songea. Majengo yatakayotumika kwa ajili ya mafunzo hayo yanafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na wadau, ilifanya upembuzi yakinifu katika Kanda za Mafunzo za Mashariki, Magharibi na Ziwa ili kubaini mahitaji katika uanzishwaji wa maabara maalum za kufundishia (*skills laboratory*). Aidha, wakufunzi 22 kutoka katika vyuo vya afya vya kanda hizo walipata mafunzo ya uendeshaji wa mafunzo ya Maabara hizo nchini Kenya na Uhlanzi. Vilevile, taratibu za ununuvi wa vifaa vya maabara hizo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ustawi wa Jamii inasimamia, inaratibu na kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa watu walio katika mazingira hatarishi ambao ni watu wenye ulemavu, wazee, watoto yatima, familia zisizo na uwezo wa kipato na zilizoathirika na UKIMWI na watoto walio katika mkinzano na sheria. Aidha, inazo afua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazowakabili watu walio katika mazingira hatarishi. Vilevile, inasimamia uandaaji wa Sera, Sheria, Kanuni 49 na Miongozo ya Huduma za Ustawi wa Jamii. Pia, inasimamia taratibu za kuwahamisha Maafisa Ustawi waliopo katika Ofisi za Wilaya na Mikoa kuingia katika mifumo ya Tawala za Mikoa na Halmashauri. Hii itawezesha Halmashauri kuomba kibali cha kuajiri na kutenga fedha za kutolea huduma za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua na kuthamini mchango unaotolewa na jamii katika kuwatunza watu walio katika makundi maalum; kwa kushirikiana na wadau, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo familia na jamii ili ziweze kutoa huduma hizi katika namna stahiki. Aidha, kwa kushirikiana na wadau, Wizara iliendelea kutambua watoto walio katika mazingira hatarishi katika Halmashauri 8 na kufanya idadi ya watoto katika halmashauri hizo kuongezeka kutoka watoto 78 (2008) hadi 86 (2009). Tangu Mpango huo uanze mwaka 2000, jumla ya watoto 746,823 walitambuliwa kuwa katika mazingira hatarishi. Kati yao, wasichana ni 358,168 na wavulana ni 388,015. Vilevile,

watoto 586,170 walipewa huduma za kisaikolojia, afya, chakula, karo na mahitaji ya shule, makazi, malazi na mavazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii 50 katika Mahabusi 5 na shule ya maadirisho Irambo, Mbeya. Mafunzo hayo yalilenga, kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuharakisha upatikanaji wa haki kwa watoto walio katika mkinzano na sheria. Aidha, jumla ya nakala 50,000 za miongozo ya uwezeshaji haki jamii na vitini 50,000 vya uhamasishaji na uwezeshaji haki jamii vilisambazwa kwa wadau. Lengo ni kuwa na mfumo unaolingana katika kuiongezea jamii kuwa na uelewa unaolingana kuhusu haki na ustawi wa watoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitoa huduma za matunzo na ulinzi kwa watu wenye ulemavu na wasiojiweza katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali. Aidha, Wizara iliratibu huduma zinazotolewa kwa wazee na wale wasio na uwezo katika makazi 23 yanayosimamiwa na Taasisi za Dini. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi yalitolewa katika vyuo 3 vya watu wenye ulemavu vya Mirongo (Mwanza), Chuo cha Wanawake Wasioona Singida na Yombo (Dar es Salaam), kati ya 6 vilivyopo. Uchambuzi wa mahitaji ya ukarabati umekamilika kwa Chuo cha Luanzari (Tabora Mjini), Masiwani (Tanga Mjini) na Mtapika (Masasi). Katika miaka 5 wanafunzi 2,500 walihitimu katika vyuo hivyo, wa kike 980 na wa kiume 1,520. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau, inaendelea na maandalizi ya mfumo wa kutambua mahitaji ya wanaojiunga na vyuo vya ufundi, wanaopata ajira baada ya kuhitimu mafunzo na mitaala iliyopo. Lengo ni kuongeza idadi ya wanafunzi na kutoa mafunzo yanayoendana na soko la ajira na kujajiri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara imeendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*) na kuondokana na dhana potofu ya kuwa viungo vyao vinaleta mafanikio katika maisha. Serikali inaendelea kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwalinda *albino* na kuondokana na dhana hiyo potofu. Aidha, Wizara inahamasisha jamii juu ya umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa makundi maalum. Maadhimisho ya Siku ya 51 Kitaifa ya Wazee (tarehe 1 Oktoba), Siku ya Maalbino (tarehe 4 Mei), Siku ya Fimbo Nyeupe (tarehe 15 Oktoba) na Siku ya Watu Wenye Ulemavu (tarehe 3 Desembra), pia hutumika kuihamasisha jamii. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu uwezo wa kutambua watu wenye ulemavu, uchambuzi wa takwimu za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na stadi za malezi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Sheria mpya ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, ilipitishwa. Sheria hiyo itahakikisha utoaji wa haki kwa watu wenye ulemavu na kuondoa unyanyapaa mionganoni mwao. Aidha, iliendelea na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki na Ulinzi kwa Watu wenye Ulemavu. Vilevile, Wizara imekamilisha takwimu za watu wenye ulemavu watakaohitaji vifaa vya kujimudu kwa utaratibu utakaoelekezwa. Vifaa hivyo vinajumuisha shimesikio, magongo ya kutembelea, fimbo nyeupe na vifaa vinavyosaidia shingo na miguu yenye matatizo. Mpango huu utachangia juhudi zinazofanywa na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii: Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, inasimamia huduma za uchunguzi wa sampuli za bidhaa za viwandani na mashambani, inasimamia udhibiti wa kemikali ili kulinda afya za wananchi, mazingira na ubora wa bidhaa katika soko la ndani kwa nia ya kukuza biashara na Pato la Taifa. Aidha, Wakala inasimamia huduma za uchunguzi wa sampuli za kijinai na toksikolojia ili kutoa haki na utengamano katika jamii. Wakala ina jukumu la kuhakikisha kuwa, vipimo vya maabara na udhibiti wa kemikali vinakuwa bora na vyenye kuaminika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ilichunguza sampuli za chakula, dawa, kemikali, maji, maji taka na sampuli za makosa ya jinai na toksikolojia. Uchunguzi huu ulichangia katika kulinda afya ya jamii, mazingira na utoaji haki. Aidha, jumla ya sampuli zilizochunguzwa zilikuwa 9,789 ambayo ni sawa na asilimia 84 ya lengo la sampuli 11,625. Kati ya sampuli zilizochunguzwa, 1,954 zilihusu chakula, dawa, kemikali, maji, maji taka na bidhaa mbalimbali za viwandani na 7,835 zilihusu makosa ya jinai na toksikolojia. Vilevile, Wakala iliandaa kanuni ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu Na. 8 ya Mwaka 2009.

Katika mwaka 2009/10, Wakala ilishiriki katika kikosi kazi kilichoundwa na Serikali kuchunguza mauaji ya walemvu wa ngozi na vikongwe katika Kanda ya Ziwa. Aidha, ilisaidia vyombo vya dola kukamilisha majalada ya kesi za watuhumiwa wa ubakaji, ujambazi na matumizi ya dawa za kulevyu ili kuharakisha mwenendo wa kesi mahakamani kusaidia haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wakala ilisimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani. Aidha, ilikagua viwanda na maghala 420, vituo 15 vya mipakani, bandari, viwanja vya ndege, 53 migodi ya dhahabu ya North Mara, Geita, Kahama na maeneo yanayozunguka migodi hiyo. Vilevile, ilichunguza sampuli 175 za uchafuzi wa mazingira na baiolojia. Pia, Wakala ilikamilisha ripoti ya matumizi salama na sahihi ya kemikali (*Strategic Approach to International Chemicals Management - SAICM*) na kupeleka Shirika la Kimataifa la Mafunzo na Utafiti (*United Nation Institute for Training and Research - UNITAR*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wakala iliandaa na kuwasilisha nyaraka katika Shirika la Kusimamia Ithibati la Afrika ya Kusini ili kupata hati ya ithibati ya maabara. Aidha, Wakala iligharamia matengenezo ya mitambo ya kisasa inayotumia kompyuta na kununua vitendanishi vya kutosha kwa ajili ya uchunguzi wa sampuli.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ya Chakula na Dawa, iliendelea kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Mamlaka kwa kushirikiana na TAMISEMI ilifanya ukaguzi wa majengo 1,929 ya biashara za bidhaa ambapo majengo 989 yalikidhi viwango. Majengo yaliyobainika kutokidhi viwango, wamiliki wake walipewa maelekezo ya kuboresha majengo. Aidha, Mamlaka ilitathmini ubora, usalama na ufanisi wa aina 3,692 za bidhaa za vyakula, dawa, vipodozi

na vifaa tiba ambapo bidhaa 1,735 zilisajiliwa na hivyo kuruhusiwa kutumika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka iliidhinisha maombi 4,901 kati ya 5,536 ya kuingiza vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yaliyopokelewa. Aidha, jumla ya shehena 1,305 za dawa, vipodozi, vifaa tiba na malighafi za kutengeneza dawa zenye thamani ya shilingi 52,807,833,041.00 na shehena 858 za chakula zenye thamani ya shilingi 23,312,877,077.00 zilikaguliwa katika vituo mbalimbali vya forodha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka kwa kushirikiana na Polisi wa Kimataifa, Jeshi la Polisi, TAMISEMI, Tume ya Ushindani, Bohari ya Dawa, Mamlaka ya Mapato na Ofisi ya Rais katika zoezi la kubaini dawa zisizokidhi viwango na bandia kwenye soko. Operesheni hiyo ilijulikana kama Operesheni Namba II. Jumla ya maeneo 144 yalikaguliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Mwanza na Shinyanga ambapo aina 3 za dawa bandia zilikamatwa. Dawa hizo zilikuwa Metakelfin (toleo Na. G043A) na *Duo-cotecxin* (toleo Na. 820308 la 2007) na dawa ya kuongeza nguvu za kiume aina ya Cialis. Aidha, operesheni hiyo ilibaini aina 28 za dawa zilizoisha muda wa matumizi, aina 56 za dawa za Serikali katika maduka ya watu binafsi, aina 155 za dawa zisizosajiliwa, aina 73 za dawa moto katika maduka ya dawa baridi na aina 17 za vipodozi vilivyopigwa marufuku. Waliopatikana na dawa hizo walichukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ilichukua sampuli 1,271 za vyakula, dawa na vipodozi na kuzifanyia uchunguzi. Kati ya sampuli hizo, 966 zilikidhi viwango. Hatua mbalimbali zilichukuliwa dhidi ya wamiliki wa bidhaa zisizokidhi viwango ikiwa ni pamoja na kuzuia uagizaji na usambazaji wake hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau ilianza ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na dawa ya kutibu Malaria aina ya *Artemether/Lumefantrine (ALu)* ambapo taarifa 36 kuhusu dawa hiyo zilipokelewa. Pamoja na tathmini ya taarifa hizo imeonesha kuwa dawa hiyo ni salama, hata hivyo Mamlaka inaendelea kufuatilia ubora wake katika soko. Aidha, Mamlaka ilisambaza fomu za njano 3,000 zilizolipiwa gharama za posta katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kukusanya taarifa za madhara ya dawa mbalimbali. Hadi sasa, hakuna tukio baya la athari za dawa lililotolewa taarifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ilifanya ufuatiliaji na uchunguzi wa madhara yatokanayo na chakula. Jumla ya taarifa 483 za wagonjwa waliosadikiwa kupata madhara kutohana na chakula kisicho salama zilipokelewa na kuchambuliwa. Maelekezo yalitolewa kwa Maafisa Afya kuchukua hatua zinazostahili katika kukabiliana na magonjwa yatokanayo na chakula kisicho salama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mamlaka ilihamasisha viongozi wa ngazi za mikoa na wilaya, wamiliki wa maduka ya dawa baridi na watoa dawa juu ya

uanzishwaji wa Maduka ya Dawa Muhimu. Uhamasishaji huo, ulifanyika katika mikoa 8 iliyobaki ambayo ni Dodoma, Kagera, Kigoma, Manyara, Mara, Shinyanga, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ya Chakula na Lishe iliendelea kuratibu utoaji wa matone ya vitamini A na dawa za kutibu minyoo kwa watoto wenyе umri kati ya miezi 6 hadi miaka 5. Katika zoezi lililofanyika mwezi Desemba 2009, jumla ya watoto 6,216,620 kati ya watoto walengwa 6,651,065 (sawa na asilimia 93), walipata matone ya vitamini A.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi iliendelea na utekelezaji wa kuongeza thamani ya zao la muhogo katika Halmashauri za Wilaya za Mtwara, Massasi, Newala na Tandahimba katika Mkoa wa Mtwara. Matokeo ya kazi hiyo yametumika katika kuweka mfumo wa kuboresha nafaka mbalimbali zinazotumika nchini kwa kutumia viini lishe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi iliendelea na uratibu wa kuongeza virutubishi kwenye unga wa ngano, mahindi na mafuta ya kula. Aidha, kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha matayarisho ya Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula. Vilevile, ilishirikiana na wadau kuboresha kanuni, miongozo na viwango vya kuongeza virutubishi kwenye vyakula.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi kwa kushirikiana na wadau ilitoa chakula tiba kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wenyе hali mbaya ya lishe, pamoja na watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira hatarishi katika vituo 8 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo wenyе maambukizi ya Virusi vya UKIMWI katika hospitali na vituo vya afya vya Halmashauri za Wilaya za Hai, Temeke, Bagamoyo, Makete, Magu, Mtwara, Kigoma, Ngara, Kasulu na Kibondo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu inafanya tafiti za afya, tiba na tiba asili ili kuboresha afya na kupunguza maradhi katika jamii kupidia vituo vya utafiti vikubwa 6 vya Mwanza, Tabora, Mbeya, Tanga, Amani (Muheza), Muhimbili na Tukuyu na vidogo 6 vya Hydom, Gonja, Kilosa, Handeni, Korogwe, Ngongongare na Aman Hills. Mpaka sasa Taasisi ina watafiti 26 wa Shahada ya Uduktari wa Falsafa, 73 shahada ya uzamili na 31 wana shahada. Aidha, inakuza na kutoa fursa ya mafunzo ya utafiti kwa watafiti wa Kitanzania ili kuwajengea uwezo wa kufanya tafiti za kisayansi. Vilevile, Taasisi ina jukumu la kufuatilia, kudhibiti na kuratibu tafiti za afya zinazofanyika nchini na kutathmini matokeo ya tafiti hizo na kuyasambaza kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ilifanikisha uzinduzi wa Jengo la Makao Makuu. Jengo hili lilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 16 Desemba 2009. Jengo hili lina maabara ya Taifa ya kupima vimelea vya mafua makali ya aina zote (nguruwe na ndege), homa ya bonde la ufa na homa ya *dengue*. Mafanikio haya yataiwezesha nchi kufanya uchunguzi na utafiti

wa magonjwa ya milipuko badala ya kupeleka nje ya nchi kwa uchunguzi kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, Maabara hii itadhibiti ubora na kuendesha programu za mafunzo ya ufuatiliaji wa magonjwa ya muda mrefu na muda mfupi. Mwaka jana Taasisi ilidahili wanafunzi 10 na mwaka huu 11 kwa mafunzo ya muda mrefu na inaendesha kozi za muda mfupi kwa wanafunzi 15 katika kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imefanya tafiti kwenye Hospitali za Mikoa na Kanda kwa Mikoa ya Arusha na Dodoma na Hospitali Maalumu za Mbeya na Bugando. Lengo la tafiti hizi ilikuwa kupata tiba sahihi kwa wagonjwa wanaokuja kutibiwa hospitalini. Tafiti hizi zimesaidia kwa kiasi kikubwa wataalamu wa afya kuweza kutoa tiba sahihi kwa wagonjwa wanaokuja hospitalini. Aidha, kwa kuthamini matokeo mazuri ya tafiti hizi, Taasisi imeandaa rasimu ya utafiti na pia mkakati kazi utakaoteklezwa kwa kushirikisha hospitali za mikoa na kanda kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi ya Ustawi wa Jamii iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kufundisha masomo katika taaluma ya ustawi wa jamii, mahusiano kazini na rasilimali watu. Aidha, ilifanya utafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala yahusuyo Ustawi wa Jamii. Vilevile, Taasisi iliwasilisha ombi la kupata ridhaa ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu ili kuanzisha masomo ya Shahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi iliongeza idadi ya wanafunzi wa masomo ya ustawi wa jamii kutoka wanafunzi 489 mwaka 2008/09 hadi kufikia 510 mwaka 2009/10. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliodahiliwa ilipungua kutoka wanafunzi 1,260 hadi 1,080. Upungufu huo ulitokana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu kusitisha udahili wa wanafunzi wa Shahada ya kwanza ya rasilimali watu, kwa sababu ya upungufu wa wahadhiri na miundombinu isiyokidhi viwango vya Baraza, kama vile madarasa na maktaba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Taasisi iliendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa na kukarabati madarasa na ofisi za watumishi. Aidha, inaendelea kukamilisha utaratibu wa upimaji ardhi wa eneo la Msoga, Chalinze ili kupata hati. Vilevile, Taasisi iliendesha kozi za muda mfupi kwa Wasaidizi Ustawi wa Jamii katika Mikoa ya Dodoma na Mwanza juu ya usuluhishi na uamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 260,599,867,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 13,029,173,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 247,570,694,000.00 zilitoka kwa Taasisi za Kimataifa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya na wale walioko nje ya Mfuko. Hadi kufikia Juni 2010, kiasi cha shilingi 170,401,477,371.47 kilipokelewa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 9,529,192,000.00 kilitolewa na Serikali ya Tanzania. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 73 ya fedha za ndani shilingi 13,029,173,000.00 iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha kutoka

kwa Wadau wa Maendeleo wanaosaidia Sekta ya Afya zilizopokelewa ni shilingi 160,872,285,371.47. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 65 ya shilingi 247,570,694,000.00 zilizoahidiwa na Wadau hao. Kiasi cha shilingi 170,401,477,371.47 zilizopokelewa zilitumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilianza ujenzi wa Hospitali ya Upasuaji wa Moyo. Ujenzi wa Hospitali hiyo, ulizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 31 Machi, 2010. Aidha, Wizara ilikamilisha uanzishwaji wa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenyewe matatizo ya figo, kwa kununua mashine ya kusafisha maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilianza ujenzi wa uzio wa kituo cha utengamao wa magonjwa ya Ubongo na Utu wa Mgongo cha Taasisi ya Mifupa Muhimbili kilichopo Mbweni. Aidha, wataalam walifanya ziara ya mafunzo katika nchi za India na Ethiopia ili kujifunza uendeshaji wa aina ya kituo kitakachojengwa. Taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilinunua vifaa vya upasuaji wa moyo na gari la wagonjwa kwa ajili ya Hospitali ya KCMC. Aidha, ilinunua vifaa vya mionzi na mzabuni wa kujenga wodi, chumba cha upasuaji, chumba cha mionzi, ofisi na madarasa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ameteuliwa. Vilevile, Wizara ilikamilisha ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dar es Salaam. Pia, Wizara ilinunua magari ya wagonjwa kwa ajili ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Taasisi ya Saratani Ocean Road.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilikamilisha michoro na kuanza ujenzi wa uzio katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma ilikamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo cha Damu Salama, Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, katika mkakati wa kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi, Wizara ilikamilisha taratibu za ununuzi wa pikipiki maalum 400 kwa ajili ya wajawazito wanapopata rufaa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilinunua radio call 40 na magari 12 ya kubebaa wagonjwa na kusambaza katika Halmashauri za Karagwe, Kasulu, Kibondo, Kigoma, Nachingwea, Kisarawe, Liwale, Ngara, Rufiji, Chunya, Ileje na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, iliendelea na ukarabati wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya katika Mikoa ya Mara, Tabora na Mtwara. Aidha, katika ukarabati huo, majengo ya upasuaji wa wanawake wajawazito katika vituo vya afya na hospitali za wilaya pamoa na nyumba za kuishi watumishi katika vituo vya afya zinajengwa. Jumla ya zahanati 78 vituo vya afya 19 na hospitali za wilaya 7 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi na ukarabati. Katika baadhi ya wilaya, utekelezaji umefikia asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Hospitali za Apollo, India, imekamilisha maandalizi ya awali ya ujenzi wa hospitali ya kisasa yenye huduma zote za ubingwa wa juu (*super speciality*) kwa kushirikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao wametoa ardhi na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) utagharamia ujenzi na vifaa. Aidha, Hospitali za Apollo zitatoa utaalamu na uendeshaji. Pia, mafunzo ya utaalamu wa juu (*super speciality*) na uuguzi yatatolewa katika hospitali hiyo. Taratibu zote za maandalizi zinaendelea vizuri na ujenzi utaanza Januari 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliimarisha utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Mtoto hususan utoaji wa haki kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kwa kukamilisha ujenzi wa mahabusu ya watoto Mtwara na kuboresha mahabusu ya watoto ya Dar es Salaam. Aidha, Wizara ilikamilisha ukarabati wa vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu vya Singida, Luanzari (Tabora) na makazi ya wazee Sukamahela (Singida). Vilevile, Wizara ilikamilisha mikataba ya ukarabati wa mahabusu ya watoto Mbeya, Kituo cha mafunzo ya walezi wa watoto wadogo Kisangara (Mwanga) na mikataba ya ujenzi wa ofisi ya Idara, Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliboresha vyuo vya mafunzo ya afya na ustawi wa jamii kwa kufanya upanuzi na ukarabati, kuwezesha vyuo hivyo kudahili wanafunzi wengi ili kukidhi malengo yaliyowekwa. Upanuzi na ukarabati ulifanyika katika Vyuo vya Uuguzi vya Njombe, Korogwe, Tanga, Tukuyu, Mbulu, Mirembe, Kondoa, Tarime, Nzega na Mbozi. Aidha, ilifanya ukarabati na upanuzi katika Chuo cha CEDHA, Chuo cha Vector Control Muheza, Chuo cha Afya ya Msingi Iringa, Chuo cha Fundi Sanifu Maabara Singida, Chuo cha Ufundı cha Afya Kagemu, Vyuo vya Afya ya Mazingira Tanga na Ngudu na Chuo cha Madaktari Wasaidizi Mbeya. Vilevile, Wizara ilifanya ukarabati katika vyuo vitatu vilivyokuwa vimefungwa kwa muda mrefu vya Kibondo, Nachingwea na Tunduru.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea na uraghibishi wa jamii kuhusu Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III (2009 – 2015), MMAM (2007 – 2017) na miongozo mbalimbali kulingana na mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya afya kupitia vipindi vya afya. Vipindi hivyo, vilitangazwa kupitia radio na televisheni za TBC kila wiki. Aidha, Wizara iliandaa vipindi na matangazo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa mabadiliko na hali halisi ya utoaji wa huduma za afya katika jamii, hospitali za wilaya na mikoa. Vilevile, Wizara iliandaa kitita maandiko cha uraghibishi wa Sera ya Afya, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III na MMAM. Kitita hicho, kitawezesha kanda za mafunzo, mikoa, halmashauri na vituo vya kutolea huduma za afya, kutafsiri Sera ya Afya 2007 katika mikakati na miongozo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliendelea kusimamia na kufuatilia upangaji na utekelezaji wa mipango ya afya katika Halmashauri. Aidha, Wizara iliendelea kutoa ushauri wa kitalaamu na kiufundi katika maeneo ya utekelezaji wa mkakati wa malipo kwa watoa huduma kwa utendaji bora wa kazi. Vilevile, Wizara kwa

kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilipitia Mwongozo wa Upangaji Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri kwa madhumuni ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi. Lengo ni kuhakikisha kuwa Mipango ya Afya ya Halmashauri inakuwa shirikishi, inayotokana na mipango ya zahanati na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uliingiza Waheshimiwa Madiwani 3,519 na Wanachama wastaafu 519. Wizara inawahimiza na kuwataka wanachama wastaafu 27,306 waliochangia na kustaafu kuanzia mwaka 2001/02 hadi sasa na wale watakaostaafu baadaye, kurudisha vitambulisho vya awali ili wapewe vitambulisho vipya. Hatua hiyo itawawezesha wanachama hao kupata huduma za afya na wenza wao bila malipo, kwa maisha yao yote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Mfuko ultengeneza na kusambaza Atlasi 500 kwenye CD, ramani kubwa 100 na nakala 100 za vitabu vinavyoonesha mtandao wa vituo vya matibabu nchi nzima. Wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa mikoa walipewa Atlasi hizo. Lengo ni kutumia Atlasi hizo kuainisha maeneo yasiyo na vituo vya kutolea huduma za afya ili wachukue hatua za ujenzi wa vituo hivyo kutelekeza azma ya Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM 2007-2017) ya kila Kijiji kuwa na Zahanati, Kata kuwa na Kituo cha Afya na Wilaya kuwa na Hospitali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kuititia Mfuko ilitoa mafunzo kwa wamiliki wa maduka ya dawa baridi katika kata 373, kuhusu Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu. Aidha, ilihamasisha jumla ya washiriki 44,792 katika kata 1,217 juu ya utaratibu wa elimu ya Kata-kwa-Kata ulioanza mwaka 2007. Vilevile, Mfuko ulihamasisha halmashauri kutumia mapato yanayotokana na malipo ya Mfuko kwa ajili ya kununua dawa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Na. 8 ya Mwaka 1999 (Sura 395 Toleo la Mwaka 2002). Lengo la marekebisho hayo lilikuwa ni kuwezesha uwekezaji katika Sekta ya Afya. Aidha, marekebisho hayo yamevezesha kuingiza Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji katika Mfuko. Wanachama hao wataanza kunufaika na huduma za Mfuko huo kuanzia mwaka wa fedha wa 2010/11. Vilevile, Wizara kuititia Mfuko ilishauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kufungua Ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Zanzibar kwa ajili ya kuhudumia wanachama wa Serikali ya Muungano. Makubaliano yakiffikiwa yatawezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzisha Bima ya Afya. Pia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekasimiwa madaraka ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwa lengo la kuongeza idadi ya wanachama na kupunguza malipo ya papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara kuititia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilikamilisha mchakato wa kuanzisha chombo cha usimamizi wa huduma za bima ya afya nchini (*Regulatory Mechanism for Health Insurance*). Lengo la chombo hicho ni kuwalinda watumiaji wa huduma za matibabu za Mifuko ya Bima ya Afya dhidi ya kutozwa fedha ambazo hazilingani na thamani ya huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/11, Wizara inaomba kiasi cha shilingi 229,978,968,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 124,220,323,000.00 zinaombwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Taasisi zilizo chini yake. Kiasi cha shilingi 105,758,645,000.00 kinaombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizi zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kutoa ajira kwa watumishi wa Kada mbalimbali. Wizara itaa jiri wataalam 160 na kuwapandisha vyeo watumishi 576. Aidha, Wizara itawapangia wataalam wapatao 7,000 wa kada za afya katika mamlaka mbalimbali za ajira. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wake wa kuhifadhia kumbukumbu. Pia, Wizara itatoa mafunzo ya maadili kwa watumishi wake wanaotoa huduma katika hospitali na pia itaandaa mkakati wa kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kushirikiana na watu binafsi wanaotoa huduma za ulinzi, usafi na chakula ili kuhakikisha huduma hizo zinatolewa kwa viwango. Aidha, Wizara itabinafsisha utoaji wa huduma za usafi na ulinzi katika vyuo viwili vilivyo chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake na itanza kutekeleza muundo mpya wa kada za Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa takwimu za afya na ustawi wa jamii, ufuutiliaji na tathmini ya huduma za afya na ustawi wa jamii, kwa kuhakikisha upatikanaji wa zana za kukusanyia na kuchanganua takwimu katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau, itaendeleza mpango wa kuweka programu ya kompyuta inayojulikana kama *District Health Information Software – DHIS*. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za maradhi na vifo vinavyotokea katika ngazi ya jamii. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kufanya utafiti wa kuimarisha huduma (*Operational Research*) kwa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa na Halmashauri kuziwezesha kutoa maamuzi ya kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaboresha Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA), kwa kuanzia na wilaya 27. Lengo ni kupata takwimu na vigezo mbalimbali katika ngazi ya Taifa katika muda mfupi. Matokeo ya maboresho katika halmashauri hizo, yatawezesha kueneza Mfumo huo nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano – TEKNOHAMA: Katika mwaka 2010/11, Wizara itaboresha na kuimarisha mtandao wake wa mawasiliano wa intaneti ili kufanikisha utoaji na upokeaji wa taarifa kwa wakati. Aidha, Wizara itakamilisha Mpango Mkakati wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea na kuratibu uundwaji wa Bodi za Afya za Halmashauri katika Halmashauri zote na kutoa mafunzo kwa Bodi hizo ili kuziwezesha kufanya kazi zake kwa mujibu wa Hati Rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kutekeleza Sera ya Serikali ya kuboresha Mfumo wa Utunzaji kumbukumbu za watumishi, ununuzi, mikataba na malipo. Aidha, itaendelea kuweka mitandao ya malipo kwa miradi ya Wizara na Mabaraza ya kitaaluma. Vilevile, Wizara itaanza kutumia mifumo ya kompyuta ya kukusanya fedha katika hospitali za umma ili kupunguza gharama za uchapishaji wa risiti. Hatua hii italeta ufanisi katika ufuutiliaji wa tija na kuondoa hoja za upungufu wa nyaraka na ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itanunua pikipiki 400 kwa ajili ya kubebia wagonjwa ili kutekeleza Mpango wa Afya ya Mama na Mtoto. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itanunua mtambo wa kujenga Zahanati kwa gharama nafuu (*Ultimate Building Machine – UBM*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa fedha, ununuzi na usalama wa mali za Serikali kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyopo. Aidha, Wizara itaendelea kufuutilia miradi ya ujenzi wa majengo yake mbalimbali na kandarasi nyingine kuhakikisha kuwa matokeo ya kazi hizo yanalingana na rasilimali zilizotumika. Vilevile, Wizara itaendelea kufuutilia usambazaji na matumizi ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotolewa na Bohari ya Dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari vikiwemo magazeti, radio na televisheni kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi. Aidha, Wizara itatoa taarifa za magonjwa ya milipuko kuitia magazeti na televisheni kila wiki. Vilevile, Wizara itaandaa vipindi maalum kwa ajili ya wananchi ili waweze kuelewa masuala yanayohusu huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Sheria za Kusimamia Utoaji wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii: Katika mwaka 2010/11, Wizara itakamilisha uandaaji wa Kanuni chini ya Sheria mbalimbali zinazosimamia huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Sheria hizo zinajumuisha Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI na UKIMWI Na. 2 ya Mwaka 2008; Sheria ya Kusimamia Vinasaba vya Binadamu ya Mwaka 2009; Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009; Sheria ya Wataalamu wa Radiolojia Na. 21 ya Mwaka 2007; Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2008; Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008; Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 na Sheria ya Wauguzi na Wakunga ya Mwaka 2010. Aidha, Wizara itakamilisha uandaaji wa mapendekezo ya Sheria ya Huduma za Afya Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itakamilisha mapendekezo ya Miswada ya kutunga Sheria za Madaktari na Madaktari wa Meno, Famasi, Taaluma ya

Kemia na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaanzisha mchakato wa kuainisha aina ya chombo kitakachosimamia Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa Mamlaka au kubakia kuwa Wakala. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za kumpata mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuandaa *Health Legislation Implementation Support Plan*, Mpango ambao utaainisha utekelezaji wa Sheria mbalimbali chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali itaratibu na kusimamia huduma za Uboreshaji wa Afya, Kinga na Tiba ya magonjwa na Utengamao ikijumuisha na mafunzo na uendelezaji wa wataalamu wa afya katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Aidha, Ofisi kwa kuititia Wakala na Taasisi zake itasimamia ubora na usalama wa dawa, vifaa, vifaa tiba, kemikali, viini lishe, utafiti, maadili na ubora wa viwango vya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi, kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo ilioandaliwa na Wizara. Vilevile, Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali inasimamia na kuimarisha huduma za uuguzi na ukunga, ukaguzi na ubora wa huduma za afya za dharura.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma vilivyo chini ya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii, itasimamia maadili ya wataalamu wa afya kwa kutumia mabaraza yao. Aidha, Ofisi itasimamia viwango vya ubora wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayoandaliwa na Wizara pamoja na kuzingatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Vilevile, Ofisi itasimamia na kuimarisha huduma za uuguzi na ukunga, ukaguzi na ubora wa huduma za afya za dharura na mabaraza ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itafuutilia utekelezaji wa Mwongozo wa Uuguzi wa kutoa huduma za msingi kwa wagonjwa na Mwongozo wa Viwango vya Ubora wa huduma za uuguzi zinazotolewa kwa jamii katika hospitali za mikoa na rufaa. Aidha, Wizara itachapisha nakala 7,000 za miongozo hiyo na kusambaza kwa wadau nchi nzima. Vilevile, Wizara itawajengea uwezo viongozi wa uuguzi na ukunga nchini kuhusu huduma za msingi kwa wagonjwa na ubora wa huduma hizo ikiwa ni pamoja na viongozi wa wilaya, mikoa na hospitali zote za rufaa. Wizara pia, itaandaa Mpango Mkakati wa Uuguzi wa miaka mitano 2010-2015 wa utekelezaji wa kazi za uuguzi ili kuboresha huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itafanya ukaguzi wa hospitali 80 za umma zikiwemo ya taifa, rufaa maalum, rufaa za mikoa na wilaya. Aidha, itatoa mafunzo kwa watumishi 1,500 kutoka katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimibili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Mirembe na hospitali zote za Wilaya katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Pwani ambazo hazijapata mafunzo. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wakufunzi 60 kutoka ngazi ya Taifa, vyuo vya mafunzo vya kanda na wajumbe wapya katika Timu za Uendeshaji za Mikoa. Mafunzo hayo, yatahusu kukinga na kudhibiti maambukizi katika utoaji wa huduma za afya, uboreshaji huduma na usimamizi shirikishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa, itaendelea kukabiliana na majanga nchini. Aidha, Timu za Dharura za Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Mbeya na Manyara zitapewa mafunzo ili kuziwezesha kukabiliana na majanga na maafa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa maazimio na kushiriki katika mikutano ya jumuiya za Afrika. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu na kushirikiana na nchi marafiki kupitia tume za pamoja kwa kubadilishana uzoefu na teknolojia ili kuimarisha huduma za afya na ustawi wa jamii nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaandaa kanuni za nidhamu kwa wanataluma pamoja na utaratibu wa kuendesha mashauri ya nidhamu ya Baraza la Madaktari. Aidha, Wizara itaandaa na kuchapisha miongozo mbalimbali na kusambaza kwa wadau. Vilevile, Wizara itafanya sensa ya Madaktari wote nchini ili kupata idadi yao halisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itafuutilia utekelezaji wa Mpango wa Kuimarisha Elimu ya Maadili. Aidha, Wizara itaanzisha tovuti ya Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na mawasiliano. Vilevile, Wizara itaanzisha jarida la wauguzi ili kutoa elimu kwa wanataluma na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Baraza la Famasi kwa kushirikiana na wadau litaandaa miongozo ya usimamizi wa taaluma ya Famasi. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Kamisheni ya Vyuo Vikuu, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na wadau, litaandaa mitaala kwa ajili ya vyuo vya taaluma ya Famasi. Vilevile, Baraza litakagua vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa mafunzo kwa vitendo kwa Wafamasia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itakamilisha zoezi la kutoa vyeti vipyta kwa wasajiliwa wote wa Baraza la Maabara kwa mujibu wa Sheria Na. 22 ya Mwaka 2007 ya Wataalamu wa Maabara. Aidha, Wizara kupitia Baraza itafanya ukaguzi wa Vyuo vya kufundisha Wataalamu wa Maabara pamoja na uteuzi wa Wasimamizi ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Baraza la Radiolojia litasajili Wataalamu wa Radiolojia kwa mujibu wa Sheria ya Radiolojia Na. 21 ya Mwaka 2007. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mionzi itafanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za radiolojia na vyuo vya taaluma ya radiolojia kwa lengo la kuboresha huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaandaa Mpango Mkakati na Mwongozo wa Usimamizi na Ulaguzi wa Wataalamu wa Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona, kwa ajili ya utekelezaji na utoaji wa huduma za optometria. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa Wataalamu wa Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona juu ya Sheria Na. 12

ya Mwaka 2007 na Kanuni zake. Vilevile, Wizara itafanya ukaguzi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi ili kutathmini viwango vya utoaji huduma za optometria nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Baraza la Wataalamu wa Mazingira litapitia na kurekebisha Mwongozo wa Mafunzo kwa vitendo kwa Maafisa Afya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Maadili ya Utumishi wa Umma, itatoa mafunzo ya maadili kwa Maafisa Afya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itasajili waganga wa tiba asili na tiba mbadala, wakunga wa tiba asili, wasaidizi wao na vituo vya tiba asili na tiba mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kusajili vituo binafsi vya kutolea huduma za afya. Aidha, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi itafanya ukaguzi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya zenyenye ubora na viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itatoa elimu juu ya magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya kujikinga na magonjwa mapya yanayojitokeza kama vile Ebola, Marburg, Homa ya Bonde la Ufa na Homa ya Mafua Makali ya Nguruwe. Aidha, Wizara itatoa chanjo za kuzuia magonjwa ya Homa ya Uti wa Mgongo na ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa katika mikoa na wilaya ili kukabiliana na magonjwa hayo.

Vilevile, Wizara itatoa dawa, vifaa na vifaa tiba ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko nchini ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa Kipindupindu, Homa ya Matumbo na magonjwa ya Kuhara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kudhibiti Malaria kwa kunyonyizia dawa za kuua mbu wanaosababisha Malaria katika kuta ndani ya nyumba katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera. Aidha, Wizara itasambaza vyandarua viwili kwa kila kaya bila malipo katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya vyandarua milioni 14.6 vyenye viuatilifu vitasambazwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itawezesha upatikanaji wa dawa mseto ya Malaria ya ALu katika sekta binafsi kwa bei nafuu. Pia, itaboresha upimaji wa vimelea vya Malaria kwa kutumia kipimo cha haraka katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma: Katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa dawa za kutibu Kifua Kikuu zikiwemo za Kifua Kikuu Sugu zinapatikana kwa kiwango cha kutosha na kutolewa kwa wagonjwa bila malipo. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha maabara za Kifua Kikuu kwa kutumia teknolojia mpya na ya kisasa ili kuongeza kasi ya kutambua maambukizi ya Kifua Kikuu. Vilevile, itapanua huduma za maabara ili kuweza kuhudumia wagonjwa wengi kwa wakati mmoja. Pia, Wizara itatoa mafunzo juu ya Kifua Kikuu Sugu kwa

wafanyakazi wa sekta ya afya katika ngazi zote ili kudhibiti na kutoa huduma sahihi na bora kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaongeza idadi ya vituo vya binafsi ili kutoa huduma za tiba ya Kifua Kikuu. Vituo hivyo, vitapewa dawa na vifaa vya maabara ili kuviwezesha kutoa huduma sahihi na bora. Aidha, Wizara itatoa mafunzo juu ya udhibiti wa Kifua Kikuu kwa watoa huduma kutoka taasisi za binafsi za kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI, Wizara itafanya majaribio ya kuzuia Kifua Kikuu kwa kutibu uambukizo wa awali wa ugonjwa huo kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) katika hospitali 11 za wilaya. Lengo ni kuzuia vifo vitokanavyo na ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa watu wanaoishi na VVU. Taarifa ya matokeo ya majaribio hayo, yatawezesha Wizara kutoa maamuzi sahihi ya tiba ya Kifua Kikuu kwa watu wanaoishi na VVU. Aidha, Wizara itatoa mwongozo mpya wa kuchunguza na kutibu Kifua Kikuu na maambukizo mseto ya Kifua Kikuu na UKIMWI kwa watoto. Lengo ni kuboresha huduma za ugunduzi na matibabu ya Kifua Kikuu kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara itanunua na kusambaza hadubini aina ya *Light Emetting Diodes (LED)* nchi nzima kwa ajili ya kuboresha huduma za uchuguzi wa maabara wa Kifua Kikuu. Aidha, Wizara itanza uchunguzi wa uoteshaji wa makohozi (*liquid culture*) katika Hospitali za Rufaa za Muhimbili na Mbeya, ili kupunguza muda wa kupatikana kwa majibu kutoka wiki 4 hadi wiki 1.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufanya kampeni za kutambua wagonjwa wa Ukoma kwenye wilaya ambazo bado zina idadi kubwa ya wagonjwa hao. Aidha, Wizara itaendelea kutoa dawa za kutibu ugonjwa wa Ukoma bila malipo kwa wagonjwa wote watakaogunduliwa.

Huduma za utengamao zitaendelea kutolewa kwa watu wenye ulemavu utokanao na ukoma kwa kuwapa viatu maalumu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendeleza mpango wa kitaifa wa kupanua huduma za tiba kwa watu wanaoishi na VVU. Wagonjwa wanaopata dawa za UKIMWI idadi yao itaongezeka kutoka 322,783 hadi kufikia 440,000. Aidha, idadi ya vituo vinavyotoa huduma hiyo vitaongezeka kutoka 909 hadi kufikia 1,400.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itahamasisha wananchi kujikinga na magonjwa ya macho yanayozuulika hususan katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Ruvuma na Singida ambayo tatizo hili ni kubwa zaidi kuliko mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itanunua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango vikiwemo vidonge, sindano, vipandikizi, kitanzu na kondomu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kinga na Udhibiti wa Saratani ya Shingo ya Kizazi. Mpango Mkakati huo, unajumuisha kupanua huduma ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na kutoa mafunzo kwa watoa huduma. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka nje ya nchi itaandaa mpango wa utekelezaji wa utoaji wa chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi. Majoribio ya utoaji wa chanjo hiyo yanatarajiwa kufanyika Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaanza kununua na kusambaza vifaa vya uzazi (*delivery pack*) kwa wajawazito. Kwa kuanzia, itanunua vifaa hivyo kutosheleza mahitaji ya wajawazito katika Mkoa wa Dodoma yanayokadiriwa kuwa 153,000. Lengo ni kila mjamzito kuwa na vifaa muhimu vya kujifungulia na hivyo, kuongeza idadi ya wajawazito wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau hususan mpango wa pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa, itafanya uchunguzi wa kubaini upungufu katika utoaji wa huduma ya uzazi salama katika mikoa 7 ya Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Mbeya, Rukwa, Pwani na Shinyanga. Aidha, Wizara itaanzisha rejista ya wazazi ngazi ya jamii ili kuwezesha ukusanyaji na ufuatilaji wa karibu wa taarifa za matukio juu ya uzazi na vifo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo ya kumhudumia mtoto mganjwa sana, kwa wahudumu wa afya na kufanya tathmini ya ubora wa huduma za afya kwa watoto ili kupunguza vifo vinavyotokea katika vituo vya afya na hospitali katika mikoa 9.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma ya kuzuia maambuki ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutoka vituo 3,626 hadi 4,200. Aidha, itaongeza idadi ya vituo vya utambuzi wa mapema wa maambukizi ya VVU kwa watoto waliozaliwa na akina mama wenye maambukizi ya VVU kutoka 730 hadi 1,200. Lengo ni kuhakikisha kuwa, hakuna mtoto atakayezaliwa na maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kununua chanjo na vifaa. Aidha, Wizara itaendelea kufanya usimamizi elekezi kwa mikoa mingine 16 iliyobaki pamoja na kurudia mikoa iliyofanyiwa usimamizi ili kupima maendeleo. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo ya huduma za chanjo kwa watumishi 185 ili kuwapa ujuzi utakaowawezesha kutoa huduma bora zaidi. Pia, Wizara itaongeza huduma za mnyororo baridi (*cold chain*) katika Bohari ya Dawa na Bohari za Mikoa kwa ajili ya kuhifadhi chanjo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kutoa kipaumbele katika kuhamasisha jamii juu ya afya shulenii, huduma ya kwanzu, uchunguzi wa afya za

wanafunzi na kupambana na ongezeko la mimba kwa wasichana shulenii. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundu pamoja na Halmashauri, itafuatilia utekelezaji wa Mpango wa kuimarisha usafi mashulenii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 500 katika sekta ya afya wanaoishi na VVU. Aidha, Wizara itaelimisha wafanyakazi juu ya kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI katika Kanda za Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Magharibi na Kaskazini yanayotokana na kugusa damu au giligili mwili zenyenye maambukizi ya VVU. Vilevile, Wizara itasambaza miongozo inayohusu kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi katika mikoa na wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuboresha Usafi na Afya ya Mazingira na kukamilisha Sera ya Taifa ya Chakula Salama. Aidha, itaandaa Mwongozo wa Usafi shulenii na Mpango Mkakati wa Maji Salama ngazi ya kaya. Vilevile, itaratibu mashindano ya afya na usafi wa mazingira katika Halmashauri zote nchini, ili kuinua kiwango cha usafi na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na milipuko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itatoa mafunzo kwa waratibu wa usafi katika Halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji nchini juu ya kupanga na kukadiria gharama za uendeshaji wa huduma za udhibiti taka kwa lengo la kuinua kiwango cha usafi. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa waratibu ngazi ya mkoa juu ya madhara yatokanayo na matumizi na utupaji wa taka za kemikali.

Mheshimiwa Spika, Afya Bandarini, Mipakani na Viwanja vya Ndege: Katika mwaka 2010/11, Wizara itadhibiti magonjwa yanayoenea kimataifa kwa kukagua wasafiri kutoka nje ya nchi pamoja na bidhaa zinazoingizwa nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha afya bandarini, mipakani na viwanja vya ndege kwa kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwawezesha kutambua magonjwa ya kuambukiza na kuwapa vitendea kazi ili kujikinga na madhara ya kiafya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuratibu na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kubadili tabia na mienendo hatarishi kwa afya. Lengo ni kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Aidha, Wizara itakamilisha Mpango Mkakati wa Kuboresha na Kudumisha Afya (2010 – 2015). Vilevile, itaandaa Mwongozo wa Usimamizi na Uhakiki wa Ubora wa Elimu ya Afya na Mpango Mkakati wa Mawasiliano ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali wa afya katika mikoa na wilaya, juu ya kupambana na magonjwa ya milipuko na majanga. Aidha, Wizara itasambaza vifaa kinga pamoja na dawa ili kujiweka tayari kukabiliiana na magonjwa ya milipuko na majanga. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaanzisha vituo vingine 8 katika Hospitali za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa ajili ya ufuatiliaji wa ugonjwa wa mafua makali (*influenza*).

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele: Katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea na zoezi la ugawaji wa dawa kwa ajili ya kudhibiti magonjwa yasiyopewa kipaumbele kwa mikoa mitano ya Morogoro, Ruvuma, Mbeya, Tanga na Iringa ambayo imeathirika zaidi na magonjwa haya kama vile usubi, matende na ngiri maji. Aidha, Wizara itazindua na kutekeleza zoezi la ugawaji wa dawa kwa ajili ya magonjwa hayo kwa mikoa mitano zaidi. Mikoa hiyo ni Dodoma, Rukwa, Tabora, Singida na Manyara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Hospitali za Rufaa Maalum (*Super Speciality Hospitals*) ili ziweze kutoa huduma zisizopatikana nchini kwa lengo la kupunguza ghamama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendeleza ujenzi wa hospitali ya kisasa ya upasuaji wa moyo katika hospitali ya Taifa Muhimbili kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Vilevile, Wizara itapeleka wataalam zaidi nchini India ili kupata ujuzi zaidi juu ya upasuaji wa moyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Serikali itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini (Mtwara). Aidha, Wizara itapanga wataalam hususan, Madaktari Bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kuziwezesha kutoa huduma za rufaa. Vilevile, Wizara itaanizisha huduma ya tiba ya saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando, Kanda ya Ziwa. Pia, Wizara itasaidia Hospitali hiyo kuanzisha huduma za upasuaji wa moyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itanunua na kusambaza vifaa vya tiba ya meno katika vituo vyote vyenye kliniki za meno. Aidha, itanunua mashine za X-ray kwa mikoa 8 ambayo ni Arusha, Dar es Salaam (Amana), Iringa, Kagera, Mbeya, Morogoro, Pwani na Shinyanga. Vilevile, itafanya matengenezo kinga ya vifaa vya tiba ya meno katika Hospitali za Bombo (Tanga), Mawenzi (Kilimanjaro), Mt. Meru (Arusha) na Kituo cha Afya Sabasaba (Morogoro).

Mheshimiwa Spika, Hospitali Maalumu *Super speciality hospitals*): Hospitali ya Taifa Muhimbili katika mwaka 2010/11, itaongeza idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo kutoka 183 hadi 340. Aidha, itaanizisha huduma za upasuaji kuititia tundu dogo (*Laparascopic surgery*) baada ya mafunzo ya madaktari kukamilika. Hospitali, itaendeleza huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenyewe matatizo ya figo. Vilevile, itaboresha uchunguzi wa magonjwa na tiba kwa wagonjwa waliopata rufaa kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuimarisha sehemu ya kutoa huduma za dharura kwa wagonjwa. Pia, Hospitali itaanizisha matibabu ya ugumba kwa kufanya *In Vitro Fertilization*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Hospitali ya Bugando itapanua huduma za upasuaji wa moyo hadi kufikia 150 kwa mwaka. Aidha, itapokea madaktari 44, wafamasia 6 na wauguzi 2 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Hospitali itaongeza huduma ya tiba ya watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kutoka 14,000 hadi 25,000.

Vilevile, Hospitali itaendeleza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa saratani na itakarabati jiko na sehemu ya ufuaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Hospitali itakarabati vyumba vya upasuaji na mfumo wa maji safi na maji taka. Aidha, itajenga mtambo wa kuchoma taka, kukarabati na kupaka majengo rangi. Vilevile, itanunua *lift* na majokofu ya kuhifadhi maiti na kusimika mtambo wa oksijeni. Pia, itanunua vifaa vya upasuaji mkubwa wa moyo vikiwemo mashine za kupumulia na kufuutilia mwenendo wa hali ya mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Hospitali ya KCMC itaendelea kutoa huduma za uchunguzi, matibabu, utafiti na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa kada mbalimbali. Aidha, Hospitali itaendeleza huduma ya upasuaji mkubwa wa moyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Hospitali ya Rufaa Mbeya itaendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa wanaopata rufaa kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Aidha, itaendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa madaktari, wafamasia na wauguzi. Vilevile, Hospitali itaendelea na uhamasishaji na kutoa huduma ya tohara kwa wanaume wapatao 10,000 ili kupunguza kasi ya maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Mifupa Muhimbili - MOI itaendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wanaopata rufaa kutoka sehemu mbalimbali nchini. Aidha, itatoa huduma za tiba na utengamao kwa majeruhi wa ajali na upasuaji wa kuweka viango bandia vya nyonga na magoti. Vilevile, itaendelea na upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo. Pia, Hospitali itaajiri wafanyakazi wapya 39 wakiwemo madaktari 15 wa fani za tiba ya mishipa ya fahamu na mifupa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Saratani Ocean Road itaendelea kutoa huduma za kinga, uchunguzi na matibabu ya Saratani. Aidha, itatoa mafunzo ya uchunguzi wa Saratani kwa wataalamu wa afya katika Hospitali za Mikoa ya Arusha, Kagera, Mbeya, Shinyanga, Singida, Rukwa na Tabora ili kuweza kubaini saratani katika hatua za awali na kutoa rufaa mapema. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na wadau, itaboresha huduma ya tiba shufaa na kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya kuhusu tiba hiyo katika Hospitali za Dodoma, Kagera, Kigoma na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itaelimisha wadau na wananchi kwa ujumla kuititia vyombo mbalimbali vya habari, tovuti, warsha na semina kuhusu kinga na matibabu ya saratani. Aidha, Taasisi itaendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi kuendeleza mpango wa kudhibiti saratani ya shingo ya kizazi kwa kuanzisha matumizi ya chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi iitwayo HPV hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itaendelea na ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kulaza wagonjwa. Aidha, itaimarisha matibabu ya mionzi na kuboresha upatikanaji wa dawa za saratani. Vilevile, Taasisi itatafuta eneo kwa ajili ya kujenga na kupanua huduma za saratani nchini. Pia, Taasisi itatoa mafunzo kwa watumishi wake ili kuwawezesha kutoa huduma kwa ufanisi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi kwa kushirikiana na Hospitali ngazi za Taifa na Kanda, itaendesha kliniki za kupima afya ili kubaini saratani na kuwezesha kuanza matibabu mapema.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga katika mwaka 2010/11, itaendelea kutoa huduma za uchunguzi, matibabu kwa wagonjwa wa akili na walioathirika na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Isanga: Katika mwaka 2010/11, Wizara itaendeleza ujenzi wa kituo cha tiba na utengamao kwa waathirika wa dawa za kulevya kinachojengwa Itega. Aidha, itatoa mafunzo kwa madaktari na wauguzi ili kuongeza ujuzi wa kutoa huduma bora zaidi katika Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Hospitali ya Kibong'oto itaendelea kutoa huduma za Tiba na Uchunguzi kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu pamoja na wagonjwa walioathirika na VVU. Aidha, Hospitali hiyo itatoa mafunzo kwa watumishi wa ngazi mbalimbali kuhusu Tiba ya Kifua Kikuu Sugu. Vilevile, itajenga jengo kwa ajili ya kutoa huduma ya uchunguzi wa njia ya mfumo wa hewa kwa kumulika kwa kifaa maalum.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na wadau itakarabati maabara 10 za Hospitali za Mikoa ya Arusha (Mount Meru), Dar es Salaam (Mwananyamala), Iringa, Kilimanjaro (Mawenzi), Manyara (Babati), Mara, Mbeya, Mwanza (Sekou Toure), Ruvuma na Tabora (Kitete). Aidha, Wizara itaendelea kufanya matengenezo ya vifaa vya tiba na vya radiololojia katika hospitali zote nchini. Vilevile, Serikali itaboresha huduma za radiolojia katika Hospitali za Rufaa Maalum na Rufaa za Mikoa. Pia, Wizara itaanzisha huduma ya tiba kwa wagonjwa walio mbali na kituo alipo daktari anayetoa tiba na ushauri (*telemedicine*) katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kuptitia Mpango wa Damu Salama inataraja kukusanya chupa za damu kati ya 180,000 na 200,000 nchi nzima. Aidha, Mpango wa Damu Salama utaielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari. Vilevile, utaanzisha klabu za wachangiaji damu, hususan shulenii na sehemu nyinginezo ili kuongeza hamasa ya kuchangia damu kwa hiari. Pia, Mpango wa Damu Salama utafungua vituo vitatu katika Mikoa ya Dar es Salaam (Mnazi Mmoja), Lindi na Dodoma kwa ajili ya kukusanya na kusambaza damu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2010/11, shilingi 61,675,172,172.00 zimetengwa kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Umma. Kati ya fedha hizo, Serikali imetenga shilingi 31,075,172,172.00 na Mfuko wa Pamoja wa Wadau umetenga shilingi 30,600,000,000.00. Aidha, shilingi 281,720,895,800.00 zimetengwa chini ya *Global Fund* kwa ajili ya kununua dawa za Malaria na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2010/11, Wizara kuptitia Bohari ya Dawa, itanunua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Zahanati 4,500,

Vituo vya Afya 500, Hospitali 135 za Wilaya na Teule, Hospitali 23 za Rufaa ngazi ya Mkoa, Hospitali 8 za Rufaa, Hospitali 7 za Rufaa Maalum, Hospitali 1 ya Taifa, Hospitali 4 za Jeshi la Wananchi na 3 Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itatoa mafunzo kwa walimu wa walimu wa kanda watakaofundisha watumishi wapya katika zahanati na vituo vya afya vya umma juu ya uagizaji dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya Dawa na kanda zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaanzisha Kamati za Usimamizi wa Huduma za Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza, Afya ya Akili na Dawa za Kulevyta katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, KCMC, Bugando na Rufaa Mbeya. Aidha, itakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kinga na Udhibiti wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatekeleza Mradi wa miaka minne wa kueneza stadi za kubaini na kutoa tiba sahihi kwa wagonjwa wa kisukari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Bohari ya Dawa itaboresha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi hadi kufikia asilimia 90, kwa kuweka mfumo madhubuti wa ugavi. Aidha, itaimarisha maeneo ya ununuzi wa bidhaa kwa kutumia mikataba maalum inayowezesha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa haraka zaidi. Vilevile, itaimarisha utunzaji wa bidhaa na taarifa. Pia, itasambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma badala ya kupitia kwa Waganga Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Bohari ya Dawa itatumia wazabuni waliobainika kuwa na bidhaa zinazokidhi viwango vya kimataifa ili kutoa huduma bora kwa wateja. Aidha, itakamilisha mchakato wa kuingia katika mfumo wa Ubora wa Kimataifa (*ISO Certification*) kwa lengo la kutoa huduma zenyenye ubora wa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Bohari itabadilisha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) unaotumika ili kuendana na mahitaji ya sasa. Aidha, itapanua uwezo wa maghala kwa mita za mraba 6,700 katika Bohari za Kanda za Dar es Salaam, Dodoma na Mbeya. Vilevile, itaboresha huduma za mawasiliano kwa wateja na wadau kupitia Mpango Mkakati wa Mawasiliano na Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuhamasisha wamiliki wa vituo vya kutolea huduma za afya vya binafsi, mashirika ya dini na ya kujitolea na makampuni kuingia makubaliano na Halmashauri ili vituo vyao vitoe huduma kwa niaba ya Halmashauri hizo. Hospitali za Kolandoto (Shinyanga), Machame (Hai), Shirati (Rorya), St. Elizabeth (Arusha) na Izimbya (Bukoba) zinatarajiwa kuingia mkataba na Halmashauri zao kuziwezesha kuwa Hospitali Teule. Makubaliano hayo yanatarajiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa MMAM.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo hospitali za rufaa maalum ili ziweze kutoa huduma zinazopatikana nje ya nchi. Aidha, Wizara itadumisha uhusiano na madaktari bingwa kutoka nchi za nje ili kuwawezesha madaktari nchini kubadilishana utaalam na uzoefu hususan katika nyanja za upasuaji mkubwa wa moyo, figo na saratani. Wizara itaendelea kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa magonjwa yale ambayo hakuna utaalam hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia tiba asili na tiba mbadala ili kuboresha afya ya jamii nchini. Aidha, Wizara itakamilisha Mwongozo wa Mafunzo kwa ajili ya wakufunzi watakaoelimisha waganga wa tiba asili na tiba mbadala na kusambaza kwa Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Vilevile, itaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa tiba asili na tiba mbadala kupitia maadhisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwfrika inayoadhimishwa tarehe 31 Agosti kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itapitia ikama ya watumishi wa sekta ya afya na ustawi wa jamii ili kukidhi mahitaji halisi ya watumishi kutokana na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea. Mabadiliko hayo ni pamoja na kujitekeza kwa magonjwa yanayohitaji taaluma na ujuzi mpya na majukumu mapya ya Wizara na Hospitali za Mikoa kuwa za Rufaa. Aidha, Wizara itaeneza mfumo wa ukusanyaji takwimu za watumishi wa sekta ya afya na ustawi wa jamii katika ngazi zote baada ya kufanyiwa majoribio katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za vyuo vya afya na ustawi wa jamii kwa kutoa mafunzo rejea kwa Waratibu katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itapitia mitaala ya stashahada za juu katika fani za Tiba na Uuguzi. Lengo la zoezi hilo ni kuainisha mafunzo na viwango vya Tuzo za Taifa (*National Technical Award - NTA*) kulingana na viwango vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Matanzas cha Cuba, itakiwezesha Chuo cha Songea kuendesha mafunzo ya Madaktari. Wizara itanunua vitabu na vifaa vinavyohitajika kuendesha mafunzo hayo yanayotarajiwa kuanza Septemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaimarisha Kituo cha Elimu ya Masafa kilichopo Morogoro ili kiweze kutekeleza majukumu yake ya kuratibu elimu hiyo kwa ufanisi. Aidha, Kanda zote 8 za Mafunzo pamoja na vituo vinavyotumika kutekeleza mfumo huo wa elimu vitaimarishwa. Vilevile, mafunzo yatatolewa kwa Wakufunzi juu ya ufundishaji na uratibu wa elimu ya masafa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuratibu huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa na asasi zisizokuwa za kiserikali. Aidha, itaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria, sera na miongozo ili kuwezesha kupatikana kwa matunzo na ulinzi kwa watu walio katika mazingira hatarishi katika vituo vya ustawi wa jamii na vya taasisi zisizo za kiserikali. Vilevile, itaendelea kulipa gharama za shule kwa watoto walio katika vituo vya ustawi wa jamii na kugharamia vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ufundis vya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itafasiri Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 ya Kulinda Haki za Watoto na Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Na. 6 ya Mwaka 2008. Aidha, itasambaza Sheria hizo na Sera ya Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii kwa wadau. Vilevile, itaandaa Kanuni za Sheria hizo na kupitia Mpango wa Taifa wa Watoto walio katika mazingira hatarishi. Pia, itafanya uraghibishi na uhamasishaji dhidi ya imani na mila potofu kuhusu watu wenye ulemavu na wazee.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itatoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Maafisa Ustawi wa Jamii na watumishi wengine. Mafunzo hayo yatahusu haki za mtoto, haki za watu wenye ulemavu na wazee, kinga ya jamii, ufuatiliaji na tathmini. Aidha, itawajengea uwezo, wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri na Mikoa juu ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika mwaka 2010/11, itaendelea kuimarisha utoaji huduma bora za uchunguzi wa sampuli na vielelezo mbalimbali na kutoa matokeo kwa wakati. Aidha, Wakala itafanya matengenezo kinga kwa mitambo ya uchunguzi ili iweze kutoa matokeo sahihi na kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wakala itaandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu Na. 8 ya Mwaka 2009. Aidha, Wakala itaendelea kushiriki katika kikosi kazi kinachojumuisha vyombo vya dola na kuchukua sampuli za uchunguzi wa vitendo vya ujambazi, ubakaji na watumiaji wa dawa za kulevyta pamoja na watuhumiwa wa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*) na vikongwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wakala itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika migodi na maeneo yanayozunguka migodi, viwanda na maghala 650, vituo vyote

15 vya mipakani, bandari na viwanja vya ndege kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wakala itatoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi salama na sahihi ya kemikali kupitia vyombo vya habari, semina, warsha na kushirikiana na mashirika ya kitaifa na kimataifa katika kutekeleza mikataba ya kimataifa ya usimamizi wa kemikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wakala kwa kushirikiana na halmashauri itateua wasimamizi wa kemikali katika kila halmashauri. Aidha, itatoa elimu katika mikoa yenye migodi kwa timu ya wataalam wa afya watakaohusika na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Kemikali Na. 3 ya Mwaka 2003 katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wakala itaendelea na mchakato wa kupata hati ya ithibati kwa baadhi ya njia za uchunguzi chini ya usimamizi wa SANAS.

Aidha, itakamilisha rasimu ya Miswada ya kutunga Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Sheria ya Taaluma ya Wakemia.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Chakula na Dawa katika mwaka 2010/11, itaendelea kufanya ukaguzi wa maeneo ya biashara ya vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kufanya operesheni ili kubaini bidhaa zisizokidhi viwango vya usalama na bidhaa bandia na kuziondoa katika soko. Aidha, Mamlaka itaendelea kufanya tathmini ya bidhaa ili kuhakiki ubora na usalama wake kabla ya kusajiliwa na kuruhusiwa kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itaimarisha mfumo wa udhibiti wa dawa za asili zinazotengenezwa hapa nchini na za kutoka nje ya nchi ili kuhakiki usalama wake kabla hazijaingizwa katika soko. Aidha, Mamlaka itaimarisha ukaguzi wa bidhaa zote zinazotoka nje ya nchi kwa kuweka wakaguzi zaidi katika vituo vya forodha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itaendelea kufanya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba visivyoofaa kwa matumizi ya binadamu ili kulinda afya ya jamii. Aidha, Mamlaka itaendelea na taratibu za kupata ithibati ya maabara ili kutambuliwa na Shirika la Afya Duniani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itaendelea kutekeleza Mpango wa Ufutiliaji wa Usalama wa Dawa Mseto ya Malaria ya *Artemether/Lumefantrine (ALu)* na dawa za UKIMWI. Aidha, Mamlaka itaendelea kukusanya na kutathmini taarifa za madhara ya dawa nyingine kwa kutumia fomu za njano ambazo zimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itaendelea kukusanya na kutathmini taarifa za magonjwa yatokanayo na kula chakula. Aidha, Mamlaka itafanya tathmini ili kubaini ukubwa wa tatizo la kuwepo kwa sumu kuvu (*mycotoxins*) katika mahindi na vyakula vya watoto vya asili ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itaendelea kuielimisha jamii na wadau kuhusu majukumu yake ya kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Aidha, Mamlaka itatoa mafunzo maalum kwa wasindikaji wadogo wa vyakula juu ya mbinu na mifumo ya kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa wanazozalisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Mamlaka itakamilisha uenezaji wa Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu (ADDO) katika mikoa iliyobaki ili kuboresha upatikanaji wa dawa katika sekta binafsi. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na TAMISEMI itasimamia, kufutilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Chakula na Lishe itaimarisha juhudi za kupambana na utapiamlo ili kuboresha hali ya lishe ya Watanzania. Aidha, itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuongeza thamani ya zao la muhogo katika

Halmashauri za Wilaya za Masasi, Mtwara, Newala na Tandahimba. Mradi utapanuliwa kwa kuongeza idadi ya kaya za wakulima watakapewa elimu ya kilimo bora cha zao la muhogo toka kaya 1,080 hadi kaya 20,000. Vilevile, Taasisi itaongeza idadi ya vikundi vyta usindikaji wa muhogo kutoka 18 hadi 30. Vikundi hivyo vitapewa elimu ya biashara na kuunganishwa kwenye masoko yaliyopo Manispaa ya Mtwara - Mikindani na Jiji la Dar es Salaam. Pia, Taasisi itawezesha kila kikundi kupata mashine moja ya kusindika muhogo, kaushio la juu na kujengewa banda la kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi kwa kushirikiana na wadau itaendelea na juhudi za kuongeza virutubishi kwenye unga wa mahindi na ngano na mafuta ya kula. Aidha, Taasisi itachapisha miongozo na vijitabu vyta maelekezo ya uongezaji virutubishi kwenye vyakula na kuvisambaza kwa wadau. Vilevile, Taasisi itahamasisha wadau katika ngazi mbalimbali kuhusu umuhimu wa kula vyakula vilivyoongezwa virutubishi na jinsi ya kuvitambua.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itaratibu ugawaji wa matone ya Vitaminini A na dawa za minyoo zinazotolewa mara mbili kwa mwaka, yaani mwezi Juni na Desemba. Aidha, itafanya uchambuzi wa taarifa za utafiti uliofanyika 2009/10 ili kujua viwango vyta upungufu wa Vitaminini A kwa watoto, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itasimamia utoaji wa huduma za matibabu ya utapiamlo katika hospitali zote za Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa inayoathiriwa na vipindi virefu vyta ukame ya Dodoma, Singida, Mtwara na Lindi. Lengo ni kupunguza athari za utapiamlo mkali kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itahamasisha viongozi katika halmashauri za wilaya na manispaa 14 zenye viwango vyta chini ya asilimia 70 ya matumizi ya chumvi yenye madini joto. Halmashauri hizo ni Iringa, Kilolo, Lindi, Ludewa, Mafia, Makete, Mpanda, Mufindi, Njombe, Nkansi, Ruangwa, Sumbawanga na Manispaa za Iringa na Sumbawanga. Aidha, Taasisi itatoa msaada wa kitaalamu kwa wazalishaji chumvi wadogo wadogo kutoka Halmashauri za Wilaya za Babati, Bahi, Chamwino, Mbozi, Iramba, Singida, Hanang, Manyoni, Meatu, Kigoma na Manispaa ya Dodoma ili kuunda chama chao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itaandaa mwongozo wa ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha na kusambaza kwenye vituo vyta kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Taasisi itafasiri Mwongozo wa huduma na matunzo ya lishe kwa watu walioambukizwa Virusi vyta UKIMWI kutoka Lugha ya Kiingereza kuwa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itachapisha kitita cha afua muhimu za lishe na kusambaza katika halmashauri zote nchini. Lengo ni kuwawezesha watendaji katika ngazi hizo kuingiza masuala ya lishe katika Mipango ya Maendeleo ya Halmashauri. Aidha, katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na tatizo la UKIMWI, Taasisi itatoa mafunzo kwa wafanyakazi 140 wa sekta ya afya

yanayohusu ulishaji wa watoto wachanga na wadogo walio na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza na Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi kwa kushirikiana na wadau itaendeleza programu ya utoaji wa chakula tiba kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wenye hali mbaya ya lishe, pamoja na watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira hatarishi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga ili kuboresha huduma za lishe kwa walengwa. Aidha, Taasisi itatoa elimu ya lishe kwa jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano zikiwemo radio, televisheni, magazeti na maonesho mbalimbali ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu itaendelea kufanya majaribio ya chanjo dhidi ya virusi vya *human papilloma* vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake. Aidha, Taasisi itaendelea kufanya tathmini ya ubora wa kipimo cha maambukizi ya kaswende ili kubaini uwezekano wa kujumuisha huduma hiyo katika mpango wa kuzuia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itafanya utafiti wa awamu ya tatu ya chanjo ya Malaria iitwayo RTS,S/ AS01E katika Halmashauri za Handeni na Korogwe. Jumla ya washiriki 1,531 wenye umri chini ya miezi 17 watahusika katika utafiti huo katika vijiji 37. Utafiti utafanyika nchini kwa muda wa miaka mitatu ili kubaini usalama wake na uwezo wa kuzuia ugonjwa wa Malaria. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na wadau itatoa elimu ya kuhifadhi vyanzo vya mito na maeneo yenye visima vya maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Ustawi wa Jamii itaaniszha mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii. Aidha, kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo ya masafa juu ya kuhudumia watoto, familia na jamii zilizoathirika na VVU/UKIMWI, watu walio katika migogoro, umaskini na wakimbizi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa wanafunzi 150. Vilevile, itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ustawi Wasaidizi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Mtwara na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Taasisi itaendesha mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Ustawi wa Jamii kuhusu *Guidance and Counseling na Child Protection, Workplace Conflict Management, Collective Bargaining and Negotiation Skills, Human Resources Management Information System na Entrepreneurship*. Aidha, kwa kushirikiana na wadau itatoa ushauri elekezi kwa Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Hai, Magu, Makete, Mtwara, Siha na Manispaa Temeke ili kuzijengea uwezo wa kuimarisha mifumo na miundo ya ulinzi wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara inaomba kiasi cha shilingi 448,442,515,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 9,873,761,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 438,568,754,000.00 zinatoka kwa Taasisi za Kimataifa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya na wale walioko nje ya Mfuko. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itakarabati nyumba ya Katibu Mkuu na ujenzi wa nyumba ya Waziri, Makao Makuu ya Serikali, Dodoma. Aidha, itakarabati jengo lake la Makao Makuu na kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea na ujenzi katika Hospitali za Rufaa za Bugando, Mbeya na Mirembe na Taasisi ya Isanga pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini, Mtwara. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Watu wa China itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Upasuaji wa Moyo Muhimbili, ujenzi wa kituo cha Mbweni Mpiji cha Utengamao, Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Vilevile, itaendelea na ujenzi na ukarabati wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Chakula na Lishe pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea na ukarabati wa Chuo cha Ufundı cha Wanawake Wasioona cha Singida, Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu Yombo, Dar es Salaam, Masiwani, Tanga na makazi ya wazee Funga Funga, Morogoro, kujenga bweni la wasichana katika shule ya maadilisho Irambo - Mbeya na mahabusu ya watoto, Mwanza na kujenga uzio wa mahabusu ya watoto Mtwara. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi na upanuzi wa vyuo vya afya 21 ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaandaa *Master Plan* ya Hospitali za Kibong'oto na Mirembe na kununua hadubini ya upasuaji wa mishipa ya fahamu katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili pamoja na vifaa vya uzazi na chanjo kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya vya umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea na uraghibishi wa jamii kuhusu utekelezaji wa Sera ya Afya, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya III, MMAM na miongozo mbalimbali inayotolewa kufuatia uboreshaji endelevu wa huduma katika sekta ya afya kwa kupitia matangazo na programu za vipindi vya kila wiki katika TBC Taifa. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za maandalizi ya uelimishaji wa jamii kuhusu mafanikio ya uboreshaji wa huduma za afya kwa "vipindi vya kuandikwa" "*documentary*" ili vitangazwe kila wiki katika TBC TV.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kusimamia na kufuatilia upangaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kiufundi katika utekelezaji wa mipango na Mkakati wa Malipo kwa Utendaji Bora wa watoa huduma za afya (*Pay for Performance – P4P*). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali

za Mitaa, itapitia Mwongozo wa Kitita cha Huduma Muhimu za Afya (*Essential Health Package*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya itaongeza uwigo kutoka asilimia 9.5 ya sasa hadi kufikia asilimia 15.3 hadi Juni 2011 wa Wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii ya Watanzania. Lengo ni kufikia asilimia 45 ya Watanzania wote ifikapo 2015. Aidha, Mfuko utatoa huduma za matibabu kwa Makamanda na Askari wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji pamoja na wategemezi wao, ambao idadi yao inafikia 244,944. Vilevile, Mfuko utaboresha bei za marejesho kwa huduma za dawa na vipimo zinazotolewa na watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kupitia Mfuko itaboresha kitita cha mafao kwa kujumuisha mafao ya miwani ya kuonea mbali na itawalipia wajawazito vifaa vya kujifungulia. Aidha, Mfuko utaingiza huduma za malipo ya kutahiri kwa watu wazima. Hatua hii itasaidia kupambana na maradhi yanayotokana na ngono. Vilevile, Mfuko utaendelea kutoa elimu kwa wadau chini ya programu ya Kata-Kwa-Kata na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kuwa na ushirikiano mzuri na wa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia sekta ya afya na ustawi wa jamii. Aidha, itaendeleza ushirikiano mzuri na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za Afya za Kitaifa na Kimataifa. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Malaria Afrika, Tiba Asili ya Mwafrika, Watu Wenye Ulemavu, Wazee, Fimbo Nyeupe na Kutotumia Tumbaku.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark, Usvisi, Uholanzi, Norway na Ujerumanu na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, *UNFPA, Ireland Aid, CIDA* (Canada), Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na *UN System* kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Pia, napenda kuzishukuru nchi nyingine za China, Cuba, Canada, Hispania, India, Ireland, Italia, Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Sweden, Ufaransa na Uingereza ambazo zimeendelea kuisaidia sekta ya afya na ustawi wa jamii kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuyashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao mzuri na Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), DFID, FINIDA, GAVI, Shirika la Umoja wa Mataifa la Uzazi wa Mpango (UNFPA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Benki ya Dunia (World

Bank), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), ORIO, Overseas Related Export Trade (ORET), Umoja wa Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi Duniani (OPEC), na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF).

Mheshimiwa Spika, wengine ni CUAMM, DANIDA, GTZ, JICA, KOICA, *Baylor College of Medicine* ya Marekani, KfW, MISERIOR, EED, SAREC, SDC, CDC, SIDA (Sweden), *Abbott Fund, Engender Health (USA)*, *CORDAID (Netherlands)*, *BASIC NEED (UK)*, *HelpAge International, ILO, Family Health International (FHI)*, *Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF)*, Shirika la Upasuaji la Spain, *Good Samaritan Foundation (GSF) na USAID*. Aidha, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo wa Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Usubi na Vikope ambao ni *African Programme for Orchorcerciasis Control, International Eye Foundation, Sight Savers International, Merck & Company, Pfizer, Helen Keller International, Christoffel Blinden Mission (CBM) na International Trachoma Initiative*.

Taasisi nyingine za Kimataifa ni *Axios International, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR)*, *Clinton Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation*, *Abbot Laboratories, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Johns Hopkins University, Global Fund, University of Columbia, CMB, Germany Leprosy Relief Association, Gabriel Project ya Marekani, Citi Bank, General Electric (GE - USA), Havard University na Duke University za Marekani, University of Maryland, Community of Saint Egidio (DREAM), Supply Chain Management System (SCMS), NOVARTIS, Saint Thomas Hospital - London, Management Science for Health (MSH), Glaxo Smith Kline (GSK), Merck, Qiagen, Labiofarm Industry, URC, Futures Group, IMA, World Vision, MEDA, Pathfinder, PATH, Jhpiego, Pharm Access International, Malaria No More, Save the Children, Research Triangle Institute (RTI) and Intrahealth, I-TECH, na Military Advancement for Medical Research, Department of Defence ya Marekani*.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarisaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na *William Mkapa HIV/AIDS Foundation, Aga Khan Foundation, AMREF, Lions Club, Rotary Club International, BAKWATA, CCBRT, CSSC, CCT, ELCT, TEC, Msalaba Mwekundu, Shree Hindu Mandal, UMATI, Counsenuth, PRIMAT, MAT, AGOTA, PAT, TPHA, USADEFU, NSSF, PASADA, PSI, TPRI, PACT, Women Dignity Project, Tanzania Diabetic Association, MEHATA, APHFTA, TANESA, MEWATA, MUKIKUTE, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii*.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuvishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, Dodoma, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Arusha pamoja na Vyuo vyote vya

Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2009/10, nimefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Aisha Omar Kigoda, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa ushirikiano mkubwa alionipa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara. Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Bibi Blandina S. J. Nyoni, kwa kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru wafuatao: Dkt. Deodatus Michael Mtasiwa, Mganga Mkuu wa Serikali, Bwana Danford Makala, Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Wakurugenzi wa Idara zote katika Wizara. Nawashukuru pia, Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa Maalum na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta nyingine ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi na taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao. Kipekee namshukuru mke wangu mpendwa, Margaret Mwakyusa na watoto wetu, kwa kuwa karibu nami muda wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Wamenisaidia, wamenitia moyo na kunipa ushirikiano mkubwa. Kwa Wananchi wa Jimbo la Rungwe Magharibi, nawashukuru kwa ushirikiano wao mzuri wanaonipa na nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa moyo mkunjufu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/11, Wizara imekadiria kukusanya mapato ya kiasi cha shilingi 2,486,500,000.00. Kiasi hiki kinatokana na makusanyo ya uchangiaji gharama kutoka kwenye Vyuo vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Usajili wa hospitali binafsi na maabara binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/11, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 229,978,968,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 105,758,645,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kiasi cha shilingi 124,220,323,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Makao Makuu na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara. Kati ya hizo, kiasi cha shilingi 22,310,323,996.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara ambazo zitatumika kulipa Mishahara ya Watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Makao Makuu, Hospitali za Rufaa Kibong'oto, Mbeya, Mirembe na Vyuo vyote vya Serikali vya Mafunzo ya Afya. Jumla ya shilingi 101,909,999,004.00 zimetengwa kwa ajili ya Mishahara ya Taasisi. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Hospitali za Rufaa za KCMC na Bugando, Hospitali Teule (DDH), Wakala wa Maabara

ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Chakula na Dawa na Hospitali za Mashirika ya Kujitolea (*Voluntary Agencies-VA's*) na Hospitali ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inakadiria kutumia jumla ya shilingi 448,442,515,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania itachangia kiasi cha shilingi 9,873,761,000.00. Fedha kutoka kwa Wahisani wanaoisaidia Sekta ya Afya ni shilingi 438,568,754,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 58,314,552,590.00 zitatolewa na Wahisani wanaochangia Mfuko wa Pamoja na shilingi 380,254,201,410.00 zitatolewa na Wahisani walio nje ya Mfuko.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutekeleza kazi zilizopangwa mwaka 2010/11, naliomba Bunge lako Tukufu litafakari, lijadili na kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Asasi zake yenye jumla ya shilingi 678,421,483,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 229,978,968,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 448,442,515,000.00 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kuwasilisha kwa ufanisi kabisa hotuba ambayo ina mambo mengi lakini imeyaweka vizuri kwenye muhtasari. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ili tuweze kuyapata maoni ya Kamati. Mheshimiwa Omari Kwaangw'.

MHE. OMARI S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Malengo ya Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha wa kufikiria na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na pia kupitia Malengo na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo kwa Serikali katika maeneo mbalimbali yafuatayo:-

- Kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Afya hadi kufikia asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali ili kutekeleza kwa vitendo Azimio la Abuja (*The Abuja Declaration*) kama lilivyoazimiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika;
- Kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa madarasa pamoja na mabweni ya Vyuo vya Afya pamoja na kukamilisha udahili wa wanafunzi wa fani za Afya;
- Kubainisha takwimu za Zahanati katika kila Kijiji na Vituo vya Afya zikionesha hatua za utekelezaji katika kila Wilaya;
- Kutenga fedha za kutosha kuboresha huduma za akina mama ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto chini ya miaka mitano;
- Kuboresha miundombinu ili kuwezesha akina mama wajawazito na watoto wachanga kufikiwa kwa urahisi;
- Kusambaza pikipiki maalum za magurudumu matatu katika Vituo vyote vya Afya;
- Wizara kuhakikisha vituo vyote vya huduma za mama na mtoto vinakuwa na dawa muhimu wakati wote;
- Serikali igharamie mishahara ya Watumishi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) na iiongezee ruzuku ili Mamlaka iweze kutekeleza jukumu lake muhimu la kulinda afya za wananchi;
- Serikali iajiri Wataalam wa Chakula na Lishe katika kila Halmashauri;
- Idara ya Bohari ya Dawa (*MSD*) ifanye mchanganuo utakaowezesha kubaini makampuni yanayotoa dawa na vifaa tiba vinyoyokidhi viwango vya ubora pamoja na kuweka *Field Officers* katika kila hospitali ili kuchambua mahitaji halisi ya dawa na vifaatiba vya hospitali;
- Kila Hospitali ya Mkao na Wilaya kuwe na Kitengo cha Ushauri wa Tiba ya Magonjwa ya Akili na Dawa za Kulevyia ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mirembe;
- Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uharakishe utaratibu wa kutoa huduma kwa wastaafu na wenza wao na pia uangalie uwezekano wa wadau wake kupata matibabu ndani na nje ya nchi;
- Wizara ianzishe utaratibu ulio wazi wa kushughulikia malalamiko ya wananchi na watumishi wasio na maadili wawajibishwe; na
- Serikali iongeze ruzuku kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu na kuwapatia fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa mafanikio yaliyopatikana na utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010 unaoishia Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kujielekeza kwenye vipaumbele hivyo, Sekta ya Afya kwa Mwaka 2009/2010 iliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Upatikanaji wa rasilimali watu watakaokidhi mahitaji halisi katika Sekta ya Afya katika ngazi zote za kutolea huduma;
- (ii) Kuendelea kuongezeka kwa makundi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi;
- (iii) Kukabiliana na ongezeko la magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza;
- (iv) Kuhakikisha kuwa fedha zinatolewa kwa wakati kutoka Hazina kwa ajili ya kazi zilizopangwa;
- (v) Ufundishaji wa Wataalamu wa Sekta ya Afya wa kutosha ili kutimiza lengo la Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) la upatikanaji wa rasilimali watu wa kutosha katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya;
- (vi) Namna ya kuhakikisha upatikanaji wa samani, vifaa tiba na vitendea kazi vingine kwa wakati, pamoja na kuwa mchakato wa manunu ni mrefu;
- (vii) Kuongezeka kwa majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi; na
- (viii) Ufinyu wa bajeti kulingana na viwango vinavyotolewa na Hazina ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ikabiliane na changamoto hizo ni muhimu Sekta hii ikapewa rasilimali za kutosha ili itekeleze vipaumbele muhimu vilivyoainishwa kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara ya Afya imejielekeza kutoa vipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

- Kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa majengo ya kutolea huduma za Afya kuititia Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM);
- Kuimarisha huduma za Afya na Ustawi wa Jamii zinazotolewa kwenye ngazi ya Halmashauri;
- Kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma ya mama na mtoto;

- Kuzuia/kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza pamoja na milipuko, kinga na tiba ya Malaria, huduma za chanjo, kuzuia na kutibu Kifua Kikuu na magonjwa nyemelezi kwa watu wanaoishi na Virusi nya UKIMWI pamoja na kununua dawa za kuzuia makali ya UKIMWI; na

- Kuongeza idadi ya Watumishi wa Afya na Ustawi wa Jamii katika ngazi zote ambapo kwa sasa sekta ina upungufu mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa miaka mitatu sasa ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2008/2009 2009/2010 2010/2011

Matumizi ya Kawaida	198,157,615,000	218,393,211,000	29,978,968,000
------------------------	-----------------	-----------------	----------------

Miradi ya Maendeleo	242,067,318,1000	260,599,867,000	448,442,515,000
------------------------	------------------	-----------------	-----------------

Jumla	440,224,933,100	478,993,078,000	678,421,483,000
-------	-----------------	-----------------	-----------------

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonesha kuwa Bajeti ya Wizara imekuwa ikiongezeka. Hii ni dalili nzuri kuwa Serikali bado inaweka umuhimu mkubwa kwenye Sekta ya Afya pamoja na matatizo na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Wizara isimamie na kudhibiti matumizi ya fedha zilizombwa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali na kama zitakavyoidhinishwa na Bunge hili. Aidha, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuzingatia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) juu ya ukaguzi wa fedha na ukaguzi wa Ripoti ya Ufanisi kuhusu utendaji na uwajibikaji kama tulivyogusia baadhi ya maeneo katika maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa vifo nya akina mama wakati wa kujifungua vinapungua, Wizara pamoja na wadau wa maendeleo imetenga Tshs. 37.3 bilioni kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuboresha huduma za akina mama wakati wa kujifungua. Aidha, Wizara imetenga Tshs. 3 bilioni kwa ajili ya kununulia vifaa nya kujifungulia ambavyo vitakuwa vinagaiwa kwa akinamama wajawazito wanapokwenda kliniki ili viwasaidie wakati wa kujifungua. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusikiliza ushauri wa Kamati katika eneo hili na kwamba hatua hizi ni za faraja kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri katika Hospitali zote za Wilaya na Vituo nya Afya nchini kuwepo na huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji. Vilevile,

Serikali itekeleze ahadi ya mpango wake wa kununua na kusambaza pikipiki za magurudumu matatu katika Vituo vyote vya Afya nchini. Haya kwa pamoja yakitekelezwa kwa ufasaha, yatasaidia sana kusogeza huduma karibu na wananchi na pia kupunguza vifo vya akinamama wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Bohari ya Dawa (*MSD*). Idara ya Bohari ya Dawa ilianzishwa mwaka 1993 ili kutekeleza majukumu makuu matatu ya kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa-tiba katika hospitali zote za umma nchini kwa niaba ya Serikali. Idara hii ni nyeti na ina jukumu la kuhakikisha dawa zenye ubora kwa ajili ya matumizi ya umma hapa nchini zinakuwepo wakati wote (hata wakati wa magonjwa ya milipuko au majanga mengine) na usambazaji wake unaratibiwa inavyopasa.

Mheshimiwa Spika, Idara hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo suala la kuongezeka kwa madeni. Kwa nyakati tofauti, suala hili lilishajitokeza na Kamati ikashauri madeni yaliyokuwepo wakati huo ya Tshs.10.6 bilioni yalipwe na kusiwepo tena na ulimbikizaji wa madeni ili kuinusuru Idara hii kushindwa kabisa kusambaza dawa na hatimaye fedha hizo zililipwa kwa awamu katika bajeti mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2010, kiwango cha madeni kimeongezeka na kufikia kiasi cha Tshs.36,762,501,305.95. Hali hii inaifanya *MSD* kulalamikiwa kwa kushindwa kufanya kazi zake vizuri. Aidha, kuendelea kukua kwa deni hili kama jedwali lifuatato linavyoonesha kutaisababishia Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kujiendesha ndani ya mwaka mmoja.

Jedwali Na.2 - Mchanganuo wa Deni

MAELEZO	KIASI
Jumla ya deni chini ya Idara ya Kinga	29,748,522,119.80
Jumla ya deni chini ya Idara ya Tiba	10,551,771,902.15
Jumla kuu	40,300,294,021.95
Malipo ambayo tayari Wizara imeshalipa	(3,538,792,716.00)
Deni lililobakia	36,762,501,305.95

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, 2010

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ieleze mikakati maalum ya kulipa deni hili mapema iwezekanavyo ili *MSD* ifanye kazi zake kwa ufanisi. Kwa mtizamo huu *MSD* haipaswi kulaumiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*). Jukumu kuu la Mamlaka, ni kulinda afya za wananchi kwa kudhibiti usalama na ubora wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa-tiba. Kamati inaipongeza Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kufanikiwa kupata Cheti cha Kimataifa cha Ubora wa Utendaji cha (*International Organisation for Standardization*) katika mifumo ya udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mamlaka ya Chakula na Dawa imefanikiwa kukamata na kuteketeza bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama ambapo iliteketeza shehena 32 za dawa na vipodozi vyenye thamani ya shilingi bilioni 1,784,261,873 ambazo zilikuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu. Pia iliteketeza bidhaa za vyakula vyenye thamani ya shilingi milioni 802, 866,044 kwa kutokidhi viwango vya ubora.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeanza ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za chakula na dawa ambapo mpango wa majaribio wa ufuatiliaji na uchunguzi wa magonjwa yatokanayo na chakula unatekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara na Mamlaka imepokea taarifa za wagonjwa 517 waliougu Kutokana na chakula kinachosadikika kuwa si salama na kati yao 16 walipoteza maisha. Kamati inaishauri jamii iendelee kuisaidia Mamlaka ya Chakula na Dawa katika kubaini bidhaa za chakula na dawa zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, awali *TFDA* ilikuwa inalipa mishahara ya watumishi wake kwa asilimia mia moja. Kamati inaipongeza Serikali kukubali kulipa asilimia 55.1 ya gharama za mishahara ya watumishi wa Mamlaka kuanzia tarehe 1 Julai, 2010 hali ambayo itawezesha fedha zinazotokana na vyanzo vya Mamlaka kutumika zaidi katika kazi za udhibiti na usimamizi wa vyakula na dawa. Tunaipongeza Serikali kwa hatua hii muhimu na kwa kuzingatia ushauri wa mara kwa mara wa Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Mamlaka ya Chakula na Dawa bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kuwepo kwa njia nyingi zisizo halali (njia za panya) ambazo bidhaa zinapitishwa na wafanyabiashara ambao si waaminifu;
- Kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwa wakati hivyo kuathiri utekelezaji wa Mpango Kazi;
- Ufinyu wa bajeti unaofanya mipango mingi kutokwenda kwa kasi iliyopangwa. Mfano, Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu (*ADDO*) kasi yake imepungua kutokana na ufinyu wa bajeti;

- Kuwepo kwa mwamko mkubwa wa Soko la Pamoja la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuliko kasi ya kuhuisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa husika;
- Upungufu katika mfumo wa uteketezaji wa bidhaa zinazokutwa wakati wa ukaguzi; na
- Utaratibu wa Mamlaka ya Mapato (*TRA*) wa kuruhusu baadhi ya mizigo kuingia moja kwa moja bila kukaguliwa kwenye vituo vya forodha na hivyo kuongeza uwezekano wa kuingiza bidhaa zisizokidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ilizonazo Mamlaka ya Dawa na Chakula (*TFDA*), Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali ione umuhimu wa kubadilisha uamuza wake wa kuruhusu watu kupidisha bidhaa bila kukaguliwa kwa vile imeonekana kwa kufanya hivyo ndipo wafanyabiashara hutumia mwanya huo kupidisha bidhaa zisizokuwa na viwango;
- Kasi iongezwe kwenye ukaguzi wa dawa za mitishamba ambazo kwa sasa wananchi wengi wanazitumia bila kujua usalama wake na mkazo zaidi uwekwe kwenye dawa za Kichina ambazo zimeonekana kuwa na madhara kwa wananchi;
- Serikali kupidia Wizara ya Afya izingatie kutoa tamko mara moja wanapoona au kusikia mtu anajitangaza kuwa na dawa fulani ili kupunguza madhara yatakayotokea kwa kuchelewa kutoa taarifa kwa wananchi wetu; na
- Kuwe na siku maalum kwa ajili ya Maonesho ya shughuli zinazofanywa na Mamlaka ili kutoa elimu juu ya usalama na ubora wa bidhaa ikiambatana na kutoa elimu juu ya usalama na ubora wa bidhaa angalau mara moja kwa mwaka kama inavyofanyika kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umefanikiwa kuongeza wigo wa wanachama wake ambapo hadi mwezi Mei 2010 ulikuwa na wanachama 372,678 sawa na jumla ya wanufaika 1,968,284 ambao wanajumuisha makundi ya Watumishi wa Umma, Waheshimiwa Madiwani, Wanafunzi, Wanachama Wastaifu na kuanzia mwaka 2010/2011 wataanza kutoa huduma kwa askari wa Majeshi ya Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huo ukiwa ndio unaosimamia Mifuko ya Afya ya Jamii (*CHF*) umeanza kuihamasisha jamii kuijunga na Mifuko hii kupidia programu yake kabambe ya Kata-kwa-Kata ambapo umeweza kuzifikia Kata 1,217 kati ya Kata 2,575 zilizokuwepo kabla ya mgawanyo mpya wa Kata. Pia kuanzia mwaka ujao wa fedha

Mfuko utaanza rasmi kutoa fao la vifaa kwa walemvu vikijumuisha, fimbo nyeupe, shimesikio (*hearing aids*) na vinginevyo. Kamati inaupongeza Mfuko na Wizara kwa hatua hii ya mafanikio. Kamati inaupongeza Mfuko na Wizara kwa hatua hii ya mafanikio.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mfuko unakabiliwa na changamoto ya kutoa elimu zaidi hasa katika maeneo ya vijijini sanjari na kuandaa mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za matibabu kwa wanachama wake vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mfuko uendelee kubuni mbinu mbalimbali za kuboresha huduma kwa wanachama wake vijijini ikiwemo ile ya kusajili Maduka ya Dawa Muhimu Vijijini (*ADDOs*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Mikoa. Hili ni eneo mojawapo ambalo Wizara imeliweka kwenye vipaumbele vyake vitano kwa mwaka 2010/2011. Mwelekeo wa bajeti ya Ujenzi na Ukarabati kwa miaka miwili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha kuwa fedha hizi zinatengwa chini ya Bajeti ya Mikoa na hivyo kuwa ndogo sana kutokana na *Ceiling* ya fedha za Maendeleo kwa Mikoa. Sh.7.4 bilioni kwa ukarabati wa Hospitali karibu zote ni fedha kidogo sana na Sh.5.0 bilioni kwa ujenzi wa Hospitali na zingine mpya ni fedha kidogo sana. Kwa mtindo huu, ni wazi kuwa ukarabati na hasa ujenzi wa Hospitali mpya za Mikoa utachukua miaka mingi isiyopungua 10 na wakati huo huo Mikoa husika haitaweza kujenga miradi mingine kutokana na *ceilings* zao.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ya Afya ya Maendeleo ni Sh.448.9 bilioni kwa miradi iliyopo chini ya Wizara. Kamati inashauri, Serikali kubadili kabisa utaratibu wa kujenga miradi mikubwa kama Hospitali za Kisasa za Mikoa na ambazo ndizo zitakazotegemewa kutoa huduma za rufaa. Fedha za kutosha za miradi ya aina hii zitengwe na Hazina kwenye Bajeti ya Wizara na Wizara itekeleze miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Huduma ya Afya ya Msingi ndiyo kiini cha Sera ya Taifa ya Afya nchini na kwa kiasi kikubwa ndio sehemu ya kwanza inayohusu Kukinga na Kutibu.

Mheshimiwa Spika, katika ziara za Kamati yangu kwenye Hospitali za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, tumegundua viashiria vingi vya matatizo katika Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya kama ifuatavyo:-

- Kwamba kuna matatizo ya utendaji katika ngazi hizo hasa Vituo vya Afya;
- Kwamba rasilimali zilizopo mara nyingi kwa Vituo vya Afya hazigawanywi kiufanisi kwa kuzingatia mahitaji na utendaji kazi;
- Kwamba Bodi na Kamati za Afya katika ngazi za Wilaya na Vituo vya Afya, zinaonekana hazitekelezi vizuri kazi ya kusimamia rasilimali kwa ufanisi unaotakiwa ili kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu kusubiri kupata huduma kwa muda mrefu Vituoni; na
- Kwamba kumekuwepo na ucheleweshaji wa mapokezi ya fedha za Serikali za Mafungu ya Misaada (*Government's Block Grants*) na fedha za Wafadhili za Mfuko wa Afya (*The Donor's Health Basket Fund*), ucheleweshaji huu wa fedha unakwamisha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, igawe dawa muhimu, vifaa na fedha kwa kuzingatia wingi wa kazi ili kupunguza muda wa wananchi kusubiri kupata huduma;
- Sekretarieti za Mikoa zifuutilie na kutathmini utendaji kazi katika ngazi ya Halmashauri na Vituo vya Afya;
- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI zichambue kwa kina taarifa na takwimu zinazotoka Mikoani na Wilayani ili kudhibiti usahihi wa takwimu na matumizi ya fedha; na
- Ni muda muafaka kufanya mapitio ya mfumo wa kusimamia huduma za afya kuititia Bodi za Hospitali na Kamati za Vituo vya Afya ili kubaini upungufu uliopo na kuleta ufanisi zaidi. Mabadiliko katika eneo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, shukrani, kwa niaba ya Kamati, namshukuru Mheshimiwa Profesa David H. Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda na Watendaji wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Blandina S.J. Nyoni, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2009/2010, na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashililah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kutuhudumia vyema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nawapongeza Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Hosiana John na Asia Paul Minja kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, tunapofika mwisho wa Uhai wa Bunge hili la Tisa, naomba kwa dhati kabisa niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa jinsi walivyonipa ushirikiano katika kuiongoza Kamati. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti Dr. Haji Mwita Haji, kwa msaada na ushauri aliota kwa muda wote wa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kuwa Wabunge wote wa Kamati yangu ni sehemu kubwa ya mafanikio ya Serikali katika Sekta ya Afya, hivyo wanastahili pongezi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina:-

Mheshimiwa Omari S. Kwaangw', Mwenyekiti; Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mjumbe; Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mjumbe; Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mjumbe; Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mjumbe;

Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mjumbe; Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, Mjumbe; Mheshimiwa Martha Mlata, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mjumbe; Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mjumbe; Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mjumbe; Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mjumbe; Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, Mjumbe na Mheshimiwa Oscar R. Mukasa, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa imani yao kwangu, kwa ushirikiano wao muda wote nilipokuwa natekeleza wajibu wangu kwa Taifa langu, kwa Jimbo langu, kwa Chama changu na kwa dhamira yangu. Imani huzaa imani, nawashukuru sana Wana Babati, bado nipo nao na sikuwaangusha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Omar Kwaang' kwa kuwasilisha maoni ya Kamati na nakushukuru kwa niaba ya wenzangu wanaokalia kiti hiki kwa kututakia heri. Pia Babati Mjini wamesikia sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuweza kutoa maoni yake kwa hiyo, namwita Dr. Ali Taarabu Ali ili tuweze kupata maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu sekta ya afya.

MHE. DR. ALI TAARABU ALI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, mwanzo namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kusimama hapa mbele yenu hivi sasa na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa kanuni za Bunge kanuni ya 99(7), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru viongozi wetu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Naibu Kiongozi Mheshimiwa Dr. Slaa kwa katuongoza vizuri katika kutimiza majukumu yetu kwa wananchi kwa kipindi chote cha miaka mitano tuliyokuwepo hapa Bungeni. Pia, namshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, kwa mchango wake mzuri katika kuandaa hotuba hii na katika majukumu yetu ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, nampongeza Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Waziri pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Aisha Kigoda, pamoja na timu nzima ya watendaji katika Wizara hii kwa kazi ya kuandaa hotuba yao na kuiwasilisha hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya bajeti zilizopita za Wizara. Sekta ya afya imekuwa ikipewa kipaumbele cha tatu kwa miaka mitatu mfululizo. Mgawanyo kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, unaonyesha kuwa sekta ya afya ilipangiwa kiasi cha shilingi bilioni 963. Kwa mwaka 2010/2011, Serikali imetenga sekta ya afya kiasi cha

shilingi bilioni 1205.9. Ukiangalia kwa uangalifu utagundua kirahisi kabisa kuwa afya imezidi kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wa Tanzania umekuwa mgumu na hii inatokana na uchakavu wa majengo. Hospitali nyingi za mikoa zimekuwa na uhaba wa vitendea kazi na majengo chakavu. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 7,446,932,000/= kwa ajili wa ukarabati wa hospitali za mikoa. Pia kiasi cha shilingi 5,012,755,000/= zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kwa Mikoa ya Pwani, Mbeya, Shinyanga, Singida na Manyara. Kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na mahitaji yaliyopo katika hospitali za mikoa.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa hospitali imelisahau Jiji la Dar es salaam. Mkoa wa Dar es salaam ambao una wakazi wengi na kuwepo kwa maofisi makubwa hakuna jitihada za makusudi zilizofanya ili kupambana na msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Mwananyamala, Wilaya ya Kinondoni, hospitali ya Temeke na pia hospitali ya Amana, Wilaya ya Ilala.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kwa macho yetu sisi wenyewe akinamama wakiwa wamelala chini kwa ukosefu wa vitanda, magodoro, shuka, vyandarua na ufinyu wa wodi. Ni jukumu la Wizara na Halmashauri kupanga bajeti toshelezi ili kuimarisha utoaji wa huduma katika Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha, bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetengewa kiasi cha bilioni 678,421,483,000/. Hii inajumuisha fedha za Serikali ambazo ni sawa na asilimia 35 na asilimia 65 zinazobaki ni fedha za wahisani. Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali ifanye juhudzi za makusudi ili kuweza kukuza mapato ya ndani ya nchi ili kuepuka utegemezi kutoka wahisani, kwani hotuba mbadala ya Bajeti ya Kambi ya Upinzani lilikwishaonesha vyanzo vipyta vya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa mipango ya maendeleo ya kiasi cha bilioni 448,422,515,000 kwa mwaka 2010/2011 ndani ya Wizara ya Afya, ni jambo zuri linaloashiria kuboresha huduma ya afya hapa nchini. Kambi ya Upinzani inauliza, kweli utegemezi uliopo hususan katika mipango ya maendeleo tutafikia lengo la mipango yetu?

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hicho, fedha za wahisani ni shilingi bilioni 438,568,754,000/= na fedha zinazotolewa na Serikali yetu ni kiasi cha shilingi bilioni 9,873,761,000/= tu. Ukiangalia ni kwamba wahisani wanachangia kwa asilimia 97.8 na Serikali yetu inachangia kwa asilimia 2.2.

Mheshimiwa Spika, hii ina madhara kwa Watanzania kwa kuwa endapo wahisani watajitoa ina maana miradi ya maendeleo ya Wizara haitatekelezwa hivyo kupelekeea ukosefu wa huduma bora kwa wananchi wa Tanzania. Kambi ya Upinzani inahitaji sana majibu ya kutosheleza kwa nini Wizara inategemea sana wahisani kwa ajili ya maendeleo

ya Miradi? Hili ni tatizo kubwa kwani kushindwa kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha kuridhisha ni sawa na kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatekeleza mipango mingi iliyojiwekea ili kuimarisha huduma za afya hapa nchini. Miongoni mwa Mipango mikakati ya Wizara ni Pamoja na *Human Resource for Health 2008-2013, Health Sector Strategic Plan (HSSP III) 2009-15* pamoja na *Primary Health Care Development Programme (PHCDP) 2007-2017* au kwa Kiswahili Mpango Maalum wa Afya ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mikakati hii inaonyesha malengo ambayo Wizara imepanga kuyafikia. Hata hivyo, cha kushangaza ni kwamba, bajeti ya Wizara ya afya kila mwaka inakuwa na malengo tofauti na yaliyoainishwa katika mipango mikakati.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajiliza ni kweli Serikali iko makini kutekeleza hiyo mipango mikakati au malengo yake yamewekwa tu katika makaratasi kwa lugha nzuri bila utekelezwaji?

Mheshimiwa Spika, vifo vinavyohusiana na uzazi vinaongezeka. Kila mwaka wanawake mia tano na sabini na nane (578) katika kila wajawazito laki moja wanakufa kutokana na matatizo ya ujauzito wakati wa kujifungua. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kiasi cha takriban bilioni 20 zilizotengwa na Wizara kwa ajili ya kupunguza vifo vyta akinamama wajawazito na watoto wachanga kwa mikoa mitatu ya Tabora, Mara na Mtware hazitoshi. Pia tunaishauri Serikali kuwa mradi huu utekelezwe katika mikoa yote ili kuweza kupunguza vifo na pia kuleta uwiano katika utolewaji na usambazaji wa huduma za afya nchini kama dira ya Wizara inavyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la vifo vyta akinamama wajawazito na watoto wachanga, pia inatubidi kuweka malengo na mikakati madhubuti ambayo itapelekea kutatua matatizo na changamoto zilizopo katika sekta ya afya. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi, kiasi cha bilioni moja kilielekezwa katika kulipa mshauri (*consultancy fees*). Je, haya ndio matumizi ya kupunguza vifo vyta uzazi? Hivyo, inabidi Wizara ikubaliane na kambi ya Upinzani kuwa imeshindwa kufikia malengo kama yanavyoainishwa katika MKUKUTA ya kupunguza vifo hadi kufikia 265 kwa wajawazito 100,000 kufikia mwaka 2010. Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali inabidi ijipange upya ili iweze kufikia malengo yatakayoainishwa katika utekelezaji wa awamu ya tatu ya MKUKUTA kwa kutenga fedha zinazotosha.

Mheshimiwa Spika, tatizo la utapiamlo ni jambo la kutiliwa maanani na Serikali hususan Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya watoto 600,000 wenye umri wa chini ya miaka mitano wanakisiwa kufa kwa kukosa lishe bora kwa muongo (miaka 10) uliopita. Lishe bora ni msingi wa afya na maendeleo. Lishe bora inaleta kinga imara mwilini, upungufu wa maradhi na afya njema kwa watu wa rika zote.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa rasilimali watu katika sekta ya afya bado ni tatizo. Mpango mkakati wa rasilimali watu (2008-13) unalenga katika kuimarisha rasilimali watu

katika sekta ya afya na angalau asilimia ishirini ya bajeti ya Wizara ielekezwe kwenye kutatua tatizo hili. Hali ilivyo hivi sasa, ni kuwa rasilimali watu imetengewa asilimia nne tu ya bajeti nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), unalenga kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwepo zahanati katika kila kijiji, kituo cha afya katika kila Kata na hospitali katika kila Wilaya. Aidha, Serikali inalenga kupandisha hadhi hospitali za Mikoa kuwa za Rufaa. Kujenga zahanati au kituo cha afya, ni jambo moja, lakini kuwapata Madaktari na Wauguzi na wataalam wengine wa Afya katika vituo hivi ni jambo lingine. Kulingana na taarifa ya Wizara ya Afya, Tanzania ina watoa huduma wa afya asilimia 32.1.

Hivyo sekta ya afya inakabiliwa na upungufu wa 67.9% ya watoa huduma, hivyo tunashauri Serikali kufanya juhudhi za makusudi ili kuweza kupunguza tatizo la ukosefu wa watumishi katika vituo vya afya vinavyoanzishwa kwani ukosefu wa wataalam kutasababisha upotevu wa maisha ya watu wasio na hatia kwa sababu ya kuhudumiwa na watendaji wasiokuwa na ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajuliza ni kweli bajeti zilizopangwa katika Mipango Mikakati kama *Human resource for Health Strategic Plan 2008-13 na Health Sector Strategic Plan (2009-17)* zinafanyiwa kazi au zimebekwa tu kwa ajili ya kufurahisha wahisani?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara iweke wazi ripoti iliyotolewa na Utumishi mwaka 2009 inayoelezea idadi ya wafanyakazi wa afya Tanzania. Ripoti hii iwekwe wazi ili itumike katika kupanga mipango ya rasilimali watu katika sekta ya afya. Tunaamini kuwa ripoti hii imehifadhiwa na Wizara na sasa wanatumia makadirio kupanga mipango ya afya ambayo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinazotolewa na *Council Comprehensive Health Plan (CCHP)* kuhusiana na watumishi wa afya kwenye wilaya zinatia shaka, ukilinganisha CCHP za Wilaya moja kwa miaka mitatu utagundua kuwa taarifa zinafanana hata pale ambapo watumishi huwa wamehama, wamefariki, wamestaafu au wapya wameajiriwa.

Mheshimiwa Spika, tumeshasema mara nyingi huko nyuma ya kuwa Tanzania, kwa mujibu wa takwimu za *WHO* za mwaka 2004, inao Madaktari 2.3 tu kwa watu 100,000, tukiwa nyuma ya karibu nchi zote ulimwenguni isipokuwa Malawi na Rwanda, wakati *WHO* yenye we inashauri nchi zetu zinazoendelea kuwa na angalau Madaktari 10 kwa watu 100,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo na juhudhi za makusudi zitakazofanywa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kutoa mafunzo kwa wataalam wa afya ili kuboresha utolewaji wa huduma inayofaa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Chuo cha Utunzaji wa Kumbukumbu za Afya (Moshi *Health Record – KCMC*) kilichoanzishwa na Wizara mwaka 1976 ikiwa mpaka sasa kinatoa mafunzo kwa ngazi ya cheti. Wanafunzi wa Chuo hicho huchaguliwa na Wizara ya Afya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini, Wizara ya Afya haiwatambui Wahitimu wa chuo hicho? Kwani kada hiyo imeondolewa katika Muundo wa Utumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matibabu nje ya nchi. Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kugharimia matibabu ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi kutokana na ukosefu wa huduma wanazohitaji hapa nchini. Kambi ya Upinzani hairidhishwi na mwenendo wa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 7,201,000,000 kwa ajili ya kugharimia matibabu hayo kwa mwaka 2010/2011. Fedha ambazo zinatumika kwa ajili ya matibabu nje ya nchi zingeweza kuimarisha taasisi tulizonazo ili ziweze kutumiwa na Watanzania wengi kwa ajili ya kupatiwa huduma. Wagonjwa wengi wamekuwa wakipelekwa nchi za nje kwa ajili ya matibabu ya moyo, figo na kansa. Tunashauri vitengo vya moyo na figo vilivypo katika Hospitali ya Taifa (Muhimbili), *KCMC*-Moshi na Hospitali ya Rufaa Mbeya viimarishwe ili kuweza kutoa matibabu kwa wagonjwa hapa nchini na sio Serikali kulazimika kupeleka wagonjwa mara kwa mara nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iimarishe hospitali ya Ocean Road ambayo inatoa matibabu ya Saratani. Kufanya hivyo kutawezesha kutoa matibabu kwa watu wengi hivyo kuimarisha huduma hizo hapa nchini na kuepuka kutenga fedha mara kwa mara kwa ajili matibabu nje ya nchi kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na Saratani. Uwezo wa kufanya hivyo tunao na itaimarisha vipimo na matibabu kwenye hospitali za rufaa kinachohitajika ni juhudzi za makusudi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana pia kutayarisha utaratibu kwa kuwaleta wataalam wa nje kuja hapa na kutoa tiba husika kwa wagonjwa hapa hapa nchini badala ya kusafirisha wagonjwa kuwapeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali hugawanya fedha kwa ajili ya dawa na vifaa katika ngazi za hospitali (Rufaa, Mkoa na Wilaya) na vituo vya afya ya msingi (vituo vya afya na zahanati) kulingana na *allocation formula* na kuziingiza moja kwa moja katika akaunti ya Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*). Katika kuagiza dawa na vifaa, hospitali huandika mahitaji yao na kuzipeleka *MSD* moja kwa moja tofauti na vituo vya ngazi za msingi ambao hupitisha kwa Mganga Mkuu (Mfamasia) kwa lengo la kuhakikiwa na kisha kupelekwa *MSD* na Mfamasia wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na matatizo mengi ya usambazaji wa madawa katika hospitali za Mikoa ambapo kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na upelekaji wa madawa yaliyokwisha muda wake wa matumizi na pia kuwepo na ucheleweshaji wa upatikanaji wa dawa pamoja na vitendanishi ambazo Halmashauri wameshalipia fedha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwepo kwa utaratibu maalum utakaoratibu upelekwaji wa madawa katika uwiano sawa wa kuangalia idadi ya wagonjwa na idadi ya watu waliopo katika eneo husika. Pia tunashauri vituo vya *MSD* vilivyopo Mikoani (katika kanda) viimarishwe ili kupelekea huduma zinazotolewa zifike katika vituo vya huduma katika muda muafaka na haraka.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *Global Fund* ni moja kati ya wahisani ambao wamechangia Tanzania kwa kiasi kikubwa katika juhudzi zake za kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Mwaka 2009, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa *Global Fund* walifanya tathmini ya mahesabu ya mfuko huo hapa nchini kama moja ya shughuli zao za ufuutiliaji wa fedha wanazotoa kwa nchi mbalimbali. Katika ukaguzi wake waligundua mapungufu makubwa katika utekelezaji wa shughuli zinazofadhiliwa na *Global Fund* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna mapungufu mengi yaliyobainishwa na yanaihusu zaidi Bohari Kuu ya Madawa hapa nchini. Baadhi ya matatizo yaliyobainishwa na Wakaguzi wa *Global Fund* ni pamoja na utunzaji mbaya wa kumbukumbu, kuwepo kwa madawa mengi yaliyohifadhiwa stoo bila kusambazwa na upungufu wa sehemu za kuhifadhiwa madawa na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ripoti ya ukaguzi ya *Global Fund* ya mwaka 2009, ilionyesha kwamba kwa mwaka 2007 ukaguzi wa ndani uliofanywa na *MSD* uligundua dawa zenye thamani ya shilingi 163.2 milioni ambazo zilikuwa zimepotea au kuibowi. Vile vile ofisi ya ukaguzi ya *Global Fund* iligundua kuwa, mwaka 2007 kiasi cha dola za Kimarekani *USD* 2.4 milioni zilizotolewa na *Global Fund* kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa dawa, mafunzo na usimamizi wa taarifa hazikutumika kutokana na urasimu ulioko katika utawala wa *MSD*.

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo imeonya kwamba kama matatizo hayo hayatatatuwa yataapelekea kudhoofisha juhudzi za wahisani hao kushirikiana na Tanzania katika kufikia malengo yaliyopangwa ya kupambana na janga la UKIMWI na magonjwa mengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasononeka sana na jitihada ndogo za Serikali katika kupambana na matatizo yanayoikabili *MSD*. Ni dhahiri kuwa *MSD* ina udhaifu mkubwa wa kiuongozi na tuna wasiwasi kama watendaji wake wakuu

wanataaluma inayohusiana na kazi wanayoifanya. Muda katika usambazaji wa madawa ni jambo muhimu sana na hili anayelielewa vizuri ni yule mwenye taaluma ya madawa. Tunaitaka Wizara iwawajibishe viongozi wanaoiongoza *MSD* ili kuimarisha utendaji wake na kulinda heshima ya nchi katika sura ya dunia.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya imekuwa ikijitahidi kufanya kazi kwa bidii sana ila kumekuwepo na matatizo yanayojionyesha mara kwa mara wakati wa ukaguzi unaofanywa na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii inatufanya sisi tujiulize wenyewe kuwa hivi ni kweli Wizara imeshindwa kufanya juhudzi za makusudi kuondokana na haya matatizo au imekuwa inalea wazembe wachache walioko katika Wizara. Tungependa kupata maelezo ya kina kuhusu ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka unaoishia 2009 zisemazo kwamba:-

- (i) Mishahara yenyе jumla ya Sh.77, 707,817 ililipwa kwa wastaaifu, watoro na wafanyakazi waliokwishesafariki na uwezekano wa kurejesha fedha hizo ni finyu;
- (ii) Masurufu ya sh 312,751,754 yaliyolipwa kwa baadhi ya maofisa yalikuwa bado ya utata;
- (iii) Malipo ya Sh 156,976,512 yalifanywa bila kuwepo nyaraka ambatanifu za kutosheleza, hivyo uhalali wa malipo hayo haukuthibitishwa; na
- (iv) Pia kulikuwepo na masuala ya kifedha yenyе utata yaliyotokea tangu mwaka 2000 ambayo hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajuliza ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu waliobainika kuwa na utendaji mbovu kwa kusababisha ubadhirifu kama ripoti inavyoonyesha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali 2008 (*Public Finance Act*) inaelezea ni hatua gani za kuchukuliwa dhidi ya watu wanaobainika kuwa na utendaji mbovu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iihakikishe inafanya juhudzi za makusudi kupambana na watumishi wasio waadilifu ili kwa miaka ijayo ripoti za Mkaguzi Mkuu ziwe safi na huduma ya afya inatolewa kwa uhakika na kwa uwiano ulio sahihi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya usimamizi wa ukuzaji wa huduma bora za afya hususan vijiji kuitia Mpango Maalum wa Afya ya Msingi (MMAM). Mpango huu ungefahaa ufanyike sawia na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya watakaotoa huduma katika vituo hivyo na kuhakikisha kunakuwepo kwa huduma muhimu kama nishati ya umeme (umeme nuru), maji na kuwepo kwa miundombinu bora.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa malaria; kambi ya upinzani imekuwa inaona juhudzi zinazofanywa na Wizara katika kupambana na mbu waenezao ugonjwa wa malaria kwa kusambaza vyandarua kwa wananchi. Ikumbukwe kuwa ugonjwa wa malaria unaongoza kwa idadi kubwa ya vifo hapa nchini, hivyo ni jukumu la Serikali kuwalinda wananchi wake dhidi ya gonjwa hili. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuimarishwa kwa usafi wa mazingira pembezoni mwa makazi ya wananchi ili kutokomeza mazalia ya mbu na kupunguza kasi ya malaria na kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Virusi nya Ukimwi na UKIMWI. Inakadiriwa kuwa watu milioni 1.4 nchini Tanzania wanaishi na virusi vinavyosababisha UKIMWI na kati yao karibu watu 440,000 wanahitaji dawa zinazopunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI na mpaka hivi sasa watu 202, 845 wako kwenye ART. Tatizo la lishe bora kwa wagonjwa wa UKIMWI limekuwa ni kubwa sana na hali hii huzorotesha juhudzi zilizofanywa za kuhakikisha kuwa wanapata dawa. Wagonjwa wengi wamekuwa wakichukua dawa za kupunguza athari za ugonjwa wa UKIMWI na kuziweka nyumbani bila kuzitumia kutokana na ukosefu wa lishe bora. Hivyo, kuwepo na mpango utakaosaidia wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU wanapata lishe stahiki.

Mheshimiwa Spika, karibu watoto 970,000 wamekuwa yatima kutokana na ugonjwa huu wa UKIMWI. Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2001 inasisitiza kuwa ugonjwa wa UKIMWI ni janga la Kitaifa na litapewa kipaumbele kwenye mipango yote ya Kitaifa. Vita dhidi ya janga hili inapata changamoto kutokana na ukosefu wa fedha ambapo Serikali inawategemea sana wahisani katika kupambana na janga hili. Kambi ya Upinzani hairidhishwi na juhudzi zinazofanywa na Serikali kupambana na maambukizi mapya. Juhudi za makusudi zinahitajika ili kuепusha jamii isitumbukie katika janga hili.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya inabidi ipunguze matumizi yasiyo na ulazima. Tumekuwa tukiidhinisha fedha kwa ajili ya matumizi ya Wizara na fedha zimekuwa zikitumika katika safari za ndani na nje ya nchi, masomo, posho, mafuta ya magari pamoja na ununuzi wa magari. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Afya imeweza kupunguza matumizi yasiyo na ulazima kwa asilimia 13. Hili ni jambo zuri ila tunapendekeza fedha ambazo zinatengwa kwa mwaka huu zielekezwe zaidi katika masuala yanayolenga kufaidisha Watanzania walio wengi na sio wachache walioko maofisini.

Kielelezo A. Kinachofuata kinaelekeza mabadiliko ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
Matumizi yasiyo na Ulazima.

Mheshimiwa Spika, huduma ya dharura bado sio nzuri. Tanzania inakabiliwa na tatizo la mfumo wa huduma ya dharura amba ni duni na mbovu sana, hii husababisha watu wengi kupoteza maisha kwa kukosa huduma hii muhimu, waathirika wakuu wa ukosefu wa huduma bora ya dharura ni akinamama wajawazito. Tafiti zinaonyesha kuwa vifo vingi nya wajawazito na watoto wachanga vinachangiwa na ukosefu wa huduma

bora ya dharura. Takwimu zinaonyesha asilimia tano tu ya vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini ndizo ambazo zina huduma ya dharura (*Emergence Obstetric Care*).

Kambi ya Upinzani inahitaji maelezo ya kina kwa nini mradi wa kupeleka *ambulance* za magurudumu matatu kwenye maeneo ya vijijini haujaanza kufanya kazi hadi hivi sasa na ulikuwa tayari umetengewa fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009 ili kuokoa maisha ya akinamama wajawazito?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatekeleza wajibu wake wa kidemokrasia wa kutoa maoni ili basi kambi ya chama kinachotawala ifanyie kazi kwa maslahi ya Taifa. Sisi tunasubiri tupewe ridhaa na wananchi ili tutekeleze mipango hii ambayo wenzetu mmeshindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali kwa yote uliyowasilisha, ila hili la mwisho nadhani itabidi msubiri muda mrefu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, timesikia maoni ya Kamati na maoni ya Upinzani kama ilivyo taratibu, sasa ni zamu ya wachangiaji. Nina orodha ndefu kidogo lakini kuna ambao hawajachangia ndiyo watapewa kipaumbele cha kwanza kabisa amba ni Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Vita Kawawa, hao wanne hawajachangia.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia mara moja ambao ndiyo watapewa kipaumbele cha pili ni Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Peter Serukamba, nadhani hawa watapata nafasi.

Waliochangia mara mbili sina hakika kama watapata nafasi, nao ni Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Lucy Owenya.

Kama ilivyo utaratibu wetu sasa tutaanza na wale ambao hawajachangia, wa kwanza mionganii mwao ni Mheshimiwa John Malecela na wakati huo Mheshimiwa Margreth Mkanga ajiandae.

MHE. DR. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuwa mchangiaji katika hoja hii ya Wizara ya Afya. Ningependa niseme kwa Watanzania wenzangu na nianze kwanza bahati mbaya nitumie neno la kigeni lakini baadaye nijaribu kulitafsiri. Nalo ni kwamba *do not judge us from the highest we have archived but judge us the depth, from which we have emerged.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania mtu asituhukumu kwa ngazi tuliyofika, atuhukumu kutokana na shimo tulilotoka, maana yake ni kwamba mara nyingine humu watu tunajilaumu kupita kiasi, Tanzania ilipokuwa inapata uhuru tulikuwa na madaktari watatu, Dr. Mwaisela, Dr. Mwanjisi na Dr. Mtawale. Huko ndiko chini tulikotoka na leo tupo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili mwanzo kwa sababu wenzetu hawa wa Upinzani na sina haja ya kulumbana nao, kila kitu kinachofanyika humu wao kwao hawakioni ni kibaya tu. Kila kinachofanyika ni kibaya tu. Nasema tukumbuke kwa wananchi ninyi Wapinzani endeleeni kusema, hakuna jema lililofanyika lakini kwa Watanzania wanaojua tulikotoka tulipofika na tunakokwenda wajue kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya makubwa na itaendelea kufanya makubwa na ndiyo sababu tutaendelea kutawala kwa muda mrefu ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake katika nchi hii, kwanza tukiangalia katika Awamu ya Nne kwa upande wa afya. Pia nimsifu Dr. Mwakyusa, mtu ambaye ni mnyenyeketu kwa watu, mtaratibu, mfanyakazi hodari na ndugu yangu Naibu Waziri wa Afya, Aisha Kigoda ambaye majibu anayotujibu humu utafikiri huyu mama ni *working dictionary* la Wizara ya Afya, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sababu katika Awamu ya Nne nimeona maendeleo makubwa sana Wizara ya Afya, nimeona suala la UKIMWI kuwa kuna utaratibu mkubwa sana na unaotumia fedha nyingi kwa sababu ya UKIMWI, tumeona Chanjo na hata haya ndiyo mazuri ambayo watu huwa hawayasemi. Tanzania ilipata medali ya dhahabu kwenye Umoja wa Mataifa kwa sababu tulikuwa nchi mojawapo ya kwanza katika suala la Chanjo ya watoto, lakini kwa wenzetu hakuna lililofanyika.

Mheshimiwa Spika, tumeona suala la Malaria mpaka sasa tunasema maelefu ya vyandarua vimegawiwa, hivi Serikali ifanye nini? Ibebe watu migongoni ndiyo waseme imefanya kazi? Tumeona mradi wa matende Tanzania na mradi huu sehemu ya Pwani umesaidia wengi ambao huko siku za nyuma ilikuwa hata kusema habari za Matende kwenye hadhara ilikuwa kama ni jambo la aibu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kama utangulizi sasa nirudi kwenye Jimbo langu mwenyewe. Napenda kusema kwanza nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mtera, ambao tumeshirikiana nao na nathubutu kusema hapa hadharani kwamba, katika Jimbo la Mtera sasa tunayo zahanati kila kijiji kilichoandikishwa. Nafikiri hii ni hatua kubwa sana ambayo tumeifikia na ndiyo sababu ningependa kutoa ushauri kwa Waziri kwamba suala la Vituo vya afya tungeliana kwenye Tarafa kwanza, suala la zahanati tuende kwa kila Kijiji, baadaye tukimaliza hii mipango ya kituo cha afya kila Tarafa, Zahanati kila Kijiji sasa ndiyo tuende kwa mpango wa kuongeza Zahanati.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nichukue nafasi hii ya kumshukuru sana na kumpongeza Waziri Mkuu kwa jinsi alivyoweza kuongoza Serikali kwa niaba ya Rais katika Bunge hili, kwa kweli anastahili sifa na pengine nirudie tena kwamba

Mheshimiwa Spika na Waziri Mkuu Mungu awajalie ili muweze kurudi tena kwenye Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi napenda kukuhakikishia kwamba siyo urudi tu kwenye Bunge hili lakini nitafanya kila litakalowezekana kwamba uwe Spika tena ili tuweze kupata ari yako na utumishi wako ambao ningesema kwamba ni utumishi ambayo umetukuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina maombi kwa Waziri wa Afya, baada ya kusema haya niliyosema, ningependa kutoa maombi yafuatayo, kwanza nawashukuru Watumishi wote wa Wizara ya Afya wa ngazi zote kwa kufanya kazi nzuri kwa wananchi na katika mazingira magumu, lakini hata hivyo leo hali ya Tanzania ni bora zaidi hata mara nyingine kuliko majirani zetu, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, nina maombi yafuatayo kwa Mheshimiwa Waziri, kwanza kwa kuwa Jimbo la Mtera ndiyo la kwanza ambalo limefika *stage* ya kuwa na zahanati kila kijiji, tunaomba kila zahanati iwe na darubini *otherwise* watu watakuwa wanatibiwa tu wanakwenda wanaulizwa kichwa kinauma unaandikiwa aspirin au unaandikiwa panado au unaandikiwa kwamba una malaria, sasa tukiwa na darubini tutakuwa na hakika kwamba hiki ni kichocho ama ni malaria, kwa hiyo, naomba hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, katika Jimbo la Mtera naomba hivi vitendea kazi ni lazima wawepo watu ambao wanaweza wakavitumia kwa ujuzi, visiletwe tu ni lazima wale watakaovitumia wawe na ujuzi wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa vipimo vya kupimia UKIMWI sasa maadam tuna *dispensary* kila kijiji watu wapime UKIMWI kwenye vijiji vyao wasilazimike tena kusafiri kwenda hospitali za mbali kwa ajili ya kwenda kupimwa. Hapo hapo dawa za kurefusha maisha sasa zigawiwe huko huko kwenye zahanati za vijiji vyao. Nina hakika wananchi walipokuwa wanajitolea kufanya kazi ya kujenga zahanati hayo ndiyo matumaini waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu kwa Waziri ni kutuongeza Watumishi wa Afya, kwa sababu mahali pengine unakuta Zahanati nzima ina mtumishi moja tu, najua ni matatizo lakini pamoja na matatizo hayo, hilo ningeliomba kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia suala la dawa za *TB*. Watu wanaougua *TB* waweze kutibiwa kwenye *dispensary* za vijiji vyao badala ya kwenda masafa marefu ili kupata huduma hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilisema sitakuwa maneno mengi kwa sababu Wizara hii naridhika na kazi ambayo wanaifanya na namwomba Mwenyezi Mungu waendelee na kazi hiyo njema. Kwa wananchi wa Jimbo la Mtera nataka niwahakikishie kwamba, hatua ambayo Mtera tumefika ni kubwa sana na nawaomba na kuwasihhi tuendelee kuwa pamoja wasisikie haya maneno ya hovyo hovyo, tuendelee kuijenga Mtera na tutajenga mpaka watu watuonee wivu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa John S. Malecela na baadhi yetu ambao tumefanya ziara Mtera kwa kweli tunaonea wivu maendeleo mazuri ya Mtera. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu kwangu, ndiyo maana nilikaa kimya na mengine sikuyachangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na shukurani kwa Chama changu cha Mapinduzi, ambacho kimeweka mfumo ulioturuhusu watu wenye ulemavu kama akina Mkanga kuingia humu Bungeni kwa kupitia Viti Maalum ndani ya UWT, nashukuru sana. Mfumo huu ndiyo umeniwezesha kuwepo hapa na naamini kwa miaka mitano iliyopita, yale mambo ambayo Mungu alinijalia kuyatekeleza kwa ushirikiano wa chama changu, UWT, Serikali, Waheshimiwa Wabunge wote, Mawaziri na watu wenye ulemavu wenyewe kwa kunisaidia kunipa mawazo, maelekezo na kila kitu. Naamini nimejitahidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ambayo watu wenye ulemavu mambo yao yamo mle, sijui kwa vyama vingine lakini, kwa Chama Cha Mapinduzi kuna ukurasa mzima kabisa, wenye maelekezo ya nini anayehusika aweze kukifanya. Namshukuru sana Mungu na wote ambao nimekuwa pamoja nanyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili la Tisa sioni aibu kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote walishiriki katika masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu. Kuna waliowanunulia vifaa, kuna michango ile ya Mfuko wa Elimu ambapo Bunge kama Bunge lilihusika kuchangia katika masuala kama hayo. Kwa kweli, kwa niaba ya wenzangu natoa shukurani za dhati kabisa kwamba, Bunge la Tisa niseme ukweli limekuwa wazi na limejitahidi kusaidia jamii hii ya watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri tu, kwa kweli inaeleweka, ina mambo mengi lakini inaeleweka, pamoja na kwamba changamoto bado ziko nyingi na changamoto ni sehemu ya maisha. Lakini shukurani zangu zaidi kwa Serikali na Wizara ni katika hali ile ya kuchapuka, kuongeza kasi, kuandaa Sheria ya Watu wenye Ulemavu, ikafikishwa Bungeni na sisi tukaipitisha na Mheshimiwa Rais nimshukuru sana amekwishaidhinisha kwamba, Sheria hii ni halali katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini hili ninalishukuru? Mimi na wenzangu wenye ulemavu tumelipigania kwa muda mrefu lakini hayawi hayawi, hatimaye ikawa na Sheria hii ndiyo ukombozi wetu sisi kwamba, masuala ya kisasa yatashughulikiwa kisheria na siyo hisani iliyowahi kutumika kwamba, aah ni kwa hisani, ooh kuwasaidia hapana, ni haki na wajibu na sisi wenye ulemavu, tuna wajibu humu ndani. Lakini pia ni haki zitakazoweza kutekelezwa kisheria kama ilivyo kwa makundi mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalishukuru Bunge, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wala hakuchelewa akasaini, mambo yamekuwa kama yalivyo. Ninaloomba, naendelea kusisitiza kama ilivyokuwa kasi ya kuandaa ya Muswada ule, basi na kasi ya kuandaa Kanuni na Taratibu iwe ile ile kusudi Sheria hii mwakani tu Julai, Septemba au Oktoba huko basi ianze kutumika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba Sera ya Ugatuaji Madaraka kwenye Halmashauri hasa kwa Idara ya Ustawi wa Jamii, iharakishwe kwa sababu katika maboresho ya mwanzo ya Serikali za Mitaa haikuwepo hiyo, lakini sasa haja imeonekana, iharakishwe kwa sababu ni Halmashauri chache tu ambazo zimekwishaajiri Maafisa Ustawi na Maafisa Ustawi hawa kazi zao ndizo hizo za kuhangaika na watu wenye ulemavu, wazee na nini. Wapo Maafisa Maendeleo, lakini nadhani tunawatwika mzigo mzito kwa shughuli ambazo zingefanywa na Wataalam waliosomea hiyo aina nyingine ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ugatuaji huu uendelee kwa sababu vinginevyo mambo bado yanakwama, watu wenye ulemavu bado wanahangaika haingaika huko katika Wilaya zetu na katika Halmashauri zetu jinsi ya kushughulikiwa. Mara waambiwu uende kwa Maafisa Maendeleo, Afisa Maendeleo naye ana shughuli zake kwa hiyo, ningeomba hilo liharakishwe.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kusikia kwamba, kuna ukarabati unaoendelea katika makazi ya watu wenye ulemavu na wazee, katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa kweli, hili nalishukuru kwa sababu hali ya makazi ya wazee na wenye ulemavu yale tuliyonayo ilikuwa ni mbaya sana kwa sababu hata huo ukarabati ni zamu kwa zamu na siyo yote kwa sababu kwa hali ya fedha tuliyonayo ni hatua kwa hatua. Makazi haya mengi miundombinu ndiyo imekwishaharibika, vyoo hakuna na mfano ambaao niliutoa hapa nashukuru sana kwamba, kwa kuweza kushauriana na Wizara mara kwa mara Fungafunga mwaka huu wamesema wanaikarabati na ndiyo niliyoitolea mfano kwamba, uuh mambo pale ni magumu kweli; choo kimoja, umeme wamekatiba, wababa wale wanatambaa kwenda maliwato kwa kushika kuta kwenye umeme ambaao haupo. Kwa hiyo, Watendaji wale wakiamka mambo yanakuwa ni ya ajabu kweli.

Kwa hiyo, nashukuru kwa hilo kwamba ni Fungafunga, lakini si Fungafunga tu, makazi haya mengi yalijengwa enzi zile yamechakaa, hivyo ukarabati huu uendelee kuharakishwa hatua kwa hatua ili angalau hali hizo za kudhalilika wazee wetu hawa wenye ulemavu zisiwepo.

Mheshimiwa Spika, katika makazi hayo hayo nina suala zima la ujumla, suala la Matibabu kwa watu wenye ulemavu na wazee. Nashukuru kwa wazee, hapa Serikali imekwishesema kwamba, baada ya kuangalia angalia kuna mambo mazuri yanafanyika, lakini kwa watu wenye ulemavu bado kwa sababu gani, katika Sera hii imechanganuliwa kwamba, wazee watatibiwa bure, watoto wadogo wa miaka mingapi, sijui na wa magonjwa gani, lakini kwa watu wenye ulemavu haijakaa sawasawa, haisemi wazi kwa hiyo, bado wanapata danadana kudandishwa dandishwa wanapokwenda kupata huduma

za matibabu, dawa hakuna wanaambiwa wakanunue na walio wengi wa hawa wenzangu ni wale waliosuswa hata na familia zao na hawawezi kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba basi hili dirisha maalum la wazee waliloshauriwa kwamba kila hospitali itenye kwa huduma basi liwe *clearly* kabisa kwamba na hata watu wenyewe ulemavu waliopo kwenye makazi na wale ambao hawako kwenye makazi, vinginevyo wanaendelea kudhalilika.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ustawi wa Jamii, ina watumishi mbalimbali, Manesi, na wengine, kinachosikitisha bado naendelea kupata malalamiko ni kwamba, watumishi hawa walioko hasa kwenye makazi mbalimbali tuliyonayo, kwenye vyuo, hawaangaliwi sawasawa kama watumishi wengine wa Wizara ya Afya. Hawapandishwi vyeo, mishahara haileweki na mpaka wanajiuliza, sisi tuko kwenye kada ipi ndani ya Wizara ya Afya?

Kwa hiyo, ningeomba kabisa kwa sababu ilisemekana kwamba, mnarekebisha mfumo wa utendaji sijui, hebu na hawa waangaliwe sawasawa. Kuna manesi ambao wamekaa tu pale miaka 20 katika makazi hawajui hata linaloendelea, kuna walinzi, pamoja na kwamba walinzi hawapati promosheni lakini basi hata ile mishahara yao iende kwa wakati unaostahili. Hilo ni kuomba tu wajue kwa kweli hawa wako kwenye kada ya aina ipi.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kwamba, vyuo vya ufundu vya watu wenyewe ulemavu kadhaa vitaendelea kukarabatiwa, vitaendelea kununuliwa vifaa ili angalau wenyewe ulemavu hawa baada ya kupata ufundu na ujuzi, waweze kujiajiri wenyewe, kazi za ajira sasa hivi kwa kweli nyingi hazipo hata kwa watu ambao hawana ulemavu. Tunasisitiza kisera kwamba, waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kuuliza, hivi kuna mpango gani unaofanyika na Wizara kuweza kukifufua Chuo cha Ufundu cha Masiwani Tanga? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kengele hiyo.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Samahani, ya kwanza au ya pili? Naunga mkono hoja kama ni ya pili. Ya kwanza! Samahani Mheshimiwa...

SPIKA: Ni ya pili

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsanteni sana Mungu awabariki. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Margareth Mkanga, daima umekuwa ni mtetezi mzuri, tena shupavu wa ndugu zetu wenyewe ulemavu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kuna mtani wa Mheshimiwa John Malecela ameniletea habari, ila sitamtaja anashangaa kwamba, hivi kule Mtera nyumba nyingi ni fupi sana, mnatumiaje vyandarua? Kwa hiyo, hiyo nayo ni salamu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii.

SPIKA: Mzee umekasirika au? Aah, basi basi. (*Kicheko*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii na mimi kuipongeza Wizara hii ya Afya kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa, inayoeleweka ambayo imeonesha kabisa ni nini kinafanyika katika nchi yetu, mikoa mbalimbali, kazi mbalimbali na jinsi huduma zinavyozidi kuboreshwa ili kuweza kuwaleta wananchi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi za Wizara naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru akinamama wote wa Mkoa wa Mtwara ambao mwaka wa 2005 waliniwezesha kushinda uchaguzi na nikaweza kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Lakini, nawashukuru zaidi akinamama wa Mtwara Mjini, Masasi, na Wilaya ya Nanyumbu kwa moyo wao waliounesha wa kunichangia pesa kwa ajili ya kuchukua fomu muda utakapofika. Nasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mwenzangu pale Malecela amezungumza mazuri mengi ambayo yamefanywa na Chama chetu cha Mapinduzi ili kuboresha maisha ya wananchi. Pamoja na mambo mazuri yaliyofanywa naomba nami nichangie machache ili kuweza kuboresha zaidi kwenye sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwenye mikoa yetu tunashuhudia kwamba, kwenye vijiji tunapata zahanati, kuna vituo vya afya, hospitali zetu za Wilaya zinafanya kazi lakini bado kuna tatizo. Tatizo lililosalia sasa hivi katika hospitali zetu na vituo vya afya ni kutokuwa na dawa za kutosha. Wagonjwa wanakwenda kwenye hospitali zetu, wanapata vipimo mbalimbali lakini inapofikia hatua ya kupewa dawa, mara nyingi wamekuwa wakiambiwa waende wakanunue kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kwa sababu wananchi wengi sasa hivi wamekwishatambua kwamba, ukienda hospitali unaandikiwa chetu tu na kuambiwa nenda ukununue mwenyewe, wengi wanaoumwa hawaendi hospitali, wanajifanya madaktari na wanakwenda moja kwa moja kununua dawa kwenye maduka ya dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba Wizara na Serikali kwa ujumla kusimamia hili suala ili wananchi wanapokwenda kwenye hospitali zetu wapate huduma zote pale kwenye hospitali badala ya kuambiwa kwamba waende wakanunue vitu mbalimbali kwenye maduka ya dawa. Inafikia wakati hata *syringe* mtu anaandikiwa, *drip* anaambibiwa nenda kanunue. Kwa kweli hili suala naona bado ni tatizo kubwa kwenye huduma hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo lingine ambalo pengine hatujalionia. Hospitali zetu zilizo nyingi hadi hivi sasa vitanda havitoshi, shuka hazitoshi, unakuta kitanda kimoja wagonjwa wanalala mpaka watatu na hii siyo kwa Mkoa wa Mtwara tu, nilipata bahati ya kutembelea kwenye Hospitali yetu ya Dodoma, kwenye Wodi ya akinamama wajawazito, sikuamini macho yangu nilichokiona. Nilikuta akinamama wajawazito wanalala watatu kwenye kitanda kimoja. Sasa nikajiuliza, hawa akina mama ni wajawazito lakini wanalala kwenye kitanda watatu na *size* yenewe ya vitanda nya hospitali inaeleweka. Ningeomba sana Serikali iangalie juu ya kuongeza vitanda kwenye hospitali zetu pamoja na shuka.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala la shuka kwa sababu majuzi tu tumeshuhudia kwenye televisheni mtoto ametoka kuzaliwa leba anakwenda kulazwa kwenye kitanda ambacho hakina hata shuka. Lakini nilifurahi kidogo kwa sababu mfano ule uliotolewa ulikuwa ni Tanga, Mkoani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba sana rai kwa taasisi zile ambazo huwa wanatoa misaada na kusaidia wangejaribu kuisaidia Serikali pia katika kutoa vitanda na mashuka katika hospitali zetu ili wagonjwa wanapolazwa basi wajisikie wanalazwa kwa sababu kulazwa watatu katika kitanda kimoja kunaweza kumfanya mtu aombe ruhusa ya kurudi nyumbani kabla hata hajapata nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imetuelekeza kwamba tujenge Zahanati kila Kijiji, maeneo mengi tumeitikia wito, zahanati zinajengwa, naomba niwapongeze sana Wilaya ya Masasi wamejithadi kwa kujenga Zahanati kwenye vijiji vyetu na hasa kupitia mpango wa *TASAF*. Tunaishukuru *TASAF* kwani imetuwezesha sana kupata zahanati nzuri katika vijiji vyetu na nampongeza sana msimamizi wa *TASAF* Wilaya ya Masasi, dada yangu Neema, jinsi anavyosimamia na kuhakikisha kwamba pesa zinazopatikana kupitia *TASAF* kweli zinafanyakazi vizuri kwa kujenga zahanati zetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mkoa wetu wa Mtwara, Kata nyingi ziliitika wito wa kujenga vituo nya afya, lakini wameishia tu wananchi walipopokea wito wa kwamba kila Kata inahitajika kujengwa zahanati, wengi waliitika wito. Tofali zimefyatuliwa lakini baadaye hawajaona *support* yoyote inayotoka upande wa Serikali ili kuwezesha ufanisi wa kujenga vituo hivi nya afya. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atuelekeze hivi vituo nya afya tunavijenga kwa utaratibu upi kwa sababu michango ya wananchi tayari inajitokeza lakini kwa upande wa Serikali bado hatujaona jitihada za kutosha. Naomba sana kwa sababu maeneo mengi matofali yanaharibika. Kwa mfano, pale Wilaya ya Masasi kwenye Kata ya Lukuledi wananchi walifyatua matofali mengi sana, sasa hivi bado yapo, tunaomba tusaidiwe ili tuweze kuanza ujenzi huo wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya majengo ya kilichokuwa Chuo cha Wasioona. Hii itakuwa ni mara yangu ya pili kuzungumzia hili suala katika mikutano yetu hii.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki cha Wasioona sasa hivi hakina mwanafunzi hata mmoja kwa miaka mingi sana, ni chuo kikubwa sana chenye majengo mengi lakini kwa

masikitiko makubwa hivi sasa miaka inavyozidi kwenda majengo haya yanaharibika na mpaka sasa hivi Serikali haijachukua utaratibu wowote wa kuweza kuyakarabati.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilipozungumza, Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho alisema zilitengwa shilingi milioni 34 kwa ajili ya kukarabati chuo hiki, lakini hadi hivi leo ninavyozungumza chuo hiki hakijakarabatiwa. Sasa swalilangu, ni lini hiki chuo kitakarabatiwa ili kiweze kutumika katika matumizi mengine? Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliyahi kuandika barua Wizarani kwa ajili ya kuomba haya majengo ili tuweze kubadilisha na kuyatumia kwa matumizi mengine, kwa sababu kilipo hiki chuo pana sekondari.

Mheshimiwa Spika, tuliomba kwamba, kama Serikali haina mpango wa kutumia haya majengo, basi yakabidhiwe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili sisi tuweze kuyatumia kama sekondari, lakini jibu tulilopata tuliambiwa kwamba, haiwezekani Serikali bado ina mpango wa kuyaendeleza yale majengo. Naomba sana Serikali, zile ni pesa zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa chuo kile, tunavyoacha kinaharibika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Ya pili!

SPIKA: Ndiyo kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia yangu machache katika sekta hii ya Wizara ya Afya. Napenda kuwapongeza Waziri wa Afya, Mheshimiwa David Mwakyusa; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Asha kigoda; Katibu Mkuu wa Wizara, Bi. Blandina Nyoni; Mganga Mkuu, Dr. Mtasiwa; Wakurugenzi wote wa Idara mbalimbali katika Wizara na sekta hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hiyo, nami naomba niendelee kwa kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Namtumbo pia kwa kunipa fursa ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu na ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi hiki cha miaka mitano sasa inakaribia na tumeweza kushirikiana kujenga zahanati 11 katika kipindi hiki na hivyo naomba tu niendelee kusema kwamba kwa jinsi Wizara hii inavyosimamia sekta hii na changamoto zote wanazokabiliana nazo zinazoibuka siku hadi siku lakini viongozi wakuu wa Wizara wameweza kuzisimamia vizuri. Hivyo, naomba niseme naiunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kupitia sekta hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupa Halmashauri yetu ya Namtumbo, hasa kwa kutupatia watumishi kila mwaka, tulipowaomba wamekuwa wanatupa watumishi mwaka hadi mwaka. Mwaka huu 2010 naishukuru sana Wizara imetupatia watumishi 23 wakiwemo Madaktari, *Medical*

Doctors, Medical Assistants, halafu *Clinic Officers, Nurse Officers* na *Medical Attendants* na kadhalika. Kwa kweli asiyeshukuru kibaba hata ukimpa gunia hawezu kushukuru. Hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Namtumbo na Halmashauri yake napenda nishukuru sana Serikali kwa kutupa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niikumbushe Serikali tena pamoja na mazuri yote wanayotufanyia na tunashirikiana nayo, lakini bado Wilaya ya Namtumbo haina hospitali ya Wilaya na tunakaribiana na tatizo kubwa la wagonjwa ambao wanapaswa kupata tiba katika hospitali ya Wilaya, hivyo tunawasafirisha kwenda kilomita nyingi kupata tiba zao katika hospitali ya Mkoa na huwa tunawapa mzigo mkubwa sana hospitali ya Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, tunaomba kama Serikali ingetutengea fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ingepunguza mzigo huu katika hospitali ya Mkoa wa Ruvuma lakini pia ingesaidia kupata huduma karibu kwa wananchi waliopo Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ina zahanati zaidi ya 33 na tumejenga mpya 11 lakini pia tuna vituo vya afya vitano. Kwa hiyo, wote wanahudumiwa katika vituo hivi vya afya wanakwenda katika hospitali ya Mkoa wa Ruvuma, tunaomba Serikali ifikirie umuhimu wa kututengea fedha kuanzia ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Pia naomba katika mgao wa zahanati mwaka huu wa dawa katika napitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Namtumbo sijaona kama tumegawiwa zahanati mpya mafungu ya dawa. Inawezekana maombi yao njiani yamechelewa, tunaomba basi yakiwa yamefika katika meza za wahusika wafikirie kwamba tuna zahanati nyingine mpya ambazo zinahitaji kuanza ,zimekamilika toka mwanzoni mwa mwaka huu. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara nayo itufikirie kwenye hili la kutuingiza kwenye orodha ya zahanati mpya zitakazopata dawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niiombe Serikali kuongeza mafungu ya fedha za dawa kwa zahanati na vituo vya afya. Msemaji wa mwisho amezungumzia hapa kwa vizuri sana, lakini sisi tunaokaa kule vijijini, tunazaliana sana na idadi ya ongezeko la watu kwa maana ya watoto limeongezeka kupita mahitaji yale ya dawa yaliyopo sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba sana, tunapata malalamiko mengi yanahu sada kutoka vijijini, lakini yote yanatokana, ukitazama kwa undani zaidi utakuta kwamba zile fedha ambazo zinagawiwa kwa mafungu ya dawa za zahanati hazitoshelezi mahitaji na ongezeko lake ni kidogo sana. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara ipitie vizuri sana, itazame ongezeko la idadi ya watoto wanaozaliwa na mahitaji ya dawa yaendane pamoja na mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi, mchango wangu ulikuwa huo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii tena. Kwa mara ya pili, naomba nianze kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu, Blandina Nyoni, lakini pamoja kwa ujumla wataalam wote katika eneo hilo wamefanya kazi nzuri. Wote nadhani lazima tuelewe mambo tuliyopigia kelele

katika jumba hili, mengi wamejitätidi kupunguza kama vile zahanati zimeongezeka hadi kijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam walionichagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka kumi na pia kunichagua kuwa Mwenyekiti wao Mkoa wa Dar es Salaam na mara ya pili bila kupingwa kwa kipindi cha miaka kumi na nazidi kuwatakia waendelee kupata heri na baraka na naomba katika *SACCOS* ambazo nilikwishazianzisha waendelee kuzikumbatia na wengi wanawake wajiunge. Kwa sasa hivi *SACCOS* inayoongoza tayari ina wajumbe 2995 na mpaka sasa hivi wanawake wanakopa hadi shilingi 23 milioni.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba sasa nichangie kwa haraka maeneo mafupi kwa angalizo tu na ufuatiliaji, najua kazi nzuri amefanya. Naomba kuzungumzia kuhusu rasilimali. Bado idadi ya watumishi haitoshi kabisa na hilo amekiri yeye mwenyewe Waziri, lakini mishahara pia ya watumishi wauguzi ni midogo ukizingatia kazi zao, kwa kweli ni za muda mrefu sana maana yake wanaitwa usiku na wakati wowote wafikiriwe. Kuna uhaba wa watumishi wengi sana vijijini na ningombaa sana tufikirie kutoa motisha, *incentives* ya kuwapeleka vijijini, wapewe ongezeko la mshahara na pia wapatiwe nyumba za kuendelea kuishi.

Kuhusu vifaa na dawa, ni tatizo la siku nyingi lakini ili kusudi liweze kupungua basi naiomba Serikali ifikirie sana katika eneo la *MSD*, wawapatie hizi pesa ambazo wanazidai, wawakamilishie ili waweze kuendelea na kutekeleza wajibu wao katika maisha mazuri kwa binaadam.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kinga ya magonjwa, katika kinga ya magonjwa kama malaria. Tunashukuru sana kuwa tumepata vyandarua vingi kutoka *Global Fund* na maeneo mbalimbali, hiyo ni shukurani nyingi. Lakini bado nasema hiyo sio kuzuia na kumaliza matatizo ya ungonjwa wa malaria. Tunaomba basi mazalio hasa yafikiriwe katika kutokomeza ugonjwa huu. Naomba katika upande wa *cancer*, nashukuru sana MEWATA, Madakitari wamejitätidi kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuhudumia upande wa *cancer* ya matiti, *cancer* ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, naomba basi katika safari hii wafikirie sana katika eneo la *cancer* ya *colon* ambayo sasa hivi ulimwenguni ndio imekuwa ni tishio kubwa, najua mashine zake ni za ghali na bei ni kubwa, tuombe wajitätidi waweze kupata hisani na Serikali nayo iingie kuwasaidia. *Nutrition*, lishe ni kitu ambacho anajua kabisa Waziri lingenigusa, safari hii sitazungumzia mengi kuhusu lishe lakini ninachotaka kuomba tu, *chips* mayai, kuku zitatuua Watanzania tumeacha ulaji wetu wa siku zote tumeingilia mambo yasiyofaa. Lakini kwa sasa hivi nchi zilizoendelea zimepata dawa ambayo wanaweka katika mafuta yote yanayozalishwa na kuuzwa madukani ili watu kuwadhibiti sasa watakula mafuta wanayotaka kula lakini *cholesterol* hawataipata, *do that research* tuone na sisi kama tunaweza kufanikisha tukafika hapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa wazazi, asilimia 22 na 23 tu ndio wanaopata *contraceptive pills*, vidonge vyta kuzuia uzazi lakini hasa wanatakiwa wapate

asilimia 60 na hiyo haijafikiwa. Dawa ya *contraceptive* haionekani kabisa, Mheshimiwa Waziri na hiyo naomba unijibu kuhusu hilo. Bajeti ya *family planning* ni kitu muhimu sana lakini kitu ambacho sikiioni katika vitabu hivi, au imejificha. Vitabu hivi vya hesabu, nataka leo nielekezwe imejificha wapi, *family planning* ni kweli tunaitafuta, tulikuwa na UMATI ambao ulifanya kazi nzuri lakini haisikiki vizuri. Kwa hiyo, tunaomba kuwa madawa pia mengine ambayo yanaweza kupatikana yapatikane.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka jana nilishika fungu katika Wizara ya Michezo na Utamaduni kuhusu dawa ya makalio. Nashukuru Serikali imeliangalia hilo na imelifanya kazi, lakini nataka kutoa angalizo, sasa hivi katika Wizara hii ni kuwa wiki iliyopita kabisa kwenye magazeti wameandika kuwa dawa ya ngao ya kuulia mbu ndio inatumika sasa kupulizia katika mboga tunazokula.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo litaathiri maisha yetu na tutaishiwa nguvu tukafa. Jambo la muhimu sana kuhusu tiba shufaa, dawa ya MOFIN ni dawa muhimu sana kwa ajili ya maumivu, lakini inasikitisha sana haipatikani kwa urahisi. Asilimia tano tu inatumiwa hapa Tanzania kwa kadri ninavyoelewa ni kuwa Tanzania inatakiwa itumie kilo 30 za dawa ya MOFIN, lakini tunatumia kilo tano tu za dawa ya MOFIN na watu 95 waliokuwa na maradhi ya maumivu kama ya *cancer* bado hawajafikiwa kupata hiyo dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ni kuwa hawa watu tunawanyima haki na wanazidi kuteseka, dawa nyingine kama *PENSODINE* ni nzuri zinasaidia lakini hazifiki kuwasaidia vizuri kama MOFIN. *Injectable mofins* kweli zinaweza kuwa *abuse* kwa maana kwamba watu wengine wanaweza kuchukua vijana hasa kama vile ni dawa za kulevyta, lakini MOFIN ya maji ya kunywa wenyewe haina matatizo. Kwa nini basi Serikali isiangalie kuwa dawa hizi zote zikafikia mpaka maeneo ya mikoa kwa sababu ni dawa muhimu itakayosaidia.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kusikitisha ni kuwa *Ocean Road Hospital* ndio pekee iliyokuwa na kibali cha kuagiza dawa hii. Kwa nini iwe *ocean road* pekee? Lazima tunahitaji maeneo mengine ili tuweze kufikia katika mikoa yote mbalimbali. Sheria irekebishwe kuhusu hii, wauguzi wengine, *Medical Assistants, Nurses na Social Workers* nao basi angalau waweze kuruhusiwa ku-prescribe hizi dawa katika meneo mengine, kwa sababu ni ngumu wagonjwa kutoka Mikoa kutafuta hizi dawa.

Kwa hiyo, tunaomba mambo haya yafikiriwe, yaangaliwe vizuri kwa sababu wenzetu Kenya na Uganda wameweza kurekebisha sheria yao, lakini sisi katika sera za afya bado hatujaweka katika tiba ya shufaa vizuri. Lakini hata hivyo, kibali huwa kinatolewa na *Medical Officer*, kwa nini Waziri basi nae asiweze aka-regulate sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, *university students* nao ni muhimu sana wanaosomea waweze kupata *palliative care*. Upatikanaji wa *Mofin na Mogadin, pethodine* na nyingine naomba uwe wa haraka katika Mikoa yote kwa sababu watu wanaumia, watu wanateseka na ni mbali kwao kuja *ocean road*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kingine ambacho nataka kusisitiza, ni sheria ya UKIMWI kama alivyokwishesema mwenzangu Mheshimiwa Margareth. Hii sheria ya UKIMWI tunahitaji kanuni sasa isichukue muda mrefu kanuni ziwepo ili kazi iweze kutendeka kwa haki na kwa upesi. Lingine nakumbuka Balozi wa Marekani, Alphonso France alikutana na *committee* ya UKIMWI na nakumbuka niliwahi pale kuomba kuwa na sisi tunaomba msaada, basi tumpate mtu kama Oprah Winfrey na *celebrities* wengine kutoka Amerika kama vile wanavyokwenda Afrika Kusini na alikubali alisema ni wazo zuri, akatuambia basi tuandike barua tupeleke. Basi naomba Wizara hii pamoja na Kamati ya UKIMWI tulijengee hoja hili jambo mara moja tumpelekee barua anayengoja ili na sisi tupate *celebrities* hao waweze kufika hapa na waweze kutusaidia katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kila la heri wewe, uweze kupita Uspika, urudi tena kuwa kama Spika ndani ya nyumba hii. Mheshimiwa Anna Makinda naye namwombea aweze kupata nafasi nzuri kule, wamchague lakini pia Waheshimiwa wengine wote mlion humu, Mawaziri, Manaibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu najua mmefanya kazi nzuri, nawatakieni kila la heri muweze kurudi katika jumba hili, muweze kuleta maisha mema na bora zaidi. Kazi mliyofanya mpaka sasa hivi ndani ya Bunge hili ni kubwa, endeleeni tena Mwenyezi Mungu awajalie, naomba nimalizie dakika zangu ili nisipigiwe kengele ya pili.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi, bahati mbaya naumwa kifua, kwa hiyo, nitaongea kwa shida kidogo. Nashukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Afya. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwa kazi nzuri sana ambayo amefanya toka alipoteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu.

Nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kazi nzuri na kama ninavyoendelea kusema ameonesha kwamba wanawake wanawenza wakipewa nafasi. Nampongeza Katibu Mkuu, Blandina Nyoni, Mganga Mkuu wa Serikali Dr. Mtasiwa na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kwa wanawake wa Mkoo wa Iringa na wananchi wa Mkoo wa Iringa kwa ujumla kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kugawa Mkoo wa Iringa kuwa Mikoa miwili, Mkoo wa Iringa na Mkoo wa Njombe pamoja na kuongeza Wilaya ya Wanging'ombe. Tumefurahi sana na sisi tunapenda kuahidi kwamba kwa shukurani hizi tutazoa kura zote kwa Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri walijofanya na wananchi wa Mkoo wa Iringa, hakuna kura hata moja itakayopotea kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamshukuru sana na Mungu ambariki sana. Nasema haya pia kwa niaba ya Mikoa mingine yote iliyogawanywa ikiwemo Mkoo wa Geita na Mkoo wa Simiu, nina uhakika watafanya kazi hiyo hiyo kwa shukurani kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niipongeze Wizara hii kwa kweli imeboresha mambo mengi sana na tumeona mabadiliko makubwa sana katika sekta mbalimbali ambazo zinahusu hii Wizara. Lakini pamoja na hayo yote napenda nizungumzie uboreshaji wa hospitali ya Wilaya ya Mufindi pale Mafinga hasa ujenzi wa wodi ya upasuaji. Ile *theater* ya Mafinga ni ya muda mrefu sana haiendani na ongezeko la wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali, namwomba Waziri wangu Profesa Mwakyusa anapita pale barabarani, naomba apite aangalie *theater* ya hospitali ya Mafinga, ni ndogo na ningeomba iboreshwe, ipanuliwe, hii ni pamoja na wodi ya akinamama wajawazito, nashukuru wodi hii imeanzwa kujengwa na naomba ujenzi uende haraka na hivyo jengo likikamilika tuweze kupatiwa vifaa ili akinamama waondokane na msongamano wa kulala kitanda kimoja zaidi ya wawili na pia wakati wa *labour* kuwa watu wawili kwenye kitanda kimoja. Kwa hiyo, nina uhakika Serikali itatilia maanani hili.

Mheshimiwa Spika, naomba pia iangaliwe kwamba hospitali ambazo ziko barabarani kwa mfano, Mkoa wa Iringa ni Mkoa ambao upo kwenye *highway*, ajali ni nyingi sana. Kwa hiyo, wanakabiliwa na wagonjwa wengi zitiliwe umuhimu unaotakiwa, ziongezewe Madaktari, Manesi pamoja na vifaa kwa sababu zinahudumia wagonjwa zaidi ya wale wagonjwa ambao wako kwenye Mkoa. Wagonjwa ndani ya nchi na nje ya nchi.

Kwa hiyo, zitiliwe umuhimu unaostahili hii ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Illembula, Kituo cha Afya Makambaku, Mafinga yenewe, Iringa, Hospitali Teule ya Kilolo ambayo iko Ihula na jirani yangu ananiambia usisahau Hospitali ya Tumbi inayokabiliwa na wagonjwa wengi sana. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie suala la afya ya uzazi. Suala la afya ya uzazi halijatiliwa umuhimu na ninaipongeza Wizara sasa hivi imetengeza mpango mkakati ambao ni wa miaka mitano unaoongelea pia suala la uzazi wa mpango. Ninapenda Serikali iangalie kwa undani jinsi ya kuongeza fedha kwa sababu suala hili limesahaulika kwa muda mrefu na huduma hizi zimerudi nyuma na kufanya nchi hii kukabiliwa na idadi kubwa ya watu. Nina hakika mpango uliotengenezwa na Wizara utapata ufadhili ili huduma zake ziweze kuboreshwa na afya ya uzazi itiliwe umuhimu na ipewe kipaumbele ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa watoto wetu walioko mashulen ikiwemo na watoto walioko Vyuo Vikuu. Kujuu afya ya uzazi itasaidia pia kupunguza mimba mashulen au mimba katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la lishe. Suala la lishe ni muhimu sana lakini kwa muda mrefu Taasisi ya Lishe imekuwa haitilii uzito unaostahili suala hili, sielewi kwa nini wakati Watanzania wengi wanakabiliwa na lishe duni. Ili tuweze kuondokana na lishe duni, njia mojawapo ni kupunguza upungufu wa *micronutrients* kwa kuweza kuweka kwenye vyakula, kama tulivyopunguza upungufu wa *iodine* au madini joto kwa kuweka madini joto kwenye chumvi. Hivi ni kwa nini nchi hii hatuweki madini

au *micronutrients* kwenye unga au kwenye mafuta ili kupunguza mafuta ya kula ili kupunguza tatizo la upungufu wa viini lishe? Ninaomba Wizara iliangalie kwa undani kwa sababu tunakabiliwa na tatizo kubwa, tatizo ambalo limejificha na ningeomba pia Wizara inijibu ni kwa nini hajafanya kitu hicho wakati kilishafanyiwa utafiti? Hata Mkoa wa Iringa walifanya utafiti kwa kuweza kuchanganya madini kwenye unga, kwa kutumia wasagishaji wale wenye mashine ndogo za kusaga, kwa nini Serikali haijalitilia umuhimu suala hili?

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba nizungumzie ni kuboresha huduma au kupunguza vifo vya watoto na hasa huduma za mama, kupunguza maambukizi ya virusi kutoka mama kwenda kwa mtoto (*PMTCT*). Huduma hizi na Serikali imeanza kuziangalia lakini ninashauri zifike ngazi za chini. Mheshimiwa Malecela amezungumza kwa nini huduma hizi zifike kwenye ngazi za Kata kwa mfano hospitali zile za Vituo vya Afya na kwenye Zahanati za ngazi za Vijiji ili kuwapunguzia wagonjwa muda mrefu wa kutembea na pia huduma za MKOBA au huduma zile zinazotembea, *Mobile Clinics* ili tuweze kuwafikia watoto wote na kupunguza watoto wanazaliwa na virusi vya UKIMWI. Tunaelewa kwamba zaidi ya watoto 100,180 wanazaliwa na virusi vya UKIMWI kila siku na kama tutaboresha hizi huduma, tutakuwa tumeponganza vifo vya watoto 43,000 ambao wanazaliwa kila mwaka na virusi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhudumia akina mama wajawazito kwa kuweka huduma hizi ngazi za chini, ina maana kwamba tutaboresha na tutapunguza vifo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inaboresha huduma hizi ili ziweze kufikia ngazi za chini na pia kuweza kuweka usafiri kama vile ilivyokuwa imeahidi kuweka pikipiki za magurudumu matatu ili kuhakikisha kwamba wale akina mama wanaopata matatizo wanahudumiwa haraka na kupunguza vifo. Hilo pia ningependa Mheshimiwa Waziri aweze kulitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *MSD* imefanya kazi kubwa sana katika nchi hii. Inahakikisha kwamba huduma zinapatikana ngazi zote zikiwemo madawa na vifaa mbalimbali. Wamefanya kazi katika mazingira magumu, wale ambao tumeweza kutembelea *MSD*, tumeweza kuona jinsi wanavyofanya kazi. Wanakabiliwa na changamoto kwa sababu ya ukubwa wa kazi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge hoja mkono, *MSD* iangaliwe na madeni yapunguzwe. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja muhimu ya Wizara ya Afya kwani tunaamini kwamba bila ya afya njema hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana akina mama wote wa CHADEMA walioweza kunipigia kura na kuwa Makamu Mwenyekiti wa Wanawake wa CHADEMA Taifa. Lakini vile vile niwapongeze wanawake wengine wote kwa kuweza pia kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti wa kile kinachoitwa *Tanzania*

Women Cross Party Platform, Mwenyekiti wangu ni Mama Anna Abdallah. Kwa hiyo, nawashukuru sana. Naomba akina mama tushirikiane ili tuweze kuingiza Wabunge wengi zaidi wanawake katika uchaguzi unaokuja bila kujali itikadi zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya, Mheshimiwa Malecela hayupo. Nilikuwa napenda niongelee mambo fulani ambayo amezungumza. Namheshimu sana na ninaamini kwamba mambo aliyoazungumza ni masuala yanayohusu siasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tulipopata uhuru tulikuwa na Madaktari watatu kama alivyoeleza Mzee wetu Malecela na akasema tunaangalia shimo tulilotoka lakini hilo shimo ni refu kiasi gani kwamba kwa miaka 50 baada ya uhuru bado halijajaa? Kwa mfano, sasa hivi tunajua kabisa Wizara ya Afya ina upungufu wa watumishi kwa 62%. Hili ni tatizo kubwa, hatuwezi kulifumbia macho na kuambiwa kwamba sisi Wapinzani kazi yetu ni kupinga tu. Hili ni suala la msingi, ni suala ambalo linapaswa kuchukuliwa hatua. Lakini kilichonishangaza zaidi ni kwamba baada ya yote haya, Mzee Malecela bado ametoa maombi. Kwa hiyo inaonyesha wazi kwamba bado Wizara ina matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda niongelee suala moja. Suala la kupunguza vifo vy a wazazi. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 81, inaeleza wazi kwamba vifo vy a akina mama vitapungua kutoka 578 katika vizazi 100,000 hadi kufikia 265 mwaka 2010. Huu ni mwaka 2010 lakini bado vifo vy a wazazi viko pale pale. Kwa hiyo, lazima sisi kama Wapinzani au wananchi wanaopenda maendeleo ya nchi hii, waone kweli nini tunachokifanya. Hatuwezi ku-support pale ambapo tunaona kabisa kuna upungufu na ndiyo kazi ya Wabunge. Kwa hiyo, nilitaka kuzungumzia hilo vile vile. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba hivi majuzi tumeona katika Vituo vingi vy a Afya na nizungumzie kituo kimojawapo mahususi, Kituo cha Afya Mlalo ambacho kina uwezo wa kulaza wagonjwa 50. Kituo kile kina shuka moja, wagonjwa wanalala kwenye mifuko ya *sulphates*, hivi kweli katika miaka 50 tuache kuzungumzia masuala kama hayo, tuendelee kuipongeza Serikali kwa sababu ipi? Nadhani kuna hoja mahususi ambazo sisi kama Wawakilishi wa wananchi tunapaswa kuzisemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nizungumzie suala zima la malaria. Ni wazi kwamba Serikali imejitahidi, imetoa vyandarua lakini mimi siamini kama vyandarua ni suluhisho la malaria. Haiwezekani tuzungumzie vyandarua tu wakati mbu wako kila mahali. Suala la msingi hapa ni kuua mazalia ya mbu na tumeona nchi nydingi zikifanya haya, mfano hai ni kule Zanzibar wameweza kumwagilia dawa ya *DDT* na mazalia ya mbu yamekufa na tunajua kabisa sasa hivi malaria kule Zanzibar imepungua kwa kiasi kikubwa sana. Sasa suala la vyandarua ni la msingi lakini cha msingi zaidi ni kuhakikisha kwamba tunaua mazalia ya mbu na siyo kuwa na vyandarua peke yake kwa sababu mbu wako kila mahali.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine, ni suala la bajeti ya Wizara. Tunajua kwamba Tanzania ni moja ya *signatories* wa Azimio la Abuja ambapo walikubaliana kwamba kila nchi iweze kutenga asilimia 15 ya bajeti ya afya katika bajeti

kuu yaani asilimia 15 ya bajeti nzima ya Serikali itengwe kwa Wizara ya Afya lakini jinsi miaka inavyokwenda, asilimia ile inaendelea kupungua. Mwaka jana tulikuwa na karibu asilimia 11 lakini ukiangalia mwaka huu *total budget* ya Wizara ni asilimia tisa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba inaonyesha fedha zimeongezeka lakini ukiangalia kwa asilimia na tukizingatia jinsi gani sasa hivi idadi ya watu imeongezeka lakini vile vile maradhi yameongezeka kwa kiasi kikubwa sana, haijaongezeka. Sasa hivi masuala ya kansa yameongezeka sana, kisukari na magonjwa mengine ya kuambukiza yamejitokeza kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea Wizara au Serikali kwa ujumla ingeweza kupandisha asilimia ya bajeti ya afya ili iweze kwenda kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tukija kwenye suala zima la kupunguza vifo vya wazazi, wote tunashuhudia ni jinsi gani akina mama bado wanaendelea kudhalilika, kina mama wanaendelea kuzalia barabarani na hivi majuzi limetokea tukio kule Mwanza, mwanamke amefika katika Kituo cha Afya lakini hakupata huduma, akaambiwa aende kwenye hospitali nyingine katika hali ile na yule mama akajifungulia njiani na nilimwuliza Waziri wa Afya katika Kamati akasema kwamba analishughulikia. Kwa hiyo, anapokuja kutoa majumuisho yake atuambie lile tatizo limefikia wapi na wale watumishi wamechukuliwa hatua gani. Kwa sababu hili lisipodhibitiwa, kina mama wataendelea kudhalilika hapa nchini. Kina mama wataendelea kufariki na wote tujuu ni jinsi gani zoezi zima la kujifungua lilitivo na mchakato mgumu na ni suala la kuheshimika.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la msongamano katika hospitali hasa za miji mikubwa kama Dar es Salaam. Pamoja na ufinyu wa bajeti, atakubaliana nami kwamba hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam zimekuwa na msongamano mkubwa sana hasa hospitali ya Mwananyamala, mtu anafika hospitalini kuanzia asubuhi saa 12 mpaka saa 11 jioni ndiyo anahudumiwa na wengine wanaambiwa warudi kesho yake. Kwa hiyo, naona hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu yule mgonjwa mara nyingi anakuwa anasindikizwa na mtu ambaye angeweza kufanya shughuli nyingine za maendeleo. Kwa hiyo, naomba Serikali iboreshe huduma za afya hasa za mijini ili wananchi wasipoteze muda mwingi wa shughuli zao za maendeleo katika kusubiri huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, niongelee suala la ustawi wa jamii, *social welfare*. Najua kwamba kitengo hiki kilikuwa katika Wizara nyingine na kikahamishiwa Wizara ya Afya na ukiangalia Kitengo hiki kinaangalia zaidi masuala ya watu wenye ulemavu lakini labda niseme tu Kitengo hiki kwa kweli ni kama kimetelekezwa. Kwa sababu ukiangalia bajeti yake imepungua sana na niseme watu wenye ulemavu siyo wagonjwa, hawa ni watu ambako wanahitaji huduma mbalimbali. Kwa hiyo, nadhani kule walikopelekwa Wizara ya Afya haikuwa sahihi kwa sababu Wizara ya Afya ina-deal na masuala ya wagonjwa ilibidi kabisa Kitengo hiki kiwe sehemu nyingine ili watu wenye ulemavu waweze kuhudumiwa kwa kiasi ambacho wanastahili.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la bajeti, ukiangalia Kitabu cha Maendeleo ambako kwa kweli huko ndiko tunaona miradi mingi ya maendeleo, hili nililiongea kwenye Kamati na naomba niliongee hapa, suala la Hospitali ya *Ocean Road*, ni suala nyeti sana. Lakini ukiangalia kwenye Kitabu cha Maendeleo, hawajapewa hata

senti tano kwa mwaka huu na wote tunajua hii ni hospitali pekee ambayo inatibu watu wenye kansa na sasa hivi kansa imekuwa tishio. Kwa hiyo, naomba Wizara iliangalie kwa kina au Serikali kwa ujumla wake iliangalie kwa kina suala hili ili waweze kupata fedha, hospitali ile iweze kupanuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ukiangalia kwenye suala la uzazi ambapo akina mama 500 wanafariki katika wanawake 100,000, wamepewa jumla ya shilingi bilioni 20 ambazo ndiyo hiyo ya kupunguza vifo vya watoto na akina mama (*mortality reduction*). Lakini ukiangalia utaona asilimia 91.4 inatoka kwa wafadhili, fedha ya ndani ni asilimia 8.6 peke yake, ni ndogo hata kuliko za mwaka jana. Mwaka jana fedha za ndani zilikuwa asilimia 17 lakini mwaka huu tunazungumzia asilimia 8. Nadhani kuna haja ya Wizara kuongeza bajeti ili kuhakikisha kwamba zile *delivery kit* ambazo naamini nazo ziko hapa, kwa sababu Ilani ya CCM inasema kwamba akina mama watakuwa wanapewa vifaa vya kujifungulia bure lakini mpaka tunavyoongea bado na kwa bajeti hii mimi nina hakika kabisa bado suala la *delivery kits* kwa akina mama halitaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo nilitaka kulizungumzia ni suala zima la upungufu wa watumishi ambalo nimezungumza kidogo. Lakini niseme tu ni lazima Wizara sasa ijipange, ije na *retention policy* ya kuhakikisha kwamba hawa Madaktari na Wauguzi ambao tumewasomesha wanabaki nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 10. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuipongeza Wizara hii inayoongozwa na rafiki yangu Profesa David Mwakyusa, kwa kazi nzuri wanayofanya, pamoa na kwamba bajeti ni finyu lakini mnajitahidi, mnaonyesha dhamira yenu ya kutaka kuwashudumiwa Watanzania, nakupongezeni sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuwapongeza wapigakura wangu wa Jimbo la Lulindi, kwa kuitikia wito wa kujenga Zahanati katika kila kijiji. Walifanya hivyo baada ya Mbunge wao kuwaleta Madiwani wote na wawakilishi wa wananchi katika Jimbo la Mtera na kuona jinsi gani wenzetu wanaweza wakatoa mchango wao katika ujenzi wa Zahanati katika kila kijiji. Hivyo ndivyo walivyofanya wananchi wa Jimbo la Lulindi, nawapongeza sana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ninapenda kuzungumzia mambo yafuatayo. Moja, hili nimewahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri, katika siku za nyuma pale Lulindi ama Jimbo la Lulindi katika kijiji cha Lulindi, Kata ya Lulindi tulikuwa na hospitali siyo Zahanati, hospitali, hospitali ambayo ilikuwa inatoa huduma katika eneo lile na kwa kweli ilikuwa inawasaidia sana wananchi. Walikuwa hawaendi masafa marefu kufuata hospitali, ile hospitali kwa sababu ambazo hivi sasa haieleweki ikaondoka. Sasa kuna juhudhi ambazo zinafanywa na Kanisa la kutaka

kurudisha ile hospitali, ninachoomba mimi Wizara yetu ya Afya iunge mkono kwa nguvu zote ile hospitali iweze kurudi pale. Naomba katika hili, Wizara ya Afya iunde Tume yake ama iagize Watendaji wake waende katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, waende pale Lulindi wakaone lile eneo ili waweze kuthibitisha kwa macho yao wao wenyewe. Ni eneo zuri, bado baadhi ya miundumbinu ipo pale na wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa ili hospitali hii iweze kurudishwa iweze kutoa huduma kama ilivyokuwa inatoa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pili, Kituo cha Afya cha Lupaso, ni jambo la kusikitisha sana. Kituo hiki kilifunguliwa rasmi na Rais, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete lakini hivi ninavyozungumza, kituo kile hakifanyi kazi kama inavyotakiwa. Kinachotokea pale, yale majengo yanaharibika. Hatuna Waganga na naambiwa kwamba vifaa ambavyo vilitolewa kama msaada na Mheshimiwa Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa vinachukuliwa, vineapelekwa katika maeneo mengine. Ni hatari kabisa. Kituo kile kilikuwa kinatoa mchango mkubwa katika maeneo yale. Naomba atakapokuja kutoa majumuisho yake hapa Mheshimiwa Waziri atueleze kituo kile kwa nini kinafumbiwa macho wakati kina vifaa vya kutosha, majengo mazuri lakini kipo kimya kabisa, kinatoa huduma ndogo kabisa, hakifanani hata kidogo na hadhi yake na watu katika Jimbo la Lulindi wanazidi kuongezeka. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri anatakapokuja kutoa majumuisho yake, atueleze nini hasa kinatokea mpaka Kituo kile cha Afya hakifanyi kazi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya kwa wazee kuanzia miaka 60. Mimi naweza nikasema kwamba hiki ni kitendawili. Nasema hivyo kwa sababu tangu Sera hii izungumzwe, nimekuwa nikifuatilia katika Zahanati zangu katika Jimbo la Lulindi bado wazee wananyanyaswa wanapokwenda katika Vituo hivi vya Afya. Hawapewi huduma hata kidogo kwa mujibu wa umri wao. Sasa tunajiuliza, kule kuna Serikali nyingine na huku kuna Serikali nyingine? Ninaomba sana pamoja na maelezo mazuri ambayo ameyatoo hapa Mheshimiwa Waziri katika hoja yake lakini bado matatizo ya wazee yapo ya kutokutibiwa kutokana na umri wao. Wazee wetu hawa wamefanya kazi kubwa sana katika nchi yetu hii, imefika mahali sasa hivi tuwaenzi. Kuwakumbuka ni pamoja na kuwapa huduma za matibabu bure kama inavyozungumzwa katika Sera yetu ya Afya.

Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa na semina ya idadi ya watu. Katika semina ile tukaambiwa kwamba bado idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa kabisa ukilinganisha na ukuaji wa uchumi katika nchi yetu ya Tanzania. Sasa hivi tunaambiwa tunafika milioni 41, lakini kitu ambacho kinatokea ni kwamba elimu hii ya idadi ya watu, elimu ya uzazi wa mpango, haifiki kikamilifu vijijini, inazungumzwa sana mijini tu, ambapo sasa hivi mijini kutokana na maisha magumu tayari wanajua kwamba wasizae watoto wengi. Lakini vijijini huko tunakotoka, bado watu wanazaana kweli kweli na ni kwa sababu elimu hii haifiki huko, semina zinaishia mijini tu. Ninaomba sana elimu hii ifike vijijini ambako ndiko waliko Watanzania wengi, ama sivyo tutaendelea kuzaana sana na tutaendelea kupata matatizo kwa sababu watu ni wengi na uchumi ni mdogo. Kwa hiyo, ninaomba sana atakapokuja hapa Waziri wa Afya kutoa majumuisho yake, atueleze ni mkakati gani ambaao upo katika kuhakikisha kwamba elimu hii ya idadi ya watu inafikishwa vijijini ambako ndiko waliko watu wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuipa hadhi hospitali yetu ya Ndanda iwe Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na pia kuipa hadhi Hospitali ya Nyangao ili iwe Hospitali Teule. Ninatoa pongezi hizo kwa sababu mpaka sasa ninapozungumza, bado ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Mtwara na Lindi ni kitendawili, pamoja na kwamba tumeambiwa kuwa pesa zimetengwa, lakini hatujaona dalili kwamba hospitali hii ya Rufaa inajengwa. Eneo la ujenzi lipo, watu wameridhia kabisa, lakini mpaka hivi sasa bado hakuna kitu ambacho kinafanyika ili kuhakikisha kwamba hospitali ile inajengwa kama Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba katika hili Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, atueleze ni nini hasa kinatoka? Mwaka jana tuliambiwa kuwa pesa zimetengwa, lakini hatuoni kitu chochote na mwaka huu ni nini kitafanywa ili hospitali hii iweze kujengwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kuniona ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii. Kwanza, ninawashukuru kwa hotuba yenye mchanganuo mzuri katika utekelezaji wa kazi za Wizara kutokana na fedha walizopewa. Pia ninawapongeza kwa kukumbuka kuwaendeleza Madaktari katika elimu ili Madaktari Bingwa waweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ndugu zangu wakiogozwa na Profesa Mwakyusa na viongozi wote wa Wizara, ninajua wanafanya kazi nzuri, lakini ninaomba nitoe changamoto moja. Ni kweli kupata Madaktari Bingwa ni wajibu, kwa sababu tunahitaji Madaktari kama hao, badala ya kuwaleta kutoka nchi za nje. Lakini kwa miaka mitatu mfululizo nimeendelea kuchangia kuhusu wahudumu katika Zahanati tulizonazo katika Majimbo yetu kuanzia Manesi, Wakunga, hata *Nursing Auxiliaries* na wataalamu mbalimbali, ambapo wananchi wengi wa vijijini wapo. Kabla ya kwenda kwenye rufaa ni lazima apate huduma katika maeneo hayo na Sera ya Serikali ni nzuri, tumejenga Zahanati za kutosha. Ninajua kutokana na Sera ya Wizara, hawahudumii Zahanati wala Vituo vya Afya katika Mikoa, wao ni hospitali kubwa na za Rufaa, lakini huwezi kuimarisha Hospitali za Rufaa, kama huku ambako wananchi wengi ndiko wanatoka hakukuimarika, dawa hawapati, wala maeneo ya kupata tiba hawayona. Ninashukuru kabisa na ninafahamu Wizara hii inahudumia sehemu hizo, lakini ningeshangaa wakatae kuona umuhimu wa kuwa na Zahanati katika maeneo ya Vijiji. Kuna Sera ambayo Chama cha Mapinduzi tunaifahamu, walisema kwamba kila Kata kuwe na Kituo cha Afya, huwezi kuamini katika Wilaya yetu ya Uyui, Kituo cha Afya ni kimoja tu Wilaya nzima. Tumehamasisha kujenga Vituo vya Afya, tumeweka maeneo kama Jimbo langu la Igalula, tumetenga karibu hekta 25, lakini hakuna dalili ya kwamba Kituo cha Afya kitaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba basi, kuititia kwao, angalau TAMISEMI ione umuhimu wa kupata Vituo vya Afya. Wananchi wapo tayari kabisa kujitolea kama

walivyojitelea katika ujenzi wa Zahanati. Tarafa ya Kizengi haina, Tarafa ya Igalula haina, hivi kweli tutaboreshaje afya katika Jimbo langu la Uchaguzi, mpaka ninasikitika. Katika Zahanati ambazo tumejenga, nimemueleza Waziri mwaka jana au mwaka juzi na mwaka huu nimechangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, kwamba Zahanati ambazo nilimueleza hakufanya kazi yoyote wala ushauri wowote. Majengo ya Zahanati zile yamebomoka, nyoka wanalala, nge wanalala, wale watu wasiokuwa na kazi wanaitwa majambazi nao wanakwenda kulala pale wamepata mahali pa kujihifadhi, kwa sababu hakuna dalili za kusema kwamba kutakuwa na wahudumu katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, ninamheshimu sana mdogo wangu, lakini ni kwa nini hili hutaki hata kunisaidia? Hata ile kusema kwamba hebu tumsikilize huyu dada! Mimi dada yako, nimekwambia Zahanati Tundaukulu, Kalangasi, Bomani, nimekueleza kwamba sasa *ceiling board* zinaanguka, tufanyeje? Majengo yale ambayo tulisema kwamba wakae Manesi, sasa hivi tumechukua Walimu ndio wanakaa pale. Sasa nikaahidiwa kwamba Tundaukulu atakwenda Nesi, akaenda Nesi siku hiyo, kakaa siku moja akasema ninarudi musiwe na wasiwasi mpaka leo ni mwezi mzima, hajarudi. Sasa haya huoni kwamba mwanzo wa kuwa na Daktari kule ni pamoja na kuwa na nyumba kwenye Zahanati, hawa wagonjwa ndio wanatoka katika Zahanati hizi, wakishindwa ndio wanakwenda kwenye Hospitali za Rufaa. Sasa basi nikasema kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, kama basi mnashindwa hata kupeleka Wakunga na dawa, basi Wizara changieni muyakarabati haya majengo ili angalau tubaki na majengo, tukifika pale tunatizama hili jengo, hii ni Zahanati, tunatoka, labda itatosha. Kwa sababu hakuna huduma inayopatikana.

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu baada ya kujenga Zahanati hizi katika kila kijiji, wananchi wamepata imani kabisa kwamba sasa watapata tiba karibu na ndio ilikuwa nia ya Serikali. Matokeo yake Zahanati ambazo zimebaki zinapata wahudumu na dawa, ile *kit* haitoshi kwa sababu mategemeo yao ilikuwa ni mgawanyo wa watu utakwenda katika Zahanati mpya tulizojenga lakini hakuna Mhudumu, Zahanati haijafunguliwa, inabidi sasa waende kule ambako *kit* inatakiwa kuhudumia watu 2000 inahudumia watu zaidi ya 5000, baada ya wiki moja, dawa zimekwisha. Matokeo yake wananchi wanahudumiwa kwa kutazamwa, aah, wewe nakuona una dalili ya malaria, basi nakupa panadol mbili mara tatu.

Mheshimiwa Spika, pale Mnazi Mmoja palikuwa na Daktari mmoja alikuwa hatazami wagonjwa, akitonga kengele tu paa, ukiingia anaandika mbili mara tatu, wakamuita jina la mbili mara tatu, unakwenda kwa Daktari wa mbili mara tatu. Hakuulizi chochote na ndivyo wanavyofanya sasa hivi wale wahudumu wetu, kwa sababu hana namna ya kumsaidia, dawa hamna. Anakwambia mbili mara tatu, nenda kanywe labda kifua kitapungua au nenda kanunue dawa ya maji ya kifua, yaani wanafanya kinadharia, hawana utaalamu, kwa sababu wale walioko pale pia hawatoshi. Utakuta Zahanati moja kuna *Nursing Auxiliary*, atahudumia kitu gani? Watu wanaletwa kwenye matela ya ng'ombe, anafika pale hakuna kitu, wiki moja, dawa imekwisha. Sasa Waziri wa Afya na TAMISEMI mnazungumza nini kuhusu huduma hii?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda
wa mzungumzaji)*

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, ndugu yangu, wasaidie hawa ndugu zako na wewe mwenyewe una asili ya huko, si kwamba lugha tu, unatoka huko, mimi najua asili yake. Kwa hiyo, hebu wahudumie wananchi hawa kama ndugu zako. (*Makofi*)

SPIKA: Kengele ya pili tayari.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, ya pili tayari? Bado haijalia.

SPIKA: Imelia.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja, lakini naomba haya yafanyiwe kazi. (*Makofi*)

SPIKA: Muda unatosheleza Msemaji wetu wa mwisho kwa mchana huu, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa namna ilivyojitalidi katika kuboresha huduma za afya nchini mwetu. Naunga mkono kauli ya Mzee Malecela, tumetoka mbali, hatujafika lakini tunaelekea kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo Uingereza, nchini ambayo ni Taifa kubwa, ina upungufu mkubwa sana wa Madakatari, lina upungufu mkubwa sana wa Wauguzi, kiasi kwamba mpaka mgonjwa raia wa Uingereza, *appointment* ya *operation* inachukua mpaka miaka miwili mpaka mitatu. Leo sidhani kama kuna mtu Tanzania anapewa *appointment* ya *operation* zaidi ya mwaka mmoja au miezi sita, sidhani, kwa hiyo hatua zimechukuliwa. Yako matatizo, lakini jitihada zinaendelea kuchukuliwa. Sasa wale wenye kupenda kuponda, waponde tu kwa sababu ndio mtindo wenyewe humu ndani siku hizi na uchaguzi ndio unakuja huo na tutawapiga bao kama kawaida. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kupandisha hadhi Hospitali za Mkoa wa Dar-es-Salaam, Mwananyamala, Temeke na Ilala. Lakini nitaomba kuwe na *inhouse information*, hospitali hizi zikishapewa hadhi ya Kimkoa kunakuwa na dawa maalum ambazo zinatakiwa wapewe. Sasa wale wanaotoa madawa kama hawana taarifa kwamba hospitali hizi sasa ni za Kimkoa, wanakataa kutoa zile dawa ambazo zinatakiwa zihudumie wagonjwa kwa *level* ya Kimkoa. Tatizo hili lipo Amana, lipo Kinondoni na Temeke. Tunaomba, kwa wale wenye kusikia leo basi waanze kutekeleza agizo hili haraka sana, watuletee madawa haya katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ziara wanazozifanya hospitali tatu za Mkoa wa Dar-es-Salaam, Mwananyamala, Kinondoni na Amana, tumepeata *X-Rays* mpya za kisasa ambazo

zinaweza zikapiga picha 100 bila matatizo yoyote. Ni *X-Rays* ambazo zina gharama kubwa sana na zimeletwa kuhudumia wananchi wa Tanzania, *progress* zipo, zinaonekana, vifo vya watoto vimepungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna msemaji mmoja hapa amezungumzia Hospitali ya Mwananyamala, mimi ningewaomba Wabunge, Haspitali ya Mwananyamala, Hospitali ya Amana na Hospitali ya Temeke, makadirio ya wakazi wetu, nikizungumzia hospitali ya Amana ambayo nina takwimu zake, ni kati ya watu 200 na 300 kwa siku ndio wanaotakiwa kuhudumiwa. Kutokana na ubora wa huduma zinazotolewa, watu wanatoka maeneo mbalimbali, kwa Wabunge mbalimbali kukimbilia Amana na kufanya mpaka wakazi wa Ilala wakose kupata huduma. Kwa hiyo, tatizo sio huduma, tatizo ni wingi wa wagonjwa katika hospitali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wauguzi wa hospitali zetu, nampongeza sana Dokta Shimwela, hawa ni binadamu, ikifika muda fulani wagonjwa wako wengi na wao wanapata *stress*, wanapata *fatigue*, ndio maana mtakuta huduma haziendi. Kwa hiyo, mimi nilitaka vilevile niombe, msikimbilie hospitali hizi tatu, mtibiwe huko huko, wanatuletea tabu huku. Chumba hiki cha *X-Ray* tulishindwa kukianzisha Hospitali ya Amana, kwa sababu tulyohitaji ni *X-Ray* kubwa na inahitaji *special facilities*. Tuliwaomba *NSSF*, ninampongeza Mkurugenzi Mkuu na uongozi wote wa *NSSF*, wametugharamia chumba kile kwa milioni 20, wiki mbili tu chumba kimekwisha na huduma sasa zimeanza, *progress* zipo. Nitawaomba Wapinzani, kuna mmoja nilimpeleka kupiga *X-Ray*, sitaki kumtaja tu hapa, alikosa mjini huko. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Amana sasa hivi tunatoa huduma ya *premature*, tunapunguza vifo vya watoto wadogo. Mtoto njiti akizaliwa, kumpeleka Muhimbili na kutokana na msongamano wa magari, kunakuwa na hatari ya watoto hawa kufa. Nawashukuru Benki ya *Barclays*, wametupatia mashine mbili ambazo zinaanza kuhudumia na kuwasaidia watoto hawa wasiweze kupoteza maisha, *progress* zipo. Sasa wale ambao wanasema hakuna tulichokifanya au hakuna maendeleo yoyote katika hospitali zetu, watakuwa na nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa naiomba Serikali, madawa wanayoyaleta kwenye hizi hospitali tatu kwa sasa, isitegemee idadi ya watu tu, itegemee mahitaji. Tuna *shortage* kubwa sana za madawa. Utakuta wazee ambao wameahidiwa kutibiwa bure, wakiandikiwa *prescription* kwenda kununua dawa nje wanalamika, sio wanalamika kwamba hakuna dawa, ni sababu tu ya mfumo wa kuwa madawa yanakuja kufuatana na idadi ya watu 300 kwa siku, ndio maana zinakosekana. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kuwa ajaribu kulitizama suala hili, alitizame hili na ajaribu kuleta madawa si kwa idadi lakini kwa mahitaji ya watu ambao tunao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Amana kuna wodi ya wazazi, hatuna shida ya vitanda, hatuna shida ya wazazi kulala wawili, hatuna shida hiyo, shida yetu ni maeneo. Hospitali yetu ni ndogo, tuna vitanda vya kutosha na vingine havifungwi lakini leo ukienda Hospitali ya

Amana, hakuna wagonjwa wawili au watatu wanaolala kwenye kitanda kimoja, haya ni mafanikio ya Serikali, haya ni mafanikio ya Chama. Kwa sasa ninatoa tahadhari, tunaposema namna hii, mtu atoke huko, anasikia kuna Hospitali ya Amana, anakuja kuifungulia Amana, inakuwa matatizo. Ninaomba watu wajaribu, wanaposhikia ujauzito, ndiko huko huko wajifungulie sio lazima waje huku. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine suala la *ambulance*. Suala hili ni muhimu sana. Naiomba Serikali inisaidie kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kabla muda wangu haujawkisha, nilitaka kumueleza Mheshimiwa Waziri, kwenye mgao wa mali za Serikali wakati Halmashauri ya Mji ilivyovunjwa, *Amana Social Hall*, iliwekwa katika mgao wa *Ilala Municipal Council*. Kwa vile eneo lile sasa halifai kutumika kwa shughuli za burudani kutokana na makelele yanayopigwa na bendi mbalimbali, tulikuwa tunaomba sasa maana tumeshaizungumzia kwenye *RCC*, tunaomba eneo hili tulichukue ili tuliboreshe, tulifanyie matengenezo, tupanue hospitali hii ili mkitoka sasa huko, mje mtibiwe pale kwa sababu, kidogo nafasi itakuwa inapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *CDCF* zimetoka, naishukuru sana Serikali na katika mchango wangu wa *CDCF* ninanunua *X-Ray* za mwaka mzima, *X-Ray films*, ambayo thamani yake ni zaidi ya shilingi milioni tano, kuhudumia wakazi wa Jimbo la Ilala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Zungu.

Waheshimiwa Wabunge, zimebaki dakika mbili tu kufikia mwisho wa shughuli zetu kwa mujibu wa Kanuni ya 28, kwa hiyo, ninasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha shughuli za Bunge mchana pale saa 7.00, nilikuwa na wachangiaji watatu waliochangia mara moja katika Wizara nyingine na kwa hiyo, sasa wana haki ya kupata kipaumbele. Hawa ni Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Peter Serukamba. Kwa mpangilio huo basi, namwita sasa Mheshimiwa Idd Azzan, ili atoe mchango wake, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Janet Mbene.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza jioni hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya.

Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa kazi nzuri uliyoifanya na unayoendelea kuifanya katika Bunge letu na *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atakujalia ili baadaye urudi tena na uendelee kuwa Spika wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma ya afya kwa ubora unaostahili, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Rais wa Awamu hii ya Nne, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi chake cha uongozi, takribani miaka mitano sasa. Yale yote ambayo tuliyaahidi kwenye Ilani yetu, ameyasimamia na kutekelezwa vizuri mno na kwa kweli, anastahili sifa ya pekee. Wanaosema kwamba hakuna kilichofanyika, kwa sababu wana midomo ni lazima waseme, kwa hiyo waendelee kusema lakini wanaoona, tunaona ni yapi ambayo yamefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu mimi kwenye mwaka huu wa uchaguzi, wale wenzetu wa Upinzani ambao mara nyingi wamekuwa wakisemasema haya tunayoyafanya, mimi ninaomba wajiangalie vizuri sana ama wajiangalie upya, kwa sababu, tunakwenda kwenye uchaguzi na kwa hali inavyoonesha ni kwamba mgombea wa Chama chetu, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, anakubalika kwa kiasi kikubwa sana na atapata ushindi mkubwa sana kuliko alioupara mwaka 2005. Kwa hiyo, wajiangalie na kama wanaweza ni bora tu waseme kwamba nafasi hiyo ya urais wanaiacha abakie mgombea pekee. Kwa sababu pia hawazuiwi pamoja na kwamba ni demokrasia, lakini kwa haya yaliyofanyika, wanaweza wakachukua uamuzi huo wa busara tu, halafu zile hela zao za kampeni sasa wakazipeleka kwenye kununua mashuka, dawa na kujenga Zahanati kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuishukuru Wizara ya Afya kwa kazi kubwa sana waliyoifanya katika Hospitali yangu ya Mwananyala. Niishukuru sana Wizara lakini nimshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam, Ndugu yangu Lukuvi, amefanya kazi kubwa sana na hali imebadilika. Niipongeze Wizara kwa mashine nzuri na ya kissasa ya *X-Ray* ambayo mmetupatia, lakini niwapongeze sana kwa ujenzi wa jengo la maabara ambalo ujenzi unaendelea, kwa kweli na lenyewe likikamilika, litawasaidia sana wananchi wa Jimbo la Kinondoni na Wilaya nzima ya Kinondoni. Kwa hiyo, ni lazima nishukuru kwa sababu binadamu unapotendewa jema na mwenzako, hata dogo basi ni vizuri ukashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niiombe Wizara, hili tumelisema na tunaendelea kulisema tena. Tunayo Zahanati ya Tandale, Zahanati ile kwa siku inahudumia wagonjwa zaidi ya 1000, ni wengi kuliko baadhi ya hospitali za Mikoa yetu, lakini bado ile ni Zahanati vilevile, dawa ni kidogo, Wauguzi, Madaktari pia ni kidogo. Tumeomba na ninaomba tena Mheshimiwa Waziri, tuangalie uwezekano na ninafikiri inawezekana,

kwamba sasa hospitali ile ya Tandale, tuiwandishe hadhi na kuwa Kituo cha Afya ili iweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, tunayo hospitali ya Sinza na yenye we tumeiombea na ninaendelea kuomba tena kwamba na yenye we basi ipandishwe hadhi kutoka Kituo cha Afya Sinza na kuwa hospitali, ili pia iweze kukidhi mahitaji ya matibabu kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni katika maeneo yetu ya Dar-es-Salaam, Jimbo langu la Kinondoni au Wilaya ya Kinondoni lakini hata Muhimbili ukienda, wagonjwa ni wengi mno na wanatoka maeneo mbalimbali. Wapo wanaotoka Bagamoyo, wapo wanaotoka Kibaha, wapo wanaotoka Kisarawe na kadhalika. Ili kuondoa misongamano hii kwenye hizi hospitali za hapa mjini na mwenzangu Zungu alizungumza hapa asubuhi, basi tuangalie uwezekano wa kujenga ama Vituo vingine vya Afya ama hospitali nyingine kwenye maeneo haya ya pembezoni, kwa mfano Bunju au Boko, Kimara au Kibamba, ili kuweza kusaidia badala ya watu wote kuja Mwananyamala, Amana ama Temeke, waweze kupata huduma kule kule. Nafikiri hii itasaidia sana kuwafanya wananchi wetu waweze kupata huduma kama ambavyo tunatarajia.

Mheshimiwa Spika, nitahitaji maelezo kutoka kwa Waziri kuhusu pesa ambazo Serikali inalipa ama ambazo inatoa kwa CCBRT. Nakumbuka kulikuwa na makubaliano kwamba sasa hospitali ile iwe ndio Hospitali yetu ya Mkoa, lakini mpaka sasa hilo bado halijafanyika, lakini bado Serikali imekuwa ikilipa mishahara na hivi sasa ninafikiri inakaribia shilingi bilioni moja kwa mwaka. Kwa hiyo, ninataka nipate maelezo kwamba hela hizi zinalipwa na Serikali kwa ajili ya nini, kwa sababu huduma bado hazijaanza kutolewa kwa wananchi wetu kama ambavyo tulikuwa tunakusudia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni matibabu kwa wazee. Tumekuwa tukilalamika mara kwa mara kwamba wazee wetu hawa wanakosa huduma ile, akienda hospitali, dawa hakuna, ataambulia kuandikiwa tu cheti, uwezo wake ni mdogo na tunapozungumza wazee, kwa Kinondoni, usifikirie kwamba labda kuna wazee 20 au 30, ujue wazi kwamba wazee pale ni wengi mno. Ukipeleka dawa zako mbili, tatu, hazichukui hata siku mbili zitaisha. Kwa hiyo, tuombe hili nalo mlione muweze kutuongezea madawa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wazee wetu hawa ili waweze kupata huduma ambayo wanaitarajia. Tumeambiwa watapata huduma ya matibabu bure, basi iwe kweli ni bure na isiwe wanakwenda wanaambulia kupewa vyeti waende kwenye maduka ya dawa kununua. Kwa kweli, uwezo huo hawana. Ninaomba sana tuwaangalie ili kuwawezesha wazee hawa na watoto waweze kupata matibabu bure kama ambavyo tumewaaahidi.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii na nisije nikasahau, kumpongeza sana Mama Salma Kikwete, eeh, maana ukimpongeza baba basi usimsahau na mama. Mama amefanya kazi kubwa kwangu, kwenye Jimbo la Kinondoni amekuja na ametoa vifaa vya Hospitali ya Tandale. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa kwa moyo wake huo wa huruma na wa kizalendo, amekuja kwangu na amesaidia. Ninamuomba asichoke, anapopata chochote basi aangalie na Kinondoni, aje atusaidie, ukiachilia kwamba ndio kwake, basi asitutupe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kinondoni, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, ya Chama cha Mapinduzi, kujenga Zahanati kwa kila Kata, tumejenga Zahanati, hatujamaliza Kata zote, lakini asilimia kubwa tumeshajenga Zahanati kwenye Kata zote 10 za Jimbo la Kinondoni. Tunayo matatizo ya watumishi ama Wauguzi, niombe sana, najua hili liko TAMISEMI lakini nikucombe sana Mheshimiwa Waziri, jaribu kuongea na watu wa TAMISEMI waone ni nini watafanya ili tuweze kupata watumishi wa kutosha. Bahati mbaya juzi hapa, walihamisha takribani watumishi 39 na badala yake wakatuletea wawili tu. Sasa pamoja na kuelemewa na wagonjwa wengi, lakini na hawa watumishi wachache tuliokuwanao mnawaondoa, mnawahamisha lakini kutuletea wengine inakuwa kidogo inachukua muda! Kwa hiyo, nikucombe sana uongee na watu wa TAMISEMI, ili waweze kuturudishia ama kutupatia watumishi kwa ajili ya hizi hospitali zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa ninataka kulizungumzia...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwenye kona ile, mnaathiri Kanuni ya 66(3)(b), mnazungumza tu kama vile tupo, sasa hivi siwataji, lakini baadaye nitawataja. Mheshimiwa Iddi Azzan, endelea.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Lingine ambalo nilikuwa nataka kulisisitiza ni suala la magari ya wagonjwa, tunaomba sana Wizara ituangalie kwa ajili ya magari haya ya wagonjwa. Najua Halmashauri yetu inatenga vihela kidogo kidogo lakini ningeomba sana Wizara ituangalie kwenye hilo ili tuweze kuwa na magari ya kutosheleza. Kwa sababu, kama nilivyosema mwanzo, hospitali hizi zinahudumia wagonjwa wengi mno kwa wakati mmoja, tukiwa na magari ya kutosha, itatusaidia kwa wale ambao wamezidiwa kuweza kuwakimbiza kwenye Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu katika mchango wangu nafikiri yametosha, ni hayo. Nimalizie tu kwa kukupongeza sana Waziri na Mheshimiwa Spika, kwa kazi kubwa mnayofanya kama nilivyosema mwanzo. Suala la afya ni suala muhimu sana, tutoe kipaumbele Dar-es-Salaam kwa sababu imeelemewa sana, wakazi ni wengi sana na hata wenzetu wanapofanya tathmini yao ya takribani miaka 50, wanafanya tathmini ya nini kipo, hawafanyi tathmini ya watu wameongezeka kwa kiasi gani. Nafikiri wangefanya hivyo wangejua ni nini kinachofanyika, Dar-es-Salaam tuna ongezeko kubwa sana la watu na wengi wanahitaji matibabu. Kwa hiyo, tunapofanya maamuzi yetu kwa Mikoa mbalimbali, Dar-es-Salaam tuipe kipaumbele cha pekee na hususan Kinondoni kwa maana ya Jimbo la Kinondoni, kwa sababu watu ni wengi mno. Mwenzangu alizungumza hapa asubuhi kwamba, aah, basi na wenzetu wengine kila siku mnakuja kujifungulia Dar-es-Salaam, mbakie huko huko kwenu, mimi nasema njooni, lakini huduma ziwe nydingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Wakati namuita msemaji ambaye ataongea sasa hivi, namwomba Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, ajiandae, amebahatisha, atapata nafasi ya kuongea. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Janet Mbene, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi wa Musoma Mjini.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuzungumza na kuchangia katika hotuba ya Wizara hii muhimu katika Taifa letu. Nami niungane na wenzangu katika kumpongeza Rais, kwa kumteuwa Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa katika Wizara hii, kutokana na utaalamu wake na utendaji wake wa kazi kwa kiwango cha juu. Vile vile nampongeza Naibu wake, Mheshimiwa Dokta Aisha Kigoda, Katibu Mkuu wake, Bibi Blandina Nyoni, ambaye ninamfahamu, ni mchapa kazi mwingine hodari sana na makini, pamoja na Maofisa wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, mimi ninapenda kuchangia kwanza katika suala zima la huduma ambazo Wizara hii inatoa na ile dhana kuwa hakuna kitu kinachofanyika. Sina haja ya kurudia yale yote ambayo yamezungumzwa na wenzangu ila tu labda niainishe uzuri wa Serikali ya CCM, ni kuwa tunatambua changamoto zetu, tunaziainisha na wala hatujifichi na tunaweka mikakati ya kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kukubalika na la kupongezwa na ni la kiungwana. Vile vile napenda kuipongeza Wizara kwa jinsi inavyoendelea kushirikiana na wadau wengine wa afya hususan asasi zisizokuwa za kiserikali, wabia katika maendeleo na hata sekta binafsi katika kuhakikisha kwamba huduma za afya zinaboreshw. Hii imejidhihirisha katika miradi ya UKIMWI, miradi ya afya ya watoto hususan kuzuia maambukizi ya mama kwa mtoto, *PMTCT*, malaria, *TB*, ukoma na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hotuba yenye. Ninapenda kujikita zaidi kwenye masuala ya vifo vya akina mama wakati wa uzazi na vya watoto chini ya miaka mitano. Ingawa takwimu zinaonesha na ukweli inadhihirisha kuwa vifo vya wazazi vimepungua, lakini nina imani kuwa idadi hii inaweza ikapungua zaidi na nina imani kuwa mikakati zaidi inaweza ikawekwa kwa ajili ya kuhakikisha hilo. Halikadhalika, vifo vya watoto chini ya miaka mitano pia vimepungua na ni jambo la kupongezwa, lakini vilevile ninaamini kwamba hili linaweza likafanyiwa kazi kwa ukubwa zaidi na vikapungua zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuyachukulia masuala hayo yote mawili kuwa ni masuala kwanza ya kijinsia na pili ni masuala ya haki za binadamu. Tunazungumzia vifo vinavyoweza kuzuilika, tunazungumzia vifo vya akina mama katika umri wao ambao bado wana nguvu za kuchangia Taifa, wana nguvu na jukumu la kuchangia familia zao,

lakini wanafariki wakati wa uzazi. Ninapenda kutoa changamoto kwa Serikali na hasa Wizara husika, walichukulie katika mtazamo mwingine kuwa ni suala la kijinsia na ni suala la haki za binaadamu na kwa hali hiyo hata mikakati itakayowekwa izingatie hayo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumeridhia Mikataba ya Kimataifa inayozungumzia masuala yote haya na ningependa tuoneshe kwa vitendo ni jinsi gani tunaridhia kwa utekelezaji. Sina maana ya kusema kuwa Serikali haijafanya vyakutosha, lakini ninaamini kuwa tukiweka mikakati mahiri zaidi, tunaweza tukafikia viwango vidogo zaidi vyakutosha. Hii kwangu mimi inaenda moja kwa moja na malengo ya Milenia, malengo ambayo hatujafanya vizuri sana ni hayo ambayo nimeyataja. Kwa hiyo, inaonesha ni jinsi gani ambavyo bado tuna hatua kubwa ya kupiga katika kuhakikisha kuwa akina mama wanapojifungua wanajifungua salama.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kupendekeza mambo machache ambayo ninafikiri yanaweza kusaidia, nayo ni katika programu nzima ambayo imejitokeza kwenye bajeti tulioisoma. Mimi naamini Ustawi wa Jamii ni Kitengo ambacho kingepaswa kuwekwa kwenye Wizara ya Afya kwa sababu ustawi wa jamii ni sehemu kubwa ya mazuio ya magonjwa, ustawi wa jamii ndiko ambako watu wanahamisishwa masuala ya afya, masuala ya lishe, masuala ya usafi wa mazingira, masuala ya lishe bora kwa watoto, masuala ya matunzo ya watoto na masuala ya maadili kwa ujumla. Vitu hivi vikifanyika ipasavyo, hata maradhi yatapungua, hata zile tabia potofu zitapungua na kwa hali hiyo itasababisha watu wachache zaidi kupata madhara mpaka kufa wakati wa kujifungua na watoto kufariki wakiwa na miaka michache. Kwa hali hiyo, ninapenda kuiomba Wizara, ikishirikiana na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kuweka mikakati ya pamoja ya kuangalia ni jinsi gani Idara ya Ustawi wa Jamii, itaboreshwa. Sijaiona kama imejidhihirisha hivyo katika bajeti. Bajeti inayohitajika kwa suala hili ni kubwa kidogo kwa sababu inaenda mpaka chini, kwenye ngazi ya shina. Sasa hii ikiweko na wakiweko maofisa watakaokwenda mpaka ngazi hizo kuhamasisha jamii, itasaidia sana katika kupunguza haya madhara ambayo tunayaona.

Mheshimiwa Spika, ninapenda vilevile kuhamasisha Serikali hasa Wizara ya Afya kuangalia jinsi gani itakavyoingia ubia na sekta binafsi katika kutengeneza hizi *kits*. Hivi vifaa vingine vinaweza kutengenezwa hapahaha nchini kwa bei nafuu ili viweze kupatikana kwa wingi na kusambazwa nchi nzima hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni suala la wazee. Inaonekana kama wazee jukumu lililopo ni kuwapatia dawa bure, lakini mimi ninaamini kuna huduma nyingi zaidi zinazohitajika kwa ajili ya wazee wetu tukiwemo na sisi wenye wazee watarajiwu. Kuna haja wazee wengi kupata njia mbadala za kupata ajira kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Wazee wengi sasa hivi wamepata jukumu la kulea wajukuu kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, wazee wengi wanastaafu lakini wakiwa na taaluma zao za kutosha, wakiwa na nguvu na uzoefu wa kutosha kuendelea kuchangia ajira kwa njia moja ama nyingine. Ninapenda kuona mkakati unaowekwa juu ya kusaidia wazee kuweza kujikimu kimaisha kwa kuititia taaluma walizokuwa nazo au uzoefu waliokuwa nao ili waweze wenye wengi kujipia gharama nyingine ambazo wanahitaji

kulipia na ili waendelee kuwa na hadhi katika Taifa letu kuliko ilivyo sasa hivi kwani wengi sana wanadhalilishwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbene kwa mchango wako, naona umeanza vizuri lakini niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kengele ya kwanza inagongwa kwenye dakika ya saba inakupa dakika tatu za kumalizia halafu zile dakika tatu sasa zikipita nazo ndiyo inagongwa ya pili. Sasa namwita Mheshimiwa Peter J.Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi wa Musoma Mjini.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii jioni ya leo. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Jimbo letu la Kigoma Mjini, ahadi zote tulizozitoa, kwa kweli tumezitekeleza kwa kiwango kikubwa sana, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini, kwa heshima walijonipa na kunifanya niwatumikie kwa miaka mitano. Ni matumaini yangu kwamba bado wana imani kwangu na nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu ileile ambayo nilianza nayo ili tuweze kufikia maisha bora kwa kila mwananchi wetu na kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Afya, rafiki yangu Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Dada yangu Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Madaktari na viongozi wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Wizara hii. Kazi iliyofanyika ni kubwa na ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tunazo *challenges* kama nchi na kama dunia ambayo bado tunaendelea. Ukienda kwenye *data* za maendeleo unaambiwa kwa nchi zinazoendelea kama za kwetu kuna watoto karibu 8,000 wanakufa kwa malaria, akina mama na akina baba karibu 5000 wanakufa kwa *TB*, vijana wanaokua kama sisi 7500 wanakufa kwa UKIMWI na magonjwa mengineyo. Kwa hiyo, naona bado *challenge* ni kubwa kama nchi na kama dunia hii ambayo tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, wakati naangalia bajeti yetu, naona inakwenda mbele yaani inaongezeka, kwa kweli naipongeza Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini najiuliza rafiki yangu Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa ambaye mimi namuombea na ninaamini watu wa Rungwe hawawezi kufanya kosa watamchagua na ningeendelea kumuombea ili ikiwezekana arudi hapo lakini nikasema sasa hivi inabidi Waziri wa Afya anayekuja pamoja yote haya mazuri anayofanya hebu tubadili turudi kwenye zile *basics*.

Nikasema ningetamani na ninamuomba Waziri wa Afya kila ninapofungua *TV* awe anahamasisha wananchi kunawa mikono, tunaporudi kutoka kazini kabla hatujafanya chochote tunawe mikono, ningependa kumuona Waziri wa Afya akiwahamasisha wananchi wote ndani ya nchi yetu wachemshe maji ya kunywa. Ukisoma historia ya China, Mao alianzisha *discipline* kwa Taifa lile na watu walivyo wengi, hakuna aliyekuwa anakunywa maji bila kuchemsha. Kwa hiyo, imefika wakati sasa Waziri wa Afya hili nalo tulianze. Nakumbuka wakati ule tulikuwa tunasoma kanuni sita za afya, turudi kwenye zile kanuni. Mimi naamini tutapunguza magonjwa mengi na tutaokoa fedha nyingi zinazopotea. Kwa hiyo, tuanze kuona kampeni kubwa kwenye *TV*, Redio na kadhalika, tuwe tunaona viongozi wananaawa mikono, wanahamasisha kuchemsha maji, lakini pia tuhamasishe watu kwenda *Gym* kufanya mazoezi ama hata kutembea unawenza ukasema *Gym* ni gharama.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wa Uingereza, Tony Blaire alivyoshinda, alianzisha kampeni ya kuondoa *obesity* kwa kutaka watu kwenda kufanya mazoezi, mwenyewe akawa anakwenda *Gym*, mnaona kwenye magazeti na *TV*, ile una-institute *discipline* kwenye *society* ili watu waone umuhimu. Kama huna uwezo wa kwenda *Gym* unawenza kutembea kwani ukitembea tu itasaidia sana na tutapunguza matatizo ya moyo na *cholesterol* yote, haya tunaweza tusitumie pesa nyingi, lakini kwa kuhamasisha wananchi wafanye hizi *basics* tunaweza kulisaidia Taifa. Pia watu wale chakula kizuri yaani kula na kunywa kwa kiasi, nayo itatusaidia katika afya. Pia kuna habari ya kulala mapema na kuamka mapema, inasaidia katika afya. Yako mambo mengi ambayo nasema tuanze kuyafanya hayahitaji pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, tuanze sasa kuiomba *society* kwa wale ambao wana uwezo wajitahidi kwenda kuangalia afya zao mara kwa mara kwa sababu ninaamini wako watu wanakwenda kugundulika na tatizo kumbe wangekwenda mapema labda wangeweza kusukuma maisha yao kwa kiasi fulani. Lakini pia tuongeze udhibiti wa vyakula vinavyoingia nchini kwa sababu sasa hivi tatizo la Kansa limeanza kuwa kubwa sana, kwa hiyo, lazima udhibiti nao uongezeko. Kwa kweli umefika wakati tuiombe *society* yetu watu wachemshe maji, wanawe mikono, wafanye mazoezi nina hakika tunapunguza magonjwa mengi sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake tumeingia mkataba Manispaa ya Kigoma na Hospitali ya Baptist, namuomba na ninamshukuru sana Waziri. Katika hili, tumehangai naye sana, ametusaidia na ametupa kibali na sasa hospitali yetu inaanza. Hospitali ile bahati nzuri Wamishenari wale waliweka kila kitu, kwa hiyo, sasa tunawaomba wale wafanyakazi waliokuwepo waendelee, tuletewe vifaa ili hospitali ianze na tuanze kutatua matatizo ya watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la bei kwenye hospitali zetu. Utakuta bei ya dirishani leo kwa Hospitali ya Mkoa fulani ni shilingi 500/=, lakini kwingine ni shilingi 1500/=, Kigoma ilianza 500/= na sasa hivi imekuwa Sh.1,500/=, mimi sina tatizo. Lakini ni vizuri kama nchi ielete we kwamba sasa ukienda dirishani mwananchi anatoa shilingi ngapi siyo Madaktari wanakaa wanajipandishia wao kama wanavyoona. Nadhani siyo jambo jema na hatutakuwa tunawasaiadia sana wananchi wetu. Kwa hiyo, namuomba sana Waziri atusaidie katika hilo ili tuweze kuwasaidia wananchi kuliko kupandisha bei ya huduma kila siku, Kigoma hali ni ngumu, wanapandisha bei kila wakati, sidhani kama ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, Kigoma pia tuna Madaktari wachache sana kama Mkoa na kama Manispaa, kwa kweli hali yetu ni mbaya sana. Tunaomba wakati mnajipanga mtusaidie tuweze kupata Madaktari na sisi tuweze kuwasaidia wananchi wa Kigoma kwani Kigoma ni moja ya Mikoa ambayo tumesaidia nchi jirani, tumejitolea sana kwa ajili ya wenzetu, kwa hiyo, nitarajia na sisi angalau kuna baadhi ya mambo na sisi yatunyookee kwa wema tuliofanya na *of course* tunafanya kwa ajili ya nchi yetu lakini tunaomba Madaktari waongezeka Kigoma.

Mheshimiwa Spika, mwisho na mimi nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao tumefanya kazi kwa pamoja kwa miaka mitano, nikushukuru wewe binafsi na niwaombee kheri Wabunge wote ambao tuko ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nichukue nafasi hii kumshukuru Mke wangu Yvette na watoto wetu Ila na Bhizi, kwa kweli wamenipa msaada mkubwa sana wa kuwatumikia wananchi wa Kigoma. Siku zote wamekuwa wakiniruhusu kile ninachoweza kufanya ili niweze kutekeleza majukumu yangu ya kuwashudumia wananchi wa Kigoma. Ninawashukuru sana kwa moyo ambao wamekuwa wanani na kwa kweli wanani *support* kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi naiunga mkono bajeti hii lakini nimalize kwa kusisitiza kwamba Mheshimiwa Waziri umefika wakati, nilikuwa nimesahau jambo la lishe, Idara hii ya Chakula na Lishe tuipe nguvu za kutosha na tuipe bajeti ya kutosha. Ninaamini wakifanya kazi watu wa chakula na lishe watasadid sana kupunguza magonjwa kwa sababu ndiyo wanaotusaidia kujua nani ale nini na kwa wakati gani, kwa akina mama wajawazito iweje na kadhalika, hawa nadhani ndiyo jukumu lao. Wataalamu wanasema *prevention is better than cure*, Idara ya Lishe zamani ilikuwa ni Idara ya...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.
(*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa mchango wako na sasa mchangiaji wetu wa mwisho kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya ni Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi ambaye ndiyo namwita sasa.

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana lakini kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya pekee ya kuwa kitinda mimba katika kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Afya maana mimi nilijua nitakuwa nimekatwa lakini kwa bahati nimepata basi nakushukuru kwa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nami kuungana na wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi yao nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Kusema kweli katika utendaji wao mzuri huo umeendelea kusababisha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi uende vizuri na mimi nakumbuka mwaka 2005 wakati ule tunaomba ridhaa kwa wananchi kusema kweli kwenye sekta hii au kwenye Wizara ya Afya tulikuwa na upungufu mkubwa. Kule Jimboni kwangu Zahanati zilikuwa hoi, Vituo vya Afya vingine havikuwepo na hospitali yetu ya Mkoa ilikuwa taabani sana. Lakini leo nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kutusaidia, tumeendelea kujenga Zahanati hata katika yale maeneo ambayo hatukuwa na Zahanati sasa leo zipo. Lakini vilevile pamoja na Vituo vyetu vya Afya na kwamba sasa wagonjwa badala ya kwenda kwenye hospitali kubwa sasa huduma nytingine kama kujifungua zinaweza kupatikana katika Vituo vya Afya. Kwa hiyo, tunapongeza Serikali kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia katika ule mji wetu wa Musoma, Serikali imefanya kazi nzuri sana katika Hospitali yetu ya Mkoa ni kwa sababu kwa bahati mbaya sana kwamba ile hospitali yetu ni ndogo, lakini imeiboreshwa katika maeneo mengi. Tulikuwa na tatizo kubwa la *X-ray* lakini sasa si tatizo tena, sasa hivi ile *theater* iko kwenye hatua za mwisho za ukarabati kwa ajili ya akina mama peke yao, lakini pia tulikuwa hatuna jengo la *grade* tulilokuwa nalo lilikuwa ni dogo sana lakini limeshajengwa jengo zuri sana la kisasa hii ni pamoja na uzio mzima wa Hospitali. Kusema kweli pale kinachopungua ni uwanja, eneo lile ni mdogo lakini vinginevvo naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo za Serikali ambazo kwa kweli mimi binafsi nadiriki kusema kwamba zimenifanya niwe hapa Bungeni nikiwa na uhakika kwamba kule kwangu sasa mambo yamepoa, lakini hii ni kwa sababu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba mambo yamekwenda vizuri kwa kadri tulivyoahidi. Pamoja na mafanikio hayo makubwa, lakini yako matatizo ambayo Serikali bado kuyaangalia. Tatizo kubwa la kwanza nilishalizungumza sihitaji kulirudi sana kwa sababu nilisema kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ni lile la Hospitali yetu ya Kwangwa. Napenda kusema kwa ufupi kwa sababu hata wewe Mheshimiwa Waziri

tumeshalizingumza sana na umeonyesha *positive* katika kuhakikisha kwamba unaisaidie ile hospitali yetu. Nguvu za wananchi zimepotea pale zaidi ya miaka 20 lakini tunadhani kuanzia sasa kwa kadri ambavyo Serikali imeahidi ni imani yangu sasa tutalipa kipaumbele kuanzia bajeti ya mwaka kesho ili tuhakikishe kwamba jengo lile, nguvu za wananchi hazipotei bure.

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo lingine ambalo ninadhani nahitaji kulisema katika zile hospitali zetu si ya Musoma tu lakini na hospitali nyingine nchini, kati ya kero kubwa ambazo zinajitokeza kule ni kwamba baadhi ya Wauguzi wetu si waaminifu. Lakini kwa kutokuwa kwao waaminifu ni imani yangu kwamba Serikali inahitaji iendelee kulifanya kazi kwa umakini zaidi. Lakini pamoja na kulifanya kazi kwa umakini, Mheshimiwa Waziri niseme tu kwamba kazi ya maslahi ya hawa watumishi ukilinganisha na wingi wa watu ambao wanahudumia inawezekana nayo inachangia kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, tunadhani kwamba kama maslahi yao yataendelea kuboreshwa sasa ni rahisi na wao wakaendelea kwa sababu wanafanya kazi mara tatu zaidi ya kazi waliyopaswa kuifanya. Tunadhani kwamba itawapa moyo zaidi ili waendelee kuvumilia kwenye hiyo kazi kubwa na ngumu ambayo wanaifanya. Kwa kweli suala la maslahi ukiangalia wale wananchi au wagonjwa wanaohudumiwa kwa kweli hiyo ni changamoto kubwa ambayo iko kwa Serikali lakini ni changamoto kubwa ambayo iko pia kwenye Wizara na kuna kila aina ya sababu ya kuona kwamba ni kwa kiasi gani Serikali au Wizara inapaswa ijitahidi kuwaongeza maslahi hii itawapa moyo zaidi katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, liko suala la wazee, hili tumelizingumza katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005/2010 kwamba wazee wetu wataendelea kupata huduma bure hasa wale wazee wasiokuwa na uwezo. Hili tunesema mara nyingi kwamba hawa wazee kazi yao kubwa sasa ni kula *pension* yao ya mwisho na tunatarajia kwamba watuombee ili tuendelee kupata baraka ili tuendelee kufanya vizuri. Lakini kusema kweli wazee wetu wanafika mahali wanasononeka na wanasononeka kwa sababu kwanza akienda hospitali inampasa afuate *process* za matibabu mpaka akubaliwe kutibiwa bure inakuwa ni *process* ndefu.

Mheshimiwa Spika, lakini licha ya hiyo, hata pale anapoandikiwa dawa mzee huyu ambaye hana fedha za kununua dawa na pale hospitali hakuna dawa basi tunadhani katika hili mwaka 2010/2015 lazima Serikali ijipange vizuri ili ione kwamba ni kwa kiasi gani sasa, kwa kuwa tumeahidi katika Ilani yetu inaweza kuwasaidia wazee hawa ili waweze kupata matibabu vizuri na waweze kuzeeka vizuri hii ni pamoja na kuwawekea dirisha maalum ili wanapofika pale wahudumiwe mara moja bila kuchelewa kisha warudi majumbani kwao, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewasaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, linaloendana na hilo katika hizi hospitali zetu pamoja na kwamba Wizara imejitahidi kiwango cha madawa kimeongezeka lakini tunadhani kwamba kutokana na ongezeko la wagonjwa kwa maana kwamba watu tunaongezeka, hii

imesababisha zile dawa zisikidhi mahitaji. Kwa hiyo, mgonjwa anakwenda hospitali analipia shilingi 1,000/= au 1,500/=, baada ya hapo anaambulia karatasi peke yake, anafika mahali anaandikiwa dawa ambazo hazipatikani hospitali hapo. Kwa hiyo, tunadhani hiyo nayo ni changamoto kubwa ambayo itaisaidia Wizara iendelee kujipanga ili kuhakikisha kwamba ni kwa kiasi gani matatizo hayo yanaisha.

Mheshimiwa Spika, liko suala zima la Madaktari na kwamba kweli majengo yapo mazuri na vifaa vya kutosha, lakini tatizo la Madaktari hasa Madaktari Bingwa maana pale kwetu sijui tuna Daktari Bingwa mmoja. Sasa ukiangalia hospitali nzima ya Mkoa ambayo inahudumia Wilaya tano, kitendo cha kutokuwa na Madaktari Bingwa wa kutosha kwa kweli ni tatizo. Lakini hata Madaktari wa kawaida nao hawatoshi kwani tuna upungufu mkubwa wa Madaktari ambayo ni sambamba na hawa Wauguzi wa kawaida. Kwa hiyo, tunadhani kwamba tuna kila aina ya sababu kwa Wizara kuendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kupata Madaktari Bingwa na wa kutosha.

Lakini vilevile na wauguzi wa kutosha na tunadhani kwamba, kwa kufanya hivyo sasa itapunguza ile kero kubwa ambayo inajitokeza kwa sababu wagonjwa wetu wengi wanapofika pale hospitali wanasubiri, wanakaa muda mrefu wakati yule ni mgonjwa ambaye kwa kusema kweli hata wengine inatokea kwa bahati mbaya sana wanapoteza maisha wakiwa pale wanasubiri huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilidhani kwamba ni vizuri nikayazungumzia hayo lakini vinginevyo kama walivyosema wenzangu, mimi ninakutakia wewe mwenyewe kheri na fanaka, pamoja na Waziri na Wabunge wengine wote ili tuweze kurudi mjengoni tuweze kuendelea na majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi. Ahsanteni sana, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mganga Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Hospital ya Taifa ya Muhimbili kwa kazi nzuri pia wanayofanya. Niipongeze serikali kwa kufanya ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo pengine ya majibu au huduma kwa wafanyakazi wachache sana. Ombi langu ni kwa uongozi kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili wafahamu dhamana yao juu ya wateja wao.

Mheshimiwa Spika, pili ni ubaba wa wataalam mbalimbali katika Sekta ya Afya. Pengine jambo hili lisiachiwe hal mashauri pekee. Watanzania wanajua serikali tu. Upo upungufu mkubwa wa wataalam. Mbinga kuna zahanati zimejengwa kwa muda mrefu lakini hakuna wahudumu wa afya. Hii inawavunja moyo Wananchi. Mkakati maalumu unahitajika ili kufundisha wataalam wa kutosha. Nitafarijika sana kama Jimbo la Mbinga Mashariki litapatiwa watumishi wa afya kuanzia na madaktari. Hospitali ya Ruanda, kwa

mfano, mpaka sasa haina tabibu licha ya ukarabati kukamilika na licha ya ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Spika, tatu ni tatizo la upatikanaji wa madawa. Hapa pia kuna tatizo kubwa, yaani malumbano kati ya Halmashauri na MSD. Malumbano hayatakiwi, kinachotakiwa ni huduma na ninaomba wizara ilichunguze jambo hili na liishe.

Mheshimiwa Spika, nne ni huduma ya *ambulance*. Jimbo langu ni lenye milima na miteremko, baiskeli si salama sana. Naomba kwa niaba ya Wananchi tupewe magari ya *ambulance* ili tuwafikishe wagonjwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, tano, ni uboreshaji wa Hospitali ya Wilaya ya Mbinga. Hasa jengo na vifaa vya *theatre* na kuongeza wodi. Halmashauri inajitahidi sana lakini msaada zaidi umetakiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kumtakia Mheshimiwa Waziri na Wafanyakazi wote wa Afya, kazi njema na mafanikio.

MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia juu ya mambo matatu muhimu:-

Kwanza, upatikanaji wa matabibu kwenye zahanati hadi sasa Wilaya ya Mkinga inakabiliwa na uhaba mkubwa wa matabibu. Zahanati tatu Mkinga hazina matabibu. Kwa niaba ya Wananchi wa Mkinga, ninaomba upendeleo rasmi.

Pili, kukosekana kwa dawa, zahanati zilizo nyingi hazina dawa hata zile za kupunguza maumivu; ALu imekuwa bidhaa adimu.

Tatu, Hospitali Teule Wilaya ya Muheza inahitaji matengenezo makubwa ya miundombinu katika chumba cha kuhifadhi maiti, hali ya sasa ya chumba hicho ni hatari. Ninaomba serikali itoe msaada wa haraka kuinusuru Hospitali hiyo ikiwa ni pamoja na miundombinu mingine muhimu katika Hospitali hiyo.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wao wote, kwa kutayarisha na hatimaye kuwasilisha bajeti hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huko nyuma (bajeti zilizopita), Bunge lako liliwahi kuelezwu kwamba, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi pale Vwawa iko kwenye mpango mkubwa wa matengenezo. Ninataka kujua, je, hadi leo serikali imefikia hatua gani katika kutekeleza mpango huo?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Mbozi kwa kushirikiana na serikali yao ya Halmashauri ya Wilaya, wamejitahidi sana kujenga zahanati na vituo vya afya. Tatizo kubwa hapa ni upatikanaji wa waganga na wauguzi; hili ni tatizo kubwa sana. Ninaomba serikali kuititia Wizara ya Afya, ihakikishe wataalamu hao wanapatikana na kupelekwa vituo vya afya na zahanati; kama hilo halitafanyika, tutawakatisha tamaa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika (*AU*) waliwahi kukutana Jijini Abuja – Nigeria na kukubaliana kwamba, kila nchi itenge si chini ya asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya Sekta ya Afya. Bado hatujafika huko na sijui tutafika lini. Hivi tatizo ni nini? Kwa nini maamuzi ya viongozi (wakuu wa nchi) hayatekelezwi? Ninataka kujua, hadi sasa ni nchi ngapi ambazo zimetekeleza Azimio la Abuja na nini siri ya mafanikio ya nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 – 2010 imeleza bayana kabisa kwamba, wazee zaidi ya miaka 60 na watoto chini ya miaka mitano watapata matibabu bure. Hata hivyo bado suala hilo halina misingi ya kisheria. Juzi wakati Waziri wa Fedha na Uchumi anawasilisha Bajeti ya Serikali alisema, wazee zaidi ya miaka 60 wasiojiweza watasamehewa kulipa kodi ya majengo (*Property Tax*) kwa jengo moja analoishi. Hili ni jambo zuri. Hata hivyo, ushauri wangu ni kwamba ili jambo hili liwe na nguvu ya kisheria, ninaomba serikali ilette Muswada Bungeni, utakaobainisha maeneo mbalimbali ya wazee na watoto kusamehewa kodi. Tukifanya hivyo, tutaondoa usumbufu kwa wazee na watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mission ya Mbozi inamiliikiwa na Kanisa la Moraviani Tanzania – Jimbo la Kusini Magharibi. Hapo awali Hospitali hii ndiyo ilikuwa Hospitali Teule ya Wilaya hadi miaka ya 1990 tulipopata Hospitali ya Wilaya ya Vwawa. Tunalishukuru sana Kanisa kwa kazi hiyo. Hata hivyo, ninataka kujua, je, kuna mahusiano gani kwa sasa kati ya Hospitali hiyo ya *Mission* na serikali? Ninauliza hivyo kwa sababu kumeanza kuwa na malalamiko kutoka kwa Wananchi kuhusu ughali wa matibabu hospitalini hapo. Aidha, kuna malalamiko ya uendeshaji wa hospitali hiyo kutoka kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Waganga Wasaidizi Mbozi, kinakabiliwa na changamoto nydingi; moja, upungufu wa wakufunzi na vitendea kazi kama vile gari. Ukizingatia kwamba, chuo kipo takriban kilomita saba kutoka TANZAM High Way, watumishi na wanafunzi hupata tabu sana kwani hulazimika kutembea umbali huo pale wanapohitaji kwenda Vwawa – Mlowo au Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba ufafanuzi wa taratibu za uendeshaji wa maduka ya dawa. Ninasema hivyo kwa sababu hivi karibuni kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara hiyo kwamba, wafunge maduka yao kwa sababu yako chini ya mita 300 kutoka duka moja hadi lingine. Hii sheria inatoka wapi na tuna chombo gani? Kibaya zaidi, wafanyabiashara hao walifuata taratibu zote za kufanya biashara hiyo na hatimaye kupewa leseni. Kwa nini wasumbuliwe leo?

Mheshimiwa Spika, ninashauri wale waliokwishaanza biashara hiyo na wametimiza masharti yote kasoro lile la mita 300 wasibugudhiwe. Waombaji wapya sawa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kujua je, wizara imelifanyia kazi agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kufuatia swali langu kwake, kupitia kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu Siku ya Alhamisi tarehe 24 Junui, 2010. Swali langu kwake lilihusu maelezo kama nilivyoandika hapo juu. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, ninaomba serikali itatue matatizo hayo ili wakufunzi na wanafunzi waweze kutimiza wajibu wao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam zote tatu zimepandishwa hadhi ya kuwa za Mikoa, lakini *in house information* hakuna. Hospitali hizi zikiwa za mikoa huwa zinapewa dawa muhimu, lakini MSD au chombo husika hawatoi kwa sababu hawana taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi wa wagonjwa katika Hospitali ya Amana, ninaiomba sasa serikali *Amana Social Hall* wapewe *Council* ya Ilala na ukarabati ufanywe iwe hospitali. Katika mgao wa mali kwenye Gazeti la Serikali, *Amana Social Hall* imepewa *Council* ya Ilala.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, ufanywe utarabitu wa kuipatia eneo hilo *Council*. Hoja hii nimeitoa kwenye RCC Mkoa wa Dar es Salaam na sasa naielekeza Wizarani.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe na Mungu akuvushe katika uchaguzi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzito inayogusa moja kwa moja maisha ya watu, chini ya Mheshimiwa Dr. David Mwakyusa na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, bila kumsahau dada yangu Blandina Nyoni, Katibu Mkuu wa Wizara. Kwa ujumla wake, ninawapongeza Watendaji wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu leo ni moja tu; elimu ya mpango wa uzazi shulenii na vijijini. Idadi ya watu ni jambo la muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Heri kukinga kuliko kutibu. Eneo hili ninaona limeanza kuwa *diverged* na *programs* nyine, watu wanaongezeka haraka na bahati mbaya kwa kuwa zaidi ya 50% ya watu wa Taifa hili ni chini ya miaka 20, ina maana endapo watu hao wakizaa hata kila mtu mtoto mmoja tu, ongezeko litakuwa ni kubwa sana na lenye wazazi wachanga ambaao pia wao wenye ni tegemezi. Hivyo basi; basi ni vyema kuendelea kutenga pesa kwa ajili ya elimu ya uzazi na idadi ya watu ili kutoa uelewa mpana zaidi shulenii na vijijini.

Mashirika yanayohamasisha mambo ya afya, yajikite zaidi kuunganisha nguvu na Wabunge kwenye maeneo yao ili kwa kushirikiana nao, watoe elimu hiyo vijiji na hata kwenye shule. Tukishirikiana mambo ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kuwapongeza Femina kwa kutuunga mkono wa vifaa na vipeperushi Siku ya Makumbusho Duniani iliyofanyika Songea.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninamshukuru Dada Amebilis, ambaye kwa kweli alitekeleza mara baada ya kuwasiliana naye kwa muda usiozidi saa mbili. Hali kadhalika, tunawashukuru *PSI* ambao pia walidhamini baadhi ya shughuli hizo za kukemea mimba za utotoni Mkoani Ruvuma na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninawaombea Mheshimiwa Waziri na Naibu wake warudi kama walivyo na waiendeleze tena Wizara yetu ya Afya na Ustawi wa Jamii, japo magonjwa mengine wanayotibu yanababishwa na wenzeni ambao hawajalipa uzito wa kutosha suala la taka.

Mheshimiwa Spika, hali ya Hospitali ya Liuli ni mbaya na hakuna *alternative* maeneo hayo.

Mlisema mtatoa vyandarua bure mbona sasa ni tofauti?

MHE. JUMA H. KILIMBAH: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Prof. Darid Homel Mwakyusa, Waizri mwenye dhamana, Mheshimiwa Dkt. Aisha Kigoda, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti ya Mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya ni nyeti sana kwa uhai wa binadamu na ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya Taifa, kwani bila afya za watu, shughuli za maendeleo zitadorora kwa maana hiyo ni wajibu wa serikali kuwa na sera madhubuti katika kulinda afya za watu wake.

Mheshimiwa Spika, serikali itoe kipaumbele katika kuhakikisha huduma bora inatolewa katika hospitali zetu, vituo vyetu vya afya, zahanati na kadhalika. Huduma hizi ni sharti ziambatane na uwepo wa wafanyakazi wa kutosha ambao watatosheleza mahitaji ya wagonjwa, vifaa vya kazi viliyvo bora na vya kisasa, madawa na kadhalika. Katika hali ya namna hii, ninao uhakika huduma zitakuwa bora na hivyo kulinda afya za watu na kuondoa hisia za shughuli za sekta hii kufanya kwa ubabaishaji zaidi kama inavyodhaniwa. Mbali na hilo, nidhamu na maadili ya watumishi yawe ya viwango vya juu.

Mheshimiwa Spika, nimeelezea hatua hii ya mwanzo kwani Sekta hii ni nyeti na inagusa uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2009/2010, serikali ilitenga Tshs. 40,000,000 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Wilaya ya Iramba (Kiomboi). Kwa nini

kazi hiyo hadi sasa haijaanza? Ninaomba Wizara ihakikishe kazi hiyo inaanza mara moja kwani hali ya Hospitali hiyo ya Wilaya hairidhishi hasa kwa masuala ya mifumo mbalimbali hasa ile ya maji, umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru serikali kwa kuweka utaratibu wa kuhakikisha kila Kata inakuwa na kituo cha afya. Pamoja na kazi hii nzuri, ninatoa wito vile vituo vya afya vilivyokamilika, serikali ihakikishe inavipatia vitendea kazi na watumishi ili utoaji wa huduma uanze mara moja. Vituo vilivyo katika hatua ya mwisho ya ujenzi vilivyopo Jimboni Iramba Magharibi vikamilishwe. Vituo hivi ni vile vya Kata za Urughu, Kyengege, Kidaru, Ulemo (Misigiri), Kaselya na kadhalika. Hatua ya ujenzi wa vituo hivi kupitia nguvu ya Wananchi imekwenda vizuri, sasa ni wajibu wa serikali kuvikamilisha vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, zahanati zilizokamilika kwa hatua zote zile za Mwandoigembe, Kikonge, Maluga, Mlandala na kadhalika, ninaombwa wizara sasa zipewe mgawo wa dawa toka MSD, kwani ni muda mrefu sasa tangu zahanati hizi kukamilika, utekeleazaji wa utoaji huduma haujaanza. Kitendo cha kuziacha zahanati hizi bila utoaji huduma kinaonekana kama kiini macho kwa Wananchi na hivyo kufanya majengo hayo kuendelea kuchakaa kabla ya hatua ya utoaji huduma iliyokusudiwa kuanza.

Mheshimiwa Spika, ninaombwa serikali iendelee kutoa elimu kwa Wananchi kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali ili kuudhibiti kabisa Ugonjwa hatari wa UKIMWI. Aidha, elimu iendelee kwa maeneo mbalimbali ikiwemo mashulen, vyuoni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bado shughuli za Idara ya Ustawi wa Jamii, henzieleweki vizuri miongan mwa Wananchi hasa waishio vijijini. Ninaombwa serikali itoe elimu ya kutosha kuhusu Wizara hii. Aidha, Watumishi wa Idara hii waongezwe.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara, Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa ujumla, kwa kuandaa bajeti hii ambayo inaonesha nini kitafanyika mwaka 2010 – 2011.

Mheshimiwa Spika, niseme juu ya kliniki za akina mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Spika, kliniki hizi zimekuwa na msongamano mkubwa sana na kusababisha akina mama wajawazito, pamoja na hali walionayo, kutumia muda mrefu sana kukaa pale na kuchoka sana, kutohana na upungufu mkubwa wa watumishi eneo hilo. Hali kadhalika, hata akina mama wenye watoto wanaohitaji huduma hutaabika na kukata tamaa juu ya tatizo hilo la upungufu wa madaktari na wauguzi pia. Naiomba wizara, kwa kuwa eneo hili ni muhimu sana, iongeze watumishi angalau kero hii ya kukaa kliniki zaidi ya saa tatu mpaka nne upunguzwe; kwani wanahitaji pia kupumzika zaidi akina mama wajazito. Ninajua serikali yetu ni sikivu na itafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niongelee juu ya upandishwaji wa vyeo watumishi hasa manesi, vinachelewa sana. Pamoja na marekebisho ya mishahara yao (kupanda vyeo), ninaomba Wizara ijitahidi sana kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanapata stahili zao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu hususan Madaktari wote, kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa moyo. Hospitali ya Wilaya ya Hanang ilijengwa na Wananchi kwa Hanang kujitolea. Wananchi hawa walifanya hivyo kwa kutambua umuhimu wa huduma za afya kwa ngazi ya Wilaya.

Je, Wizara itasaidia juhudi hizi za Wananchi kukamilisha maeneo muhimu kama wodi ya watoto, ukuta wa kuzunguka Hospitali na kadhalika?

Nitashukuru kupata Kauli ya Waziri kuhusu hili. Hospitali hiyo inahitaji *Ambulance* ya kubeba wagonjwa kwa kuwa Wilaya ni pana sana na ina vituo vichache vya afya. Nitashukuru kama Wizara itaisaidia Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Dr. Mtasiwa, kwa kutusaidia kutuletea Mganga Mkuu wa Wilaya na Daktari mwingine. Tutashukuru kama tutapata Waganga zaidi kwani zahanati na vituo vya afya havina wataalamu wa ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana kwa uamuji wa kuifanya Hospital ya Haydom kuwa Rufaa. Mungu awabariki.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizari hii na sekta yote ya afya kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri na maombi rasmi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utoaji vifaa na dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati uangaliwe upya. Bado *MSD* inapokea fedha kutoka halmashauri za wilaya na kuchelewa kupeleka dawa. Hii bado inaendelea kuathiri tiba sahihi na kwa wakati kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, bado wapo watendaji (*DMO'S*) katika halmashauri wanaokosa uwezo wa kuainisha mahitaji ya afya kwa ufanisi na kwa wakati na pia kuhodhi vifaa kama vile vitanda kwa wajawazito, magodoro na vitendea kazi na hivyo kuzorotesha huduma za afya wilayani.

Mheshimiwa Spika, pongzai maalum kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Wizara kuitikia wito niliota wa kupunguza kasi ya kuacha kazi na kutafuta ajira Serikalini kwa watendaji wa Idara ya Afya kutoka Hospitali

Teule ya Muheza. Mfumuko huo sasa umetulia baada ya waliohitaji ajira Serikalini kuweza kuajiriwa, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kwa ajili ya Hospitali Teule ya Muheza ambayo inamilikiwa na Kanisa la Anglicana na kuendeshwa kwa ubora na Serikali na upo mkataba rasmi. Hali ya hospitali hii ni mbaya na utendaji unaendelea kushuka kila siku. Ukweli ni kwamba wahisani waliokuwa wanaisaidia hospitali hii teule kutoka nje ya nchi kwa mfumo wa Kanisa Anglicana wamepunguza misaada yao na kuiacha hospitali katika hali ngumu ya kukosa vifaa na dawa, kwa msingi huo Serikali ichukue jukumu lake la kutoa huduma kama hospitali ya Wilaya ya Muheza ili kunusuru hali mbaya iliyopo katika Hospitali Teule ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, ombi rasmi la dharura pamoja na ombi hili kuwafikia wakati ambapo Bajeti ya Wizara imekwishaandaliwa, ombi rasmi la dharura lifikiriwe, ni kuomba *mortuary* (chombo cha kuhifadhi maiti) hivi sasa Hospital Teule ya Muheza haina huduma hiyo na maiti kulazimika kupelekwa Hospitali ya Bombo – Tanga zaidi ya kilomita 30.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi la maalum na ombi hili la dharura kwa njia hii ya mchango hapa Bungeni nitatuma ombi lingine kwa maandishi na kuonyesha makadirio ya baadhi ya vifaa vinavyoweza kupatikana kwa haraka kusaidia Wilaya ya Muheza na Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza kupata huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa jitihada zake za kupambana na malaria nchini. Ningeshauri ifanye kazi kwa mashirikiano na sekta nyingine kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mazingira, taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, hali ya nyumba zilizo nyingi zilivyojengwa nyingine ni vigumu kutundika *net* lakini Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Ardhi na Nyumba zikajengwa nyumba bora na zikawa na *drainage* nzuri zilizotumiwa tutapunguza mazalio ya mbu pamoja na magonjwa mengine ya mlipuko kama *cholera* na *typhoid*.

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa *net* unahusu mama na mtoto kama ikiwezekana *net* hizi zingepewa kwa familia nzima sababu baba mwenye nyumba anaweza kung'atwa na mbu mwenye vimelea vya malaria na kuiambukiza familia.

Mheshimiwa Spika, mapambano haya ya Serikali ya kupambana na malaria na UKIMWI kwamba tujuavyo ugonjwa wa Kifua Kikuu ni mtu na ndugu. Hivyo naiomba Serikali juhudzi zinazofanyika katika mapambano dhidi ya malaria na UKIMWI basi zielekezwe pia katika ugonjwa wa Kifua Kikuu. Nasema hivi kwa sababu ukienda hospitali katika *medical ward* kuna wagonjwa wengi waliolazwa kwa ugonjwa wa Kifua Kikuu hivyo fedha za UKIMWI na Malaria zipelekwe kusaidia Kifua Kikuu vile vile.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Afya wafanyakazi katika sekta hii wanafanya kazi katika mazingira magumu sana ikiwa ni pamoja na kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha na pia waongezewe ujuzi mara kwa mara. Kwa mfano katika hospitali nyingi haswa huduma katika nyumba za uzazi ni duni, vitendea kazi ni vichache mwishowe tuna walaumu wafanyakazi hawafanyi kazi kwa umakini. Ni mfano halisi katika hospitali ya Mawenzi Moshi katika wodi ya wazazi wanavyo vitanda vitatu tu vya kuzalishia na kwa siku wanajifunga watu zaidi ya 20 kwa siku, inabidi madaktari kutumia vitanda vya kawaida kwa ajili ya kuzalisha, siyo hilo tu Mawenzi hawana dawa za sindano kwa ajili ya kuongeza damu kwa waliopungukiwa kwa sababu *MSD* hawana dawa hizo. Pamoja na Serikali kutueleza mama wajawazito watapatiwa vifaa vya kujifungulia bure (*delivery kit*), vifaa hivyo havitoshi, bado kina mama wengi wanunuua vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, moja ya huduma muhimu katika hospitali ni kuwepo na maji (*running water*) lakini tumesikia baadhi ya hospitali hawana maji. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha hospitali ya Kibaha na Mwananyamala wanapata maji? Kama tujuavyo wakati daktari anapima mgonjwa katika *examination bed* lazima kila mgonjwa abadilishiwe shuka sababu kila mtu anakuja na ugonjwa tofauti na magonjwa mengine yanaambukiza kama ungonjwa wa ngozi na kadhalika hivyo hawawezi kushirikiana shuka, kama hakuna maji shuka haziwezi kuoshwa na wanaweza kuishiwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri, je, Serikali kwa nini katika vitanda vya ku-*check* wagonjwa visitumie *disposal paper* hii ni *more hygienic*, hatuhitaji maji ya kufulia, tutatunza mazingira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa dhamira yake ya kujenga zahanati katika kila kijiji lakini hata zile zilizopo bado zinafanya kazi kwa saa 9 tu, vitendea kazi havitoshi pamoja na wahudumu.

Mheshimiwa Spika, japokuwa mimi siyo mtaalam wa afya naamini ugonjwa hauna saa wala dakika wala ni muda gani utaugua. Kitendo cha zahanati kutokufanya kazi saa 24 kuchangia kwa kiasi kikubwa vifo vya kwa mama na watoto, zahanati hizi hazifanyi kazi wakati wa sikuu na siku za Jumapili hivyo ucheleweshaji wa huduma unaweza kuchangia vifo. Zahanati hizi zikifunguliwa saa 24 zitapunguza msongamano kwenye hospitali za ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali iwapatie hospitali ya Mawenzi Moshi dawa za watu wenye ugonjwa wa akili, siku za hivi karibuni tulisikia mama aliywakata kwa shoka watoto wake watatu na kuwauwa wote, maana yule ana matatizo ya ugonjwa wa akili lakini inasemekana alikosa dawa kwa siku tatu sababu zilikuwa hazipo. Pengine kama dawa zingepatikana malaika wale labda wangepeewa kuna yale maana angeweza dawa zake.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wake *danger fevers*, wataalam wanatueleza homa hii inaambukizwa pia na mbu hao wakimuumu mtu mchana anaweza kupata ugonjwa huo, je, Serikali ina mpango wowote wa kupuliza dawa kwenye mazalia ya mbu katika mji wa Dar es Salaam na Zanzibar pana kosekana na ugonjwa huo upo?

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya kusaidia ustawi wa wananchi kiafya. Nawatakieni mafanikio makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naona Wizara yako bado haijafahamu kuwa wilaya ya Njombe kabla ya mgawanyo wa hivi karibuni tulikuwa na halmashauri mbili ambazo ni halmashauri ya wilaya ya Njombe yaani majimbo ya uchaguzi Njombe Kaskazini na Njombe Magharibi. Halmashauri ya mji wa Njombe ni jimbo lote la Njombe Kusini, kwa hiyo, Jimbo la Njombe Kusini ambalo ndiyo halmashauri ya mji wa Njombe inayo hospitali ya Kibena na vijiji 44, mwaka huu wa fedha 2010/2011 hospitali ya Kibena imehamishiwa halmashauri ya mji wa Njombe. Hali na huduma za hospitali hii inatisha kabisa, hakuna dawa, hakuna mganga mkuu wa hospitali, hakuna gari la wagonjwa, wahudumu waliopo pale ni kama wamekosa mwongozo. Wananchi wamekatishwa tamaa kabisa na hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kabla halmashauri ya Mji wa Njombe haijapokea hospitali hiyo tume au wataalamu kutoka Wizarani waje wakague na waangalie hali ya hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumeongea na Mheshimiwa Waziri kuhusu hali ya hospitali hii, tafadhalii hatua za haraka kutoka Wizarani zitasaidia kurudisha hadhi ya hospitali hii ambayo ni moja ya hospitali kongwe nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo hospitali ya mkoa Maweni - Kigoma kwa kuwa hadi sasa Wilaya ya Kigoma haina hospitali ya wilaya, matatizo ni mengi katika hospitali ya mkoa kwani wagonjwa ambao walitakiwa kuishia hospitali ya wilaya inabidi watibiwe hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, nashauri vifaa na dawa ziongezwe ili hospitali ile ikidhi haja ya kuhudumia wagonjwa. Hospitali haina vitanda vya kutosha haina mashuka vile vile wauguzi ni wachache mno.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya mkoa ya Kigoma haina madaktari bingwa hali inayosababisha gharama kubwa kwa wagonjwa ambayo inawalazimu wasafiri kutafuta hospitali zenye madaktari wenye uwezo huweza kwenda *private hospital* na wengi wasio na uwezo wengine hupoteza maisha kabla hawajafanikiwa kufika hospitali kuonana na madaktari bingwa. Hivyo basi naomba Serikali ione umuhimu wa kuongeza wauguzi na madaktari bingwa katika hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, kampeni ya Zinduka Malaria haikubaliki ni kampeni nzuri lakini bado juhudii hazijatosha kwa kuwa bado maeneo ya kuzalia mbu ni mengi katika jamii zetu, ukizingatia maji machafu yaliyotapakaa kwa mfano jijini Dar es Salaam.

Mazingira mengi katika nchi hii ni machafu mno hali inayopelekea mazalia ya mbu na maradhi mengine ya kuambukiza. Hivyo Serikali ichukue hatua za makusudi kuelimisha wananchi na kushirikiana na halmashuri zetu ili kufikia lengo la kutimiza lengo la kuondoa tatizo sugu la malaria. Tukitokomeza mazalia ya mbu tutakomesha malaria na maradhi kama matende na magonjwa mengine yanayoletwa na mbu.

Mheshimiwa Spika, wazo la kutoa vyandarua ni zuri lakini maeneo mengi ya vijijini vyandarua vinatolewa kisiasa kwa kufuata itikadi za vyama na mara nyingi kesi hizo zimeonyesha usipokuwa CCM hupewi. Serikali ikomeshe hili, vile vile yabidi vyandarua vitolewe kwa familia nzima kwani maambukizi yanaweza kutoka kwa mwanafamilia mwingine asiyetumia chandarua kwani mbu huvuma muda wowote ambao wanafamilia huwa pamoja kabla ya kulala kwenye vyandarua vyao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itoe mafuta aina ya *lotion* maalum kwa watu wenyewe ulemavu wa ngozi yaani kwa maalbino bure kwani *lotion* hizo ni kama dawa kwao ambayo ina-*protect* kuharibu ngozi zao, vile vile Wizara ishirikiane na iwasiliane na Wizara ya Fedha ili iondoe kodi kwenye mafuta hayo maalum ya kulenga uharibifu wa ngozi za wenzetu maalbino.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa mazingira na maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya afya yaani madaktari na wauguzi. Ni muhimu ili kuwavutia kufanyakazi Serikalini kwani wengi hukimbilia hospitali binafsi kwenye maslahi mazuri, kwa mujibu wa taarifa ya CAG wapo watumishi hewa ambao wameshalipwa takribani shilingi bilioni nne kwa watumishi hewa, Serikali ichukue hatua ambapo inawezekana ni *chain* iliyopo Wizarani, Hazina mpaka kwenye halmashauri zetu. Kiasi hicho kingeongezwa kama tija kwa wauguzi waliopo kingesaidia kuongeza tija kwenye utendaji wa wafanyakazi kila siku.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Katibu Mkuu mama Blandina Nyoni, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii ambayo imejikita katika kuboresha huduma ya afya ingawa fedha walizotengewa ni ndogo sana kulingana na vipaumbele vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, nimetoa pongezi hizi ni kwa Waziri, Naibu Waziri kwa sababu wamekuwa hodari wa kujibu maswali ya Wabunge humu Bungeni vilevile wamekuwa hodari wa kufuatilia na kutekeleza vile vile hata ukiwakuta ofisini wamekuwa na moyo wa kuwasikiliza Wabunge hata wananchi pia hawana tabia ya kuweka viongozi na wananchi mlangoni kwa muda mrefu bila sababu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatambua uchapakazi wa rafiki yangu Katibu Mkuu Mama Blandina Nyoni kwa uwezo wake mkubwa wa utendaji na huduma nzuri kwetu sisi Wabunge tufikapo ofisini kwake na wananchi kwa ujumla. Ni kweli Wizara ina watu bora, niwaombee Mungu wapendwa wangu Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, wapiga kura wao wawape

kura za kishindo ili warudi kuendelea na yale mazuri mengi waliyoyatenda. Kwa Singida sina deni na Wizara hii yenye viongozi waungwana sana.

Mheshimiwa Spika, huduma ya Shirika la Dawa (*MSD*), ninaisifu Serikali kwa huduma yao nzuri ya dawa kupitia Shirika la *MSD* katika Kanda mbalimbali mfano Singida Kanda yetu ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ombi langu nashauri Serikali kuangalia mambo yafuatayo ili kuboresha huduma hii ya dawa kwenye halmashauri zetu. Mgawo wa dawa kulingana na mahitaji ya hospitali zetu, vituo vya afya na zahanati dawa zinapofika kwenye halmashauri huchelewa kufika katika vituo vya afya na zahanati naomba Shirika la *MSD* lipeleke dawa hadi kwenye vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dawa zinazopelekwa kwenye vituo vya afya, zahanati au hospitali mengi huwa yamekaribia sana kumaliza muda wa kutumika. Nitafurahi endapo Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri watatoa maelezo ya kuboresha huduma.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa leseni wa maduka ya dawa, napenda kukiri kuwa maduka ya dawa yanasaidia sana kutoa huduma ya dawa kwa wagonjwa hasa pale mgonjwa anapoandikiwa dawa kisha dawa hizo zinakosekana hospitalini, vituo vya afya na zahanati pia hivyo mgonjwa hukimbilia kwenye maduka ya dawa baridi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa kuna tatizo la utoaji leseni za maduka ya dawa kwani hutolewa kwa upendeleo mfano maduka mawili yanapokuwa karibu sana utastaajabu yule mwenye duka la muda mrefu anafungiwa na yule mwenye duka la muda mfupi anapewa leseni mfano Manyoni Mjini tatizo hili lipo, naomba Serikali ifuatilie na Singida Vijijini, kata ya Minyuge kijiji cha Mtavila.

Mheshimiwa Spika, huduma bubu ya wakunga, ni kweli wananchi hususani wanawake wanahitaji sana huduma ya wakunga hasa vijijini pale wanapotaka kujifungua. Tatizo bado kuna kliniki bubu ambazo zinatoa huduma kwa wanawake wanapotaka kujifungua wakati huduma zenyе kibali zipo lakini mama anaposhindwa kujifungua au kukosewa ndipo anapelekwa kliniki ambazo zimesajiliwa na Serikali wakati mwengine uongozi ngazi ya juu hupewa taarifa bali hufumba macho. Suala hili tatizo hili lipo Singida Vijijini, jimbo la Singida Kusini kata ya Minyuge kijiji cha Mtavila ninapenda kusikia kauli ya utawala.

Mheshimiwa Spika, wakuu wa idara hospitali ya Kiomboi kukaa muda mrefu, naishukuru sana Serikali kwa kutuletea daktari wa wilaya ya Iramba, Daktari Dorothy Kijugu anayejituma na mwenye uwezo mkubwa wa uongozi, ningependa Serikali itambue uwezo wake wenye kuambatana uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo ambalo linampa shida sana katika utendaji wake kwa sababu ya wakuu wa idara wenye muda mrefu pale na wanafanya kazi kwa mazoea.

Naiomba Serikali itoe uhamisho kwa wakuu hawa wa idara ambao Daktari Kiongozi akishirikishwa atawataja. Nasubiri maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtaalamu wa *X-ray* katika hospitali ya Kiomboi, napenda kuitaarifu Serikali kuwa hospitali ya wilaya ya Kiomboi ina upungufu mkubwa wa vifaa vya *x-ray*, na mtaalamu hakuna kwani aliopo hapa anafanyakazi kwa mazoea na hajasomea. Nitashukuru ombi hili likipokelewa.

Mheshimiwa Spika, chumba cha kuhifadhi maiti hospitali ya Kiomboi na Manyoni, napenda kuileza Serikali kuwa kila jambo zuri pia lina mapungufu au madhara yake mfano tangu tumepata barabara ya lami ajali ni nyingi sana na ajali hizo pia abiria wengi hupoteza maisha yao. Hivyo basi inawapa shida sana madaktari kuhifadhi maiti za marehemu hasa wale ambao kwao inakuwa mbali kwani kukosa majokofu ya kutosha na vyumba vya maiti ni vidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ombi, naomba Serikali ifikirie kujenga vyumba vya maiti vikubwa na kupatiwa majokofu ya kutosha kuhifadhi maiti. Upungufu wa watumishi pamoja na madaktari, ni kweli mkoa wa Singida una upungufu mkubwa wa madaktari na watumishi, naiomba Serikali kumpatia watumishi wa kutosha mapema, vilevile kwa vile tayari Serikali ilikwisha tupatia madaktari wanne kwa ajili ya hospitali ya mkoa kutoka Januari mpaka sasa hawajafika na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Waziri mwenye dhamana aliahidi kufuatilia suala hili kuititia swali langu katika Bunge hili la ishirini, napenda kujua ufuatiliaji umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusus huduma ya *TACAIDS*, kwa namna yoyote *TACAIDS* ina mahusiano ya karibu sana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hivyo ni vyema mahusiano yaendelezwe ili mikakati ya kupambana na UKIMWI yaweze kutekelezwa vyema, mfano suala la kutambua watoto yatima na walio kwenye mazingira magumu unahitajika ushirikiano wa karibu.

Mheshimiwa Spika, pia vizuri watendaji wa pande zote wakishirikiana ili kasi ya kutokomeza gonjwa hili la UKIMWI liweze kupungua kama siyo kumalizika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumaliza mchango wangu kwa kurudia kuwapongeza na kuunga mkono hoja hii kwa mikono miwili niwatakie utekelezaji mwema.

MHE. JOYCE M. MASUNGA: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake pamoja na wasaidizi wao wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya na Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga na hasa wanawake tunaishukuru wizara hii kwa kutupatia fedha kwa ajili ya ukarabati wa hospitali yetu. Nasema asante, kwa hospitali yetu sasa inapendeza.

Mheshimiwa Spika, aidha pamoja na shukrani hizo, napenda kumweleza waziri kuwa kutokana na uwingi wa wananchi wa Shinyanga tumefurahi kuiachia hospital hiyo iwe ya Manispaa ya Shinyanga. Tunasema asante.

Mheshimiwa Spika, Shinyanga tumetenga eneo kubwa sana kwa ajili ya hospital kubwa sana kwa ajili ya hospital ya Rufaa. Ombi kwa vile Wasukuma tunazaana sana tunaomba hospital hiyo ya rufaa ijengwe haeraka ili nasi tuweze kuhudumiwa pale pale Shinyanga kuliko hivi tunavyohangaika kwenda Bugando Mwanza au Muhimbili Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, napongeza bajeti na naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Handeni ni moja iliyotawaliwa na mazingira magumu. Hususan kutokana na ukubwa wake pamoja na umbali wa maeneo. Kupitia wizara naomba hili liwe considered.

Mheshimiwa Spika, elimu ya afya ya uzazi itolewe katika kata hususan tukizingatia up hill task ya kuvunja *cultural traits*.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa wataalam umekithiri uko mkakati gani? Wilaya ilituma maombi ya vijana waliomaliza Kidato cha Nne ili wapate fursa ya kujifunza katika vyuo vya afya, kulingana na sifa zao za masomo waliohitimu. Zoezi hili limefikia wapi, kama mkakati wa kupunguza uhaba wa watumishi kwenye zahanati za vijiji, vituo vya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuwatakia waziri na naibu waziri wake kila la kheri hususan huko tuelekeako kwenye uchaguzi mkuu.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospital ya Mkoa Mbeya, kwa niaba ya wananchi wa Jiji la Mbeya, natoa pongezi nyingi kwa serikali kwa kutimiza azma yake ya kutupatia hospitali ya Mkoa na kutenge wataalam wa tatribu katika hospitali hiyo. Ni faraja sana kwetu, pia kuwepo kwa hospitali ya Mkoa Mbeya kutatoa nafasi nzuri kwa hospitali yetu ya Rufaa, ambayo kwa muda mrefu imekuwa msaada mkubwa, kwa wakazi wa Jiji la Mbeya. Ninaomba nikumbushe ahadi ya ombi langu la gari kwa hospitali ya Mkoa Mbeya. Ni mwaka wa pili sasa naomba ombi hili, naamini gari hilo nitapatiwa sasa. Aidha, kwa kuwa tayari hospitali ya Mkoa imeanza kulaza wagonjwa naomba serikali iendelee kutoa

huduma ya vitanda na magodoro pir kuongeza idadi ya wauguzi kwenye hospitali hii ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, kustaafishwa kwa watumishi hospitali ya rufaa mbeya. Wapo watumishi waliostaafishwa/kuachishwa kazi hasa waliokuwa wanahusika na ulinzi na uhudumu, ambao mpaka sasa wanadai haki zao za mafao yao ya kuachishwa kazi. Idadi yao haipungui 25. naomba serikali inipatie majibu mbali na ahadi ya kuwalipa, pia ipo haja ya uhalali wa kuachishwa kwao kazi. Ni lini watalipwa stahili zao zote, pia je kuachishwa kwao kazi kulienda sambamba na taratibu za utumishi?

Mheshimiwa Spika, uhaba wa madaktari bingwa – Hospitali ya Rufaa Mbeya. Uhaba wa madaktari bingwas katika hospitali hii huleteleza huduma mbovu, hivi sasa wapo wakazi wa Jiji la Mbeya hupeleka wagonjwa wao Peramiko – Songea kwa matibabu ya mifupa badala ya hospitali ya rufaa Mbeya. Nashauri huduma hii iboreshwe kwa kuongeza zaidi madaktari bingwa wa mifupa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hotuba hii.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa wanachi wa jimbo langu la Tarime kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote cha kuwawakilisha bungeni baada ya kifo cha mpendwa marehemu Chacha Zakayo Wangwe. Mungu iweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuwashuru na kuwapongeza Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa hotuba nzuri yenye matumaini, napenda vile vile kuwapongeza watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri pamoja na changomoto nyingi ndani ya wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba zahanati zimejengwa nyingi sana na zipo katika hatua mbali mbali zikiwa zingine zimemaliza kujengwa, zingine zikiwa bad. Tatizo kubwa ni wataalamu yaani waganga, nurses, wataalamu wa maabara, kuanzia katika hospitali ya Wilaya hadi za vijijini hatuwezi kuimarisha afya na wananchi kama hospitali, vituo vyta afya hazina wataalamu pamoja na upungufu mkubwa wa dawa.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikalini kuhakikisha kuwa inawapelekea wanafunzi wengi vyuoni ili kupunguza kama sio kumaliza tatizo na wataalamu ni vema wanachuo wahitimu mafunzo kwa muda uliopangwa, kama ni miaka mitatu iwe mitatu, ni bora kuchelewa kupata waganga kuliko kupata wanganga ambao hawakuhitimu vizuri kama ilivyotokea katika Wizara ya Elimu ambapo walimu wamepatikana wasiohitimu vizuri matokeo yao elimu imeshuka sana iliyopelekea kupata wahitimu wasiofaulu vizuri ili wawe na sifa ya ufaulu mazuri kuingia vyuo vyta utabibu.

Mheshimiwa Spika, ni vema serikali ingali mpya mishahara ya wafanyakazi pamoja na posho ili kulipuka migomo ya mara kwa mara inayopelekea wananchi kupoteza maisha baada ya madaktari kugoma .

Mheshimiwa Spika, nashukuru serikali kukagua zahanati, vituo vya afya na hospitali mara kwa mara na kubaini mapungufu ambayo yapo, na kubaini zahanati hewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri serikali, wakati wa ukaguzi kama kuna mapungufu katika zahanati hizo wapewe maelekezo ili kurekebisha kero hizo, tunafahamu umuhimu wa sekta katika kutoa huduma ya afya kwa wananchi kwa zahanati ambazo zimesajiliwa zirekebishe kero hizo na zile zahanati hewa zifungwe na wahusika kupelekwa kwenye vyombo vya sheria. Afya ni muhimu sana kwa binadamu ili hata kimoja kwanza kiweze kufanikiwa ni lazima wananchi wake wawe na afya nzuri.

Mheshimiwa Spika, huduma duni ya Bohari za Dawa (*MSD*) bei ya madawa kutoka *MSD* ipo juu sana, kulinganisha na maduka ya binafsi ya jumla ya dawa. Na mara nyangi halmashauri zinapoagiza madawa huwa hakuna dawa kwenye Bohari.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Tarime haina madaktari, nurses wa kutosha kuna upungufu mkubwa. Niombe serikali kuipatia maktari, clinical offer, nursers hospitali ya Tarime, vituo vya afya vya Muriba, Nyarwana, Sirari pamoja na zahanati ambazo kwa ujumla zina uhaba mkubwa sana. Kuna zahanati zimefunguliwa lakini hazina wahudumu, zahanati kama za Kenyamanyuri, Gibaso, Geakuru, Nyamwanga, Bumera na nyagine nyangi.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watumishi katika hospitali na zahanati wanakuwa na lugha mbaya kwa wagonjwa hasa kwa akina mama ambao wanaenda kujifungua. Watumishi hao wanakuwa na lugha chafu sana kwa wagonjwa. Naishauri serikali kuwachukulia hatua za kisheria ni kuwa watumishi wenyewe lugha nzuri kwa wagonjwa na wenyewe nidhamu kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika zahanati na hospitali ni kubwa sana, nafahamu kuwa akina mama wanaendea kujifungua ni bure na watoto chini ya miaka mitano wanapata matibabu ya bure, lakini ni zahanati gani au hospitali gani inatoa huduma hii bure? Akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano wanalipia gharama za matibabu kinyume cha utaratibu na sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuiomba serikali kuwa makini wakati wa kukagua zahanati na vituo vya afya ili pale mapungufu yapo yaweze kurekebishwa, nawapongeza wamiliki wa maduka, zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa huduma nzuri kwa watanzania na kuisaidia serikali kutoa huduma hii muhimu ya afya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ahsante.

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru wizzara kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Aisha Kigoda kutembelea Tarime hasa maeneo ya Mgodi wa North Mara unaomilikiwa na Kampuni ya Barrick baada ya kupata taarifa ya madhara ambayo yamewapata wananchi wa vijiji vya Nyarwana, Nyakunguru, Weigita, Nyandoto, Matongo, Mrito, Kerende, Geukuru, Nyamwaga baada ya kutumia maji yenye sumu kutoka Mto Tigite.

Mheshimiwa Spika, serikali ilichukua sampuli za damu na kuzipeleka maabara kwa uchunguzi zaidi mpaka sasa wananchi hawajapata majibu ya sampuli za deamu na vipimo vingine ili kufahamu madhara waliyoyapata baada ya kutumia maji yenyе kemikali kutoka mto Tigit. Je ni lini vipimo hivyo vitakuwa tayari? Na kama matokeo tayari, majibu yake ni yapi?

Mheshimiwa Spika, na kama kulikuwa na madhara kwa afya kwa binadamu ni lini wananchi watalipwa fidia? Ni hatua gani za muda mfupi muda wa kati na muda mrefu zinachukuliwa na wizara ili madhara yanasiendelee kuwapata wananchi wanaoishi maeneo ya modi wa North Mara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, naopenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali, wakurugenzi wote na watendaji waote waliohusika katika kuboresha huduma za afya na pia kuandaa bafeti hii iliyopo imbele yetu..

Mheshimiw aSpika, maoni/ushauri, ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Kalekivule katika Kata ya Kitunda. Ujenzi wa hospital mpya ya Wilaya ya Ilala. Naomba kupata maelezo ni sababu gani ujenzi wa hospitali mpya ya Wilaya ambayo ilipangwa tangia mwaka wa fedha wa 2008/2009 mpaka hivi leo inasusua. Je wizara kwa kushirikiana na halmashauri ya Manispaa ya Ilala iko tayari, kusimamia ujenzi huo uende kwa kasi zaidi kama ilivyo kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais kwa kipindi hiki cha pili cha uongozi wake?

Mheshimiwa Spika, zahanati za Kata za Msongola, Chanika na Pugu ziboreshwе kwa kujengwa wodi za wazazi na watoto pia kutoa huduma masaa 24 ni kupatiwa huduma ya magari ikizingatia kuwa kuna idadi kubwa ya watu na umbali ni Km.40 toka katikati ya Mji/Jiji ambako kuna huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, hospitali maalum kwa wazee, kwa kuwa wagonjwa wengi walioko katika hospitali ya Muhimbili. Kata yao asilimia 70 ni wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea ambao maradhi yao huchukua muda mrefu kwa uchunguzi/vipimo hali ambayo huchangia kuongezeka kwa wagonjwa na kusababisha mlundikana na wagonjwa wengi kulala chini na kuleta adha na ugumu kwa madaktari na wauguzi kuelemewa. Ushauri serikali kupitia wizara hii iwe na utaratibu wa kujenga hospitali maalumu kwa ajili ya wazee kwa kanda kama Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam yenye kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza mlundikana wa wagonjwa hasa na muda mrefu ni kupatia nafasi wagonjwa wa muda mfupi na pia kuwapa hafueni madaktari na waguzi kufanya kazi kwa mazingira mazuri na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, operation maalum ya kuua mazalia ya mbu ifanyike katika Mkoa wa Dar es Salaam na sheria ndogo zitumike kwa kuelimisha wananchi kuweka mazingira yao kuwa safi na kwa kutotimiza hivyo sheria itumike.

Mheshimiwa Spika, itungwe sheria mpya kali ya usafi wa mazingira. Naunga mkono hoja.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wakurugenzi na watendaji wa wizara hii kwa hotuba nzuri sana na kazi nzuri sana hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na wizara hii ninaomba kuchangia mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa madaktari, wauguzi na kadhali. Lipo tatizo sugu sana katika Jimbo langu la Korogwe Mjini ambayo ni halmashuri ya mji Korogwe. Halmashauri hii imejenga zahanati tano moja ambazo ni Msambiazi Katonga, Kwakombo, Kwamsisi na Majengo. Juhudi kubwa sana zimefanyika kuwashamasisha wananchi kujenga,lakini chakusikitisha hadi leo hii zahanati hizo zinashindikana kuanzishwa kwa sababu hakuna madaktari na wauguzi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupatiwa msaada wa wataalamu hao haraka ili zahanati hizo zianze kutoa huduma haraka inavyowezekana ili wananchi wajenge imani na serikali yao. Inakatisha sana tamaa wananchi kuendelea kuchangia maendeleo iwapo zahanati hizi hazitafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, mafunzo. Yapo malalamiko mengi toka kwa wauguzi wasaidizi toka hospital na zahanati mbali mbali kwamba hawa wamesahaulika kuendelezwa hasa ikizingatiwa kwamba wengi wao ni darasa la saba. Lakini ieleweke hawa ndio wanafanayakazi kubwa ya kuhudumia wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini hawaendelezwi kimasomo na hali wanapenda kuijendeleza. Je serikali ina mpango gani wa kuendeleza kada hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, ambulance> Korogwe ni mji ipo halmashauri ya mji lakini cha kusikitisha hatuna kabisa gari la wagonjwa. Tunapata taabu sana kwa wagonjwa wetu toka vijiji 34 kupata huduma kwa wagonjwa wanaozidiwa. Ninaomba sana nipatiwe gari la wagonjwa la halmashauri ya mji wa Korogwe.

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya Majengo. Halmashauri ya Mji wa Korogwe imehuishwa zahanati ya Majengo kuwa na Kituo cha Afya. Bado kunahitajika vifaa na majengo mengi ili kituo hicho kiwe na hadithi ya kufanana na kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana msaada wa kuimarisha kituo hiki. Kituo hiki cha Majengo kikiimarisha kituo hiki. Kituo hiki cha Majengo kikiimarisha kitasaidia sana kupunguzwa idadi ya wagonjwa wengi kupata huduma hapo badala ya kwenda hospitali ya Wilaya Maagunga ambayo inazidiwa na awagonjwa wengi sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana iliyonisaidia kufanikisha kazi ya kupata majokofu ya kuhifadhiya maiti katika hospitali yetu ya Wilaya,

Mheshimiwa Spika, aidha napongeza Wizara hii kwa misaada mbali mbali waliyonisaidia katika wilaya yengu ya Korogwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuimarisha Afya yangu hadi leo. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote kwa ushirikiano wao mzuri na watendaji wengine katika Wizara hii, kutekeleza vyema majukumu yao na hatimaye kuleta Bungeni hotuba yao nzuri ya Bajeti kwa mwaka 2010/2011. Nawapongeza sana.

Napenda vilevile kuwapa pole kwa kazi ngumu wazifanyazo kila siku hasa kwa kuzingatia ugumu wa mazingira yanayowazunguka. Baada ya pongezi hizo ninayo michango yangu kama ifuatavyo:-

Kwanza ni shukrani, kwa niaba ya wapiga kura wangu napenda kutoa shukrani kwa Serikali kwa kukipatia gari la wagonjwa Kituo cha Afya cha Mwamashimba licha ya kuwepo gari lingine katika Hospitali ya Wilaya ilichopo Ngudu.

Aidha, kwa niaba ya wapiga kura wangu naishukuru sana Serikali kukubali kupandisha hadhi ya Zahanati za Nyamilama na Zahanati/Kliniki ya Ngudu kuwa Vituo vya Afya. Hii imekamilisha lengo la kila tarafa kuwa na Kituo cha Afya katika Jimbo langu. Naishukuru sana Serikali kwa vibali hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuishukuru Serikali ambayo imeweza Zahanati Saba na Vituo vya Afya vyote kufanyiwa ukarabati wa kutosha. Kwa macho vituo hivyo vyote kwa sasa vinavutia sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo ninayo maombi kadhaa kama ifuatavyo, kwanza naomba Serikali iendelee kuboresha utoaji wa huduma ya afya katika Kituo cha Afya cha Mwamashimba. Kituo hiki kimeelemewa na wagonjwa licha ya kutegemewa na wakazi wa kata tano, sasa tisa katika tarafa hiyo, wagonjwa wengine kutoka maeneo ya Kaskazini ya Jimbo la Solwa na sehemu ya Kusini mwa Jimbo la Misungwi. Hivi sasa gari la wagonjwa hulazimika kusafiri mara tatu mpaka nne kwenda Ngudu na kurudi kwa siku! Hofu yetu kubwa ni kuwa baada ya muda si mrefu hatutakuwa na gari la wagonjwa kutokana na gari lililopo kufanya kazi sana. Hali hiyo ikitokea wananchi watakuwa wakilalamika kulipa shilingi laki mbili hadi tatu kwa kukodi magari ya watu binafsi kupeleka wagonjwa Ngudu! Naomba sana tusirudishwe tena huko.

Mheshimiwa Spika, niombacho ni kutuo cha Afya cha Mwamashimba kuongezewa madaktari na wataalamu wengine kuwezeshwa kutoa huduma ndogo kama upasuaji mdogo, kuongeza maji na damu na ikiwezekana kuongezewa gari moja zaidi la wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo nimeyatoa siyo mara ya kwanza, nimeyarejea kwa kuwa haya ndiyo maombi ya wananchi, wadau na watumiaji wa Kutuo hicho cha Afya.

Mheshimiwa Spika, watumiaji wa kituo hicho cha afya idadi yao inaongezeka kila leo na ugonjwa sugu wa malaria hasa kwa watoto hali ipelekeayo watu waamini kuwa eneo hilo wachawi ni wengi hali inayowaweka akina mama hasa wenye umri mkubwa kuwa katika hatari ya kukatwa mapanga. Kutekelezwa kwa maombi hayo sio tu kutaliokoa gari hilo liweze kudumu kwa muda mrefu bali pia kutaokoa maisha ya watoto, akinamama, wazee na wagonjwa wengine wote hasa wale ambao maradhi yao yatahitaji msaada wa kuazimishwa kupelekwa Ngudu.

Kukosekana kwa dawa ya malaria, kwa siku za karibuni kumekuwa na juhudi kubwa ya kutokomeza ugonjwa wa malaria. Kampeni nyingi zimeanzishwa na hapo hapo kumekuwa na maelekezo ya kukataza matumizi ya dawa hizi na zile na kupendekeza matumizi ya dawa zile na zile! Kilichonihuzunisha ni kuona kuwa dawa iliyotangazwa sana ya dawa mchanganyiko imekuwa mali adimu katika Hospitali za Serikali na za watu binafsi. Je, kwa utaratibu huu malaria si itakuwa inakubalika?

Mheshimiwa Waziri wakati wa kufunga hoja yake naomba atoe maelezo ili kuwasaidia wananchi maswali haya yatasaidia yakinuwa kama mwongozo. Kwanza, ni kitu gani kimetokea dawa hii ya *ALU* kupotea ghafla. Pili, ni nini hatma ya upotetu huu katika kipindi hiki mbadala wa dawa hiyo ni dawa gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hospitali ya Ngudu ambayo ni ya Wilaya ya Kwimba iliyopo Ngudu inahitaji msaada mkubwa wa Serikali ili ifanye kazi kama Hospitali. Sifa zake kwanza ina wodi tatu tu ambazo ni kwa ajili ya wanaume, wanawake na wazazi, haina wodi ya watoto wadogo, haina wodi ya maradhi ya kuambukiza, majengo yake mengi ni ya zamani sana ikiwa ni pamoja na *theatre* na zaidi madaktari hawatoshi. Naomba Serikali iweke mkono wake ili kuboresha mazingira na kuboresha huduma ya utoaji huduma. Upungufu wa mazingira bora ni pamoja na kutokuwepo na vyoo vya wagonjwa wodini! Si rahisi kuamini lakini ndiyo ukweli kwa kuwa ilianzishwa kama Zahanati kisha ikapandishwa kuwa Kituo cha Afya na hatimaye kuwa na hadhi ya Hospitali ya Wilaya. Huduma nyingi zimekuwa zikitolewa katika Hospitali ya Sumve ambayo hata leo mazingira yake ni bora zaidi kuliko mazingira ya Hospitali ya Ngudu.

Mwisho ombi tayari nimelifikisha Wizarani la kuomba mafunzo ya Uuguzi kutolewa katika Chuo cha Afya cha Ngudu. Hii itapunguza upungufu wa wauguzi uliopo Ngudu na Kwimba kwa jumla. Bado ninaamini marekebisho hayo yanawezekana kama Serikali ikiamua. Kama mpaka leo halijakubalika ni kwa kuwa suala hili halijafanyiwa kazi. Naomba ombi hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, hoja yangu kubwa ni kuhusu ruzuku au msaada kwa Hospitali ya Mtakatifu Gasper – Itigi, Chuo cha Waugazi – Itigi (*St. Gasper*).

Mheshimiwa Spika, mapema mwaka huu tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ambapo alielezwa/alipewa matatizo yanayoikabili Hospitali ya Mtakatifu Gasper na Chuo chake cha Uugazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni hatua gani zimechukuliwa *so far* kuzisaidia Hospitali na Chuo cha Uugazi hapo Itigi? Vinginevyo, kama yamekaa vizuri nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazozifanya Waziri na Naibu Waziri wake.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Nampongeza sana Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa akiwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Kweli Mheshimiwa Naibu Waziri amedhihirisha kwamba akina mama tunaweza tukipewa nafasi. Hongera sana kwa wote. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waweze kurudi katika Bunge lako hili Tukufu. Kweli ni wachapakazi hasa katika taaluma yao hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ikazie au ifufue *Family Planning* (Uzazi wa Mpango).

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kuondokana na umaskini wa familia au kujikwamua kiuchumi, mimi naamini Wizara ipange mikakati ya kutosha ili familia izae watoto ambao inaweza kuwashudumia kwa lishe, elimu, afya za watoto na kadhalika na hivyo, kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, pia itapunguza watoto wa mitaani au watoto waishio kweye mazingira magumu. Kama watu wote wenye jinsia zote tutajua wakati gani wa kufanya tendo la ndoa ili tupate watoto, na wakati gani tendo la ndoa linafanyika na hakuna mtu kupata mimba. Elimu hii ni muhimu kwa wote yaani mke na mme kujua.

Tukiweza kuelimisha watu wote na tukizingatia hili, mimi naamini hatutapata au tutapunguza sana watoto wa mitaaani na mimba zinazokuja bila mpangilio, hasa kwa wasichana, mimba za umri mdogo. Hivyo elimu hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, basi naomba Wizara hii ipewe fedha ya kutosha kwa ajili ya uzazi wa mpango ili iwafikie wananchi wote na ndio hapo tutapata kujikwamua kiuchumi na kila mtu atazaa watoto wake anaowataka na anaoweza kuwatunza.

Mwisho ila si kwa umuhimu, naomba *ambulance* angalau nne kwa ajili ya Jimbo la Bukene. Tukiwa na *ambulance* hizi, zigawike kwa kila Kata nne tupate *ambulance* moja, kwani kuna Kata kumi na sita. *Ambulance* hizi zikiwa ziko kule ziweze kusaidia kukimbiza akina mama wajawazito haraka kwenda Hospitali ya Wilaya ambayo iko Nzega na hivyo itapunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, hivi wale Maafisa Afya wako wapi? Naomba hawa watimize wajibu wao, watoe dawa za kunyunuzia kwenye madimbwi ya maji, ili kuuwa mazalio ya mbu. Pia hawa wawashauri wananchi kufyeka majani na kufukia makopo, vifuu, takataka zote kama vigae ambavyo vinaweza kuwa mazalio ya mbu.

Mheshimiwa Spika, Waingereza husema *prevention is better than cure* yaani kuzuia au kinga ni bora kuliko tiba kama kweli tunataka kuachana kabisa na malaria.

Mheshimiwa Spika, kutoa vyandaurua sikatai ni moja ya kinga ni kulala kwenye chandarua, lakini mtoto au mama mjamzito na wananchi kwa ujumla, wanakaa nje bila chandarua kabla ya kulala na mtu yuko pale, wanaumwa na mbu na hivyo kupata malaria. Kwa misingi hiyo kinga ni muhimu kuliko tiba hawa maafisa afya wafanye kazi yao ipasavyo, wasikae mezani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, hongera na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ipeleke waganga na wasaidizi wao kwenye zahanati za Jimbo la Ismani haraka, kibali mnacho.

Mheshimiwa Spika, naomba magari ya kubeba wagonjwa sita kwa vituo vya afya vitano na moja katika Hospitali Teule ya Pamba.
Hongereni sana.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini na kwa niaba yangu binafsi kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na watumishi wote wa Wizara kwa mafanikio yaliyopatikana katika kudhibiti mlipuko ya malaria na vifo vya watoto, mama zao na hata watu wazima kutokana na gonjwa la hatari la malaria. Ahsante sana Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iendelee kuwa karibu nasi muda wote. Tunawapenda sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mmefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa vita ya malaria iendelee hasa kwa kuua mazalia, tunyunuzie dawa katika mifereji, maji yaliyosimama ili kumaliza vyanzo vya mbu, nyasi zifyekwe karibu na nyumba, iwe kampeni ya usafi wa mazingira hakika malaria ni adui na pia halmashauri zitunge *by laws*.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wizara ni nzuri.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana nia nzuri kwa Serikali kwa kupunguza vifo vya wanawake na watoto, mafanikio ya Wizara kwa kutumia Bajeti finyu ni la kupongezwa. Hata hivyo naomba Serikali iongeze Bajeti kufikia ile ya Abuja ya 15% ya kipato cha nchi yetu kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vingi vya mkoa wa Rukwa havijapata zahanati naomba Serikali isaidie zahanati hizi zijengwe Wabunge na Madiwani watasaidia hamasa.

Mheshimiwa Spika, mbanano wa wagonjwa katika hospitali za wilaya na mikoa nchini bado ni tatizo naomba hilo litazamwe. Nashauri pia elimu wa wahudumu wote wa afya iendelee kwa sababu huduma yao bado ni mbovu na hasa lugha wanazotumia zinakatisha wagonjwa tamaa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuteua hospitali ya *mission* ya Khristo Mfalme katika manispaa ya Sumbawanga naipongeza. Hata hivyo hospitali ile ina majengo yasiyotosha hasa wodi ya watoto na *maternity ward*, pia wodi ya magonjwa ya kuambukiza haipo. Naomba Serikali ilitimize hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa kuteua hospitali ya Tosamaganga kuwa Hospitali Teule ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, hata hivyo naomba hospitali hii iboreshwe ili kuendana na ongezeko la wagonjwa pia chumba cha kuhifadhia maiti kiboreshwe.

Mheshimiwa Spika, naomba zahanati ya Mgama iwe kituo cha afya na majengo yaboreshwe. Mfuko wa bima ya afya uboreshwe na uweze kusimamia vizuri *CHF* na wanachama wa *CHF* waweze kupata matibabu popote nchini badala ya kupata huduma maeneo yao tu.

Mheshimiwa Spika, huduma za mazoezi ya viungo zikiimarishwa katika hospitali za wilaya na mikoa vifaa pamoja na wataalamu waongezwe.

Mheshimiwa Spika, suala la unyanyaswaji wa kijinsia (*Gender Based Violence*) huduma kwa waathirika wa unyanyasaji ikiwa ni pamoja na kubakwa na kunajisiwa wapewe huduma vizuri badala ya kesi kuhesabiwa kama za polisi (*Police cases*). Wizara iharakishe utengenezaji wa mwongozo wa kusaidia kutoa huduma kwa waathirika hawa (*comprehensive health services for survivor of gender based violence*) mradi utakaoanza kwa majaribio mkoani Iringa, Wizara iwe bega kwa bega kusaidia utekelezaji wake, ikiwa nia kuweka chumba maalum.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kuwa Wilaya ya Kongwa kwa miaka mitatu sasa haina Mganga Mkuu wa Wilaya (*DMO*), inaongozwa na afisa afya, tuleteeni *DMO*.

Mheshimiwa Spika, Kongwa tuna zahanati 13 zimejengwa na zimekamilika, lakini hazina manesi na waganga na kwa hiyo, zimefungwa hazifanyi kazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuboresha vituo vyta afya kwa kila kata (MMAM) umefikia wapi? Mbona hausikiki tena?

Mheshimiwa Spika, *training* ya *nurses* na *clinical officers* iboreshwe kwa kuongeza idadi ya wanafunzi na wahitimu hali ni mbaya hakuna wataalamu vijijini.

Mheshimiwa Spika, mishahara na posho za madaktari na manesi ingaliwe upya, madaktari hasa wanaotibu hali zao dhoofu kimapato.

Mheshimiwa Spika, huduma za vipimo ni kidogo sana vijijini hasa maabara na wataalamu wake wachache sana.

Mheshimiwa Spika, fedha za kununua dawa na vifaa hospitalini ziongezwe. Serikali iwalipe *MSD* kuwapa uwezo wa kumudu shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya ya Kongwa madaktari waongezwe idadi na manesi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, kwanza natuma salamu za pongezi sana kwa Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Waziri na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Naibu Waziri, Ndugu Blandina Nyoni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya pamoa na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kuendesha vizuri Wizara hii ngumu na muhimu katika Taifa letu, wamejitatidi sana kufanya vizuri katika miaka mitano hii ya awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hoja yao ningependa kuwashauri kwamba Bima ya Afya ya Taifa imeanza kueleweka vizuri nchini lakini Wizara ijitahidi zaidi katika kutoa elimu vijijini ili wananchi waweze kunufaika, bado kuna matatizo sana katika utoaji wa huduma hii vijijini na hasa pale ambapo hakuna zahanati za Serikali. Wananchi wengi hukosa huduma za matibabu kwa sababu hawana Bima wala fedha za kulipia gharama za matibabu.

Kwa upande wa UKIMWI, Wizara inajitahidi kutoa huduma lakini bado kuna tatizo la uelewa na hasa kwa waathirika vijijini hali zao huwa mbaya zaidi kutokana na kukosa lishe bora na ARV's. Tukiwasaidia kwa mpango wa chakula bora ama lishe tutaweza kuwaokoa wengi zaidi. Siku hizi kuna mchanganyiko wa lishe bora unaotengenezwa viwandani hasa Afrika ya Kusini ambapo tukitumia kupitia mifuko ya misaada ya akina Bill Clinton tutaweza kupunguza vifo na mateso kwa wagonjwa wengi.

Kwa ndugu zangu wa *TFDA* nawapongeza kwa kuanzisha shirika (*strong*) linaloonyesha kukomaa. Matatizo ya dawa feki zinazoingia nchini bado yapo na hasa dawa za chini ya kiwango kutoka India. Kuna wakati mimi binafsi nilikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya mwaka 1995 -1998 na wakati huo nilithubutu kuwaagiza *MSD* wasilingize dawa toka India. Ilisaidia kupuguza dawa feki, sina maana kuwa viwanda vyote vya dawa toka India ni vibaya ila kuna *black market* ya zaidi ya viwanda 40,000 vinavyotengeneza dawa zisizo na viwango. Ukizua hizi tutasaidia sana kupunguza dawa feki na usugu wa vijidudu kwa dawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa ndugu zangu, leo nitashika mishahara yenu kwa kile kiwanja cha Chalinze ambacho nilitenga kwa ajili ya kuniletea wale Wazungu wajenge Hospitali. Sasa kile kiwanja tutajenga (*garage*) miaka ya utumishi wangu imekwisha sina majibu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hotuba hii mambo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka kila siku na idadi ya vifo na maradhi mbalimbali yanaongezeka na kupelekea kuwa na mahitaji ya Madaktari

Mabigwa katika hospitali zetu, je, Serikali imejiandaje na kuwapata Madaktari Mabigwa ambao watapelekwa kwenye Wilaya zetu na hata kwenye Tarafa au Kata? Hii itasaidia uboreshaji wa huduma za afya na pia kupunguza vifo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna mkakati gani wa kudhibiti uingizaji wa “*Pads*” wanazotumia akina mama ambazo hazifai na ziko chini ya kiwango na kuwasababisha maradhi?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Hazina iongeze bajeti ya Wizara hii ili kuwa na uhakika wa uendeshaji na utoaji huduma za afya kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya kuboresha afya za Watanzania wote. Lazima tukiri kuwa pamoja na juhudi zao hizo bado Wizara hii inakabiliwa na changamoto nyingi kufikia malengo yaliyokusudiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mkakati wa Kudhibiti Malaria 2008 -2013, Wizara imefanya jambo zuri kwa vyandarua vyenye viatilifu kwa hati punguzo kwa mama wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka mitano lakini Wizara lazima ielewe kuwa mbu na malaria hawapo kwa ajili ya mama wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka mitano tu bali kwa watu wa umri wote na jinsia zote, kufanya hivyo ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu kwani wale wasio na vyandarua watawaambukiza hata wale wenye vyandarua.

Hivyo, Wizara haina budi kugawa vyandarua kwa watu wote. Ikiwa haiwezekani kwa nchi nzima kwa wakati mmoja basi ifanyike kwa Kanda za Jiografíia lakini pia kuna tatizo kubwa la mazalio ya mbu. Miji yetu na vijiji vyetu ni vichafu sana kiasi kwamba vinaruhusu mazalio holela ya mbu, kwa ajili ya kutokomeza malaria ni lazima tuuve mbu kwenye mazalio yao. Kwanza kwa kusisitiza usafi katika maeneo yetu ya kuishi na pili kwa kunyonyuzia dawa ya kuuwa mbu maeneo ya maji yaliyotuama.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya madawa ya kulevyta, nikiri hili ni tatizo linaloikabili dunia, ni tatizo linaloua nguvu kazi kubwa ya vijana wa Kitanzania na hivyo linaloathiri uchumi wa nchi yetu. Tatizo lililopo ni kwamba mkazo umewekwa zaidi kuwashudumia waathirika wa madawa ya kulevyta kwa ushauri nasaha na hata kwa kuwatibia lakini Serikali haina mikakati ya kudhibiti uingiaji wa madawa ya kulevyta nchini.

Tatizo hili limepigiwa kelele sana hapa Bungeni akiwemo Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa, kwa nini hatuoni harakati za Serikali kuwatia nguvuni wahusika na kuwafikisha Mahakamani au Serikali imeshindwa au wahusika wanakula na wakubwa kama tetesi zinavyoeleza? Tukiachia hali iendelee kama ilivyo sasa tutakuwa na Taifa lenye vijana wasiweza kujisaidia wenyewe na wala kusaidia Taifa lao katika

kujenga uchumi imara. Tunatarajia Serikali itatekeleza wajibu wake kutokomeza madawa ya kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda (Mb), Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara ya Afya na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kuboresha huduma za afya kupitia MMAM na programu nyingine. Hata hivyo, kasi kubwa ya wananchi kuitikia wito na kujenga Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali haiendani na kasi ya upatikanaji wa Madaktari, Wauguzi na vitendea kazi hasa magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, huduma ya bure kwa ajili ya wazee bado haitekelezwi kwa jinsi ilivyotarajiwa. Bado katika maeneo mengi wazee vikongwe hawapati huduma za afya kwa mujibu wa sera.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa dawa kutoka *MSD* bado si wa kuridhisha, ipo haja ya kuimarisha utaratibu wa kuhakikisha dawa zinafikishwa Hospitalini, Vituo vya Afya na Zahanati, kwa utaratibu mzuri usioukuwa na upungufu wa mara kwa mara wa dawa.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kwa hatua za kuhudumia watu wenye ulemavu. Hata hivyo, bado ipo haja ya kuwa na taratibu bora zaidi za kuhudumia walemvu wa ngozi, maalibino.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kupambana na malaria, nashauri Kada ya Mabwana Afya, ambao wana jukumu la kulinda usafi wa mazingira, tuirudishe na pawepo na sheria kali za usafi wa mazingira, Halmashauri za Miji zielekezwe kuwa na Sheria Ndogo za kuhakikisha usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoa na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri na ngumu wanazozifanya kila siku, baada ya shukrani hizo, naomba nichagie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vyombo vya habari hasa kupitia Luninga (*TV*), vimekuwa vikionyesha matokeo ya kufunga baadhi ya vituo au maduka yanayouza dawa na vituo vinavyotoa huduma mbalimbali katika maeneo tofauti hapa nchini. Zoezi hilo lililalamikiwa na watu wengi kwani wengi walikuwa wakijuliza, vituo na maduka hayo yalifunguliwa miaka mingi iliyopita, hivi muda wote huo wahusika walikuwa hawaoni au

kuna ajenda gani? Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee usafanuzi jambo hili ili wananchi waelewe ni kwa nini hatua hiyo ilichukuliwa ikiwa imechelewa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, Waziri alisikika kwenye vyombo vya habari hivi karibuni (siku sikumbuki) akisema kuwa asilimia tano (5%) ya wagonjwa waliopewa damu waliambukizwa VVU. Je, ni hospitali zipi hizi zilizowapa wagonjwa hao damu yenyе virusi vya UKIMWI na je, wahusika walichukuliwa hatua gani za kisheria baada ya tukio hilo?

Mheshimiwa Spika, maambukizo ya virusi vya UKIMWI (VVU), kwa mujibu wa mchoro Na.3 wa Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, inaonekana kuongezeka mwaka hadi mwaka. Je, ni asilimia kiasi gani ya Watanzania wenye VVU kwa sasa na je, Serikali haioni ni vema kila Mtanzania apime VVU kwa lazima ili kujua idadi halisi ya watu walioambukizwa kuliko ilivyo hivi sasa ambapo mtu hupima kwa hiari. Serikali haioni kuwa uhiari huu ndio unaongeza kasi ya ongezeko la VVU nchini?

Mheshimiwa Spika, napenda pia nifahamu ni Wilaya zipi zenyе idadi ya watu walioambukizwa VVU na Serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa maambukizi haya yanapungua au kumalizika katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Serikali.

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza viongozi wote wa Wizara hii. Pia napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kilio changu kiko palepale, chumba cha kina mama wanaojifungua kukosa hata taa na hatimaye mama anakwenda kujifungua anatakiwa kutoa pesa ya mafuta ya taa, si kama hamfahamu hata kama ni TAMISEMI wanafanya hivyo je, Wizara imetoa tamko gani? Naimani kulingana na umri ambao Waziri na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wanao, wamezaliwa vijijini, wakumbuke walikotoka, waangalie maisha ya watu, uongozi ni dhamana kwa kila mmoja mahali alipo. Vifo vinavyoongezeka vinawagusa. Nadhani kwa leo inatosha kutokana na michango yangu niliyotoa kwa muda wa miaka mitano niliyokuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza, kwa hotuba nzuri yenyе usafanuzi mzuri na wa kina kuhusu Wizara hii. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. pamoja na kuunga mkono, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti ya kununua madawa kwa kuwa fedha zinzotolewa ni kidogo sana na hivi sasa kuna ongezeko kubwa la watu na hasa vijijini na madawa hayatoshi kwenye zahanati ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa?

Pili, je, Serikali imedahili wanafunzi wangapi mwaka 2009/2010 waliojiunga na Vyuo vya Uganga (*Clinical Officers* na *Clinical Assistants*) ili kupunguza tatizo la upungufu wa wataalamu hao katika Vituo vya Afya na Zahanati hapa nchini?

Tatu, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha masharti ya watumishi wa Afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Maafisa wa Afya, Mafamasia, Maabara na kadhalika?

Nne, je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Vyuo vya Maafisa wa Afya kikiwemo Chuo cha Maafisa wa Afya Mpwapwa kwa kuvipatia vitendea kazi, vifaa vya kufundishia na kuwatengea fedha za mazoezi kwa vitendo? Je, jengo la Chuo cha Maafisa wa Afya Tanga litakamilishwa lini kwa kuwa halijakamiliha hasa mabweni ya kuishi wanachuo na madereva?

Tano, je, Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa itaongezewa lini Madaktari kwa kuwa ni wachache sana?

Sita, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kukagua maduka ya madawa mara kwa mara ili kudhibiti madawa yaliyopitwa na wakati (*expired drugs*)?

Saba, kwa kuwa katika Wilaya ya Mpwapwa inajenga Zahanati katika vijiji vya Kiboriani, Kiyeghea, Mwenzele, Mlembule na Mwanakianga, je, Serikali imetenga bajeti ya madawa katika Zahanati hizo kwa kuwa zitakamilika mwaka huu wa 2010?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri, maelezo yalikuwa “*Well Balanced*”. Hata hivyo, Sera ya kuwa na Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kwa kila Kijiji, ni changamoto ambayo inahitaji maandalizi ya Waganga, *Nurses* na wataalamu wa kutosha ili tuisiwakatishe tamaa wananchi ambao wana imani kubwa kwa Chama na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzito.

Mheshimiwa Spika, nashauri utaratibu wa kugawa dawa Mahospitalini/Vituo vya Afya na Zahanati kuititia *MSD*, upatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, umekuwepo ukaimu wa muda mrefu mno wa Mkurugenzi wa *MSD*, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, upungufu wa dawa, Watumishi katika Zahanati vituo vya Afya na Hospitali, upatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, matibabu ya Wazee na wasiojiweza, yanasmubua.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Prof. Mwakyusa Waziri wa Afya na Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya siku hadi siku. Kwa niaba ya Wananchi wa Mpanda, natoa shukrani za dhati kwa hatua inayochukuliwa sasa ya kukarabati, ujenzi na hatimaye kufunguliwa kwa Chuo cha Matibabu Mpanda, Chuo ambacho kilikuwa cha Afya hapo awali. Niombe tu kasi iongezeke ili kikamilike haraka na niwashukuru wote ambao wamekua wakipata usumbufo toka kwangu kwa kipindi cha miaka yote mitano juu ya Chuo hiki angalau sasa nafarijika jitahada zangu na kilio cha watu wa Mpanda kimesikilizwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pekee ambalo bado tunalo Mpanda ni uchache wa Madaktari na Wauguzi. Nitumie fursa hii, kuiomba Wizara kuangalia namna itakavyoweza kutupa misaada wa kuongeza Madaktari (*M.O*) kwani Madaktari Wasaidizi angalau wapo (*A.M.O*) pia tupate Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Wanawake na Watoto ili kupunguza ghamama kwa wananchi wetu kufuata huduma hiyo Hospitali ya Mkoa Sumbawanga ni mbali. Naamini Wizara italifikiria na kulikubali ombi hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. MARGRETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, Wizara imetenga fedha za kutoa misaada ya kijamii kwa makundi maalum. Naomba kufahamu utaratibu wa kupata misaada hiyo ukoje?

Mheshimiwa Spika, bado nyenzo za kujimudu kwa wenye ulemavu ni aghali hivyo wengi wao hawamudu kuzinunua. Naishauri Serikali ione uwezekano wa kutoa ruzuku kwa nyenzo hizo. Naipongeza Wizara kupitia Mfuko wa Bima ya Afya kwa kuanza kutoa huduma za nyenzo hizo kwa wanachama wao.

Mheshimiwa Spika, kwa vile suala la ulemavu ni mtambuka, nashauri kila Wizara iweke dawati la masuala ya wenye ulemavu kama ilivyo kwa Madawati ya Wanawake ili kuwezesha kuharakisha utekelezaji wa haki zao kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, Naibu Spika, Wenyeviti, Katibu wa Bunge na Watumishi wote, kwa ushirikiano mlionipa katika kutekeleza majukumu ya Kibunge humu ndani na nje ya Bunge. Nitaendelea kuwakumbuka kwa yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja. Pamoja na hayo, naipongeza Hotuba ya Waziri kwa jinsi ilivyojaa takwimu na maelezo yanayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa dawa Hospitali za Rufaa Bugando. Inashangaza sana kama mgonjwa amepelekwa rufaa Bugando halafu mgonjwa anaambwa dawa fulani hazipo aende akanunue katika maduka ya dawa nje ya Hospitali! Hivi hii ni sahihi? Nimeshuhudia.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa majengo na hasa rangi. Nashukuru sana kwa Wizara kulitambua hili katika *budget* hii. Inatisha kuliona jengo refu halafu lina rangi chafu. Rai kwao ni kuanza mapema mara *budget* itakapopitishwa.

Mheshimiwa Spika, Wazee sharti waheshimiwe sehemu zote. Moja ya maeneo ambayo wanastahili heshima na huduma za haraka ni Hospitalini lakini lililopo ni kutoheshimika. Naomba Wazee wote wenyewe vitambulisho vyenye picha zao watengewe maeneo yao ili mara wafikapo Hospitalini watibiwe bure na haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugawaji wa vyandarua, naipongeza sana sana Serikali kwa hatua waliyofikia katika utoaji na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa hapa nchini.

Tatizo langu ni kwa Wazazi. Naomba Waziri atoe tamko tu la kila mzazi anapojfingua akiwa Hospitalini mara atokapo kwenda nyumbani kwake apewe chandarua chenye dawa. Hii itakuwa kinga kubwa sana kwa mama na mtoto na hasa mtoto kujikinga na ugonjwa wa malaria. “Malaria haikubaliki”.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote kwa kuandaa Hotuba hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Ukaguzi wa hospitali za *Private* na *Dispensary* zilizoanzishwa na Serikali kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza ni mzuri sana. Naomba ukaguzi uendelee kwa Mikoa mingine ili kuondoa tatizo la hospitali bubi zinazoteketeza maisha ya Watanzania. Kitendo cha Hospitali, *Dispensary* ya *Private* kufanya *operation* wakati hawana Wataalam wenyewe utaaliam huo ni hatari sana. Wengi wanaopoteza maisha huko ni watoto na akina mama.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke taratibu na viwango vinavyotakiwa kufikiwa/kutimizwa kabla ya watu binafsi kupewa vibali na kufungua/kuanzisha hospitali. Ukaguzi makini ufanyike kwenye *site* kabla ya Hospitali/*Dispensary* kuruhuswa kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, wale wote wanaobainika kutoa vibali holela kwa kula rushwa washughulikiwe kisheria. Watumishi wa Afya pamoja na wale wanaota Elimu ya Uzazi Salama, Uzazi wa Mpango maeneo ya vijiji ni wachache sana. Serikali lazima

ihakikishe kila Kituo cha Afya/*Dispensary* ina mtaalam wa huduma ya uzazi, watoto na uzazi wa mpango. Idadi ya watu vijijini inatisha, elimu inatolewa zaidi mijini ambapo viro vyombo vya habari kama radio, televisheni, Magazeti kule vijijini ambapo hata habari haifiki, huduma hazifikishwi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Urambo – Tabora ilikuwa na zaidi ya Zahanati 15 zilizojengwa na wananchi pamoja na nyumba za wahudumu, zilikaa zaidi ya miaka 5 – 7 bila kupata wahudumu. Baada ya kuomba sana Serikali isaidie Wilaya hii, badala ya kupeleka wahudumu kwa kuwaajiri, iliamua kuhamisha kutoka kwenye *dispensary* za humo humo ndani. Palipokuwa na wahudumu wawili aliondolewa mmoja, akabaki mmoja. Kwa kweli Serikali kuondoa mtumishi mmoja na kubakiza mmoja kwenye *dispensary* ya Kata inayohudumia vijiji vitano hadi saba vyenye wananchi zaidi ya laki moja ni matatizo juu ya matatizo. Kina mama wanateseka na watoto kuunga foleni hospitali kuanzia asubuhi hadi jioni na baadhi yao wanakosa huduma, wanarudi nyumbani na kesho yake wanarudi tena.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye juu chini kuongeza Wahudumu wa Afya katika Wilaya ya Urambo. Mkoaa wa Tabora unaongoza kwa kuwa na Watumishi wachache ni ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, Maduka ya Dawa baridi yanayofunguliwa maeneo mengi hayatimizi matakwa na vigezo vya utunzaji wa dawa kwenye hali inayotakiwa. Madawa yanatunzwa kwenye *temperature* kubwa tafauti na inavyoolekezwa. Dawa zinapoteza nguvu wananchi wanauziwa, wanatumia bila kujuua zinawadhuru na hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, zipo *pharmacy* zinahudumiwa na mtu asiyekuwa na uelewa wowote wa madawa, hajui chochote! Ni wale wa *Standard Seven*. Huku ni kucheza na maisha ya watu/wagonjwa. Tuweke mikakati ya kuangalia na kuhakikisha maduka haya.

Mheshimiwa Spika, watumishi wanakatwa fedha katika mishahara yao kwa maana kwamba wapatiwe huduma ya Afya kwa Bima. Lakini wanapohitaji huduma hii inakuwa taabu sana. Dawa hakuna, wanakaa foleni siku nzima, wanaandikiwa waende *pharmacy* wakanunue. Nini maana ya Bima ya Afya kwao? Wengi wanakwenda hospitali binafsi ili Bima ya Afya ambayo ni *Pre-paid* iwe na maana. Serikali ihakikishe dawa zote muhimu zinapatikana hospitalini na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini pamoja na Serikali kutamka hapa Bungeni mara nyingi na kutangaza kwa umma huduma za afya kwa akina mama wajawazito, watoto na wazee ni bure, hakuna utekelezaji?

Mheshimiwa Spika, Serikali itaeleza ni hospitali zipi ambazo (kwa majina) huduma hizi zinatolewa bure? Katika hospitali za Serikali akina mama wanaambiwa huduma za afya ni kuchangia. Wasipokuwa na pesa watasota hapo hadi jioni bila kuhudumiwa. Fedha zinazotengwa kwa makundi haya zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuwahamisha watumishi walioonekana wameshindwa kazi/wanakiuka maadili ya Utumishi kuwatukana wagonjwa, kudai rushwa wazi na kama hatoi rushwa hapati huduma; kutoa lugha chafu kwa wagonjwa na hasa

kwa akina mama kwani ndio wengi wanaokwenda hospitali; unapomhamisha mtu huyu unampeleka hospitali nyingine anakwenda kuhudumia wanyama? Unamhamisha kutoka Mwananyamala unampeleka Temeke au Muhimbili, hapa umesaidia nini? Huku siyo kulea uzembe na kuhamisha matatizo? Kwa kufanya hivi tunalindana na hatusaidii wananchi. Ahsante.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie maeneo machache ya Hotuba yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa maelekezo yake ya kuwa na Zahanati kila kijiji na Kituo cha Afya kila Kata.

Hatua hii itakapofikiwa Watanzania wengi watapata huduma ya aya bila kufuata huduma hiyo mbali na wanakoishi. Kutokana na maelekezo haya, wananchi wamehamasika sana na kuanza ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya nchini. Changamoto iliyopo ni upatikanaji wa vifaa vya kukamilishwa majengo yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Ninaomba Serikali ipange mpango maalum wa kusaidia nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sera nzuri ya kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi, changamoto inayokabili Sekta ya Afya ni upungufu mkubwa sana wa watumishi kiasi kwamba baadhi ya Zahanati zimejifunga zenyewe kutokana na kukosa watumishi. Aidha, Zahanati na Vituo vya Afya vingi vinaendeshwa na watumishi mmoja mmoja. Kutokana na majukumu mengi ya watumishi hawa, huduma mara nyingi hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ichukue hatua za haraka kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo ya Wizara kuwa wazee wenyе umri zaidi ya miaka 60 wapatiwe huduma ya afya bila malipo. Agizo hili halizingatiwi kwasababu ya ugumu wa kuwatambua wanaostahili.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali iweke utaratibu bayana wa kuwatambua wazee wanaostahili ili wapatiwe vitambulisho maalum ili kuondoa usumbufo wanaopata hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache ninatamka kuwa ninaunga mkono hoja hii.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri wa Afya - Mheshimiwa David Mwakyusa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Katibu Mkuu Wizara ya Afya - Bibi Blandina Nyoni, Mganga Mkuu - Dr. Mtasiwa na Wakurugenzi wote wa idara mbalimbali sekta hii ya Afya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jinsi inavyosimamia sekta hii yenye changamoto nyingi zinazoibuka kila siku, lakini wameendelea kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono bajeti ya Wizara hii kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kupitia sekta hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupa Halmashauri yetu ya Namtumbo kutupatia watumishi kila mwaka na mwaka huu 2010 kutupatia watumishi wakiwemo *Medical Doctor, Assistant Medical Officers, Clinical Officers, Nurse Officers Medical Attendant* na kadhalika. Kwa kweli asiyeshukuru kibaba hata ukimpa gunia hawezি kushukuru. Hivyo, kwa niaba ya Halmashauri na wananchi wa Wilaya ya Namtumbo tunawashukuru sana kwa kutupatia watumishi.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niikumbushe tu Serikali tena pamoja na mazuri yote mnayotufanya Wilaya ya Namtumbo bado haina Hospitali ya Wilaya na ina Vituo vya Afya vitano. Tatizo tunalokabilina nalo, wagonjwa wanaostahili tiba ya Hospitali ya Wilaya huwa tunawapeleka Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma ambayo inazidiwa na kama tunetengewa fedha za ujenzi, Hospitali hiyo ingepunguza mzigo kwa Hospitali ya Mkoa. Lakini pia ingerahisisha huduma karibu kwa wananchi. Naomba pia Zahanati mpya zilizojengwa Namtumbo ziingizwe katika mpango wa *ADO*.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niiombe Serikali kuongeza mafungu ya fedha za dawa kwa Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, sisi kule vijijini tunazaliana sana, hivyo idadi ya ongezeko la watu linakua zaidi ya mahitaji ya dawa kwani nayo yameongezeka maradufu. Hivyo tunapata malalamiko ya upungufu wa dawa sana katika vijiji vyetu, lakini ukiangalia kwa undani utaona dawa zinazoletwa kwa fedha zilizotengwa bado hazikidhi mahitaji ya wagonjwa. Naomba Serikali/Wizara ione umuhimu wa kuongeza fungu la fedha za dawa katika Zahanati zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE: EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kugawa Wilaya ya Kahama (kuipat Wilaya mpya ya Ushetu). Naomba Wizara ya Afya ifanye yafuatayo:-

- (a) Kuboresha Miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Kahama;
- (b) Ipandishe hadhi Kituo cha Afya cha Kungunya kuwa Hospitali ya Wilaya; na
- (c) Isaidie magari ya wagonjwa katika Vituo vya Afya Ushetu, Chela, Mpera na Lungunya.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara isimamie vizuri fedha zinazopelekwa Sekta ya Afya kupitia Wafadhili/Wahisani mbalimbali kwani zinafujwa sana kwenye Halmashauri katika Wilaya. *DMO* na fungu lake la afya hayuko kwenye udhibiti wa *DED* wala Madiwani (kwa *practical experience*).

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, itupie macho *NGOs*. Ziko *NGOs* zinafuja fedha sana. Kuna *NGOs* zinatumia vibaya misaada ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wajane na waathirika wa *HIV/AIDS*. Naomba utendaji kazi wa *SHIDEPHA+* Kahama umulikwe kwani wahitaji wa Kahama hawapati misaada kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE: VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi yako nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya CCM. Pamoja napongezi hizo, napenda kuchaingia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado namwomba Waziri wa Afya alipe kipaumbele suala la Hospitali ya Rwanwa kwani nguvu kubwa ya wananchi wa mara zisipotee bure.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Waganga bado Hospitali yetu ya Mkao bado ni kubwa sana hasa Madaktari Bingwa. Napenda kujua mikakati ya Wizara kuhusiana na kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya CCM inasema wazee na akina mama, watapata huduma za afya bure. Hii ni ahadi ambayo imeshindwa kutekelezeka. Ni nini mikakati ya Wizara kutatua tatizo hilo?

Mwisho, napenda kuzungumzia maslahi ya watumishi. Tunakubali wapo wachache ambao sio waaminifu, kwani hawatoi huduma nzuri; pili, wanaomba na kupokea rushwa. Swali langu ni kwamba Serikali inaboreshaje maslahi yao ili kupunguza kero hii kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

MHE: BRIG. JEN. HASSAN NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala huduma za afya katika Kituo cha Afya – Mlalo ambalo linaongelewa leo humu Bungeni. Ni vyema Wizara (Waziri) akalitolea maelezo. Hata hivyo, ninavyoolewa hili, nikiwa Mbunge wa Mlalo, limeongezwa chumvi za kisiasa kwa malengo ya uchaguzi wa mwaka 2010. Kituo kile cha Afya kina vitanda 28, shuka zipo zaidi ya 36, vyandarua visto. Waliokwenda pale walikuwa na malengo yao, walitoa msaada wa shuka tano na vyandarua vitano.

Ninamshauri Waziri alitolee maelezo hili la Kituo cha Afya cha Mlalo.

MHE: COL. FETECH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza nina heshima kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri iliyojumlisha hali kwa ujumla wa maendeleo na mafanikio makubwa juu ya Wizara ya Afya jinsi ilivyofikia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli juhudini kubwa ya kupambana na Malaria imechukuliwa na kweli inawezekana kabisa Tanzania bila ya Malaria.

Mheshimiwa Spika, hatua ilifikiwa nzuri, bali nina heshima kuiomba Wizara juhudini iongezwe zaidi vijijini na sehemu ambazo zina maziwa mengi, mifereji na baadhi ya mito.

Mheshimiwa Spika, homa za *typhoid* bado inasumbua katika maeneo mengi ya Tanzania. Kwa mfano, Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Morogoro na baadhi ya Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, visima vingi vinachimbwa, lakini vingine ninatumika bila ukaguzi mzuri wa Idara inayohusika kuchunguza maji hayo ipasavyo na kuweza kutumika.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara na hasa katika eneo la Ustawi wa Jamii, juhudini kubwa katika kuwasaidia wazee na wasiojiweza hasa katika kuwasaidia matibabu ya bure na kadhalika. Lakini bado ninazidi kuiomba Wizara iendelee na juhudini zake ili wazee hao wasipate usumbufu mkubwa wakati wanapohitaji huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, nina heshima kubwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati ambapo kwa utaratibu watakaokuwa wamejipangia, Waziri anazo dakika zisizozidi 30, Mheshimiwa Naibu

Waziri zisizozidi 10. kwa hiyo, kwa pamoja wanazo dakika 40. Waliomtangulia walikuwa wanatumia dakika 15 kwa Naibu Waziri, na 25 kwa Waziri lakini, kama ni tofauti, basi *time keeper* ataangalia mambo yanavyokwenda. Aah, ni dakika 15 kwa 25. Basi, kwa hiyo, sasa ninamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Aisha Kigoda, ana muda wa dakika zisizozidi 15, baadaye atafuatiwa na mtoha hoja Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru pia kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, lakini kabla ya kufanya hivyo, ninaomba nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunipa heshima kubwa na kuniamini kumsaidia kama Naibu wa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kipindi chote cha utawala wake wa awamu ya kwanza, kipindi cha miaka mitano. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na mafanikio makubwa katika awamu yake ya pili na ninampongeza sana kwa utendaji (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nakushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeverti kwa maelekezo wakati walipokuwa wanakalia kititako na Mwenyezi Mungu awabariki sana. Naomba nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa uongozi wake akiwa kama kiongozi wa Serikali hapa Bungeni.

Lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri wenzangu na pia Wabunge wenzangu kwa ushirikiano walionipa. Nimejifunza mengi kupitia kwao nami nawatachia mafanikio mema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Prof. David H. Mwakyusa kwa jinsi tulivyoshirikiana kumsaidia Mheshimiwa Rais katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuitekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi.

Nawashukuru sana wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuanzia ngazi ya Taifa hadi Vijijini. Ninawatachia utendaji mzuri kwa manufaa ya Watanzania pamoja na changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, shukurani za dhati kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga zikiwemo Wilaya za Mkinga, Pangani, Muheza, Korogwe Vijijini na Mjini, Lushoto, Handeni, na kwa umuhimu wake Wilaya ya Kilindi ambako nimezaliwa pamoja na viongozi wa chama changu na Serikali kwa ushirikiano wanaonipa. Ninaahidi kuwaenzi kadri nitakavyojaliwa na Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ingawa siyo kwa umuhimu, napenda niishukuru sana familia yangu. Namshukuru sana mume wangu Mheshimiwa Muhammedi Seif Khatib - Mbunge wa Uzini na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano, lakini vilevile nawashukuru sana watoto wangu ambao leo dada

yao Neema amewawakilisha hapa na ndugu zangu ambao yupo dada Farida, ambaye amewawakilisha kwa *support* kubwa ambayo wamenipa wakati wote. Mwenyezi Mungu awabariki sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba niseme kwanza, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa asilimia mia moja na pia sasa niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimejitokeza walipokuwa wanachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo zimeulizwa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi, ninaamini Mheshimiwa Waziri atazijibu lakini nitazitolea maelezo kwa sababu ni nyingi, lakini tunashukuru sana kwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wabunge ina lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya alizungumzia kwamba kuna wagonjwa wengi waliolazwa katika *medical wards* kwa ugonjwa wa Kifua Kikuu hivyo, fedha za Ukimwi na Malaria zipelekwe kusaidia Kifua Kikuu vilevile.

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara imepanga utaratibu endelevu wa kudhibiti Kifua Kikuu hususan katika *medical wards*. Wagonjwa wengi wanatibiwa majumbani kwao kwa kusimamiwa na ndugu zao. Wanaolazwa ni wale tu ambao afya zao siyo nzuri kutibiwa nyumbani. Aidha, Wizara imeandaa mwongozo mpya kudhibiti kuenea kwa Kifua Kikuu katika *medical wards*. Mfuko wa Dunia pia unachangia kikamilifu katika kudhibiti Kifua Kikuu kama ilivyo katika Malaria na Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, suala la uondoaji wa mazalia ya mbu kwa kutumia usafi wa mazingira ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge Feteh, Mbarouk Mwandoro, Salim Hemed, Stella Manyanya na wengine.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (*WB*) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), imepanga kuinua kiwango cha usafi wa mazingira katika Halmashauri zote nchini. Mpango huu unaoanza kutekelezwa mwaka 2010/2011 utahusika na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua, mabwawa, madimbwi, matumizi ya vyoo bora na usafi wa mazingira kwa ujumla.

Kwa kuzingatia Sheria ya Afya ya Jamii, kila kaya itawajibika katika kusimamia utekelezaji wa majukumu haya na ufuatiliaji utafanywa kutumia wataalamu wa Afya ya Mazingira. Wale wote watakaobainika kukiuka Sheria hii, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Kwa kupitia utaratibu wa mpango huu, maeneo mengi ya mazalia ya mbu yataondolewa au kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Kassembe alisema Zahanati kila kijiji wananchi wamechangia matofali kwa ajili ya ujenzi, lakini hakuna msaada wowote wa Serikali, na Waheshimiwa wengine wamehoji utaratibu ukoje katika Mpango wa *MAM*.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa majukumu katika mpango wa MAM ni kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya na Bodi zao za Afya, Vijiji vyote na Kamati zao za Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na wananchi. Utekelezaji wa mpango huu utafuata muundo wa Serikali na ushirikishwaji wa Serikali ndiyo nyenzo muhimu sana katika uendelevu wa mpango wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi.

Wilaya zinatakiwa kuanisha miradi na kuweka katika *Comprehensive Council Health Plan* ili iweze kupata fursa ya kupatiwa fedha kutoka *Health Window* ya Mfuko wa Maendeleo katika Halmashauri zao. Wizara inawashauri Waheshimiwa Wabunge kufuutilia miradi hii ili pale wananchi watakapokuwa wanachangia, basi Wilaya nayo basi itumie fedha inayotengwa kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo kutoka katika bajeti zao.

Mheshimiwa Suleiman Kumchaya aliulizia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mtwara, mpaka sasa hakuna dalili. Ni nini kinafanyika? Wizara inapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kazi ya kuanzisha Hospitali ya Rufaa kwa ajili ya Kanda ya Kusini katika Manispaa ya Mtwara inaendelea kama ilivyopangwa. Hadi wakati huu majukumu yafuatayo yamekamilika na mengine yanaendelea.

Wizara imekwishalipia gharama zote na kwa sasa imekamilisha uwanja kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Pili, Wizara imemteua Mshauri Mwelekezi na sasa amefikia hatua za mwisho na makabrasha yote yatakabidhiwa Agosti, 2010. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imekamilisha ujenzi wa uzio na uwanja. Wizara inajiardaa kuanza ujenzi wa majengo kwa ajili ya magonjwa ya nje kwa ajili ya kliniki maalum katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011

Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Chilolo na wengine wamezungumzia kuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wafanyabiashara wa dawa wenye leseni ambao hutakiwa kuyafungwa maduka yao kwa sababu yako chini ya mita 300. Je, ni Sheria gani inatumika?

Wameshauri wale walio na leseni wasisumbuliwe halafu pia agizo alilolitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 24 Mwezi wa Sita, 2010 wakati akijibu swalii la Mheshimiwa Zambi kuhusu suala la umbali wa maduka, lifuatwe.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha umbali kati ya duka la dawa muhimu kimeanishwa katika kanuni za dawa muhimu za mwaka 2004 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2009. Kanuni hizi zimetungwa chini ya Sheria ya Chakula na Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Kufuatia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la tarehe 24 Mwezi wa Sita, 2010 wakati akijibu swalii la Mheshimiwa Zambi, Wizara imeagiza Mamlaka ya Chakula na Dawa kutokuzingatia kigezo cha umbali katika kupandisha hadhi maduka ya dawa baridi yenye leseni kuwa maduka ya dawa muhimu. Aidha, kigezo cha umbali kitatumika kwa maduka mapya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zainab M. Vullu - Mbunge wa Viti Maalum anahoji, kuna mkakati gani wa kudhibiti uingizaji wa *pads* wanazotumia akina mama ambazo ziko chini ya kiwango na hivyo kusababisha maradhi?

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Chakula na Dawa itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine za udhibiti ikiwa ni pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) kufuatilia ubora wa *Sanitary pads*. Aidha, ili kuimarisha udhibiti wa bidhaa hizo Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 itafanyiwa marekebisho ili kuipa Mamlaka ya Chakula na Dawa uwezo zaidi wa kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mng'ong'o alizungumzia kuhusu uboreshaji wa hospitali ya Wilaya ya Mafinga kikiwemo chumba cha upasuaji. Shughuli zote za uendeshaji wa huduma ya afya ikiwemo ujenzi kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati hushughulikiwa na TAMISEMI. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunatoa miongozo tu na kuleta wafanyakazi.

Mheshimiwa Kayombo anasema Wizara iendelee kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili wafahamu dhamana yao juu ya wateja wao. Wizara ina Kitengo maalum kinachoshughulikia mafunzo ya kujiendezea, mwongozo wa utekelezaji upo na Kanda Nane za Mafunzo ambazo zinashirikiana na Timu za Menejementi ya Mkoa na Wilaya kupanga na kuendesha mafunzo ya kujiendezea katika ngazi zote. Wizara pia imeandaa mpango wa mafunzo wa kujiendezea ambaeo unamhusisha kila mtumishi.

Mheshimiwa Spika, upandishwaji vyeo pamoja na marekebisho ya mishahara kwa watumishi vinachelewa sana. Wizara ihakikishe Watumishi wanapata stahili zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, watumishi wote ambaeo wako chini ya Wizara ya Afya, Fungu 52 hupandishwa vyeo vyao kwa wakati ilimradi wanakuwa wametimiza masharti ya miundo yao ya utumishi kwa kuwa na utendaji mzuri wa kazi. Aidha, marekebisho ya mishahara hufanywa mara baada ya watumishi kukubali kwa maandishi, vyeo vyao walivyopewa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, amesema Serikali imeweka mkakati gani wa kukagua maduka ya dawa mara kwa mara ili kudhibiti madawa yaliyokwisha muda wake wa matumizi?

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa dawa hufanywa mara kwa mara na wakaguzi walioko katika Halmashauri, Mamlaka ya Chakula na Dawa hufanya ukaguzi hakiki kwa kuzingatia mpango wa kazi na upatikanaji wa fedha. Ukaguzi hakiki wa maduka ya dawa hufanywa aghalabu mara moja kwa mwaka kutokana na upungufu wa raslimali watu na fedha. Pale mfanyakishara anapopatikana na kosa la kuuza dawa zilizokwisha muda na matumizi hatua za kisheria huchukuliwa ikiwa ni pamoja kufikishwa Mahakamani na dawa husika kuteketezwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Abdallah Kigoda wamehoji juu ya kukithiri kwa uhaba wa wataalam na upo mkakati gani na Wilaya ambazo zimetuma maombi ya vijana waliomaliza kidato cha nne ili wapate fursa za kujiunga katika vyuo? Lakini vile vile wamezungumzia suala zima la Elimu ya Uzazi wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepokea maombi ya Wabunge wengi ambao wameleta vijana wengi waliomaliza kidato cha nne na sita na sasa hivi maombi hayo yameshaporelewa na Wizara na yanafanyiwa uhakiki ili kuweza kuona kama wana sifa na baada ya hapo watapangiwa kutokana na yale maombi. Lakini kwa sababu nafasi ni chache, hatuwezi kuahidi kwamba wote watapatiwa nafasi lakini pale inapoonekana Katibu Mkuu anasikia, Mkurugenzi wa Tiba pia yuko hapa, katika hayo maeneo ambayo yametajwa basi tutayapa kipaumbele. Lakini pia wale Wabunge wengine wote walioleta maombi yao, basi tutayaangalia kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ikishirikiana na Wadau wamehamasisha viongozi katika ngazi za jamii na familia kupitia Tarafa na Kata juu ya umuhimu wa uzazi wa mpango na faida zake. Jumla ya Makatibu Kata 4,500 Watendaji katika ngazi ya Tarafa wapatao 3,750 na Viongozi wa Madhehebu ya dini 2,500 walishirikishwa katika shughuli mbalimbali za uhamasishaji na uzazi wa mpango.

Aidha, Wizara kupitia kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma inaendelea kuelimisha jamii juu ya uzazi wa mpango kwa njia ya radio, televisheni na majarida mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ilizindua Mpango Maalum wa Uzazi wa Mpango uliokasimiwa (*National Family Planning Costed Implementation Plan 2010-2015*) kwa lengo la kuboresha huduma hiyo, kuboresha upatikanaji wa dawa na kuongeza idadi ya watumiaji wa njia za kisasa za uzazi wa mpango kutoka asilimia 20 mwaka 2004/2005 hadi asilimia 60 mwaka 2015

Mheshimiwa Spika, Wizara ikishirikiana na wadau inaendelea kununua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango na katika mwaka 2009/2010. Wizara kupitia *Basket Funds* imenunu dawa aina ya vipandikizi na sindano kwa thamani ya shilingi bilioni 6.1 na wadau nje ya *Basket Funds* wamenunu dawa za uzazi wa mpango aina ya vipandikizi, sindano, vidonge na vitanzi kwa thamani ya dola za kimarekani milioni sita.

Katika mwaka wa 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na wadau itanunua na kusambaza dawa za kutosha kwa uzazi wa mpango aina ya vipandikizi, sindano, vidonge, vitanzi na *condom* katika vituo vya kutolea huduma za afya. Wizara kwa kushirikiana na wadau itanunua dawa za uzazi wa mpango za shilingi bilioni 14.3. Dawa hizo ni pamoja na sindano na vipandikizi.

Mheshimiwa Juma Killimbah alishauri Serikali ishirikiane na Taasisi mbalimbali kutoa Elimu ya Ukimwi katika shule, vyuo na kadhalika. Serikali inaafiki ushauri huo. Hayo ndiyo yamepangwa kwenye mpango mkakati wa pili wa kudhibiti Ukimwi katika Sekta ya Afya 2008 - 2012.

Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya amesema kulingana na taarifa ya CAG, wapo watumishi hewa ambapo takribani shilingi bilioni nne zililipwa kwa wahusika. Serikali ichukue hatua kwa waliohusika kwa upotevu wa kiasi hicho cha fedha ambapo inawezekana ni *chain* iliyopo Wizarani, Hazina mpaka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilihojiwa juu ya kuendelea kuwalipa watumishi waliostaafu, waliofariki na walio katika likizo bila malipo na kutumia kiasi cha Sh. 77,707,817,000.17. Sababu zilizopelekea kuwepo kwa tatizo hili ni pamoa na mfumo mzima wa Serikali wa ulipaji wa mishahara kufanyika *centrally*, yaani Wizara ya Fedha na Uchumi. Hali hii imesababisha kuchelewa kuwaondoa watumishi wanaofariki, kustaafu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali na Wizara ni kama zifuatazo:-

Kwanza, Serikali imeanza kuimarisha mfumo wa ulipaji wa mishahara ambapo usimamizi wa *pay roll* ya Wizara utafanywa na mwajiri mwenyewe. Mfumo huu utamwezesha mwajiri mwenyewe kumfuata mtumishi wake mara tu anapoacha kazi, anapofariki, kustaafu na kadhalika na mfumo huu mpya utapunguza na kuondoa kabisa tatizo la kuendelea kulipa mishahara kwa wasiostahili.

Pili, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuimarisha udhibiti wa malipo ya mishahara kwa wasiostahili imefanya yafuatayo:-

Mwaka 2009/2010 Wizara imefanya ukaguzi wa watumishi wanaolipwa mishahara na Serikali katika hospitali, vituo vya afya na vituo vya Ustawi wa Jamii wapatao 130. Ukaguzi huo umeweza kupata watumishi wasiokuwepo katika vituo na wapo katika *pay roll* za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana (*Makofi*)

SPIKA: Pole sana. Tunabanwa kidogo na muda na sasa ninamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi nyingine tena ili niweze kutoa majibu ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Kabla sijaendelea na mimi ninakutakia kila jema unapopambana na ndugu zetu kule Usisya na sehemu zote za Jimbo lako. Hicho kiti kimekupendeza sana, tungependa kukuona tena kwa miaka mitano mingine. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ungechangia kidogo Mheshimiwa Waziri kama ungeshughulikia mchango fulani wa kukarabati hospitali ya Wilaya ya Urambo. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Kwa kuwa hiki ni kipindi cha majeruhi, tunganeza mapema, lakini tutajitahidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi wakati wa hotuba yangu. Napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw' aliyewasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya mwaka uliopita pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. Aidha, Wabunge karibu wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi wameipongeza Wizara yangu kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake. Kwa niaba ya wafanyakazi wote wa sekta ya afya na Ustawi wa Jamii, naomba nipokee pongezi hizo kwa moyo mkunjufu. (*Makofi*)

Vile vile, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba hii na vile vile zilizotangulia hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tumepta waombaji wengi na kwa muda ulionipa wa dakika 25, hata niende kwa *speed* namna gani siwezi nikamaliza hoja zote, lakini majibu ninayo, naahidi tu kwamba Wabunge watayapata kwa maandishi. Kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yangu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri hatutauhesabu muda huo katika dakika zako ule wa kutaja majina, dakika 25 zako zimebaki pale pale. Ahsante.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Ahsante sana. Mheshimiwa Spika, Wabunge 54 wamechangia hotuba yangu. Kati ya hao, 12 wamechangia kwa kuzungumza na 42 wamechangia kwa maandishi. Aidha, Waheshimiwa Wabunge nane walichangia wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda walikuwa Wabunge 24 kama ifuatavyo:-

Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw' - Mwenyekiti wa Kamati za Huduma ya Jamii na Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali - Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mbunge wa Konde, Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Idd Azan, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mheshimiwa Joel Nkya Bendera, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mheshimiwa Zainab Matitu Vulu, Mheshimiwa Said Hemed Khamis, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Brig. Hassan Athumani Ngwilizi, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Col. Feteh Said Mgeni, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa William Lukuvi, na Mheshimiwa Raynald Mrope. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii katika hotuba ya Mheshimiwa Mkulo ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Halima Omar Kimbau, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Dr. Lucas J. Siyame, Mheshimiwa Dr. Willibrod Peter Slaa, Mheshimiwa Fatuma Othman Ali, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukimbwa, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Halima Mamuya na Mheshimiwa

Zulekha Yunus Haji. Naomba niwapongeze wote waliochangia na ninaahidi kwamba yote waliyotushauri tutayazingatia ili kuboresha utendaji wa Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naanza na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Alisema kwamba kiwango cha madeni cha *MSD* kimeongezeka na kufikia shilingi bilioni 36.7. Hali hii inaifanya *MSD* kulalamikiwa kwa kushindwa kufanya kazi zake vizuri. Kamati imeagiza Wizara ilipe deni hili. Wizara imepokea maelekezo hayo na itaifanyia kazi kwa kipindi chote cha mwaka ujao wa fedha. Aidha, naomba kutoa maelezo kuhusu deni hilo.

Deni hili limetokana na kwamba dawa na vifaa vinavyotolewa na wadau wa maendeleo kama msaada na miradi misonge ambapo fedha za kukomboa vifaa hivi hazijatengwa. Ili kuondokana na deni hili Wizara katika mwaka tunaomaliza hivi sasa tumefanikiwa kulipa kiasi cha shilingi bilioni sita na Wizara imeandaa mpango wa kuendelea kulipa hilo deni na kwa kuanzia tumetenga shilingi milioni 500 katika mwaka ujao kama fedha za dharura.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuelimisha watu dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na kuhamasisha wajitokeze kupima. Tunachukua ushauri huo na mgao wa bajeti ya Serikali kwa sekta ya afya kulingana na Azimio la Abuja ambalo linalekeza Sekta ya Afya kutengewa asilimia 15 ya bajeti ya Serikali uongezwe.

Katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Sekta ya Afya ilitengewa takriban asilimia 11.2, mwaka uliofuu ambaa ndio mwaka unaokwisha hivi sasa ilikuwa asilimia 11.6 na katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011 imetengewa asilimia 12.2. Kwa hiyo, utaona kwamba tunaelekea hiyo asilimia 15 na jinsi uwezo wa kifedha utakapopatikana tuna imani kwamba tutafika huko tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa na suala la uboreshaji wa huduma vijijini, Mfuko uendelee kubuni mbinu mbalimbali za kuboresha huduma kwa wanachama wake vijijini ikiwemo elimu na kusajili maduka ya dawa muhimu vijijini. Hii ilikuwa tunazungumzia Mfuko wa Afya wa Taifa.

Wizara imeagiza mfuko kuhakikisha kwamba unabuni mbinu mbalimbali kwamba kuanzia sasa program ya elimu ya Kata kwa Kata ihushe pia elimu ya Mfuko wa Afya ya Jamii na kwamba mfuko utenge zaidi ya asilimia 30 ya fedha zake katika kasma ya mikopo nafuu ya vifaa tiba na ukarabati wa vituo ili zilenge Vituo vya Afya ya Msingi Vijijini. Mfuko uhakikishe unayasajili maduka ya dawa muhimu katika mikoa mbalimbali kila Mamlaka ya Chakula na Dawa inapokuwa imekamilisha taratibu husika ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa dawa.

Hoja za Kambi ya Upinzani ambazo zinajibu hoja za Wabunge wengine wengi waliochangia nitazisoma kama ifuatavyo:- Hospitali nyingi za mikoa zina uhaba wa vitendeakazi na ni chakavu. Kiasi cha Sh. 7,446,932,000/= kilichotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali za mikoa ni ndogo. Jibu letu tulikuwa tunatenga fedha hizo kuanzia mwaka 2007 na tunakarabati hizo hospitali kwa awamu kutokana na ufinyu wa fedha, hatuwezi tukakarabati zote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifanye jitihada ya kupambana na msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Mwananyamala, Temeke na Amana katika Mkoa wa Dar es Salaam na hii imechangiwa vile vile na Wabunge kutoka Ilala na Kinondoni mkoani Dar es Salaam. Sababu kubwa ya mlundikano wa wagonjwa katika hospitali hizo ni kwamba kumekuwa na ongezeko la wagonjwa, lakini rasilimali za kutolea huduma haziendi sambamba.

Pia kumekuwa na ongezeko la ufaamu wa jamii kuhusu tiba ya hospitali na ongezeko la vyombo vya moto vya usafiri, vimesababisha ajali nyingi na pia kumekuwa na kutokufuata utaratibu wa rufaa, watu wanajiendea tu ambapo wangeweza kutibiwa katika hospitali nyingine.

Hatua zilizochukuliwa ni kwamba tumeipandisha hadhi hospitali ya *CCBRT* kuwa Hospitali ya Rufaa, vile vile na hospitali ya Jeshi ya Lugalo. Tumeipandisha hadhi hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala kuwa za rufaa za mkoa, lakini vile vile hospitali ya Sinza aliyoizungumzia Mheshimiwa Azan, Mnazi Mmoja, Vijibweni na Rangi Tatu Mbagala kuwa hospitali za Wilaya. Tuko katika mazungumzo na Serikali ya Korea Kusini kwamba tujenge hospitali *Satellite* moja maeneo ya Temeke, nyingine unapoelekea Kibaha na nyingine maeneo ya Bunju na hizi zikifanya kazi vizuri hakutakuwa na haja ya wagonjwa kuja mpaka katikati ya mji.

Mheshimiwa Spika, kuna swalii lililohusu Bajeti ya Maendeleo ya shilingi milioni 448, kwamba asilimia kubwa ni za wahisani: Je, kwa nini Wizara inategemea sana wahisani kwa ajili ya maendeleo ya miradi? Tunakiri kwamba asilimia kubwa ya bajeti ya maendeleo inatoka kwa wahisani, lakini na wao kufuatana na makubaliano ya Kimataifa ndivyo inatakiwa iwe. Kwa sababu magonjwa tunayokabiliana nayo hapa tunawaambia tusipokabiliana nayo hapa watakwenda wakabiliane nayo nyumbani kwao. Lakini kwa jinsi uchumi unavyoendelea kukua kiasi hiki kinapungua kwa maana ya kwamba mchango wa Serikali unapanda mwaka hadi mwaka.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina mipango mingi iliyowekwa kwa ajili ya kuimarisha huduma. Hata hivyo, bajeti ya Wizara kila mwaka zinakuwa na malengo tofauti yaliyoanishwa katika mipango mikakati. Bajeti ya Wizara kila mwaka ilikuwa ikielekezwa katika kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika mpango mkakati wa Wizara. Hatukurupuki na hatuendi nje ya mipango ambayo tumejiwekea, mipango ya Ilani ya Uchaguzi na vilevile MKUKUTA na Dira ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na uhaba wa rasilimali watu ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi kwamba ni tatizo kubwa. Tunakiri kwamba ni tatizo kubwa lakini linapungua na takwimu aliyoitoa Mheshimiwa Msemaji alisema kuna upungufu wa asilimia 67.5. Ukweli ni kwamba upungufu kwa sasa hivi ni asilimia 62.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeandaa mipango mikakati, tumefanya mapitio ya mitaala na sasa hivi tumeanzisha mafunzo ya cheti na nafurahi kusema kwamba *batch* ya kwanza wanaomaliza hivi sasa ni 1,793 kwa upande wa *Nursing* na *Clinical Assistant*

592 wameiva na wako tayari kupelekwa katika vituo na tuna *batch* mbili kwa kila mwaka. Kwa hiyo, nataka niwaambie kwamba tuko *serious*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kwamba katika bajeti ya mwaka 2009/2010 kiasi cha shilingi bilioni moja kilichotengwa kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kupunguza vifo vya akina mama na watoto kimeelekezwa kulipia mshauri (*Consultant fees*). Je, haya matumizi ya kupunguza vifo vya uzazi, anasema ni matumizi mabaya.

Hapa ningesema kwamba tunao mradi wa mikoa mitatu; Mara, Tabora na Mtwara ambao umefadhiwa na *ABD*. Katika fedha hizo walizotenga kuna *counterpart funds* na sisi lazima tulipe. Sasa hili la *consultant fees* ni code tu ya Hazina, lakini *otherwise* ni *counterpart funds* na wala sio fedha za kumlipa mshauri.

Kwa mujibu wa takwimu za *WHO* Tanzania ina Madaktari 2.3 kwa watu laki moja. Kiwango kinachopendekezwa na *WHO* ni madaktari angalau 10 kwa watu laki moja, hivyo Wizara iweke juhudzi za makusudi kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya ili kuboresha utoaji wa huduma.

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii inakusudia na ina mpango wa kufikia kigezo hicho cha Madaktari 10 kwa wananchi laki moja. Vyuo Vikuu vinavyofundisha Madaktari vimeongezeka kutoka Chuo Kikuu cha Muhimbili na vyuo vingine vinne na idadi ya madaktari wanaodahiliwa imeongezeka kutoka 440 hadi kufikia 778 kwa mwaka 2009/2010. Aidha, wapo wanafunzi wengine wanaosoma katika vyuo vya Udaktari nje ya nchi kwa kujigharamia.

Kwa nini Wizara haiwatambui wahitimu wa Chuo cha Kumbukumbu cha *KCMC* kuwa *Medical records?* Tunasema tunawatambua. Ni kweli walikuwepo, lakini katika maboresho yaliyokuwa yanaendelea katika Idara ya Utumishi waliwachukua Watunza Kumbukumbu wote wakawaweka pamoja. Lakini baada ya kuujaribu huo muundo kwa muda tukaona haufai na sasa hivi tumerudisha kwetu na kinachongojewa sasa ni kwamba upitishwe kwenye Baraza letu la Wafanyakazi.

Hoja kwamba Vitengo vya Huduma za Moyo na Figo vilivyopo katika Hospitali za Muhimbili, *KCMC* na Mbeya Rufaa viimarishwe ili kuweza kutoa matibabu kwa wagonjwa wengi, tunakubali hilo na tunafanya hivyo na ni ripoti tu kwamba kuanzia mwaka 2006 tulipoanza hizi shughuli hadi kufikia Juni, 2010 wagonjwa waliopatia operesheni za moyo ni 310,000 katika hospitali hizi tatu. Mbeya bado hatuzaanza.

Lakini vile vile tutanza kusafisha damu Muhimbili mwezi Agosti na tunaendelea kuzijengea uwezo hospitali zetu ili ziweze kufanya shughuli za *super speciality*.

Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa hospitali ya kisasa ya upasuaji wa moyo pale Muhimbili. Tumepeleka wataalamu kutoka katika hospitali hizo kwa mafunzo nchini Urusi, India na Afrika Kusini ili kuendeleza huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala kwamba Serikali iimarishe huduma ya tiba ya saratani pale *Ocean Road*. Tunakubaliana na hili. Hivi sasa tumeanza kujenga jengo jipya ambalo litakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 170.

Tumenunua mashine mpya inaitwa *hydorate machine* ya kutibu saratani ya shingo ya kizazi na daktari imoja tayari yuko Afrika ya Kusini anasomea udaktari bingwa wa magonjwa ya saratani na tunaanzisha *speciality* ya mambo ya saratani Muhimbili, muhula ujao mwezi Oktoba na tuna uhusiano wa *tele-medicine* na Taasisi za India.

Mheshimiwa Spika, vilevile Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* imekamilisha taratibu za kuingia mkataba na Bima ya Afya ya Taifa ili wagonjwa walio na Bima ya Afya wapate huduma kupitia mfuko huko.

Kuwepo na utaratibu maalum utakao ratibu upelekwaji wa dawa katika uwiano sawa na kuangalia idadi ya wagonjwa waliopo katika eneo husika ndivyo tutakavyofanya mwaka 2010, mgao wa fedha utazingatia hilo na sasa hivi tunaboresha takwimu kwa kuzikusanya upya ili tujuje kwa uhakika ni watu wangapi wanakaa katika eneo fulani.

Mheshimiwa Spika, vituo vya *MSD* vilivyopo Mikoani viimarishwe ili kutoa huduma zinazotolewa zifike kwenye vituo vya kutolea huduma kwa wakati muafaka na haraka. Tumeendelea kuimarisha hizo huduma, tunao mpango wa mkakati hivi sasa na tunajenga maghala ili kuongeza na safi kwa sababu katika mpango wa *Integrated Logistics System* makasha yatakuwa yanatengenezwa kwenye vituo vya Kanda na pia Wizara iliagiza *MSD* kwa sababu malalamiko mengi yanatoka kwenye vituo vya afya na zahanati.

Kwa hiyo, tuliwaelekeza wajaribu kuangalia namna ya kuzifikisha hizo dawa mpaka kwa mtumiaji wa mwisho katika zahanati na walifanya hivyo katika Mkoa wa Tanga ripoti ilitolewa na tumeona ni kitu kinachowezekana. Kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011 kama mtaipitisha tutaanza katika baadhi ya mikoa na kwa jinsi tunavyopata uzoefu tutakwenda nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna ripoti ya ukaguzi ya *Global Fund* ya mwaka 2009 ilionyesha kwamba mwaka 2007 ukaguzi wa ndani uliofanywa na *MSD* uligundua kwamba dawa zenye thamani ya shilingi milioni 163 zilikuwa zimepotea au kuibwa. Pia *Global Fund* iligundua kwamba mwaka 2007 kiasi cha *USD* milioni 2.4 kilitolewa na *Global Fund* kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa dawa. Lakini hizo pesa hazionekani zilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dawa tunazozizingumza ni hizi dawa mseto. Tulianza kuzitumia mwaka 2006 na zilipokuja kuingiza kwenye vitabu tulitumia mkono lakini kompyuta. *Price water coopers* walipewa kazi ya kuja kuzihakiki na wao walitumia kompyuta zile zilizoingizwa kwa kompyuta peke yake. Sasa tulipowaeleza hilo wakarudi tena ikaonekana kwamba rekodi zote ni safi na hiyo barua ya kutuambia kwamba kuna matatizo tunayo na wanaendelea kutoa michango yao.

Mheshimiwa Spika, uwepo mpango wa kuhakikisha kwamba wanaotumia dawa za *ARV* wapatiwe lishe stahiki. Tunakadiria kwamba kuna wagonjwa milioni 1.4 wanaoishi na *VVU* hapa nchini. Gharama za kuwapatia chakula wagonjwa bila malipo ni kubwa sana na Serikali kwa sasa haina uwezo. Ili kutoa maelekezo ya kiufundi katika suala hili Serikali imeandaa muongozo wa lishe kwa watu wanaoishi na virusi vya *UKIMWI* ambao kwa lugha nyepesi kabisa inaeleza maelekezo jinsi wanavyowenza kutengeneza vyakula kwa kutumia vyakula vya hapa hapa nchini na muongozo ninao hapa. (*Makofi*)

Aidha, Serikali inashauri kwamba kila Halmashauri iandae mikakati ya kusaidia watu wanaoishi na virusi vya *UKIMWI* wanaohitaji huduma za chakula pamoja na huduma nyininge za kimaisha. Pamoja na ushauri huo tunafanya kitu kinaitwa *food fortification*. Serikali inaandaa mpango maalum wa kuongeza virutubisho katika vyakula na tayari tunafanya hivyo katika vyakula vingine. Lakini vilevile kuna vyakula ambavyo vinaingizwa kama *food supplement*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna mpango wa kuiomba Serikali kwamba hivi vitambuliwe kama ni dawa. Kwa hiyo, kodi na nini ziondoke kama inavyokuwa kwa dawa, vikipunguzwa watu wanaweza wakamudu wale wenye uwezo. Kwa nini mradi wa kupeleka *ambulance* zenye magurudumu matatu kwenye maeneo ya vijiji haujaanza hadi hivi sasa na ulikuwa umetengewa fedha hapo mapema?

Mheshimiwa Spika, tunakili kwamba tumelizungumza hapa na pesa zilitolewa lakini hiki ni kitu kigeni, kumekuwa na utaratibu wa mlolongo kidogo, kwa sababu ilibidi tuwapeleke vijana wetu kwenda kuangalia na kujadiliana nao hao wanaotengeneza ili tupate chombo ambacho kinaweza kikahimili barabara zetu. Lakini ninachowenza kusema ni kwamba kwa sasa taratibu hizi zimekamilika na hivi karibu tutaona tuna *launch* na kuzipeleka hizo *ambulance* 400. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katibu amenisemesha kwa dakika moja naomba niongezewe. (*Kicheko*)

SPIKA: Endelea tu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nijaribu kujibu hoja ambazo zimeibuliwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Mzee Dr. John Melecela ambapo aliomba kila zahanati iwe na darubini na vilevile wawepo wataalam wa maabara na vipimo vya *VCT* na mambo yote yanayohusiana na magonjwa kama ya *TB*. Tunasema Wizara kupitia bohari ya dawa itasambaza darubini katika zahanati na vituo vya afya vyote vijijini, mijini na Manispaa zinashauriwa kuingizwa kwenye makadirio ya mahitaji ya watumishi wakiwemo wataalam wa maabara ili Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma iweze kutoa kibali vya ajira kwa wataalam hao. Hivi sasa Wizara yangu imeanza kusambaza matumizi ya kipimo ambacho kinatoa majibu kwa haraka (*rapid diagnosis test*). Hii itakuwa rahisi zaidi hata wale ambao hawawezi kutumia darubini inaweza ikatambua wagonjwa wenye malaria kwa urahisi na kwa muda mfupi. Kipimo hiki kimeanza kutolewa katika Mikoa ya Iringa, Pwani, Kagera, Manyara na

Arusha. Mkoa wa Dodoma utajumuishwa katika awamu inayofuata. Kwa hiyo, tunakwenda awamu kwa awamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Margreth Mkanga ametuhimiza kwamba kanuni za sheria ya watu wenye ulemavu iharakishe. Tunakubalina na hilo, tuna mpango gani wa kufufua Chuo cha Watu wenye Ulemavu Masiwani ukiangalia kwenye hotuba yangu mwaka huu imetengewa fedha. Ubatuaji wa huduma za ustawi wa jamii uende haraka. Ni kweli na tumewaagiza Halmashauri kwamba katika mipango yao waweke hayo mahitaji, wapeleke watumishi na sasa hivi tunazalisha kada hii kwa kasi kidogo. Kwa hiyo, tusiwe na sababu katika miwili ijayo kwa nini watu wasipate wataalam wa namna hii.

Mheshimiwa Mariam Kasembe amesema zahanati kila kijiji wananchi wamechangia matofali kwa ujenzi. Hizi zahanati zinajengwa na wananchi na Serikali inatoa pesa kutumia Halmashauri na Halmashauri ndio inaweka vipaumbele isaidie zipi. Kwa hiyo, napenda kushauri kwamba sote kwa sababu tunaingia kwenye vikao vyta Halmashauri tuhusike katika kujua kwamba pesa zimepatikana kiasi gani na zahanati gani ambazo Halmashauri imetambua kwamba zisaidiwe katika mwaka husika wa fedha.

Mheshimiwa Suleiman Kumchaya amezungumzia habari za kituo cha afya cha Lupaso kwamba hakitumiki kinavyopaswa na tunavyosema kwamba ukarabati wa zahanati ya Lupaso iliyo chini ya Jimbo la Katoliki la Tunduru, Masasi na iliziunduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya nne Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kufunguliwa Wilaya ya Masasi kwa kushirikiana na wamiliki wa kituo kipyaa cha afya cha Lupaso imekuwa ikiendesha shughuli za kinga na tiba katika kituo hicho. Kwa mfano Wilaya imipeleka Afisa Tabibu yupo pale. Hata hivyo Wizara inamkaribisha Mheshimiwa Mbunge kufafanua zaidi ni kitu gani hasa kilichokuwa kikitarajiwaa ambacho hakifanyiki kwa hivi sasa. Wizara pia inatoa ushauri kwa Wilaya na wamiliki wa hospitali ikiwa ni pamoja na viongozi kukaa pamoja na kupanda mipango ya kuimarisha zaidi mazingira ya utoaji huduma. Habari za ujenzi wa Hospitali ya Rufaa imezungumziwa na Hospitali ya Nanyumbu ambayo tumewahi kuzunguza ni kwamba Halmashauri iamue inataka kuitumia kwa shughuli gani. Sisi tutakuja tuikague na kama tutaona inafaa kwa sababu Hopitali ya Wilaya ipo ile inawenza ikaingia kwenye Mfumo wa *Voluntary Agency* (VA) na tutasaidia kifedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mariam Kasembe alisema majengo ya Chuo cha Watu Wasioona cha Mtapika yamekuwa chakavu. Ni kweli lakini tumeshaanza mchakato wa kukarabati vyuo vyote vyta watu wenye ulemavu kikiwemo cha Mtapika tunakwenda hatua kwa hatua viko vingi, vilikuwa katika hali mbaya lakini *Inshallah* Kituo cha Mtapika tutakifikia vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Susan Lyimo alisema Kitengo cha Ustawi wa Jamii kimetelekezwa na Bajeti yake ni finyu. Kitengo hiki ndicho kinachohudumia watu wenye ulemavu kwa kuwa ulemavu si ugonjwa pengine kitengo hiki kingekuwa mahali pengine. Nikianza na

hili la mwisho kitengo hiki kiende wapi, ni Mheshimiwa Rais ambaye anaamua hivyo lakini si kweli kwamba Idara ya Ustawi wa Jamii imetekelawa ila ufinyu wa Bajeti unaonekana ni tatizo ambalo limeathiri shughuli za Wizara nzima. Aidha, suala la mahali gani, kama nilivyosema na ukiwaliza uitaona wanaona kwamba Wizara ya Afya ndiyo mahali pake na tunawatengea pesa za maendeleo na waliniambia kwamba walikuwa hawapati huko walikotoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Tatu Ntimizi nadhani nimejibu swal lako uliposema kwamba Uyui ina Kituo kimoja cha afya, nawatupia huo mzigo kama Halmashauri na sisi tutasaidia pale tunapoweza. Haitakuwa vibaya kuiga majirani zenu wa Urambo kwa sababu katika kitabu changu utakuta katika vituo vya afya na zahanati nilizoidhinisha zianze kupata dawa mwaka huu wao ziko ishirini na leo jirani pale tukisema kwamba hakuna inatia simanzi. Wivu wa maendeleo si kitu kibaya twende tukajifunze Urambo tuone wao wamefanya fanyaje mpaka wakapata vituo vyote hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Susan Lyimo alisema Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* haina mradi wowote wa maendeleo na hilo nimelisema kwamba taasisi imetengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 400 na ziko chini ya mradi wa kuimarisha Hospitali za Rufaa kifungu 2001 - 5411.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena na naomba nirudie nilichosema pale awali kwamba Wizara hii inagusa kila mtu. Kwa hiyo, hatukushangaa kuona kwamba michango ilikuwa ni mingi. Michango tunayoipata sisi tunaithamini sana, tuna mipango yetu ya namna ya kufuatilia nini kinaendelea huko lakini wenzetu wako kule Majimboni vilevile na kila tunachowaambia hakuna tunachokipuuza na naahidi kwamba tutazingatia na wale ambao hatukuwajibu moja kwa moja niahidi kwamba mtapata majibu kwa njia ya kawaida ya maandishi. Kwa maana hiyo msiwe wakali sana tunapokuja kwenye vifungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini tuingie katika utaratibu wa Kanuni ya 100 ili kuweza kuhitimisha hoja hii. Katibu.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu – 52 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Kifungu 1001 *Administration and General* Sh. 4,772,188,004

MWENYEKITI: Nilijua ndiyo maana sikuwahoji haraka haraka. Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Iddi Azzan. Tunaanza na Mheshimiwa George Lubeleje. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu tu, kuna zahanati mpya ambazo tumejenga katika Wilaya ya Mpwapwa. Kuna zahanati ya Kiyagea, Mhenzele na Mwanakianga. Zahanati ya Mwanakianga ni jengo ambalo tumelikarabati na itasaidia sana kuhudumia wanachuo wa Chuo cha Ualimu Mpwapwa. Sasa Ombi langu lilikuwa nimeomba kwamba je, katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 imetengewa fedha kwa ajili ya kununua dawa?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni ndiyo na nikimuelekeza kwenye kurasa 127 wa kitabu cha hotuba yangu. Zahanati zilizoidihinishwa katika Wilaya ya Mpwapwa ni Chaludewa, Kiegea, Kizi, Rufu, Mwanakianga na Mhenzele na alitaka kujua ya Mwanakianga imo katika orodha hii.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami siko mbali sana na mzungumzaji aliyeketi hivi sasa Mheshimiwa George Lubeleje. Katika mchango wangu wa maandishi nimeelezea juu ya zahanati zilizojengwa takribani miaka miwili iliyopita katika Jimbo langu la Iramba Magharibi. Zahanati za Mwanduigembe, Maluga, Mlandala na zahanati ya Kikonge. Zahanati hizi tangu zimejengwa na hivi sasa yale majengo sasa yanaanza kupoteza ile hadhi lakini nimeangalia katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri pamoja na mgao ambaa amesema kwamba zahanati zitapatiwa dawa lakini nimeona kwa Mkoa wa Singida Wilaya ya Iramba zahanati hizi hazipo. Sasa Waziri anipe ufanuzi, zahanati hizi za Jimbo la Iramba Magharibi itakuaje na hivi sasa zina muda mrefu na hali tukiwasitiza wananchi wajenge zahanati?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningeanza kwa kuwashukuru wananchi kwa muitikio mzuri wa kujenga zahanati kitu ambacho kilionekana hakiwezekani, sasa tunaona zinaibuka na tunalifahamu tatizo la wafanyakazi, tatizo la dawa hatuna. Lakini sisi kama Wizara hatuvezi tukajua kuna zahanati wapi na wapi, ni Halmashauri ambazo zinaletwa maombi. Sisi tukizikagua na kuridhika ndiyo tunaziweka kwenye vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi zahanati alizozisema Mheshimiwa Juma Killimbah sijui kama utaratibu ulifuatwa lakini siyo vibaya akiwaliza Halmashauri halafu tujaribu kufuatilia kama zilikuwa zimeombewa makasha ya dawa hatutakuwa na sababu ya kuzinyima. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, utaratibu ndiyo huo Waheshimiwa Wabunge lazima Halmashauri zetu zitoe taarifa kwa Wizara ama sivyo itakuwa ni vigumu kwa Wizara peke yake kuelewa. Mheshimiwa Janet Kahama.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa sijakusudia lakini naona ni muhimu sana kwa sababu sijaridhika kabisa katika upande wa *Pariatic care* kama nilivyosema. Wanafunzi vyuoni waanze kuchukua masomo haya ambayo ni muhimu sana, najua nitajibowi kwa majibu baadaye *by writing* lakini nilitaka nijibiwe sasa ili niweze kuridhika na hasa kinachoniumiza mimi ni kuona kwamba hii dawa ya *morphine* haifiki mikano sasa hivi, sasa ninavyozungumza 95% ya wagonjwa wanahangaika kule wanaumwa hawapati hii dawa, nilitaka kujua na anieleze vizuri wanarekebisha sheria ili kusudi wauguzi waweze kupewa mafunzo haraka ili waweze kuhudumia mikano wagonjwa wa kansa zaidi. Naomba nielekezwe hilo nipate majibu, ahsante.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Janet Kahama amezungumzia habari za dawa ya *morphine* na anachojaribu kuishawishi Serikali ni kwamba iwe ni dawa inayopatikana kwa urahisi, sasa tuna dawa na dawa, dawa hii tunayoizungumzia ina *tendency* ya *addiction* kwamba unapompa mtu ni kama dawa za kulevyo kwa hiyo, haiwezekani ikawa inapatikana kiholela mtu akawa anaipata hivi tulivyo hapa sasa hivi hospitali za Mikoa zinaweza zikaagiza kwa hiyo, hata hospitali za Wilaya zikihitaji ina maana kwamba ni lazima zijenge hoja na ijulikane kuwa ni kweli zinakwenda kwa watu ambao wana maumivu na wanaishi kwa kutumia dawa hiyo, lakini jambo la kuwa ipatikane hivi hivi tu na kwamba tubadilishe sheria tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi huo, kumbe dawa hii inalevya halafu inakuwa ya mazoea na halafu mtu unaendelea kuitafuta. Mheshimiwa Vita Kawawa. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliochangia asubuhi nilizungumzia kuwa Wilaya yetu ya Namtumbo haina Hospitali ya Wilaya. Lakini katika majibu ya Mheshimiwa Waziri sikusikia lakini pia wakati nasoma kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri niligundua kwamba mwaka huu Wizara au Serikali imeongeza takribani shilingi bilioni 20 katika ugawaji wa dawa na vifaa tiba katika Zahanati, Vituo vya Afya na hospitali zetu na huko nyuma niliomba Serikali kwa kuwa hatuna Hospitali ya Wilaya angalau Kituo chetu cha Afya kilichopo pale Wilayani Namtumbo kipandishwe kiwe kinapata dawa kwa hadhi ya Hospitali ya Wilaya, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutupa ufanuzi leo watu wa Namtumbo wamo katika fedha hizi shilingi bilioni 20 zilizoongezeka mwaka huu wa 2010/2011 tunaweza kupata dawa kwa ngazi ya Wilaya katika Kituo chetu cha Afya cha Wilaya ya Namtumbo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mheshimiwa Vita Kawawa alituletea maoni yake kwa maandishi na nimezungumza naye. Na hicho kituo cha Afya anachokizungumzia nimewahi kukiona sijui kama kimeendelea lakini tunatoa dawa kwa hospitali ya Wilaya ambayo ina hadi ya

Wilaya hatuwezi kutoa dawa kwa kituo cha afya lakini kama kuna kuendelea zaidi katika Majengo na *facilities* zingine sisi tutakwenda kukagua na hatuna sababu ya kuwanyima hizo dawa kwasababu ni Wilaya na ina stahili kuwa na Hospitali ya Wilaya, lakini kama *facilities* zilizopo ni za kituo cha afya kama *theataer* na vitu kanma hivyo huwezi ukapeleka dawa unazopeleka kwenye Wilaya ambayo tayari ina vitu vyote vinavyohitajika, lakini niseme tu kwamba tutapeleka watu waende wakaangalie ili tutafute *formula* nzuri ili watu wasihangaike kupata dawa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi kwa kweli maeneo mengi yamejaa pongezi. Pongezi kwa Waziri, kwa Naibu Waziri, kwa Katibu Mkuu kwa sababu karibu Wabunge wote wa Singida tuliyokuwa tunayaomba hapa katika Wizara hapa katika Wizara ya Afya yametekelzeza, tunawashukuru sana, kwa unyenyekevu kabisa nilikuwa naomba jambo moja tu kwamba Wilaya ya Iramba katika Hospitali ya Kiomboi ina tatizo la mtaalamu wa Bingwa wa *X-ray* yaani mtaalamu hakuna, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ni mtu wa huruma na anajua kabisa kuwa wana Singida tunahitaji kushikwa mkono, naamini katika hili nimkumbushe labda anaweza akatamka jambo. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue hilo kama ombi tutalifanya kazi.

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kuna suala nilikuwa nimeuliza la kuhusu ujenzi wa hospitali. Mbunge aliyenitangulia katika Jimbo la Chalinze wakati ananikabidhi ofisi ikiwa pamoja na kiwanja chenye ukubwa wa ekari 100 amenishauri na kuniambia kuwa hiki tunaweza kujenga hospitali kubwa ya kuweza kusaidia wananchi wa Chalinze pamoja na maeneo mengine nilishafanya mazungumzo ya muda mrefu na ofisi ya Wizara ya Afya ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Waziri na kuniambia kuwa wako kwenye mkakati wa kutafuta wafadhilli ikiwezekana tuweze kujenga hospitali pale Chalinze, nilikuwa naomba nipate ufanuzi tu kuwa sasa tumefikia miaka mitano na muda umeisha tumbakiza mwezi mmoja ile mikakati bado ipo ya kuweza kujenga hospitali pale au haipo, naomba kupata ufanuzi.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tulikuwa na mazungumzo na mwekezaji sijui nimuite mwekezaji, hili tulizungumza naye alionyesha nia ya kujenga hospitali ya kisasa eneo la Chalinze na wenzetu wa Chalinze wakaainisha eneo kuwa ni wapi pa kujenga, tulipofuatilia tukagundua kuwa huyu Bwana alitaka sisi ndiyo tumdhagini ili aweze kupata mkopo wa kujengea hiyo hospitali, sasa hiyo kwetu ikawa ngumu tukawa tunajiuliza kwa nini tusitafute mkopo wenye kwa sababu kuitia kwa mtu mwengine ni gharama kwa sababu kutakuwa na *charges* kwa hiyo, tuliona kama huyu mtu nilitaka kusema tapeli sijazoea kutumia lugha kama hizo lakini ni kwamba hakuwa na nia njema na sisi, alionyesha kuwa anataka kutusaidia lakini kumbe anataka kufanya hivyo kwa mgongo wetu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ndiyo matapeli tu wenye kwenye hao, Mheshimiwa Switi.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia hospitali ya Kristo Mfalme ambayo kwa sasa inatumika kama Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga. Nimesema kuwa hospitali hii imezidiwa, haina wodi ya watoto, haina *maternity* inayoridhisha na wala haina mahali ambapo wanawenza wakatenganisha watu wenye magonjwa ya kuambukiza, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nikiri kwamba tumepata mchango wa mama Switi. Hospitali anayosema ni hospitali binafsi ni ya Hertman na kwa sababu Halmashauri inastahili kuwa na Hospitali lakini kwa Sumbawanga mjini hapakuwa na hospitali kwa hiyo, wakaomba hiyo hospitali iwe ya Halmashauri tukaenda kuikagua tukakuta ina *basic facilities* ya kuitwa hospitali na tukairuhusu itumike kama *council hospital DDHCDH* lakini pia kulikuwa na maelewano kwamba ina *minimum requirements* kwa hiyo, wapanue kwa hiyo, hili suala la kupanua ni la mmiliki wa hiyo hospitali pamoja na Halmashauri na pale tunawenza kusaidi kama Serikali itafanya hivyo kama tunavyofanya katika hospitali zingine za Wilaya. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhakika nafikiri na hata Waziri anajua kuwa sina shida na mshahara wake maana yake utanipa taabu kidogo kwa kuwa ni jirani itabidi aje kwako tena ukimyima mshahara. Katika mchango wangu nilizungumzia juu ya wafanyakazi waliokuwa wafanyakazi wa Hospitali ya Rufaa ya Mbeya kama 25 hivi ambao waliachishwa kazi wengi wao walikuwa walizni na wahudumu na mpaka sasa hawajapata haki zao ni takribani miaka miwili wamekuwa wakihangaika, nilikuwa namuomba Waziri ajaribu kulitatta tataizo hili kabla hatujavunja Bunge. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, sijui walipunguzwa au walifukuzwa au sijui vipi.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumepata mchango wa Mheshimiwa Benson Mpesya na ni suala ambalo nimezungumza naye nje ya ukumbi. Pale Hospitali ya Rufaa Mbeya kuna kazi ambazo tunaziita *non-core work activities* kama kufagia, kufyeka hakuna sababu ya kuwaweka watu kwenye kada kama yetu, sasa wale waliokuwa wanafanya hizo kazi wakapunguzwa na kinachozungumzwa hapa ni kwamba hawakupata stahili zao, niahidi tu kuwa ninalichukua na nitalifanya kazi mimi mwenyewe na kama nilivyosema kabla Bunge halijaisha sijui kama hapo ni mtaji wa kura ama vipi lakini nitajaribu kwa kila nitakachowenza ili tupate kauli ni nini kinaendelea.

MHE. SUSAN J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi vilevile sina haja na mshahara wa Waziri kwa kuwa Mheshimiwa Waziri tuna heshimiana sana na amekuwa akitujibu kwa ufasaha mzuri sana. Lakini nilikuwa nina jambo moja tu ambalo nimelichangia kwa kuwa wanawake wajawazito wameendelea kufariki kwa sababu ambazo ziko ndani ya uwezo wa wauguzi kwa mfano tukio lililotokea Mwanza tunashukuru Mungu kuwa yule mama hakufariki lakini tayari alikuwa amefika kwenye kituo cha afya na hakupata huduma, lakini mambo haya yamewafanya wanawake wengi

wajawazito sasa wawe na hofu ya kwenda kwenye vituo vya afya na hivyo kuamua kujifungulia sehemu wanazozijua wao ambazo siyo salama.

Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba utuambie yule muuguzi au wale waliohusika na kitendo kile wamechukuliwa hatua gani ili akinamama wajawazito wawe na imani na vituo vyao vya afya au na wauguzi wao.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hili suala lilitokea tukiwa Dar es Salaam na siku hiyo nilikuwa nimeitwa mbele ya Kamati tunajadili Bajeti hii. Aliyeliibua alikuwa ni Mheshimiwa Susan Lyimo, mimi nilikuwa sijasikia ila yeye aliona kwenye vyombo vya habari asubuhi ile na wakati huohuo nikatuma watu watupe majibu na nikayapata kabla hata hatujamaliza kikao na nikamueleza Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Kwaangw' ni kweli hili tukio limetusikitisha wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyotokea ni kwamba huyu mgonjwa alipokuwa anapimwa katika kituo kinaitwa Karume maeneo ya Pasiansi aliambiwa ikifika siku ya kujifungua hapa sisi hatuwezi lakini akapata uchungu akaenda pale Karume, ndiyo wakamwambia kuwa tulikwambia hatuwezi kwa hiyo, nenda huko, sasa makosa yalifanyika kwa kuwa hawakumpima kumuangalia kuwa je, atafika kule na isitoshe pale Halmshauri ya Jiji kuna *ambulance*, wangeweza kuita *ambulance* ije imchukue, hawakufanya hivyo kwa hiyo, tunakiri ni kosa kubwa sana ambalo linastahili kukemewa na lisirudie tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hiyo hiyo nikawa nimepata ripoti na nikaongea na wakubwa wa kule kuwa tuko katika kituo kuangalia nini kimetendeka na jioni yake nikaambiwa kuwa wamesimamishwa kazi na uchunguzi ulikuwa unaendelea. Kwa siku ya leo siwezi kujua hatua gani zimechukuliwa lakini hatua za awali zilichukuliwa wakati tunajaribu kutafuta nini kifanyike lakini muhimu zaidi ni kwamba haya matukio yasitokee tena hilo tuliwekee mikakati kuwa lisitokee tena. (*Makofi*)

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, katika mchango wangu wa maandishi nilimpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima kwa kazi nzuri waliyofanya kudhibiti milipuko ya Malaria na kupunguza vifo vya watoto na nilikwenda na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa mpaka Rubya. Unavyomsikia kwa unyeyekevu na uchungu yanapotokea majanga ndivyo alivyodhahirisha pale hospitalini Rubya, wanamkumbuka kweli na tunaomba asipingwe na mtu yoyote huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikujibiwa kwa kuwa muda ulikuwa hautoshi. Kwa sababu huwa nakuwa na machungu sana ninaposema hapa na Serikali inaniitikia haraka sana, tunaenda mpaka Jimboni sasa nikaona kuwa huu ni Mkutano wa mwisho wa Ishirini, hizi pongozi za dhati kwa kweli ambazo zimenusuru watoto na akinamama kutoka bila kujibiwa, najua alikosa muda, upokee shukrani za dhati. Je, unazipokea? Ndiyo nilichosema tu kwenye mchango wangu huu siyo ufanuzi lakini lina umuhimu

wake na waandishi wa habari waandike kwamba Masilingi alifurahi sana akashukuru, akaondoka na kicheko siyo kwamba huwa analia tu humu Bungeni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwenye **mnyauko** waliandika nimelia Bungeni nilieleza masikitiko sikutoa machozi. Lakini nilikuwa nalia kimoyomoyo lakini sasa ni furaha tele, je, unapokea pongezi na kwa Mheshimiwa Rais utafikisha? Watoto hawafi na haya ni mambo mazito mtu anaweza kudhani kuwa ni mzaha watoto hawafi na haikupungua kutoka 40% hadi 10% sisi tunadhani imepungua kutoka 40% mpaka 2% maana sasa hawafi sasa mnasema bado 10% mkae karibu na sisi wasife watoto tena umepokea pongezi? (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri inabidi useme kitu hapo.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Masilingi alituandikia barua ya pongezi na sisi katika Wizara yetu utekelezaji wetu ni shirikishi kwa hiyo, nazipokea kwa moyo mkunjufu kwa niaba ya Wizara nzima. Ni kweli mwaka 2006 kulikuwa na mlipuko wa Malaria kule Muleba na Karagwe tulikuwa hapa Bungeni nikaenda mwenyewe na kujonea hali na tulipoanza hii hatua ya upuliziaji tuliona tuanzie kule, katika hospitali ya Rubya kulikuwa na watoto zaidi ya 250 wote wako kwenye *drip* wauguzi walikuwa wanne, Karagwe wao walizidiwa wakapiga *tent* nje maana yake wodi zilikuwa zimejaa na kwa ujumla katika miezi mitatu tulipoteza watoto kama 286.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho watoto walikuwa hawaendi shule. Lakini sasa hivi wanakwenda shule kwa sababu afya yao ni nzuri na *infection rate* ya Malaria ilikuwa 40%, sasa hivi ni chini ya 10% na ukienda wodini hukuti watoto wenyne Malaria kwa hiyo, rai yangu ni kwamba huu upuliziaji wa viwatilifu ambayo inapigwa sana kelele na watu wanaojiita wana mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia habari za maisha ya watoto, mtakapofika maeneo yenu tungeomba mtoe ushirikiano wa kutosha ili tukiingia kwenye kijiji kila mmoja nyumba yake aturuhusu tuipige viwatilifu, kwa sababu utakapogoma, sisi kuingia kwenye nyumba yako ina maana hawa mbu hawatakuwa lakini watakapotoka pale hawatasema tumuumbe fulani aliykataa, watakwenda hata kwa wale walioturuhusu kupiga viwatilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba niishie hapo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Pengine itasaidia Waziri mkitunga sheria ndogo za kuwashughulikia watu wa aina hii, kwa sababu ni tabia ambayo ni kinyume kabisa na utamaduni wetu, uamue tu kwa makusudi ukatae huduma, mbu waendelee kuua watoto na watu wazima. Ni jambo la kufikiria hilo.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipokuwa nachangia nilizungumzia Kituo cha Afya cha Lupasu, nilisema kwamba tangu kifunguliwe na Mheshimiwa Rais hakijafanya kazi ipasavyo kwa sababu zifuatazo, kwanza hatuna mganga mtalaam, kuna wakati tulikuwa tunapata mganga kutoka

Mkomaingo sasa hafiki tena na kile ni Kkituo cha Afya, kuna *Clinical Officer* ambaye utalaam wake tunautilia mashaka. Hivi ninavyozungumza kulikuwa na *operation* ndogo ndogo pale hazifanyiki tena zimesimama na baadhi ya majengo yamefungwa tu, naomba kauli yako Waziri mwanzoni ulisema hukunielewa lakini sasa umenielewa, unajua mimi ni mtangazaji by *profession*. (*Makofi*)

Mheshmiwa Mwenyekiti, pili,...

MWENYEKITI: Hairuhusiwi sasa, unaruhusiwa moja tu. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulimsikia hapa akichangia, kituo kile ni kituo ambacho kimejengwa vizuri na katika moja ya ziara za Mheshimiwa Rais katika maeneo hayo yeye ndiye alikizindua na Naibu wangu alikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza habari za watalaan kama nilivyosema wakati najibu hoja za uhaba wa wafanyakazi ni kweli tunao uhaba wa wafanyakazi lakini tunaanza kupata wafanyakazi. Nilieleza kwamba baada ya kubadilisha mitaala sasa karibu vijana 2,000 tutawapangia kazi. Kwa kituo cha afya stahili yake ni kuwa na *Assistant Medical Officers* yaani Madaktari Wasaidizi siyo Daktari mwenye *degree* ya *MD*. Lakini sisi tunapeleka hao madaktari baada ya kuombwa, kwa hiyo kama kituo kinahitaji mtalaam wa namna ile, ina maana Halmashauri ijue maana yake kile kituo kipo chini ya Halmashauri, wao ndiyo wanaomba kupitia Utumishi, Utumishi wakitoa kibali sisi ndiyo tunatoa watalaan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ripoti ndiyo tunaipata kwa mara ya kwanza na tunasikitika kwamba kituo kile ni kizuri kwa taarifa nilizonazo na tungependa kifanye kazi ili kiokoe maisha ya wananchi. Namuomba ndugu yangu Mheshimiwa Suleiman Kumchaya kwamba mtuletee ripoti nini mnataka tufanye, lakini vile vile kwa upande wa wafanyakazi waombwe kwa sababu kuna maeneo tumepeleka wafanyakazi kumbe hawakukasimiwa utakuta wanakaa miezi sita hawana pesa za kuwalipa. Kwa hiyo, tunaanza na kusema kwanza mahitaji yetu ni watalaan hawa na hawa na pesa zao tumetenga, mtueleze sisi tutatafuta hao watalaan tuwalettee. (*Makofi*)

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni jambo la kawaida sana kwa sasa hivi unapokwenda hospitali unaandikiwa ukununue dawa kwenye maduka ya dawa, lakini kama tunavyofahamu katika kila duka la dawa lazima kuwepo na Mfamasia na msaidizi. Maduka mengi yamekuwa yakifungwa kwa kutokuwa na mtalaam huyo mfamasia hata kama msaidizi yupo, je, Serikali haiioni kwamba iruhusu Mfamasia mmoja aweze kusimamia duka labda zaidi ya moja ili wananchi waweze kupata huduma hiyo kwa sababu wanategemea maduka ya dawa zaidi kupata dawa kuliko katika hospitali zetu? Ahsante.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ndivyo ilivyo kwamba kuna mafamasia wengi ambao wana-supervise phamacy nydingi tu,

kwa hiyo, kama hilo lilikuwa wazo niseme lipo na unawazo sawasawa na Serikali ya CCM. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ndivyo taratibu zinavyoruhusu ama mmefumba macho tu?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndivyo tunavyoruhusu.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nashukuru kwanza Serikali kwa jitihada zake za kutokomeza Malaria, lakini ningependa kupata maelezo kutoka Waziri, hapo zamani wanawake wajawazito walikuwa wanatumia dawa za *chloroquine* ili kuzuia Malaria, nilitaka kujua je, kwa sasa hivi wanatumia dawa gani? Na kama dawa za Mseto zimeshafanyiwa utafiti kwa wanawake wajawazito wakitumia wanaweza kupata madhara gani baada ya muda mrefu. Kuna madhara yoyote wanaweza kuyapata kutokana na matumizi ya dawa hizo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunatumia dawa ya *SP* kwa wanawake ambao wana ujauzito, wanameza hizo dawa mara mbili katika kipindi cha ujauzito wao. Dawa ya mseto ya *ALU* imekuwepo kwa miaka michache si zaidi ya sita, sasa linaelekeza miaka kumi kusema kweli inakuwa vigumu. Lakini tumewahi kujibu swali hapa Bungeni kwamba imeonekana kwamba haina madhara na ndiyo dawa ya mstari wa mbele dunia nzima. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, kwa kweli na mimi sina haja ya kunyofoa mshahara wa kaka yangu lakini kuna usafanuzi kidogo nahitaji.

Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani ilizungumzia kuhusu ripoti ya *CAG* na kuainisha maeneo yale matatu ya shilingi milioni 77.7 za mishahara hewa, shilingi milioni 312.7 ya masurufu pamoja na malipo ya shilingi milioni 156 ambayo hayakuoneshwa stakabadhi nzuri yana utata. Kuna malipo ya namna hiyo mengine tangu mwaka 2000 ambayo hatua zake zilizochukuliwa hazionekani. Kwa hiyo, pamoja na majibu ya Naibu Waziri alipokuwa anazungumzia njia za kuepukana na mishahara hewa sasa hivi, lakini ni hatua gani zimechukuliwa kwa upotevu wa fedha hizi kuanzia mwaka 2000 na hili halijatokeza katika ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009. katika usafanuzi wake Naibu Waziri katika upande wa madaktari kwamba kwa mujibu wa *Wonder Health* kuna madaktari kumi kwa watu....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge unauliza swali la pili sasa ambayo Kanuni haziruhusu. Mheshimiwa Waziri kwa swali la upotevu na ubadhilifu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika hoja zilizotolewa za Mkaguzi Mkuu tulisema kwamba hizi ni shilingi 77,770,817.17 zilikuwa zimeonekana na kwamba tulizifanyia

ufuatiliaji. Hatua ambayo tulichukua baada ya kuona kwamba vituo vya afya na vituo vya ustawii wa jamii ambapo watu 130 walikaguliwa wakaonekana kwamba wengine walikuwa hawapo tukaweka mfumo mzuri wa ulipaji. Wizara iliwasiliana na Mfuko wa Pensheni wa PSPF na NSSF ili wakatwe katika pesheni zao, watumishi waliostaa fu na katika mirathi ya watumishi waliofariki, aidha, Wizara imewaandikia na kupitia waajiri wao watumishi walichukua likizo bila malipo ambao wameajiriwa katika taasisi mbalimbali lakini wanaendelea kulipwa mishahara na Serikali Kuu ili watumishi hao warejeshe fedha za mishahara yao waliolipwa kulipitia akaunti zao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, hatua zimechukuliwa.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu kuhusu wale wananchi wa vijiji vya Igita, Nyarwana na vile vijiji vya Nyamwaga pamoja na Nyamongo wale waliochukuliwa sampuli za damu kwa ajili kupata vipimo baada ya kutumia maji machafu katika Mto Tigite, je, wananchi wale wameshapata vipimo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mbunge alichangia kwa maandishi na aliuliza kuhusu sampuli za wananchi 115 ambao walichukuliwa sampuli za damu kule *North Mara*. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilichukua sampuli za damu kutoka kwa wananchi hao na kuzifanya uchunguzi wa kimaabara na matokeo kupelekwa ofisi ya Makamu wa Rais ambao walikuwa wanaratibu kazi hiyo. Kwa hiyo, sisi tumeshapeleka kule taarifa kwa ripoti sasa inatakiwa itolewe upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, itabidi ifuatiliwe hiyo.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka ufanuzi kutoka kwa Waziri kwamba kwa miaka mingi wauguzi wenyewe shahada walikuwa hawapati mishahara yao stahili. Badala ya kupewa mishahara ya shahada walipewa mishahara ya *diploma* na hii ni uonevu kwamba miaka mingi unajifunza katika vyuo vyetu wenye nchini unapata shahada lakini unalipwa mshahara wa *diploma*. Wizara mara nyingi imekuwa ikiahidi, nilitaka kujua utaratibu ukoje sasa hivi, na hii imesababisha kwamba udahili wa wanafunzi hawa wa shahada katika fani ya uuguzi ikapungua mno. Je, wanapata haki zao sasa hivi? Kama hawapati ni lini wataanza kupata haki zao stahili?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali alitoa mawazo ya Kambi ya Upinzani na hili suala halikuwemo lakini lilikuwemo mwaka jana, ni kweli tulianzisha shahada ya uuguzi ambayo huko nyuma haikuwepo, kwa hiyo, vijana wetu walipokuwa wakihitimu wanajikuta hawako katika mfumo mzima na kama alikuwa *Staff Nurse* anarudi kuwa *Staff Nurse* na hili liliwavunja moyo sana, lakini sasa tuna utaratibu mpya ambao na wenye wameingizwa katika utaratibu mzima wa Wizara na ile miaka yao walijotumikia kusomea zaidi imezawadiwa kwa maana wanapowekwa ni mahali ambapo hatujasikia malalamiko tena. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia habari ya Chuo cha Uuguzi cha *St. Gasper* cha Mjini Itigi na kwamba mapema mwaka huu tulipata bahati ya kutembelewa na Naibu Waziri wa Afya ambapo alielezwa matatizo mbalimbali ya chuo hicho. Lakini kubwa zaidi ni suala la ruzuku katika kusaidia uendeshaji wa chuo hicho kwa sababu chuo hicho kinatoa mafunzo mbalimbali kwa wauguzi kutoka hospitali za Serikali na binafsi. Ningependa kujuu katika Bajeti hii kuna nini kwa ajili ya chuo hicho?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vyuo vingi vya binafsi, vingi ni vya Makanisa mbalimbali na katika mpango mzima wa MMAM ambapo tunaongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa na vile vile watakaofuzu tumeona ni lazima kuwe na *public private partnership*. Kwa hiyo, tumewaendea hawa wenzetu waliokuwa na vyuo wapanue, ambao hawana kama wana uwezo waanzishe vyuo vya namna hiyo ya *St. Gasper* ya Itigi. Katika kufanya hivyo sisi tunatoa ruzuku kwa sababu wanafanya kazi kwa niaba ya Serikali na ndiyo utaratibu uliopo. Najua *St. Gasper* mlikuwa na matatizo ya walimu tukaahidi kwamba tutasaidia na tumefanya hivyo kwa hiyo nadhani najibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwamba ruzuku inatolewa kama waliopo hawajapata basi hili liwe kama lalamiko kwamba hatujatimiza ahadi yetu.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi, kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ningependa kumpongeza sana Waziri pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Afya kwa kitendo cha kupandisha hadhi hospitali zetu za Amana, Temeke na Mwananyamala, tunashukuru sana kwa hilo, sidhani kama kuna haja ya wananchi wa Dar es Salaam hawa kwa sababu wamepambana sana, hoja hii ni ya tangu mwaka 2006 tumekuwa tukipambana na hatimaye limefanikiwa tunashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo dogo tu la kutaka ufanuzi, kwenye mchango wangu nimezungumzia suala la Hospitali ya *CCBRT* na zile pesa ambazo Serikali inapeleka kule kwa ajili ya kulipa mishahara ambazo sasa zinakaribia shilingi milioni 900 ama shilingi bilioni moja. Huduma kwa wananchi wetu bado hazifiki kama vile ambavyo tulikubaliana lakini Serikali imekuwa ikilipa ile mishahara. Nataka kupata maelezo ni kitu gani kinachoendelea na Serikali kuendelea kulipa pesa hizi. Najua utanijibu kwa maandishi lakini vyema ukonijibu sasa ili wananchi wangu wa Dar es Salaam wasikie na waelewe ni kitu gani kinachoendelea. Tumetafuta ufanuzi kwa Halmashauri ya Jiji hatujapata, kwa hiyo, tunaomba ufanuzi wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Iddi Azzan ukishajibiwa na Waziri baadaye tuonane au leo au kesho mimi ndiyo mlezi wa Hospitali ya *CCBRT* nina taarifa zote kamili, lakini Waziri endelea si wajibu kujibu hapa. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kujibu hilo swali kwa sababu mlezi yupo hapa na Mwenyekiti wa Bodi yupo hapa hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali tunayoizungumza ya *CCBRT* iliingia mkatuba na Halmashauri ya Jiji. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam hawana hospitali ya Mkoa kwa hiyo, wakakubaliana kwamba ile itumike kama hospitali ya Mkoa na moja ya kipengele ilikuwa ni kwamba tuanze kuwasaidia kuwalipia mshahara wafanyakazi wao kwa mategemeo kwamba baadaye itakuwa Hospitali ya Mkoa kama zilivyo zingine ambazo tutaziendesha sisi. Nadhani kinachoibuka hapa ni kwamba mishahara inalipwa lakini mwananchi wa kawaida akienda pale analipa. Hilo ni suala ambalo itabidi tushirikiane na wenzetu wa Jiji tuone kwamba kuna matatizo gani, kwa utaratibu wa kawaida kama Serikali inachangia basi mwananchi wa kawaida apate unafuu anapokwenda pale. Niseme tu kwamba tukae tuangalie ni kitu gani kifanywe lakini naona wanaendelea sasa hivi na Mheshimiwa Rais alikuwa mgeni rasmi tunauchangiaji wa ujenzi wa hospitali ya akinamama. Kwa hiyo, tusiende haraka sana. (*Makofî*)

Lakini mambo yote haya yanaweza yakazungumzika tuone nini cha kufanya. Nadhani tunachotaka ni unafuu wa mwananchi wa kawaida akienda hospitalini kwa sababu sisi kama Serikali tuna mkono wetu kifedha. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Azzan ajue tu kwamba hata kabla ya uamuvi wa kuwa hii hospitali ifanye shughuli kama hospitali ya Mkoa, hospitali hii inafanyakazi kubwa sana kwa miaka mingi, kushughulikia matatizo maalum ya watoto wa aina mbalimbali na walemvu wa aina mbalimbali kwa mfano watoto wote wanaozaliwa na vichwa vikubwa Tanzania nzima wanatibiwa pale, watoto wote ambao wana ugonjwa *clubfoot* yaani ametoka mtoto ambaye mguu umepinda kwa ndani unanyooshwa ili mradi wapelekwe kabla ya wakati na utaratibu wa malipo ni kwamba asiyeweza halipi, anayeweza anachangia. (*Makofî*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 704,590,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh. 884,507,760
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 91,850,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1005 – <i>Information Education and Communication</i>	Sh. 268,175,470
---	-----------------

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 1005*, kifungu kidogo 221300, *Educational Material, Supplies and Services*. Nilitaka ufanuzi katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu madaktari hawa ambao kwa kila madaktari wawili wanahudumia watu 100,000 kwa Tanzania, lakini *World Health Organization* wanasema angalau *standard* ipatikane madaktari 10. Katika mipango ya Serikali alivyofafanua ni kwamba tunaongeza vyuo, madaktari wengi

watapatikana kielimu. Lakini nilitaka kujua suala la kupata madaktari zaidi na kuongeza vyuo zaidi haijatosha, mimi sijaifahamu kwa sababu hivi sasa kuna mtindo wa watu ku-*graduate* lakini wakahamia nchi za nje wanakopata mafao zaidi.

Je, Serikali ina mpango gani kuongeza tu vyuo na mipango zaidi ya kupata madaktari nchini kufundisha watu au wale ambaa baada ya kufundisha kuwa-*Maintain* wasiondoke Serikali ina mpango gani kuzuia hawa madaktari wasiondoke tuliokuwa nao angalau kama tuko na madaktari wawili angalau tufikie madaktari watano kwa watu 100,000?

MWENYEKITI: Ili nimruhusu Mheshimiwa Waziri kujibu nataka usimame useme umechomekea tu hapo siyo mahali pake.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakubaliana na wewe.

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waziri majibu. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Ni kweli hili suala halihusiani na hiki kifungu. Lakini suala la watalaaam kuhamza nchi kwenda nchi nyingine ni changamoto ya nchi zetu ambazo zinaendelea. Niliwahi kuambiwa kwamba madaktari walioko Paris wa kutoka Senegal ni wengi kuliko wale waliobaki nyumbani kwao. Kwetu hatuna shida kubwa lakini ni kweli sensa tuliyofanya mwaka juzi ni kwamba madaktari 100 walikuwa wamekimbia nchi. Kwa hiyo, tunalijadili suala hili ni kwamba siyo matatizo yetu sisi peke yetu, hatuwezi tukapata *solutions* sisi peke yetu ni lazima tuwahusishe na wale ambako wanakimbilia watu. Lakini vilevile tuangalie huku kwetu wanakimbia kwa nini. Kwa hiyo, kuna *pull factors* na *push factors*. Ina maana tuangalie hapa nchini nini kinawakimbiza, lakini nini kinawafanya waende kule wanakwenda huko kwa sababu kuna fedha nyingi, mishahara mikubwa na sisi *certainly* hatuwezi tukashindana na Marekani, Ujerumanu au Uingereza. Kwa hiyo, inabidi tuongee na wenzenetu.

Sasa kulikuwa na wazo kwamba labda hawa wanaopora madaktari wetu watulipe kwa maana ya kutoa fidia, lakini wao wanasema kwamba sisi hatukua kuwachukua wao wenyeve wamekuja. Sasa ina maana basi kwamba kama wanakwenda kule na wanapokelewa kule kuna nafasi za kazi. Kwa hiyo, tunawaambia na wao wa-*train* zaidi. Sisi tunasema watusaidie ku-*train* zaidi kwamba tunajua watu watahama, lakini kama tulikuwa tuna-*train* watu 100 halafu wanachukuliwa watano ambaa ni 5% tukitoa na 1,000 wakichukua 5% tutabaki na wengi. Kwa hiyo, ndiyo mazungumzo yaliko sasa kwamba watuonee huruma. *It is cheaper to train them here* kuliko kule kwao. Kwa hiyo, mazungumzo yaliyopo sasa hivi na nadhani yatakulika. Ahsante sana. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1006 – Procurement Management Unit.... Sh. 236,342,000

Kifungu 1007 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 82,200,000
Kifungu 2001 – <i>Curative Services</i>	Sh. 159,486,499,336
Kifungu 2003 – <i>Chief Medical Officer</i>	Sh. 8,877,971,890
Kifungu 3001 – <i>Preventive Services</i>	Sh. 28,896,218,252
Kifungu 4002 – <i>Social Welfare</i>	Sh. 3,891,251,338
Kifungu 5001 – <i>Human Resources Development</i> . .	Sh. 21,787,173,950

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Fungu 52 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Kifungu 1003 <i>Policy and Planning</i>	Sh. 67,345,289,760
Kifungu 2001 – <i>Curative Services</i>	Sh. 70,247,573,233

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3001 – *Preventive Services* Sh. 304,022,804,007

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana, kifungu 3001, kifungu kidogo cha 5485 - *Health Sector Development program* na kifungu kidogo cha 5492 - *HIV/AIDS Control Program* 5498 *Support to TB/Leprosy Control Program*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, unaruhusiwa swali moja kwenye Kamati ya Matumizi, sasa wewe unauliza ukoma na kadhalika.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tuchukue kifungu kidogo cha 5492 *HIV/AIDS Control Program*, naona Serikali haikuchangia chochote kwa mwaka huu katika mapambano dhidi ya UKIMWI, wakati fedha zote za mapambano dhidi ya UKIMWI inatoka kwa *donors*, nataka ufanuzi.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni moja ya programu ya kupambana na *HIV* katika *sub votes* zingine pesa zipo zinatolewa na Serikali. Lakini niseme tu kwamba hawa wahisani mpango tulionao moja ni wa mfuko wa pamoja ambao ni *Basket Funding*, lakini kuna wengine wanatoa pesa kwa *specific programmes*. Kama hapa *Global Fund* ndiyo wanatoa hizi pesa. *Global Fund* inashughulikia *HIV*, Malaria na *TB*, sisi tunajenga hoja tunaandika *proposal* tunapewa hizo hela. Sasa kama nimepata hela kwa ajili ya hii shughuli haitakuwa busara nikazika hela zingine tena za Serikali wakati kuna mapengo mahali pengine. Kwa hivyo, hiyo ndivyo ilivyo kwamba hizi zinakuja kwa programu hii, kama watapunguza sisi tuta *chip in* na kuongeza hela ya Serikali. (*Makofii*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 4001 - *Tanzania Food and Drugs Authority*.... Sh.500,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 4002 - *Social Welfare* Sh. 1,355,278,000

MHE. DR. ALI TARAB ALI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwenye kifungu 5485 *Supports to Social Welfare Services* hapa naona hakuna *donors* wala Serikali ambayo imechangia. Je, tulielewe vipi Mheshimiwa Waziri? Ahsante sana.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kifungu kilichotangulia na hiki kinachofuata maneno ni yale yale. Tuliona tu-consolidate na hela zote tumeziweka katika kifungu kidogo kimoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kweli.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 5001 – *Human Resource Development* ... Sh. 4,971,570,000

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 5001* kifungu kidogo 2204 kwenye jedwali hili la kitabu hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika watumishi waliogaiwa kwenye Mikoa yote Mkoa wa Mara haumo. Sasa nilitaka kujua wamesahaulika au imekuwaje? Labda nipate majibu.

MWENYEKITI: Naye amechomekea hayo ni mambo ya kitabu cha pili. Lakini kwa faida tu ya sisi sote kuelewa Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema kweli kachomekeea. Hii kasma inahusu vyuo vyetu ambavyo tunavipanua ili kuendana na mambo. Lakini katika zahanati na vituo vya afya ambavyo tumeidhinisha mwaka huu ilikuwa baada ya kupata ripoti, baada ya kupata maombi na tukavikagua. Sasa itasaidia kama Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi ametuambia kwamba walileta maombi lakini anaona kwamba hayamo humu. Tuko tayari kuya-accommodate pale yatakapopita taratibu kama nilivyoeleza pale awali. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Kabla sijamuita Mheshimiwa Waziri kutoa taarifa ya shughuli za Kamati, nimepokea malalamiko hapa kwamba humu ndani kuna mbu wanawang'ata Wabunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atajua namna ya kulishughulikia pamoja na sehemu nyingine ya Serikali. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaniruhusu nije kupulizia kuta za jumba hili ili tusing'atwe na mbu. (*Makofii*)

SPIKA: Safi kabisa.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA NA BISHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2010/2011
yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina furaha kutangaza kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo hii tarehe 28 Juni, 2010 yameyapitisha rasmi Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka unaofuata wa 2010/2011. Nampongeza Waziri, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kazi yao ngumu. Natumaini kwamba fedha hizi zilizoidhinishwa na Bunge watazitumia vizuri kuweza kutupa huduma iliyo bora zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

Kabla ya kufikia mwisho nakumbusha kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnatakiwa kwenye mkutano utakaofanyika pale Ukumbi wa Pius Msekwa. Naambiwa itakuwa ni kwa kifupi kwa sababu mambo ya mpira yanaendelea saa tatu na nusu. Kwa hiyo, ni kipindi kifupi tu. Mnajua Mwenyekiti ni msikivu, Mheshimiwa Waziri Mkuu na yecheza pia alipata kucheza mpira zamani kule Mpanda. (*Makofii/Kicheko*)

Baada ya kusema hayo nawashukuru sana kwa siku nzima hii na sasa naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.40 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 29 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)